

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Ishirini na Nne – Tarehe 9 Mei, 2019

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae.

Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

MHE. ASHA MSHIMBA JECHA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU):

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

MHE. QAMBALO W. QULWI – NAIBU MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Taarifa ya Msemadi Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Kuhusu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea.

Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Maswali, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi sasa aulize swalii lake.

Na. 196

Serikali Kuzipatia Waganga Zahanati za Jimbo la Manyoni Magharibi

MHE. YAHAYA O. MASSARE aliuliza:-

Wananchi wa Manyoni Magharibi kwa kushirikiana na Serikali kuitia miradi mbalimbali ikiwemo *TASAF* wamejenga zahanati katika Vijiji vya Gurungu, Sanjaranda, Kitopeni, Ipande, Doroto, Itagata, Kalangali, Makale, Mwamagembie na Kintanula, lakini mpaka sasa zahanati hizi hazina Waganga:-

Je, ni lini Serikali itazipatia zahanati hizo Waganga, ili wananchi wapate huduma kufuatana na sera yake?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Omari Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na 2018/2019 Serikali imeajiri watumishi 8,444 wa afya katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambapo watumishi 46 walipangwa kwenye vituo vya afya na zahanati katika Jimbo la Manyoni Magharibi. Zahanati za Gurungu, Sanjaranda, Kitopeni, Ipanda, Doroto, Itagata, Kalangali, Makale, Mwamagembe na Kitanula zimepatiwa Waganga na wataalam mbalimbali wa afya ambao wanatoa huduma hadi hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya vituo vya afya vya kutolea huduma za afya sambamba na kuajiri wataalam wa afya kwa awamu kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali na tumeona kweli Serikali sasa imeonesha nia ya kupunguza kadhia hii ya watumishi wa kada ya afya. Nina maswali madogo mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, dhamira ya Serikali, lakini na wananchi katika Jimbo la Manyoni Magharibi, Halmashauri ya Itigi ni kujikwamua, wameanza kutumia nguvu zao katika kujenga zahanati na vituo vya afya katika vijiji vyao, lakini nguvu zao zinaonekana kuisha. Je, Serikali iko tayari sasa kuwasaidia wananchi wa vijiji ambao wameanza kujenga zahanati kwa nguvu zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika swali ambalo niliuliza mwaka jana kipindi kama hiki majibu ya Serikali ilikuwa yameonesha kwamba na *Hansard* iko hapa ninayo kwamba, Serikali ilikuwa imetenga milioni 600 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, lakini hadi tunapozungumza leo hii bajeti nyingine ya Wizara ya TAMISEMI ilishasomwa, hospitali hii bado hatujaletewa pesa. Je, Serikali iko tayari sasa basi kupeleka hizi pesa ambazo iliahidi na wananchi walisikia kwamba zitapelekwa katika Halmashauri ya Itigi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge na nimpe pole sana kwamba, alipata ajali mbaya hivi karibuni, lakini pamoja na kwamba, alikuwa na machungu ya maumivu aliweza kuwakumbuka wananchi wake wa Manyoni na akaanza kuandika swali hili ambalo nalijibu hapa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijibu maswali ya nyongeza mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, sisi Serikali tunahimiza wananchi na wenyewe Waheshimiwa Wabunge wamekuwa mstari wa mbele kuwahamasisha wananchi kushiriki kujenga vituo vya afya na zahanati na kuna maboma mengi.

Naomba nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, jitihada na nia ya Serikali iko palepale, kadri ambavyo uwezo utapatikana tutapeleka fedha za maboma, lakini pia kupeleka wataalam na vifaa tiba ili kuweza kuboresha huduma za wananchi wetu katika maeneo yao na hii itakuwa ni kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, anauliza habari za hospitali yake ya Itigi; naomba nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaendelea kuliangalia hili kulingana na uwezo wa Serikali. Kama mwaka huu bajeti hii haikupelekwa katika eneo lake la Hospitali ya Itigi kama alivyotaja Mheshimiwa Mbunge, basi tunalichukua kulifanyia kazi ili wakati ujao aweze kupata fedha na kuweza kupata huduma na kuboresha hospitali yake ya wilaya.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa swali la nyongeza.

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Nitangulize kutoa shukrani za wananchi wa Bagamoyo kwa juhudini kubwa ya Serikali katika kuboresha huduma ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Bagamoyo kwa muda mrefu sana wamehanganya na ujenzi wa zahanati katika Vijiji viwili, kimoja cha Buma Kata ya Kilomo, kingine Kitame katika Kata ya Makurunge. Hivi sasa zahanati ya Makurunge imekamilika na Buma wakati wowote tutamaliza, tunamalizia ujenzi wa choo. Swali langu kwa Mheshimiwa Waziri, je, ni lini tutaweza kupatiwa watumishi na vifaa tiba katika zahanati hizi kwa kuzingatia kwamba, kwa muda mrefu wananchi hawa hawajapata huduma?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nijibu swali la Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshaomba kibali maalum kwenye Ofisi, Wizara ya Utumishi cha kuajiri Madaktari, Waganga na Wauguzi. Naomba nimwahidi

Mheshimiwa Mbunge kwamba, maeneo yote ambayo zahanati zimekamilika na vituo vya afya ambavyo vinajengwa nchi nzima na hospitali za wilaya na pale palipo na upungufu mkubwa tutazingatia maeneo hayo ikiwepo na eneo lake la Bagamoyo na zahanati mbili ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Venance Mwamoto, swali la nyongeza.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, Wilaya ya Kilolo inapitiwa na barabara kuu (*High Way*) kutoka Tanzania kwenda Zambia, lakini pia ni barabara ambayo ukitoka Mikumi ni mpakani na Ruaha Mbuyuni mpaka ukifika llula ni kilometra zaidi ya 200, lakini hapo hakuna kituo cha afya. Mara nyngi *accidents* zimekuwa zikitokea, wananchi wa Mbeya, Malawi, Zambia, wamekuwa wakipata matatizo na wamepoteza maisha kwa sababu, inabidi waende wakatibiwe Iringa Mjini ambako ni mbali; na kwa kuwa, wananchi sasa wa Ruaha Mbuyuni wameonesha nia ya kujenga Kituo cha Afya, je, Serikali itakuwa tayari kuwasaidia kwa haraka ili kuokoa maisha ya watu ambao wamekuwa wakiyapoteza pale?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge Venance Mwamoto, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwa swali mojawapo la nyongeza hapa, hivi leo asubuhi kwamba, ni nia ya Serikali kuendelea kuboresha huduma za afya na

maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja yatazingatiwa katika kuboresha. Kama wananchi wamechukua juhudzi za kuanza ujenzi tunawapongeza sana, sisi kama Serikali tuko pamoja nao na mimi hivi karibuni nitaenda kutembelea Jimbo la Mheshimiwa Mwamoto. Hivyo nitaomba tutembelee eneo hili tuone juhudi za wananchi ili tuweze kutia nguvu katika eneo hilo. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Paschal Haonga, swali la nyongeza.

MHE. PASCHAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Mji Mdogo wa Mlowo ulioko Wilaya ya Mbozi una wakazi wapatao elfu 70 na zaidi, lakini bahati mbaya sana mji huu una zahanati tu ambayo inahudumia watu hao zaidi ya 70,000.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kujenga kituo cha afya ili kuweza kuwahudumia wale wananchi ambao ni wengi na wanapata tabu sana na wanasumbuka wakati wa kupata matibabu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mwalimu Paschal Haonga, Mbunge wa Mbozi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeanza kujenga vituo vya afya awamu ya kwanza bajeti hii ya 2019/2020 awamu ya pili, naomba nimwahidi Mheshimiwa Mbunge awamu ya tatu tutazingatia maeneo yote ambayo hayajapata huduma hii, likiwepo Jimbo lake la Mbozi na hasa eneo mahususi ambalo amelitaja hapa asubuhi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Saul Amon.

MHE. SAUL H. AMON: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

Kwanza nishukuru Serikali kwa kuboresha Vituo vya Afya vya Masukulu na lkuti, hapo nashukuru sana, kwani sasa hivi vinaonekana kama hospitali, lakini wananchi wa Kata ya Mpuguso na Kata ya Isongole kwa nguvu zao wamejenga vituo vya afya kufikia hatua ya maboma, wengine mpaka kumalizia kwenye *ceiling board*.

Je, Serikali ina mpango gani wa kumalizia hivi vituo vya afya kwa hao watu wanaotoka mbali sana ili viweze kwisha kwa haraka na waweze kuvitumia? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba nijibu swali la Mheshimiwa Amon la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshaanza kutekeleza kuunga mkono juhudzi za wananchi ambapo wameongeza nguvu zao. Tumeshaeleka fedha katika kumalizia maboma ya shule za sekondari, tupo kwenye mchakato wa kupeleka maboma kumalizia maboma ya shule za msingi; awamu ya tatu ni maboma ya zahanati na vituo vya afya na maweneo ambayo tutazingatia ni maeneo ambayo wananchi wameshaonesha juhudzi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba mchakato huu ukikamilika aneo lake pia, ambalo amelitaja tutalizingatia sana. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Geita, sasa aulize swali lake.

Na. 197

Hitaji la Gati – Izumacheli Geita

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA aliuliza:-

Meli ya *MV Chato* inafanya safari zake kati ya Chato, Senga, Mshalamba, Izumacheli na Nkome. Inapofika Izumacheli huegesha kwenye jiwe kutokana na kukosekana kwa gati:-

Je, ni lini Serikali itajenga Gati katika Kijiji cha Izumacheli?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ENG. ATASHATA J. NDITIYE):** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Geita Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Tano ina mkakati wa kuhakikisha kuwa huduma za usafiri zimeboreshwa katika maeneo yote nchini, huku kipaumbele kikiwekwa kwenye maeneo yenye mahitaji maalum na pia maeneo yenye kuchochea kwa haraka shughuli za kiuchumi. Kwa kutambua hilo Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (*TPA*) pamoja na *TEMESA* imeandaa programu ya namna bora ya uboreshaji wa huduma za usafiri katika Ziwa Viktoria (*Lake Victoria Modernisation Programme*) kwa lengo la kubaini maeneo yote yanyohitaji ujenzi wa ama bandari au gati.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mpango huu unaendelea ambapo ujenzi wa gati, maghala ya kuhifadhi mizigo na majengo ya abiria katika Bandari za Magarini

ambayo iko Muleba na Nyamirembe ambayo iko Chato, Mwigobero ambayo iko Musoma na Lushamba ambayo iko Geita unaendelea. Naomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Izumacheli Mkoani Geita kuwa, Serikali inatekeleza mpango wake kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha hivyo, Serikali itatoa kipaumbele kwa eneo hili awamu zinazofuata, ili kuruhusu kukamilika kwanza kwa miradi iliyokwishaanza katika Ziwa Victoria.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, Kata ya Izumacheli inaundwa na Vijiji vitatu, Kijiji cha Izumacheli, Kijiji cha Butwa na Kijiji cha Runazi na ina takriban wakazi kama elfu 40 wako katikati ya ziwa. Tunaishukuru pia Serikali ilituletea meli ya *MV Chato* ambayo inapita pale mara mbili kwa wiki. Swali langu, meli hii haina sehemu ya kupaki, inapaki juu ya jiwe, kitendo ambacho ni hatari sana kwa maisha ya Wananchi wa Izumacheli.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri ni nini kauli ya Serikali kulichukulia hili suala *serious*, ili kuwaepusha wananchi wale wasipate matatizo katika maisha yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa, wananchi hawa tumewaahidi sana zaidi ya mara tatu sasa kwamba, daraja litatengenezwa, gati itatengenezwa na Mheshimiwa Naibu Waziri na Serikali imeonesha nia ya kuweza kuwasaidia wananchi hawa. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari sasa baada ya Bunge hili kwenda kujonea sehemu ambayo meli inaendelea kupaki kupakia abiria mpaka sasa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHATA J. NDITIYE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Joseph Musukuma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Musukuma kwa jitihada kubwa mbalimbali anazozifanya katika kuwatetea na kuwapigania wananchi wa Jimbo la Geita Vijiji ambako yeye ni Mbunge mahiri. Sasa naomba nijibu maswali yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ni kweli kwamba, tumekwishaanza mchakato karibu miaka miwili iliyopita ambapo upembuzi yakinifu umefanyika na usanifu wa kina umeshafanyika kwa ajili ya kujenga gati eneo la Izumacheli, lakini pia tumeshatoa shilingi milioni 200 kwa ajili ya hatua za mwanzo za kuanza ujenzi wa gati hiyo. Kwenye bajeti ya mwaka huu kama Mheshimiwa atapigana ipitishwe tunategemea kutenga pesa nyingine zaidi kwa ajili sasa ya kuendelea kwa kasi kubwa sana ili wananchi wa Izumacheli na maeneo ya Butwa, llsasi na vijiji vinavyozunguka waweze kupata huduma ya kivuko.

Mheshimia Naibu Spika, swalii la pili, mimi niko tayari baada ya kipindi hiki cha Bunge kwenda na Mheshimiwa Musukuma kutembelea maeneo ambayo yana changamoto ya usafiri.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joseph Mkundi, swalii la nyongeza.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Baada ya ajali ya Kivuko cha *MV Nyerere* tarehe 20 Septemba, mwaka jana pale Ukala, Serikali iliahidi kutengeneza kivuko kipyaa kwa ajili ya kusaidia wananchi eneo lile. Hivi sasa kuna kivuko cha muda cha *MV Sabasaba* ambacho kimekuwa na changamoto nyingi sana. Nataka kujua kutoka Wizara, ni hatua ipi imefikiwa ya ujenzi wa kivuko kipyaa kitakachofanya kazi kati ya Bugolora na Ukara? Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHATA J. NDITIYE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ile ajali Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari imeshatangaza tenda na Mkandarasi amepatikana na mkataba umeshasainiwa na sasa hivi tunaendelea kununua *engine* haraka ili kitakapokamiliika kifungwe, lakini pamoja na Kivuko cha Nyamisati, Mafia.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Dau, swali la nyongeza.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kivuko cha Nyamisati, Kilindoni mpaka leo bado hakijakamiliika. Ningependa kusikia kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri ni lini kivuko hiki kitakamiliika? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHATA J. NDITIYE): Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimetoka kumwambia Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Ukerewe ni kwamba hivi vivuko viwili manunuvi yamekamiliika na sasa hivi mkandarasi ameanza kazi na tunanunua *engine* haraka ili baada ya matengenezo sasa vivuko hivyo vianze kufanya kazi. Tulikuwa hatuna kivuko ambacho kilikuwa kinaenda Nyamisati na Mafia, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge pamoja na wapiga kura wake ni kwamba, Serikali imeshachukua hatua, tunajenga kivuko kipyaa ambacho kita-*operate* kati ya Nyamisati na Mafia.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kwa niaba yake aulize Mheshimiwa Abdallah Chikota.

Na. 198

Ujenzi wa Reli ya Mtwara – Mbambabay

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA (K.n.y. MHE. HAWA A. GHASIA) aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa reli kutoka Mtwara – Mbambabay na matawi yake ya Liganga na Mchuchuma utaanza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHATA J. NDITIYE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali (*feasibility and preliminary design*) wa ujenzi wa reli kutoka Mtwara – Mbambabay kuititia matawi ya Mchuchuma-Liganga zenyet urefu wa kilometra 1,092. Mshauri Mwelekezi wa kifedha na uwekezaji (*transaction advisor*) tayari amepatikana, mkataba na mshauri wa uwekezaji unatarajiwa kusainiwa ifikapo Juni, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mshauri wa Uwekezaji atakuwa na jukumu la kuunadi mradi huu kwa wawekezaji mbalimbali, ikizingatiwa kuwa mradi huu unatekelezwa kwa utaratibu wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (*PPP*). Hii ni katika kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika ujenzi wa reli nchini kwetu. Hivyo, baada ya kukamilika kwa

utaratibu wa kumpata mwekezaji kwa njia ya *PPP*, ujenzi wa reli hii utaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa hata sasa tumekuwa tukipokea wawekezaji wanaotaka kuwekeza katika reli hii ambapo tumekuwa tukiwaelekeza kufuata sheria na taratibu za ununuzi kwa miradi inayotekelawa kwa mfumo wa *PPP*. Taratibu hizo zinawaelekeza kuandaa na kuwasilisha wazo lao (*proposal*) la kufanya uwekezaji kwa Shirika la Reli Tanzania (*TRC*) ambalo litawasilishwa katika Wizara yetu baada ya kuwa wamejiridhisha. Aidha, baada ya kuchambuliwa kwa kina na Wizara, litawasilishwa katika kitengo cha *PPP* kilichopo Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uchambuzi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Fedha na Mipango kupitia kitengo hicho, wakimaliza uchambuzi na kuridhia, mwekezaji atatakiwa naye kufanya upembuzi yakinifu wake ambao baadaye utalinganishwa na upembuzi yakinifu uliofanywa na Serikali kabla ya kukamilisha taratibu za uwekezaji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Abdallah Chikota, swalı la nyongeza.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swalı la kwanza, ujenzi huu wa reli utakuwa na maana sana endapo upanuzi wa Bandari yetu ya Mtwara utakuwa umekamilika. Kwa sasa hivi mpango ulikuwa ni kujenga gati tatu lakini kinachoendelea sasa hivi Bandari ya Mtwara ni ujenzi wa gati moja tu. Je, hizo gati mbili zilizobaki ujenzi wake utaanza lini? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalı la pili, ili reli hii itumike vizuri, tunatarajia hata Mkoa wa Lindi utumie vizuri Bandari

ya Mtwara lakini barabara ya kutoka Mtwara hadi Mnazi Mmoja imejengwa miaka 50 iliyopita. Je, Serikali ina mpango gani wa ujenzi mpya siyo ukarabati wa kuweka viraka viraka kutoka Mtwara hadi Mnazi Mmoja?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHATA J. NDITIYE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abdallah Chikota, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tunashukuru kwa pongezi alizotupatia kutokana na jitihada mbalimbali ambazo Serikali inafanya kuhusu ujenzi wa reli kutoka Mtwara mpaka Mbambabay. Tunajua kwamba ili ujenzi wa reli hiyo uwe na tija, ni lazima tuanzie Mtwara kwenye bandari yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba sasa hivi tumekwishaanza utekelezaji wa upanuzi wa Bandari ya Mtwara kwa awamu ya kwanza na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea na awamu ya pili na ya awamu ya tatu mpaka tutakapokamilisha upanuzi wa Bandari yetu ya Mtwara ili iwe ya kisasa kuweza kuhudumia mzigo mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalı lake la pili anataka kujua kuhusu upanuzi wa barabara ya Mtwara mpaka Mnazi Mmoja. Jibu lake ni kwamba mpaka sasa hivi tayari taratibu zote za kuanza ukarabati mkubwa wa barabara hiyo zimeshakamilika na tumekwishatangaza tenda hivi karibuni mkandarasi ataingia kazini kwa ajili ya kurekebisha barabara hiyo. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Oran Njeza, swalı la nyongeza.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

Na mimi napenda kujua pamoja na ujenzi wa hii reli ya Mtwara -Mbambabay, Serikali ina mkakati gani wa kujenga reli kati ya Inyala (Mbeya) na Kyela kwenye Ziwa Nyasa ambayo itakuwa ni kiungo kizuri kuunganisha reli ya *TAZARA* pamoja na Bandari yetu ya Mtwara? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijiini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, reli ya *TAZARA* ilijengwa kwenye miaka ya 1975. Sasa hivi Serikali ya Tanzania na Zambia tunafanya ukarabati mkubwa pamoja na kuongeza vichwa na mabehewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Ziwa Nyasa tumejenga matishari matatu ambayo tayari yanabebe mzigo. Hata hivyo, baada ya kukamilisha ukarabati huu na kuimarisha ili reli ile iweze kubeba mzigo uliotarajwa wa tani milioni 5 kwa mwaka, basi tutaanza na stadi kwa ajili ya kuunganisha hicho kipande cha kutoka Mbeya kuelekea kule Kyela. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Justin Monko, swali la nyongeza.

MHE. JUSTIN J. MONKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naipongeza sana Serikali kwa juhudhi kubwa ambayo inafanya kwenye ujenzi wa reli mbalimbali ikiwepo ya *standard gauge*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kipande cha reli kutoka Manyoni kwenda Singida ambacho ni muhimu sana kwa uchumi wa wananchi wa Mkoa wa Singida. Je, Serikali ina mkakati gani wa kufufua kipande hiki ambacho hakijafanya kazi kwa muda mrefu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali ilijenga kipande cha reli hii ya katika kuelekea Singida lakini baada ya ukarabati mkubwa wa barabara ya kutoka Dodoma kwenda Singida hapo katikati mizigo milungi imekuwa inatumia barabara. Suala hili tumeshaanza kulifanyia kazi ili tuweze kuona ni namna gani tunaweza tukakarabati hiyo reli na kushawishi sasa wabeba mizigo ikiwepo ni pamoja na kuweka taratibu na sheria ndogo ndogo ili wengi watumie reli badala ya barabara. Kwa sasa suala hili Serikali inalifanyia kazi. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Qulwi Qambalo, swali la nyongeza.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pia kumekuwa na mpango wa kujenga reli itakayopita Kaskazini mwa nchi itakayounganisha Miji ya Tanga, Moshi, Arusha hadi Musoma. Je, mpango huo umefikia hatua gani? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali moja dogo la Mheshimiwa Mbunge Qambalo lakini kikubwa nimwombe leo

tunawasilisha bajeti, asiwalishe shughuli, taarifa zote atazipata kwenye kitabu cha bajeti.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, watu wote wenye reli kwao kila Mbunge amesimama hapa, kwa hiyo, itabidi tu uwasilikilize wote halafu uone namna ya kusema hicho unachotaka kusema baadaye. Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, swali la nyongeza.

MHE. DANIEL N. NSANZUKWANKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya matawi ya reli ya *SGR* ni kujenga reli kutoka Uvinza – Kasulu - Msongati nchini Burundi. Je, mchakato wa kuanza upembuzi yakinifu umefikia hatua gani?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, niomba kujibu swali moja dogo la Mheshimiwa Mbunge Nsanzugwanko ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati yangu ya Miundombinu na ye ye pia najua anafahamu, kwa hiyo, tutoe muda kidogo, ni dakika chache zimebaki ili nitoe hotuba ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano halafu mambo mengine yatafuata, tusiwalishe shughuli, dakika bado ni chache. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa majibu haya ya Mheshimiwa Waziri bado mnataka kuuliza maswali? Waziri watazame kidogo huko, kuna Mheshimiwa Getere kwake nadhani kuna reli, kuna Mbunge wa Ulanga Mheshimiwa Goodluck; nadhani Waheshimiwa Wabunge tusubiri bajeti ya Mheshimiwa Waziri, anasema majibu yetu yote yapo mle, kwa hivyo, tutapata fursa ya kuchangia kwenye eneo hilo.

Tumalizie na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Othman Omar Haji, Mbunge wa Gando, sasa aulize swali lake.

Na. 199

Kodi ya Pango ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu

MHE. OTHMAN OMAR HAJI aliuliza:-

Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu (*ACPHR*) inatumia jengo la *TANAPA* liliopo Arusha kwa mkataba wa upangaji baina ya *TANAPA* na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ulioanza tarehe 1 Desemba, 2008 kwa kodi ya dola za Marekani 38,998.89 kwa mwezi:-

Je, kati ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu ni nani mwenye jukumu la haki za binadamu na nani mwenye jukumu la kulipa kodi ya jengo hilo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Othman Omar Haji, Mbunge wa Gando, kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo mwaka 2007, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Umoja wa Afrika Mashariki ziliingia Mkataba wa Uenyeji (*Host Agreement*) wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Katika mkataba huo, Wizara ya Mambo ya Nje na

Ushirikiano ndiyo msimamizi na mtekelezaji mkuu wa mkataba huo kwa niaba ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 5(1) ya mkataba kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Umoja wa Afrika Kuhusu Uenyeji wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, inaeleza kuwa Tanzania kwa gharama zake inawajibika kutoa majengo kwa ajili ya ofisi ya mahakama na makazi ya Rais na Msajili wa Mahakama hiyo. Aidha, Ibara ya 5(2) inaipa Tanzania jukumu la kutoa ofisi ya muda kwa ajili ya mahakama husika wakati ikiendelea na taratibu za kupata jengo la kudumu la mahakama. Kutokana na kipengele hicho Serikali iliingia mkataba na TANAPA wa kukodisha majengo yale ili kuwa ofisi ya muda ya Mahakama ya Haki za Binadamu na Watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelezo hayo, ni dhahiri kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuititia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ndiyo yenye jukumu la kulipa kodi hiyo kutokana na makubaliano yaliyofikiwa. Hata hivyo, suala la kulinda haki za binadamu ni suala la kila mtu na kila taasisi sehemu yoyote duniani. Kimsingi, hata Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inahusika moja kwa moja katika kulinda haki za binadamu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Othman Haji, swali la nyongeza.

MHE. OTHMAN OMAR HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, hadi natuma swali hili Mei 8, 2017, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ilikuwa inadaiwa na TANAPA zaidi ya shilingi bilioni 3 za Tanzania. Je, deni hili limeshalipwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Wizara kuititia Shirika lake la A/CC inamiliki majengo ya kutosha pale Mjini

Arusha ambapo ingetumia majengo yale ingeweza mahakama hii kufanya shughuli zake kwa ufanisi mkubwa sana. Je, Mheshimiwa Waziri haoni upo umuhimu kuhamisha mahakama hii huko inakokodi na kuipeleka katika majengo haya ya A/CC ili kuokoa matumizi yasiyokuwa ya lazima? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Othman Haji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba *TANAPA* inadai fedha ya pango kwa ajili ya ofisi za Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu lakini taratibu zinaendelea ili ziweze kulipwa. Hata hivyo, naomba nimueleweshe Mheshimiwa Mbunge kwamba siyo mahakama ndiyo inadai Serikali bali ni Serikali na Serikali. Kwa hiyo, ni suala la kawaida, pesa hiyo italipwa muda ukifika na kama nilivoyesema mchakato unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la pili kwamba kwa nini majengo ya A/CC yasitumike kama ofisi za mahakama hiyo. Naomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Serikali imetafuta hekari 20 Arusha kwa ajili ya kujenga ofisi za mahakama hiyo na taratibu za ujenzi zimefika mbali sana. Kwa hiyo, tunategemea baada ya muda mfupi ofisi hizo zitajengwa na hakutakuwa na haja ya kwenda kubanana kwenye Ofisi ya A/CC. Hata kama mahakama hiyo ingeenda kwenye majengo ya A/CC labda suala lile lile la kudaiwa na *TANAPA* lingeweza kujirudia. Kwa hiyo, tunachotaka kufanya ni kujenga ofisi ambazo zitatosha na changamoto hii haitatokea tena.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Abdallah Mt Olea, swali la nyongeza.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili la wanadiplomasia kutolipa kodi za pango halipo tu Arusha lakini pia lipo kwenye baadhi ya Balozi. Kwa mfano, Ubalozi wa Palestina nchini umepanga katika jengo linalomilikiwa na Halmashauri ya Temeke toka mwaka 2003 na mpaka leo hawajawahi kulipa kodi hata shilingi moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri imejaribu kufuata hatua mbalimbali za kudai ikiwa ni pamoja na kuripoti ofisi ya Wizara ya Mambo ya Nje lakini hakuna lolote lililofanyika. Tunahofia kuwaondoa kinguvu kwa sababu ya kulinda hiyo *image* ya ushirikiano wetu. Je, Mheshimiwa Waziri upo tayari leo kuwapa *notice* Ubalozi wa Palestina kwamba ndani ya miezi mitatu kuanzia leo wahame katika jengo hilo huku Halmashauri ikiendelea na taratibu nyongeza za kudai deni lao? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mtolea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kuna utaratibu wa kidiplomasia wa kudaiana kati ya Serikali na Serikali na kwa vyovypote haiwezi ikawa kwa kupitia matamko ya Bungeni. Kwa hiyo, naomba tu nimuhidi Mheshimiwa Mbunge kwamba hili suala linafanyiwa kazi. Madeni yapo kila mahali, ni kawaida, awe na subira, nina hakika Serikali italifanyia kazi na changamoto hii itaondoka. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Wizara ya Mambo ya Nje imekuwa na madeni

mengi hasa kwenye Balozi za nje ambazo Mabalozi wetu wanaishi na ni tabia ambayo inatuletea *image* mbaya kama taifa. Je, ni lini Serikali italipa hayo madeni ya pango za nyumba za Mabalozi wetu katika nchi mbalimbali za dunia hii tuliyopo sasa? (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Mwakagenda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili katika bajeti zake za miaka ya hivi karibuni limekuwa likitenga fedha mara kwa mara kwa ajili ya kulipa madeni hayo. Kwa hiyo, naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli madeni yapo na kila wakati madeni ni sehemu ya maisha lakini Serikali itaendelea kulipa kadiri uwezo unavyopatikana. Hata hivyo, mkakati mkubwa wa Serikali sasa ni kuzuia madeni mengine kutokea kwa kulipa madeni kwa wakati. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba suala hili litafanyiwa kazi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa John John Mnyika, swal la nyongeza.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Katika swal hili Serikali imeeleza inalipa Dola za Marekani 38,000 kwa mwezi ambazo ukipiga kwa mwaka ni takribani shilingi bilioni 1 na Serikali imeanza kulipa kuanzia 2008, kwa hiyo, ni takribani shilingi bilioni 9 kama *all facts are being equal* zimelipwa. Wizara hii ina *experience* kwenye ujenzi wa hosteli za chuo kikuu pale walisema *block* moja iligharimu shilingi milioni 500, ukigawanya kwa wastani wa hizo shilingi bilioni 9 kwa kipindi hiki kungeweza kujengwa maghorofa kati ya 18 mpaka 20. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali kama hii, ni kwa nini Serikali imeachia hali ikae muda mrefu na ni lini hasa ujenzi

huu utafanyika ili pesa zisiendelee kutumika kwa kiwango kikubwa namna hii kwenye kulipa kodi? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba gharama hizo ni kubwa, hata hivyo, ujenzi wa majengo ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni suala la kimkataba na wala haliamuliwi na Serikali peke yake, inabidi kukaa kukubaliana, michoro. Kwa hiyo, ni suala ambalo sio sisi wenyewe, ingekuwa ni kawaida kwamba ni la kwetu tungeshajenga lakini kama nilivyolarifu Bunge lako Tukufu, tayari hatua za ujenzi zimefika mbali. Tumeshapata eka 20, michoro tayari, kwa hiyo muda wowote jengo hilo litajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba avute subira sanasana ucheleweshwaji umetokea kwa sababu majadiliano yanaendelea kuhusu namna gani jengo hilo lijengwe kwa sababu sio letu peke yetu lazima tuongee na Mahakama ya Afrika pamoja na Umoja wa Afrika.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali. Na kabla sijaleta matangazo, kuna jambo moja ambalo limejitokeza katika upande wa majibu ya Serikali, na nimuombe Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, kuangalia namna bora ya upande wa Serikali kuwahusisha Wabunge katika yale mambo yanayohusu maamuzi ya majimbo yao. Kwa sababu wakati mwingine Wabunge wanauliza maswali wakiwa hawana taarifa kwamba Serikali imeshafanya jambo kwenye maeneo yao, kwa hiyo, kidogo inaleta sintofahamu hivi. (*Makofi*)

Kwa mfano, Mbunge akiuliza kuhusu kivuko halafu kumbe mkataba umeshaingiwa na kazi imeshaanza maana yake ye ye hajui lakini Serikali imeshachukua hatua, jambo ambalo ni jema, lakini Mbunge akifahamu basi inamsaidia pia kuwajulisha wananchi wake kwamba Serikali imeshachukua hatua na sasa iko kwenye utekelezaji wa jambo ambalo iliahidi. (*Makofi*)

Yale mambo mengine sawa Serikali inaweza kuendelea kwa upande wake lakini yale ambayo Wabunge wanayasemea sana ni vizuri kuwasiliana pia na Wabunge ili Wabunge wasiulize maswali ambayo Serikali tayari imeshachukua hatua.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu leo hayupo amekwenda kushiriki maziko ya mmoja wa watu muhimu sana ambao tumewapoteza kama Taifa, na kwa niaba yake humu Bungeni Kiongozi wetu wa Shughuli za Serikali atakua Mheshimiwa Prof. Mbarawa. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge nilete matangazo tuliyonayo. (*Makof*)

Ahsante sana, naona Mheshimiwa Mbarawa atakuwa amefurahi sana leo. Waheshimiwa Wabunge, nilete kwenu matangazo ya wageni tulionao siku ya leo hapa Bungeni; tutaanza na wageni 44 wa Mheshimiwa Mhandisi Isack Kamwelwe ambaye ni Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambao ni viongozi wa Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo.

Tunaanza na..., sasa hivi vifupisho vimeandikwa Kiingereza – Arch. Elius Mwakalinga ambaye ni Katibu Mkuu Ujenzi, tunaye pia Dkt. Leonard Chamuriho ambaye ni Katibu Mkuu Uchukuzi, tunaye pia Dkt. Mary Sasabo ambaye ni Katibu Mkuu Mawasiliano; tunaye pia Dkt. Jim Yonaz ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Mawasiliano; tunaye Prof. Ninatubu Lema ambaye ni Mwenyekiti Bodi ya Wasajili wa Wahandisi; tunaye pia Dkt. Damas Nyaoro ambaye ni Mwenyekiti Bodi ya Wakala wa Barabara nchini (*TANROADS*). (*Makof*)

Tunaye ndg. Joseph Haule ambaye ni Mwenyekiti Bodi ya Mfuko wa Barabara; yupo pia Ndugu Consolata Ngimbwa ambaye ni Mwenyekiti Bodi ya Wasajili ya Wakandarasi; tunaye pia Arch. Ludigija Bulamila ambaye ni Mwenyekiti Bodi ya Usajili wa Wasanifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi. (*Makof*)

Tunaye pia *Engineer Emmanuel Korosso* ambaye ni Mwenyekiti Bodi ya Kampuni ya Ndege Tanzania (*ATCL*); tunaye pia *Captain Ernest Bupamba* ambaye ni Mwenyekiti Bodi ya Chuo cha Bahari Dar es Salaam (*DMI*); tunaye *Balozi Hassan Kibellor* ambaye ni Mwenyekiti Bodi ya Kampuni ya Maendeleo ya Kiwanja cha Ndege Kilimanjaro (*KADKO*). (*Makofi*)

Tunaye Profesa *Blasius Nyichomba* ambaye ni Mwenyekiti Bodi ya Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (*NIT*); tunaye *Ndugu Mbwana Juma* ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Usimamizi wa Anga Tanzania (*TCAA*); tunaye *Ndugu Michael Ntagazwa* ambaye ni Mwenyekiti Bodi ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (*TMA*). (*Makofi*)

Tunaye Profesa *Ignas Rubaratuka* ambaye ni Mwenyekiti Bodi ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (*TPA*); tunaye Profesa *John Kondoro* ambaye ni Mwenyekiti Bodi ya Shirika la Reli Tanzania (*TRC*); tunaye Profesa *Tadeo Satta* ambaye ni Mwenyekiti Bodi ya Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (*TASAC*); tunaye *Ndugu Omary Nundu* ambaye ni Mwenyekiti Bodi ya Shirika la Simu Tanzania (*TTCL*). (*Makofi*)

Tunaye Dkt. *Jones Kilimbe* ambaye ni Mwenyekiti Bodi ya *TCRA*; tunaye Dkt. *Joseph Kilongola* ambaye ni Mwenyekiti Bodi ya *UCSAF*; tunaye *Luteni Kanali Mstaafu Dkt. Harun Kondo* ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Posta; tunaye pia *Ndugu Luckson Kataraiya* ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya *TCRA – CCC*. (*Makofi*)

Tunaye *Ndugu Fabio Di-Stefano* ambaye ni Mwakilishi wa *European Union* ambaye ni *Mkuu wa Idara ya Miundombinu na Ushirikiano wa Kikanda*; tunaye pia *Ndugu Ally Mwinchande* ambaye ni mwakilishi wa *European Union* na yeje ni *Meneja wa Miradi ya Miundombinu*. (*Makofi*)

Tunaye pia *Eng. Patrick Mfugale* ambaye ni *Mtendaji Mkuu TANROADS*; tunaye pia *Arch. Daudi Kondoro* ambaye ni *Mtendaji Mkuu TBA*; tunaye pia *Ndugu Eliud Nyauhenga*

ambaye ni Meneja wa Mfuko wa Barabara (*RFB*); tunaye *Engineer* Julius Ndyamkama ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji Mamlaka ya Usimamizi wa Viwanja vya Ndege Tanzania (*TAA*). (*Makofii*)

Tunaye ndg. Masanja Kadogosa ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji *TRC*; tunaye pia *Engineer* Deusdeddit Kakoko ambaye ni Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (*TPA*); tunaye *Engineer* Peter Ulanga ambaye ni Mtendaji Mkuu Mfuko wa Fursa kwa Wote (*UCSAF*); tunaye pia Ndugu James Kilaba ambaye ni Mkurugenzi Mkuu *TCRA*; tunaye pia ndg. Waziri Kindamba ambaye ni Mkurugenzi Mkuu *TTCL*. (*Makofii*)

Karibuni sana wageni wote wa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano hapa Bungeni.

Tunao pia wageni wengine wa Mheshimiwa *Engineer* Kamwelwe ambao ni wanafunzi 23 kutoka Chuo cha Taifa cha Usafirishajji (*NIT*) wakiongozwa na Mshauri wa Wanafunzi ndg. Abel Luzibila; karibuni sana. (*Makofii*)

Pia wapo jamaa zake ambao ni ndg. Privatus Kamwelwe na Ndugu John Ikowelo; karibuni sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge na kundi la kwanza ni wageni 65 wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa ambaye ni Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na hawa ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu Joseph Shilole; karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni tisa wa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambao ni Makatibu wa CCM kutoka Kata ya Kilolo, nadhani ni Jimbo la Kilolo, kutoka Mkoa wa Iringa wakiongozwa na Katibu wa CCM Wilaya Ndugu Clement Mponzi; karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni saba wa Mheshimiwa Sonia Magogo ambao ni familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam

wakiongozwa na baba yake mzazi Ndugu Jumaa Magogo; karibuni sana na tunafurahi kumuona baba yetu amekaa hapo juu. (*Makofii*)

Tunao pia wageni saba wa Mheshimiwa Jitu Soni Patel ambaa ni Jumuia ya Maliasili Tanzania kutoka Babati, Mkoa wa Manyara wakiongozwa na ndg. Marcel Yeno; karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Risala Kabongo ambaa ni jamaa zake kutoka Mkoa wa Arusha wakiongozwa na kaka yake, Ndugu Mohamed Kabongo; karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni 40 wa Mheshimiwa George Simbachawene ambaa ni wanafunzi 37 na walimu watatu kutoka Shule ya Sekondari *Mtera Dam* iliyopo Mtera Mkoa wa Dodoma ambaa wamelitembelea Bunge kujifunza jinsi linavyofanya kazi; karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Aisharose Matembe ambaa ni jamaa zake kutoka Dodoma wakiongozwa na Ndugu Yagi Kiaratu; karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wanafunzi 87 na walimu sita na madereva watatu kutoka Shule ya Sekondari Amani iliyopo Wilayani Manyoni, Mkoa wa Singida ambaa wamelitembelea Bunge kujifunza jinsi linavyofanya kazi zake; karibuni sana vijana kutoka Manyoni. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, haya ndio matangazo ya wageni lakini ninalo tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, anawatangazia Wabunge wanawake wote kuwa leo, tarehe 09 Mei, 2019 kutakuwa na kikao kwa ajili ya Wabunge wote wanawake, kikao hicho kitafanyika *Morena Hotel*mara tu baada ya kuahirishwa kikao cha Bunge saa saba mchana. Kwa hiyo, Wabunge wote wanawake mnaombwa muelekee Morena baada ya

kuhitimisha shughuli za Bunge kwa sehemu hii ya asubuhi.
(*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa ntamuita Mheshimiwa Zungu ambaye atakuja kuendelea na ratiba iliyopo mbele yetu.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mwongozo wa Spika.

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mwongozo wa Spika.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mwongozo.

MWENYEKITI: Jamani, si mnganje nikae basi, eeh.

MBUNGE FULANI: Ulishakaa Mheshimiwa.

MWENYEKITI: Hapa hukai hivi hivi mpaka ukae kwa maandalizi. Haya mwongozo, nani kaanza? Mheshimiwa Musukuma, Mheshimiwa Mchungaji Msigwa.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 06, Siku ya Jumatatu, nilikuwa nimeomba hoja ya dharura juu ya Ndugu Mdude ambaye alikuwa ametekwa na kupotea, na Kiti kililiagiza Serikali itoe taarifa na Serikali iliahidi kwamba ingetoa *development* za tukio hilo, na Serikali kwa bahati mbaya haijaleta. Lakini kwa taarifa nilizonazo ni kwamba yule bwana amepatikana maeneo ya Inyala kule Mbeya lakini hali yake sio nzuri na sasa hivi yuko hospitali ya rufaa anatibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba yetu, Serikali ina wajibu wa kulinda raia na mali zake. Sasa ninataka kujua kama Serikali itachukua hatua zozote za kushughulika

na matibabu yake wakati ikiendelea na uchunguzi wa tatizo hilo, ninaomba Kiti chako kitoe maelekezo na mwongozo ili Serikali iwajibike katika kulinda raia na mali zao, na ye ye ana hali mbaya sana sasa hivi huko hospitali ya rufaa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Musukuma!

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo yanaendelea humu Bungeni, nimeona niombe mwongozo wako; ukiangalia Wabunge karibia wote sasa hivi wana-*chat*, kila mtu yuko kwenye simu. Na mfano mzuri simu ya Mheshimiwa Mwakajoka pale anarekodi, sasa ninaomba huu utaratibu sio wa Kibunge, utaratibu wa Kibunge tuna *Hansard*, tuna vitu vingi ambavyo tunaweza kuwa na kumbukumbu. Na ninyi Waheshimiwa Wabunge mtakuwa mashahidi sasa kumekuwa na tabia watu wanarekodi wanatuma kwenye majimbo ya wenzao wanassema Mbunge wenu hajui kuongea, Mbunge wenu hafanyi hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba mwongozo wako; kwa nini Wabunge tusiziache simu nje ama jengo hili liwe na utaratibu wa kukatwa *network* tunapoingia humu ndani; ninaomba mwongozo wako.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa, Mheshimiwa Mwakajoka, Waheshimiwa *order please*. Nina miongozo miwili; mwongozo wa kwanza wa Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, Serikali ilishatoa taarifa kuwa inaandaa taarifa, tusubiri taarifa rasmi ya Serikali ambayo karibuni italetwa kama ilivyoahidi.

Mwongozo wangu wa pili kuhusu Mheshimiwa Musukuma; Kiti kilishawahidi kutoa *ruling* na kwenye Kanuni zetu vyombo vyा mawasiliano vyा kielektroniki na *hard copy*

haviruhusiwi ndani ya Bunge. Kwa mujibu wa Kanuni zetu nimewambia wewe nenda katafute Kanuni ya ngapi.

Katibu!

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi,
Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri. (*Makof*)

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye kwa rehema zake nyingi ametujalia afya njema na kutuwezesha kukutana katika Bunge hili tukufu la Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa naomba kutoa pole kwako binafsi, Bunge lako Tukufu na taifa kwa kuwapoteza wapendwa wetu katika majanga mbalimbali yaliyotokea hapa nchini. Kwa namna ya pekee nitoe pole kwa ndugu, jamaa na marafiki waliopoteza ndugu zao katika ajali ya Kivuko cha MV Nyerere kilichokwuwa kinatoa huduma kati ya Bugorora na Ukara Wilayani Ukerewe. Pia nitoe pole kwa familia zilizopoteza watoto kutokana na imani potofu za kishirikana Mkoani Njombe; vifo hivyo sio tu vimeleta simanzi bali tumepoteza nguvu kazi ya Taifa .

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mbunge), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wao thabiti ambao umewezesha kutekelezwa kwa mafanikio

makubwa llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015, ahadi za viongozi pamoja na kutatua kero mbalimbali za wananchi. Hakika Watanzania tunajivunia uongozi huu unaoacha alama kwa Taifa na tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kuwapa viongozi wetu hawa afya njema na hekima katika utekelezaji wa majukumu yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee namshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini na kunithea kuongoza Wizara hii ya ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Jukumu hili ni kubwa, hivyo naamini kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, na kwa ushirikiano wa wadau mbalimbali nitaweza kutekeleza majukumu yangu kikamilifu.

Mheshiiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kurejea ahadi yangu kwa Mheshimiwa Rais na Watanzania wenzangu kuwa nitaendelea kutumia uwezo na maarifa yangu yote kutekeleza majukumu niliyopewa kwa weledi na uadilifu ili kuhakikisha kuwa Wizara yangu inatoa mchango wa kutosha katika kuiwezesha nchi yetu kupiga hatua kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa adhimu kumpongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na wewe Mwenyewe Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kuliongoza Bunge hili tukufu na hekima na busara. Uongozi wenu umeweza Bunge kutimiza kikamilifu jukumu lake na kuisimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya uongozi wa Mwenyekiti Mheshimiwa Selemiani Moshi Kakoso, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Pwani pamoja na Waheshimiwa wabunge ambaao pia ni Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na ushauri wao wanaoutoa katika kuboresha utendaji wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii imekuwa nguzo muhimu kwa Wizara katika kutoa ushauri, maelekezo, usimamizi na ufuatiliaji wa majukumu mbalimbali yanayotekelvezwa na Wizara na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa katika maendeleo ya Sekta ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wafuataao waliochaguliwa katika chaguzi ndogo zilizofanyika nchini katika mwaka 2018/2019 nikianza na Mheshimiwa *Engineeer* Christopher Chiza, Mbunge wa wa Jimbo la Buyungu; Mheshimiwa Pauline Gekul, Mbunge wa Jimbo la Babati Mjini; Mheshimiwa James Ole Milya, Mbunge wa Jimbo la Simanjiro; Joseph Mkundi, Mbunge wa Jimbo la Ukerewe; Mheshimiwa Marwa Ryoba, Mbunge wa Jimbo la Serengeti; Mheshimiwa Abdallah Mtolea, Mbunge wa Jimbo la Temeke; Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara, Mbunge wa Jimbo la Ukonga; Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Jimbo la Liwale Mjini; na Mheshimiwa Julius Kalanga, Mbunge wa Jimbo la Monduli. Wizara inawatachia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao na kuwaahidi kuwapatia ushirikiano wakati wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza na kuwashukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Dkt. Philip Isidory Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango kwa kuwasilisha Bungeni hotu Dkt. Philip Isidory Mpango ba za mapitio ya utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka 2018/2019 na kutoa mwelekeo wa kazi za Serikali kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuweka mezani Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Aidha, naomba Bunge lako

Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019; kwanza ni Sekta ya Ujenzi fungu 98. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Sekta ya Ujenzi ilitengewa kiasi cha shilingi 34,256,124,485.20 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 31,075,545,000.00 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara ya Ujenzi na Taasisi zake na shilingi 3,180,579,485.20 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara, Sekta ya Ujenzi na Taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika Bajeti ya Matumizi Mengineyo Sekta ya Ujenzi ilitengewa shilingi 9,768,067,270.00 kwa ajili ya manunuzi ya magari ya Viongozi wa Serikali. Hivyo, Bajeti ya Matumizi Mengineyo ya Wizara ilikuwa shilingi 44,024,191,755.20. Hadi mwezi Machi, 2019, shilingi 24,890,428,245.85 zilikuwa zimetolewa na Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kiasi hicho ni asilimia 72.66 ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kati ya fedha hizo, shilingi 22,481,837,450.00 ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi na shilingi 2,408,590,795.85 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Wizara na Taasisi, Sekta ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa miradi ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2018/2019, Sekta ya Ujenzi ilitengewa shilingi 1,976,442,353,141.38. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni shilingi 1,540,514,754,141.38 na shilingi 435,927,599,000.00 zilikuwa ni fedha za nje. Fedha za ndani zilijumuisha fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali shilingi 904,348,754,141.38 na fedha za Mfuko wa Barabara ni shilingi 636,166,000,000.00.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Machi, 2019 Wizara katika Sekta ya Ujenzi ilikuwa imepokea shilingi 1,205,175,488,808.07. Kati ya fedha hizo, shilingi 952,850,032,917.07 ni fedha za ndani na shilingi

252,325,455,891.00 ni fedha za nje. Kwa upande wa fedha za Mfuko wa Barabara, kiasi kilichopokelewa ni shilingi 404,029,032,387.73. Kwa ujumla, fedha zilizotolewa na Hazina hadi Machi, 2019 ni sawa na asilimia 60.98 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, linginei ni Miradi ya Barabara na Madaraja. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara katika Sekta ya Ujenzi kuititia *TANROADS*lipanga kujenga kwa kwa kiwango cha lami barabara zenyet urefu wa kilometra 597.10, ujenzi wa madaraja 15 pamoja na ukarabati wa kilometra 72.10 kwa kiwango cha lami katika barabara kuu. Kwa upande wa barabara za mikoa, lengo lilikuwa ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara zenyet urefu wa kilometra 61.18 na kukarabati kilometra 1,084.12 kwa kiwango cha changarawe na madaraja 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwezi Machi, 2019 miradi ya barabara kuu iliyokamilika kujengwa kwa kiwango cha lami ilikuwa ni kilometra 190.59. Aidha, kilometra 36 za barabara kuu zilikarabatiwa kwa kiwango cha lami. Kwa upande wa barabara za mikoa, kilometra 12.43 zimejengwa kwa kiwango cha lami na kilometra 128.50 zilifanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019, ujenzi wa barabara za kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam uliendelea ambapo ujenzi wa daraja la juu la Mfugale kwenye makutano ya *TAZARA* ulikamilika, ujenzi wa barabara za juu (*Interchange*) kwenye makutano ya Ubungo unaendelea. Aidha, ujenzi wa daraja jipya la Salender, upanuzi wa barabara ya Morocco – Mwenge kilometra 4.3 kuwa njia sita na barabara ya Kimara – Kibaha kilometra 19 kuwa njia nane, unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maandalizi ya kuanza ujenzi wa miundombinu ya mabasi ya endayo haraka (*BRT*) awamu ya pili yanaendelea. Aidha, Wizara imekamilisha ujenzi wa

madaraja makubwa matano ambayo ni Sibiti, Mkoa wa Singida; Mara, Mkoa wa Mara; Mombasa, ambalo linaunganishwa Mkoa wa Songwe na Rukwa; Lukuledi, Mkoa wa Lindi na Mlalakuwa, Dar es Salaam. Ujenzi wa madaraja ya Ruhuhu, Ruvuma; Wami, Pwani; Sukuma, Mwanza; Kigongo, Busisi, Mwanza; Msingi, Singida; na Kitengule, Kagera unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maelezo ya kina kuhusu hatua ya utekelezaji kwa miradi ya barabara na madaraja katika mwaka wa fedha 2018/2019 yamefanuliwa kuanzia ukurasa wa 12 hadi 50 wa Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya vivuko, nyumba na majengo ya Serikali; katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara kupitia Wakala wa Ufundji na Umeme, TEMESA ilipanga kuendelea na ujenzi wa maegesho ya vivuko, ununuzi wa vivuko vipyta, ukarabati wa vivuko pamoja na manunuzi ya vitendea kazi vya karakana za TEMESA kwa ajili ya kuboresha huduma za matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwezi Machi, 2019 miradi ya upanuzi wa maegesho ya Kigamboni awamu ya kwanza inayohusisha upanuzi wa jengo la abiria na ujenzi wa maegesho ya Bwina katika kivuko cha Chato, Nkome umekamilika. Ujenzi wa jengo la abiria, ofisi katika kivuko cha Lindi – Kitunda Mkoani Lindi umekamilika kwa asilimia 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara kupitia Wakala wa Majengo Tanzania (*TBA*) ilipanga kuendelea na ujenzi na ukarabati wa majengo ya Serikali pamoja na nyumba kwa ajili ya makazi ya Viongozi wakiwemo Majaji na Watumishi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwezi Machi, 2019, ujenzi wa nyumba nne za Majaji katika mikoa ya Dar es Salaam nyumba moja, Kilimanjaro nyumba moja, Mtwara nyumba moja na Shinyanga nyumba moja na ulikuwa katika

hatua mbalimbali za utekelezaji. Ujenzi wa nyumba katika kambi ya kufua umeme ya Mto Rufiji unaendelea ambapo jumla ya nyumba 21 kati ya 28 zimekamilika na nyumba saba zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Miradi mingine ya ukarabati wa majengo na nyumba kwa ajili ya makazi ya Viongozi mkoani Dodoma na Watumishi wa Serikali inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maelezo zaidi kuhusu hatua ya utekelezaji kwa miradi ya vivuko, nyumba na majengo ya Serikali katika mwaka wa fedha 2018/2019 ni kama ilivyooneshwa katika ukurasa wa 50 hadi 53 wa Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara pia iliendelea kuratibu shughuli za usalama barabarani na kudhibiti uzito wa magari yanayotumia barabara. Hadi Machi, 2019 kazi ya ujenzi wa mizani ya Mikese Morogoro ilikuwa imekamilika ambapo ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi katika maeneo ya Manyoni na Nyakanazi umefikia asilimia 60. Kwa upande wa kazi ya uwekaji wa kamera za udhibiti mwendo barabarani katika maeneo ya Bwawani na Ubena Zomozi imekamilika kwa asilimia 95.

Aidha, Wizara imeendelea kutekeleza Sheria ya Udhibiti wa Uzito wa Magari ya Jumuuya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2016 ambayo ilianza kutumika rasmi hapa nchini Machi, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa Viwanja vya Ndege. Hadi Machi, 2019, Utekelezaji mradi wa ujenzi wa jengo la Tatu la Abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere umefikia asilimia 96 na unatarajiwu kukamilika mwishoni mwa Mei, 2019. Mikataba kwa ajili ya ujenzi wa Viwanja vya Ndege vya Sumbawanga, Tabora na Shinyanga imeshasainiwa na Serikali inasubiri idhini (*No Objection*) kutoka kwa Benki ya Uwekezaji ya Ulaya ambayo ni kwa ajili ya ufadhilli wa mradi huo. Kuhusu mradi wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe, zabuni za manunuzi ya

kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ukarabati wa tabaka la juu la barabara ya kutua na kuruka ndege zimefunguliwa na uchambuzi unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Mkandarasi kwa ajili ya kazi ya usimikaji wa taa za kuongozea ndege amepatikana na utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi Mei, 2019. Kazi za ukarabati na upanuzi wa njia ya kuruka na kutua ndege, maegesho ya ndege, ujenzi wa jengo la mizigo pamoja na maegesho ya ndege za mizigo, jengo la kuongozea ndege, kituo cha kupooza umeme, maegesho ya magari, kusimika taa za kuongozea ndege na mfumo wa maji zilikuwa zimefikia asilimia 87.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara, kazi za ukarabati zilikuwa zinaendelea. Vilevile, Wizara iliendelea kufanya usanifu wa kina wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro, Kiwanja cha Ndege cha Arusha na Kiwanja cha Ndege cha Msalato ambapo viwanja vipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu ya Viwanja vyta Ndege yapo kuanzia ukurasa wa 55 hadi 62 wa Hotuba ya Bajeti ya mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara kuititia Sekta ya Ujenzi iliendelea kuzisimamia taasisi zilizo chini yake ili kuhakikisha kuwa huduma muhimu zinaendelea kutolewa kwa ufanisi. Kwa ujumla, utekelezaji wa majukumu ya taasisi ulikuwa ni wa kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maelezo kuhusu utendaji wa Taasisi zilizo chini ya Ujenzi yamefanuliwa kwa kina katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia ukurasa wa 62 hadi 78.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uchukuzi fungu 62 katika mwaka wa fedha 2018/2019, Sekta ya Uchukuzi iliidhinishiwa jumla ya shilingi 2,387,031,678,278.00 Kati ya hizo, shilingi 86,292,678,278.00 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi, 2019, kiasi cha fedha za matumizi ya kawaida kilichotolewa ni shilingi 54,920,905,599.00 sawa na asilimia 63.6 ya bajeti ilioidhinishwa na Bunge mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Sekta ya Uchukuzi iliidhinishiwa fedha za miradi ya maendeleo kiasi cha shilingi 2,300,739,000,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2019, fedha za maendeleo zilizotolewa ni shilingi 485,084,462,824.16 sawa na asilimia 21.08 ya bajeti ilioidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mradi wa ujenzi wa reli ya *standard gauge* uliendelea kutumia fedha za Akaunti ya Amana zilizobaki katika mradi huo kwa mwaka 2017/2018 ambapo shilingi 556,561,013,252/= zilitolewa kutoka kwenye Akaunti hiyo. Hivyo, kwa ujumla fedha zilizotumika katika utekelezaji wa miradi ni shilingi 1,041,645,476,076.00.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri kwa njia ya barabara; katika mwaka wa fedha 2018/2019, usafiri kwa njia ya barabara umeendelea kuimarika katika kufanikisha shughuli za kiuchumi na kijamii nchini. Huduma hizo zimeendelea kutolewa kwa kiasi kikubwa na sekta binafsi ambapo usajili wa leseni za usafirishaji wa abiria uliongezeka kutoka leseni 53,784 hadi 58,933 na leseni za malori kutoka leseni 99,377 hadi 111,345 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2017/2018. Ongezeko hili la leseni limetokana na mkakati wa kutoa leseni za muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza ajali za magari yanayotoa huduma za usafiri wa umma *SUMATRA* kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani imendelea kusimamia na kudhibiti mwendo kasi wa mabasi ya mikoani kwa kutumia mfumo wa ufuatiliaji mwenendo wa

mabasi ya masafa mrefu ujulikanayo kama *Vehicle Tracking System* kwa lugha ya kigeni au *VTS*. Hadi mwezi Machi 2019 jumla ya mabasi 3,083 yaendayo mikoani yalikuwa yameunganishwa kwenye mfumo huo ikilinganishwa na mabasi 1,682 yaliyokuwa yanatumia mfumo huo hadi mwezi Machi, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri kwa njia ya reli; Serikali imeendelea kutoa huduma za usafiri wa reli katika Jiji la Dar es Salaam ili kupunguza msongamano wa magari barabarani. Aidha, *TRC* na *TAZARA* zimeendelea kutoa mchango mzuri katika utoaji wa huduma za usafiri wa reli nchini. Maeleo ya kina kuhusu huduma za usafiri kwa njia ya reli yametolewa katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia ukurasa wa 81 hadi 83, ukurasa wa 88 hadi 89 na ukurasa wa 91.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya reli chini ya *TRC*; katika mwaka 2018/2019, Wizara kuititia *TRC* iliendelea na ujenzi wa reli ya kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro kilomita 300 na Morogoro hadi Makutupora kilomita 422. Ujenzi wa kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro umekamilika kwa asilimia 45.8. Ujenzi wa kipande hiki unatarajiwa kukamilika Novemba, 2019 kulingana na mkataba. Kuhusu ujenzi wa reli sehemu ya Morogoro hadi Makutupora (kilomita 422), kazi imekamilika kwa asilimia 7.12 na inatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2021.

Aidha, zabuni za ununuvi wa vichwa vya treni, mabehewa na mitambo itakayotumika kutoa huduma ya usafiri kwenye reli ya *standard gauge* zimefunguliwa tarehe 7 mwezi, Machi, 2019 na kwa sasa majadiliano na mzabuni yanaendelea. Vile vile, kuhusu ujenzi wa mfumo wa umeme wa *SGR*, mwezi Desemba, 2018, Serikali kuititia *TRC* na *TANESCO* ilisaini Mkataba wa miezi 11 na Kampuni ya *Larsen and Tourbo (L&T) Construction* kwa ajili ya kuanza kazi hiyo. hivi sasa Mkandarasi huyo anaendelea na kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutambua umuhimu wa reli ya katika inayotumika sasa ambayo inajulikana kwa jina la *meter gauge railway* katika kusafirisha

bidhaa na abiria. Aidha, reli inatumika kwa ajili ya ujenzi wa reli ya *SGR* unaoendelea. Hivi sasa kazi ya kuiboresha reli hii inaendelea kufuatia kusainiwa kwa Mkataba wa ukarabati wa njia ya reli kutoka Dar es Salaam hadi Isaka mwezi Julai, mwaka 2018. Ukarabati wa njia ya reli kutoka Dar es Salaam - Kilosa kilomita 283 umekamilika kwa asilimia 10 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, mwaka 2020. Aidha, ukarabati wa sehemu ya Kilosa - Isaka kilomita 687 umekamilika kwa asilimia 10.8 na unatarajiwa kukamilika mwezi Januari, 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kukarabati reli ya Tanga – Arusha (kilomita 439) kwa ajili ya usafiri wa abiria na mizigo inaendelea. Kazi ya ukarabati wa reli hii sehemu ya Tanga – Same (kilomita 199) umekamilika. Kazi inayoendelea ni ujenzi wa madaraja sita. Aidha, sehemu ya Same – Arusha (kilomita 186) kazi ya ukarabati wa njia, ujenzi wa madaraja na makalavati unaendelea. Kwa ujumla mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, mwaka 2019. Maelezo zaidi kuhusu utendaji wa *TRC* yametolewa katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia ukurasa wa 83 hadi 88.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Tanzania na Zambia kwa pamoja zimeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha utendaji wa *TAZARA*. Hatua hizo ni pamoja na kuboresha miundombinu na huduma za reli na Serikali kuchangia uendeshaji wa Mamlaka upande wa Tanzania. Hadi mwezi Machi, 2019, *TAZARA* ilikuwa imefanya matengenezo makubwa ya njia kwenye sehemu zilizowekewa katazo la mwendokasi ya jumla ya kilometa 82.5 kati ya kilometa 150 zilizowekewa katazo la mwendokasi.

Aidha, *TAZARA* imeagiza vipuri vyta Injini na mitambo ya kusaidia uzalishaji wa mataruma ya zege ambazo ni *Dumper Truck, Excavator and Drill Rig* katika mgodi wa kokoto ulioko Kongolo, Mbeya. Vifaa hivi viliagizwa na vitaanza kuwasili nchini mwishoni mwa mwezi Mei, 2019. Vifaa vyote vitakuwa vimepokelewa ifikapo mwezi Septemba, 2019. Maelezo zaidi kuhusu *TAZARA* yametolewa katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia ukurasa wa 88 hadi 91.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Huduma za Uchukuzi katika Maziwa; huduma za uchukuzi wa abiria na mizigo katika Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa zimeendelea kutolewa na Kampuni ya Huduma za Meli pamoja na vyombo vya watu binafsi. Aidha, Serikali kupitia Kampuni ya Huduma za Meli imeendelea kuboresha usafiri wa abiria na mizigo katika maziwa hayo kwa kuanza kutekeleza mradi wa ununuzi wa meli mpya na ukarabati wa meli zilizopo. Hadi mwezi Machi, 2019, kazi zilizotekelawa ni pamoja na:

Mikataba ya ujenzi wa meli mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na mizigo tani 400 katika Ziwa Victoria ilikuwa imesainiwa; Ujenzi wa chelezo pamoja na ukarabati wa meli ya *MV Victoria* na *MV Butiama* ilisainiwa mwezi Septemba, 2018 na kazi zinaendelea; Mikataba kwa ajili ya ukarabati wa meli za *MV Umoja* na *MV Serengeti* zilizopo katika Ziwa Victoria inatarajiwa kusainiwa kabla ya mwezi Julai, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa upande wa Ziwa Tanganyika, Mikataba ya ujenzi wa meli mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 600 na tani 400 za mizigo pamoja na ukarabati mkubwa wa meli ya *MVLiemba* imekamilishwa na inatarajiwa kusainiwa kabla ya Julai, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Huduma za Bandari Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ilihudumia shehena za mizigo tani milioni 6.658 katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2017 ikilinganishwa na tani 6.952 milioni zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2018/2019. Aidha, katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2018, Vitengo vya Makasha *TPA* na *TICTS* katika Bandari ya Dar es Salaam vilihudumia makasha 363,145 ikilinganishwa na makasha 361,430 yaliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2017/2018. Hili ni ongezeko la makasha 1,715 sawa na asilimia 0.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kupanua soko la bandari zetu, kuongeza

shehena na kukabiliana na ushindani kutoka bandari za jirani. Hatua hizo ni pamoja na kusogeza huduma za kibandari karibu na wateja kwa kufungua ofisi katika Miji ya Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Lusaka, Zambia; Kigali, Rwanda; Bujumbura, Burundi; pamoja na kuanzisha ofisi inayosimamiwa na wakala (*agent*) Mjini Kampala, Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ilikamilisha utekelezaji wa miradi ifuatayo:-

Uboreshaji wa gati Na.1 katika Bandari ya Dar es Salaam umekamilika mwezi Desemba, 2018 na limeanza kutumika. Ukarabati wa jengo la kuhifadhi mizigo katika Bandari ya Kilwa ulikamilika Septemba, 2018 na Awamu ya kwanza ya ujenzi wa Bandari Kavu ya Kwala, Ruvi, Vigwaza iliyohusu ujenzi wa uzio na kusawazisha eneo kwa kiwango cha changarawe ulikamilika mwezi Septemba, mwaka 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine ya uboreshaji wa bandari za bahari kuu na kwenye maziwa inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na uboreshaji wa gati Na. 1-7 na ujenzi wa gati jipya la kushusha magari katika Bandari ya Dar es Salaam. Ujenzi wa gati Na.1, ujenzi wa gati la kushusha shehena ya magari linalojulikana kwa jina la (*RoRo Berth*) ikiwa ni pamoja na ujazaji wa kifusi na kuongeza kina umefikia asilimia 45. Ujenzi wa gati moja (*multiple terminal*) katika Bandari ya Mtwara kwa ajili ya kuhudumia shehena mchanganyiko umekamilika kwa asilimia 35. Ujenzi wa Gati la Nyamisati, Rufiji umekamilika kwa asilimia 32, ukarabati wa Bandari ya Tanga unaojumuisha upanuzi wa eneo la kuhifadhi mizigo na ukarabati wa miundombinu umekamilika kwa asilimia 83.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuimarisha ulinzi na usalama kwenye mipaka ya nchi yetu na kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato. Hatua hizo ni pamoja na kudhibiti bandari buba nchini. Serikali kuititia Taasisi zake za *TPA*, *TASAC* na Halmashauri za Miji na Wilaya, ilifanya kazi ya kubainisha

bandari bubu nchini ambapo jumla ya bandari bubu 437 zimebainishwa. Hatua inayoendelea ni kufanya tathmini ya bandari zinazofaa kurasimishwa au kufungwa. Tathmini hiyo itakamilika mwezi Juni, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa ujenzi wa Bandari Kavu eneo la Kwala, Ruvu unatekelezwa katika awamu mbili. Awamu ya kwanza ya kujaza kokoto na kushindilia imekamilika kwa asilimia 100 katika eneo lenye ukubwa wa hekta 20.8. Awamu ya pili ya mradi inahusisha kazi ya kujenga reli ya kuunganisha bandari hiyo inayofanywa na Shirika la *TRC*. Kazi hii imefikia asilimia 70 na inatarajiwa kukamilika mwezi huu Mei, 2019. Maelezo zaidi kuhusu utendaji wa *TPA* yametolewa katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia ukurasa wa 94 hadi ukurasa wa 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (*TASAC*) imeendelea kudhibiti masuala ya usafiri majini katika eneo lote la maji la Tanzania kwa kuzingatia matakwa ya Shirika la Bandari Duniani (IMO) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Bandari Zanzibar (*Zanzibar Maritime Authority - ZMA*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usafiri na Uchukuzi wa Njia ya Anga; katika mwaka wa fedha 2018/2019, Mamlaka ya Usafiri wa Anga iliendelea kutekeleza mradi wa ufungaji wa Rada nne za kuongoza ndege za kiraia katika viwanja vya ndege vya Julius Nyerere, *KIA*, Mwanza na Songwe. Hadi mwezi Machi, 2019, utekelezaji wa mradi huu ulikuwa katika hatua mbalimbali. Katika Kiwanja cha Ndege cha Mwalimu Julius Nyerere, ujenzi wa jengo la mnara wa rada umekamilika kwa asilimia 100. Kuhusu Kiwanja cha Ndege cha Mwanza, ujenzi wa jengo la mnara na mitambo ya rada umekamilika kwa asilimia 50 na mtambo utaanza kufanya kazi mwezi Mei, 2019. Kuhusu Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro, ujenzi wa jengo la mnara wa rada na jengo la mtambo wa rada umekamilika kwa asilimia 90. Aidha, kuhusu Kiwanja cha Ndege cha Songwe, mtambo wa rada umeshawasili nchini na kazi ya ufungaji inatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Septemba, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019, Serikali ilipokea ndege tatu mpya. Ndege moja kubwa ya masafa marefu aina ya *Boeing 787 - 8 Dreamliner* yenye uwezo wa kubeba abiria 262 iliwasili Julai, 2018. Ndege mbili za masafa ya kati aina ya *Airbus A220 - 300* zenye uwezo wa kubeba abiria 132 kila moja, moja iliwasili Desemba, 2018 na nyininge iliwasili Januari, 2019. Ongezeko hili la idadi ya ndege limesababisha *ATCL* kutoa huduma za usafiri wa anga katika vituo tisa vya ndani ya nchi na vituo 5 vya kikanda. Vituo vya ndani ya nchi ni pamoja na Dar es Salaam, Mwanza, Bukoba, Kigoma, Kilimanjaro, Tabora, Dodoma, Mbeya, Mtwara, Iringa na Zanzibar. Vituo vya Kikanda ni Entebbe, Uganda; Bujumbura, Burundi; Harare, Zimbabwe; Lusaka, Zambia; na Hayahaya, Comoro. Aidha, *ATCL* inatarajia kuanza kutoa huduma za usafiri wa anga katika Miji ya Bangkok, Thailand; Mumbai, India; Johanesburg, Afrika Kusini; na Guangzhou nchini China. Kwa sasa maandalizi yanaendelea na safari hizi zinatarajiwa kuanza kabla ya mwishoni mwa mwaka wa fedha wa 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali illenga kununua ndege mbili mpya. Ndege moja aina ya *Bombardier Dash 8 - Q400* yenye uwezo wa kubeba abiria 76 na ndege kubwa moja ya masafa marefu aina ya *Boeing 787-8 Dreamliner* yenye uwezo wa kubeba abiria 262. Hadi Machi, 2019, asilimia 36 ya malipo ya ununuzi wa ndege aina ya *Boeing 787-8 Dreamliner* yalifanyika na ndege hiyo inatarajiwa kuwasili nchini mapema mwezi Januari, 2020. Kuhusu ndege moja mpya aina ya *Bombadier Dash 8 Q400*, malipo ya asilimia 30 ya ununuzi wa ndege hiyo yalifanyika na ndege hiyo inatarajiwa kuwasili mwezi Novemba, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudzi za kuendelea kuboresha huduma zake, hadi mwezi Machi, 2019, *ATCL* imewapeleka mafunzoni Marubani 51, Wahandisi 14 na Wahudumu wa Ndani ya Ndege 66. Aidha, *ATCL* imeendelea kuboresha miundombinu ya biashara kwa kujunga kwenye mfumo wa uuzaaji wa tiketi ulimwenguni ambao unajulikana kwa jina kwa lugha ya kigeni (*Global Distribution System -*

GDS), ambapo hadi Machi, 2019, *ATCL* imeweza kuuza tiketi zake katika nchi 25 duniani. Pia, *ATCL* imerejea katika mfumo wa usuluhishi wa mauzo ya tiketi ujulikanao kama *IATA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio mengine ni pamoja na kuanza ukarabati wa Karakana ya Ndege au (Hangar) iliyoko katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro Ijulikanalo kama *Kilimanjaro Maintenance Facilities – KIMAFA*. Vilevile kuboresha mifumo ya TEHAMA na tovuti yake ambapo kwa sasa inawapa wateja urahisi wa kukata tiketi. Mifumo ya TEHAMA na tovuti yake ambapo kwa sasa inawapa wateja urahisi wa kukata tiketi, kufanya usajili wa kuingia katika ndege kwa njia ya mtandao (*on line*) na kuboreshwa mfumo wa ufuatiliaji wa mzigo (*Cargo Tracking System*) kutoka kituo kimoja hadi kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji wa utendaji na utoaji huduma umeiwezesha *ATCL* kumiliki soko la usafiri wa anga la ndani kwa asilimia 40.8 kutoka asilimia 2.5 za mwaka 2017. Aidha, *ATCL* imeongeza idadi ya abiria kutoka 216,798 katika kipindi cha Julai, 2017 - Machi, 2018 hadi abiria 307,192 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/2019. Hili ni ongezeko la asilimia 41.69.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu usafiri wa anga yametolewa katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia ukurasa wa 104 hadi 114.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za hali ya hewa. Katika mwaka 2018/2019, Wakala wa Hali ya Hewa (*TMA*) uliendelea kutoa tahadhari dhidi ya hali mbaya ya hewa na majanga yanayohusiana na hali ya hewa. Viwango vya usahihi wa utabiri wa hali ya hewa viliongezeka kutoka asilimia 81 na kufikia asilimia 87.5. Katika kipindi hicho, *TMA* imesaini mikataba kwa ajili ya ununuzi wa Rada tatu za hali ya hewa. Rada hizo zitafungwa katika Mikoa ya Mtwara, Mbeya na Kigoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi za mafunzo. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara iliendelea kusimamia

vyuo vinavyotoa huduma za mafunzo mbalimbali. Vyuo hivyo ni pamoja na Chuo cha Ujenzi Morogoro, Chuo cha Teknolojia Stahiki ya Nguvu Kazi Mbeya, Chuo cha Bahari Dar es Salaam, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (*NIT*), Chuo cha Usafiri wa Anga Dar es Salaam na Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo zaidi kuhusu utendaji wa taasisi za mafunzo yameoneshwa katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti ukurasa 138 hadi 143.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya mawasiliano. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2018 hadi Machi, 2019, sekta ya mawasiliano imekusanya jumla ya shilingi bilioni 99.032 kwa mchanganuo ufuatao: *TCRA* imekusanya jumla ya shilingi bilioni 58.939 ambapo kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 15.057 zinatokana na asilimia 15 ya pato ghafi la Mamlaka, shilingi bilioni 12.282 ni kutokana na Mfumo wa *TTMS*, shilingi bilioni 22.339 ni kutokana na mauzo ya masafa na shilingi bilioni 9.26 ni rejesho la mtaji uliozidi. Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote umechangia kiasi cha shilingi bilioni 8 kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, shilingi bilioni 32.093 zilikusanya na Shirika la Mawasiliano Tanzania (*TTCL*) kutokana na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi za sekta ya mawasiliano katika mwaka wa fedha 2018/2019 zilipata faida na hivyo zimetoa gawio Serikalini la jumla ya shilingi bilioni 81.558 kwa mchanganuo ufuatao: Mamlaka ya Mawasiliano imetoa shilingi bilioni 79.808; Shirika la Mawasiliano limetoa shilingi bilioni 1.5 na Shirika la Posta limetoa shilingi millioni 250.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019, sekta ya mawasiliano ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 3.856 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 1.93 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na shilingi bilioni 1. 925 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Hadi Machi, 2019 shilingi bilioni 2.728 zilikuwa zimetolewa na Hazina. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 1.096 zimetolewa kwa ajili ya

Mishahara na shilingi bilioni 1.632 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019, sekta ya mawasiliano ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 15 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo zikiwa ni fedha za ndani. Hadi Machi, 2019 shilingi bilioni 3.67 zilikuwa zimetolewa na Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, laini za simu za viganjani zimeongezeka kutoka laini milioni 40.08 mwaka 2017 hadi laini milioni 43.62 mwaka 2018 na idadi ya watumiaji wa intaneti iliongezeka kutoka milioni 22.99 mwaka 2017 hadi kufikia milioni 23.14 mwaka 2018. Vituo vya kurusha matangazo ya redio vimeongezeka kutoka vituo 156 mwaka 2017 hadi kufikia vituo 158 mwaka 2018 na vituo vya kurusha matangazo ya runinga kwa kutumia mitambo iliyosimikwa ardhini vimeongezeka kutoka vituo 34 mwaka 2017 hadi kufikia vituo 37 mwaka 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Sekta ya Mawasiliano imeendelea na maandalizi ya utekelezaji wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa Awamu ya Tatu Sehemu ya Pili kwa lengo la kuboresha matumizi ya miundombinu hiyo na kuwezesha upanuzi wa Mkongo hadi kwenye Makao Makuu ya Wilaya zote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2018/2019, Wizara imeweza ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za Mkongo wa Taifa katika maeneo ya Tukuyu, Kibaha, Kahama, Ifakara, Kidatu na Mafinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea na programu ya kuunganisha taasisi za Serikali kwenye Mkongo wa Taifa ambapo Halmashauri kumi 10 za Katesh, Sikonge, Mbulu, Monduli, Kaliua, Urambo, Kiteto, Simanjiro, Uvinza na Wanging'ombe zimeunganishwa na Mkongo wa Taifa na hatua ya mwisho ya uhakiki wa maunganisho hayo inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, nisije nikapigwa kengele ya pili niombe tu hotuba yangu yote iingizwe kwene *Hansard*.

MWENYEKITI: Omba pesa.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati viongozi wenzangu katika Wizara ninayoongoza nikianza na Mheshimiwa Elias John Kwandikwa (Mb), Naibu Waziri Ujenzi; Mheshimiwa Mhandisi Atashasta Justus Nditiye, Naibu Waziri Uchukuzi na Mawasiliano; Makatibu Wakuu *Arch. Elias Asangalwisiye Mwakalinga*, Sekta ya Ujenzi; Mhandisi Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho, Sekta ya Uchukuzi; Mhandisi Dkt. Maria Leticia Sasabo, Sekta ya Mawasiliano; na Dkt. Jim Yonaz, Naibu Katibu Mkuu, Sekta ya Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwatambua na kuwashukuru washirika mbalimbali wa maendeleo ambao wamekuwa bega kwa bega na Wizara katika utekelezaji wa programu na mipango yetu ya Sekta za Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Washirika wa Maendeleo wanajumuisha mashirika na taasisi za kimataifa zinazochangia katika kuboresha utoaji huduma na miundombinu ya sekta zetu. Washirika hao wa maendeleo ni pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Dunia, Japan, Korea Kusini, Abu Dhabi Fund, Ujeruman, Uingereza, Uhlanzi, Jumuiya ya Nchi za Ulaya, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya, Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Kuwait, Uturuki, OPEC Fund, BADEA, HSBC, TMEA, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za SADC, Taasisi za fedha za CRDB, NSSF na TIB, Asasi zisizokuwa za Kiserikali pamoja na sekta binafsi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwashukuru wananchi na wadau mbalimbali hasa sekta binafsi kwa ushirikiano wao katika kutekeleza malengo ya sekta zetu. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango yenu ambayo imesaidia katika kuimarisha huduma

zitolewazo na Wizara. Naomba muendelee na moyo huo huo ili tuweze kuendeleza sekta hizi ambazo ni kichocheo katika maendeleo ya sekta nyingine za kiumbe na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Katavi kwa ushirikiano wanaonipa na kwa jitihada wanazozionyesha katika kutekeleza miradi mbalimbali ya katika jimbo letu. Kipeke kabisa, napenda kuishukuru familia yangu hasa mke wangu Mwalimu Bora Kamwelwe kwa uvumilivu na kwa kuendelea kunitunza na kuisimamia familia yetu wakati nikitekeleza majukumu ya kitaifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhtasari wa maombi ya fedha ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano katika mwaka wa fedha 2019/2020. Katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano naomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 4,963,297,839,163. Kati ya fedha hizo shilingi 1,330,194,268,268 ni kwa ajili ya Sekta ya Ujenzi; shilingi 3,628,130,373,895 ni kwa ajili ya Sekta ya Uchukuzi na shilingi 3,973,197,000 ni kwa ajili ya Sekta ya Mawasiliano. Mchanganuo wa fedha zinazoombwa kwa kila Fungu zimefanuliwa katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba hii nimeambatisha miradi ya Wizara itakayotekeliza katika mwaka wa fedha 2019/2020, kiambatanisho namba 1-6 ikiwa ni pamoja na kiasi cha fedha kilichotengwa kutekeleza miradi hiyo. Naomba viambatanisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
(*Makofii*)

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante, hoja imeungwa mkono.
(*Makofii*)

**HOTUBA YA WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
MHESHIMIWA MHANDISI ISACK ALOYCE KAMWELWE (MB),
AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA
MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA
2019/2020 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

A. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, baada ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuweka mezani Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuitisha Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

2. Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na kutuwezesha kukutana tena leo kujadili maendeleo ya shughuli zinazosimamiwa na sekta za Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

3. Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Alli Mohammed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao thabiti ambao umeweza kutekelezwa kwa mafanikio makubwa llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015, ahadi za Viongozi pamoja na kutatua kero mbalimbali za wananchi. Hakika Watanzania tunajivunia uongozi huu unaoacha alama kwa Taifa na tunamuomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwajalia afya njema Viongozi hawa ili waendelee kutuongoza kuelekea kwenye Tanzania mpya ya uchumi wa kati na hali bora zaidi ya maisha kwa kila mwananchi.

4. Mheshimiwa Spika, kipekee namshukuru Mheshimiwa Dkt.

John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini na kunteua kuongoza Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano. Jukumu hili ni kubwa, hivyo naamini kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na kwa ushirikiano wa wadau mbalimbali nitaweza kulitekeleza kikamilifu. Nichukue fursa hii kurejea ahadi yangu kwa Mheshimiwa Rais na Watanzania wenzangu kuwa nitaendelea kutumia uwezo na maarifa kutekeleza majukumu yangu kwa weledi na uadilifu ili kuhakikisha kuwa Wizara yangu inatoa mchango unaotarajiwa katika kuiwezesha nchi yetu kuingia kwenye uchumi wa katи.

5. Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri mwenzangu aliyenitangulia kuongoza Wizara hii, Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb) kwa kuanzisha shughuli mbalimbali za maendeleo katika sekta ninazozisimamia. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wafuatao waliochaguliwa katika chaguzi ndogo zilizofanyika nchini katika mwaka 2018/19. Wabunge hao ni: Mheshimiwa Timotheo Paul Mzava, Mbunge wa Jimbo la Korogwe Vijiji; Mheshimiwa Eng. Christopher Kajoro Chizza, Mbunge wa Jimbo la Buyungu; Mheshimiwa Pauline Phillipo Gekul, Mbunge wa Jimbo la Babati Mjini; Mheshimiwa James Kinyasi Milya, Mbunge wa Jimbo la Simanjiro; Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Jimbo la Ukerewe; Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Jimbo la Serengeti; Mheshimiwa Abdallah Ally Mtalea, Mbunge wa Jimbo la Temeke; Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara, Mbunge wa Jimbo la Ukonga; Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Jimbo la Liwale Mjini na Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, Mbunge wa Jimbo la Monduli. Ushindi walioupata umeonyesha imani kubwa waliyonayo wananchi wa majimbo hayo kwa Chama Cha Mapinduzi. Wizara yangu inawaahidi ushirikiano na kuwatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao.

6. Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kutoa pole kwako binafsi pamoja na Bunge lako tukufu kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wa Korogwe Vijiji marehemu Stephen Hilary Ngonyani. Tunaendelea kuwaombea subira familia,

wananchi wa Jimbo la Korogwe Vijijini pamoja na wote walioguswa na msiba huu.

7. Mheshimiwa Spika, vilevile, nitoe pole kwa wananchi walioathirika kwa kupoteza ndugu, mali au kupata majeraha kutokana na ajali za vyombo nya usafiri nchini. Kipekee natoa pole kwa waathirika wa ajali ya kivuko MV Nyerere iliyotokea katika Kisiwa cha Ukara, Wilaya ya Ukerewe siku ya Alhamisi tarehe 20 Septemba 2018. Serikali inaendelea na jithada mbalimbali za kudhibiti ajali za vyombo nya usafiri nchini ikiwa ni pamoja na kuandaa kanuni maalum kwa ajili ya kuhakikisha usalama wa huduma za vivuko. Aidha, ili kuhakikisha kuwa huduma za vivuko katika visiwa hivyo inaendelea kutolewa, Wizara imepeleka kivuko mbadala wa MV Nyerere ambacho kinatoa huduma kwa sasa. Pia, Wizara kuititia Wakala wa Ufundu na Umeme inaendelea na manunuzi ya kivuko kipyaa kitakachohudumia visiwa nya Bugolora na Ukara ili kuboresha huduma ya usafiri katika visiwa hivyo.

8. Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii adhimu kukupongeze wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kuliongoza Bunge hili Tukufu kwa hekima na busara. Uongoziwenu umewezesha Bunge kutimiza kikamilifu jukumu lake la kuisimamia na kuishauri Serikali.

9. Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, lakini si kwa umuhimu, naomba kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Moshi Seleman Kakoso (Mb.) na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma (Mb.) kwa ushirikiano na ushauri waliotupa katika kuboresha utendaji wa Wizara yangu. Aidha, ninawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Miundombinu kwa kuititia Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na kutoa ushauri na mapendekezo yaliyoniwakesha kuwasilisha Hoja hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

10. Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea kuelezea kuhusu

Wizara ninayoisimamia, nitoe pongezi zangu kwa Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) kwa hotuba yake ambayo imefafanua kwa kina utekelezaji wa mipango na mikakati ya Serikali ya kuimarisha na kuboresha huduma za jamii kwa lengo la kupunguza kero za wananchi zinazotokana na umaskini, ujinga na maradhi. Aidha, nampongeza Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango (Mb) kwa hotuba ya ujumla iliyofafanua utekelezaji wa sera na malengo ya uchumi na fedha, uimarishaji wa huduma za kijamii na kutoa malengo kwa mwaka 2019/2020. Naomba pia kuwapongeza Mawaziri wote waliotangulia kuwasilisha Hotuba zao hapa Bungeni.

11. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa Wizara yangu, napenda kumpongeza Dkt. Agnes Lawrence Kijazi, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kwa kuteullwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuwa mjumbi wa kamati ya Umoja wa Mataifa yenye wajumbe 10 itakayotoa ushauri wa masuala ya teknolojia (Technology Facilitation Mechanism - TFM) kwa Umoja huo. Kamati hiyo itasaidia pia katika masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika mchakato wa kufikia malengo 17 ya Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals – SDGs) ifikapo 2030. Uteuzi huu umeleta heshima kubwa kwa Taifa letu. Nintakie kila la kheri katika kutekeleza majukumu yake na awe balozi mzuri wa nchi yetu katika ngazi hiyo ya Umoja wa Mataifa. Aidha, napenda kumpongeza Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Bwana Hamza Said Johari ambaye amechaguliwa bila kipingwa kuwa mwenyekiti wa Shirikisho la Kimataifa la Utoaji Huduma za Usafiri wa Anga na Uongozaji Ndege katika kanda ya Afrika. Hatua hii imeifanya Tanzania kuingia kwenye Kamati Kuu ya Shirikisho hilo ili kushiriki katika uandaaji wa sera na sheria mbalimbali zinazohusu usafiri wa anga.

MAJUKUMU YA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

12. *Mheshimiwa Spika*, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inajumuisha sekta kuu tatu ambazo ni Sekta ya

Ujenzi, Sekta ya Uchukuzi na Sekta ya Mawasiliano.

13. *Mheshimiwa Spika*, majukumu ya msingi ya Sekta ya Ujenzi ni kusimamia utekelezaji wa Sera ya Ujenzi (2003) pamoja na Sera ya Taifa ya Usalama Barabarani (2009); ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara, madaraja na vivuko; ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya viwanja vya ndege; ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali; usimamizi wa masuala ya ufundi na umeme; usimamizi wa shughuli za ukandarasi, uhandisi, ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi; usimamizi wa maabara na vifaa vya ujenzi; usimamizi wa masuala ya usalama na mazingira katika Sekta; uboreshaji utendaji na uendelezaji wa watumishi wa Sekta na usimamizi wa majukumu ya taasisi zilizo chini ya Sekta.

14. *Mheshimiwa Spika*, Sekta ya Uchukuzi ina majukumu ya kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uchukuzi ya mwaka 2003; ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya reli na bandari; usafiri na usafirishaji kwa njia ya anga, reli na bandari; utoaji wa leseni za usafirishaji; usalama katika usafirishaji; usimamizi wa huduma za hali ya hewa; kuendeleza rasilimali watu na kusimamia Taasisi na Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Sekta ya Uchukuzi.

15. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa Sekta ya Mawasiliano, majukumu yake ni pamoja na kusimamia Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003; na Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ya mwaka 2016 na utekelezaji wake. Aidha, Sekta ya Mawasiliano ina dhamana ya kuhakikisha kuwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano inachangia katika maendeleo ya nchi yetu, pamoja na usimamizi wa majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Mawasiliano.

16. *Mheshimiwa Spika*, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kuwasilisha hotuba yangu ambayo imejikita katika Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2018/19 na Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2019/20.

B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19

17. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21), Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 - 2020, Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2015 - 2030, Ahadi za Serikali Bungeni, Maagizo ya Viongozi Wakuu wa Serikali na Sera nyinginezo za Kisekta, Kitaifa na Kimataifa.

B.1 SEKTA YA UJENZI

Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

18. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara ilitengewa kiasi cha Shilingi **34,256,124,485.20** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi **31,075,545,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake na Shilingi **3,180,579,485.20** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara (Ujenzi) na Taasisi zake. Aidha, katika Bajeti ya Matumizi Mengineyo Wizara ilitengewa Shilingi **9,768,067,270.00** kwa ajili ya manunuzi ya magari ya Viongozi wa Serikali. Hivyo Bajeti ya Matumizi Mengineyo ya Wizara ilikuwa Shilingi **44,024,191,755.20**. Hadi Machi, 2019, Shilingi **24,890,428,245.85** zilikuwa zimetolewa na HAZINA kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kiasi hicho ni asilimia **72.66** ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka wa fedha 2018/19. Kati ya fedha hizo, Shilingi **22,481,837,450.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi na Shilingi **2,408,590,795.85** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara na Taasisi.

Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

19. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/19, Sekta ya Ujenzi ilitengewa **Shilingi 1,976,442,353,141.38** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo,

fedha za ndani ni **Shilingi 1,540,514,754,141.38** na **Shilingi 435,927,599,000.00** zilikuwa ni fedha za nje. Fedha za ndani zilijumuisha fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali (Consolidated Funds) **Shilingi 904,348,754,141.38** na fedha za Mfuko wa Barabara **Shilingi 636,166,000,000.00**. Hadi Machi, 2019 fedha zilizopokelewa ni **Shilingi 1,205,175,488,808.07**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 952,850,032,917.07** ni fedha za ndani na **Shilingi 252,325,455,891.00** ni fedha za nje. Kwa upande wa fedha za Mfuko wa Barabara kiasi kilichotolewa hadi Machi, 2019 ni **Shilingi 404,029,032,387.73**. Kwa ujumla fedha zilizotolewa hadi kufikia Machi, 2019 ni sawa na asilimia **60.98** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2018/19.

UTEKELEZAJIWAMIRADI YA MAENDELEO

Miradi ya Barabara na Madaraja

20. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara kuititia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ilipanga kujenga barabara zenyе urefu wa kilometa **597.10** kwa kiwango cha lami, ujenzi wa madaraja **15** pamoja na ukarabati wa kilometa **72.10** kwa kiwango cha lami katika barabara kuu.

Hadi kufikia Machi, 2019, jumla ya kilometa **190.59** za barabara kuu zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami na jumla ya kilometa **36** za barabara kuu zimekarabatiwa kwa kiwango cha lami.

21. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara za mikoa, Wizara kuititia TANROADS ilipanga kujenga kwa kiwango cha lami barabara zenyе urefu wa kilometa **61.18** ambapo kilometa **36.51** zilipangwa kujengwa kwa kutumia Fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na kilometa **24.67** kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Aidha, kilometa **1,084.12** zilipangwa kukarabatiwa kwa kiwango cha changarawe ambapo kati ya hizo kilometa **606.12** na madaraja **15** yalipangwa kukarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali

na kilometra **478** pamoja na madaraja **15** kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara.

Hadi Machi, 2019 jumla ya kilometra **12.43** za barabara za mikoa zimejengwa kwa kiwango cha lami na jumla ya kilometra **128.50** zilifanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe na ujenzi wa madaraja ulikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

22. Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ya matengenezo ya barabara kuu na barabara za mikoa, Wakala ulipanga kufanya matengenezo ya barabara kuu na barabara za mikoa ambayo yanahuisha matengenezo ya kawaida (routine and recurrent maintenance) kwa kilometra **34,747.30**, matengenezo ya muda maalum na sehemu korofi ya kilometra **7,577.90** na matengenezo ya madaraja **5,499**.

Hadi kufikia Machi, 2018/19 utekelezaji wa matengenezo katika barabara kuu na za mikoa ulifikia kilometra **10,968.40**, matengenezo ya muda maalum na sehemu korofi kilometra **2,766.2** na matengenezo ya madaraja **1,086**.

Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa miradi minane (8) ya barabara umekamilika na inasubiri kutengewa fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi. Miradi kumi na tatu (13) inaendelea kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wakati miradi iliyobaki ilikuwa katika hatua ya manunuzi.

23. Mheshimiwa Spika, kazi ya kudhibiti uzito wa magari iliendelea kwa kutumia mizani **46** ya kudumu na **22** inayohamishika katika barabara kuu za lami. Hadi kufikia Machi, 2019, magari **2,880,288** yalikuwa yamepimwa ambapo kati ya hayo, magari **907,790** sawa na asilimia **32**, yalikuwa yamezidisha uzito. Jumla ya Shilingi **1,605,160,376.30** zilikusanywa kutohana na tozo ya uharibifu wa barabara na malipo ya kupitisha mizigo mipana na isiyo ya kawaida.

24. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya barabara hadi Machi, 2019 ni kama ifuatavyo:

25. Mheshimiwa Spika, mradi wa ukarabati kwa kiwango cha

changarawe wa **Barabara za Kuelekea kwenye mradi wa Kufua Umeme katika Maporomoko ya Mto Rufiji**; ambazo ni Ngerengere – Kisaki – Selous (km 166) na Kibiti – Mloka – Selous – (km 201) ulifanyika kuititia fedha zilizotolewa na Wizara ya Nishati.

26. Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa barabara ya **Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro** sehemu ya Dar es Salaam – Chalinze (km 144) umepangwa kutekelezwa kwa kiwango cha "Expressway". Kazi za ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam – Chalinze haziijaanza kutokana na uamuzi wa Serikali kusogea mbele utekelezaji wa mradi huu ili kukamilisha kwanza miradi mingine inayoendelea. Mradi huu pia unahusisha ukarabati (overlay) kwa kiwango cha lami sehemu ya Mlandizi – Chalinze (km 44) unaofanyika kwa awamu ambapo hadi Machi, 2019 mkataba kwa ajili ya ukarabati wa kilometra 12.4 umesalniwa na maandalizi ya ukarabati yanaendelea. Aidha, ujenzi wa barabara ya Kwa Mathias – Msangani (km 8.3) kwa kiwango cha lami upo katika hatua ya manunuzi. Kuhusu mradi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Urema Zomozi – Ngerengere (km 11), kazi za usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni zimekamilika. Kwa upande wa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Morogoro – Dodoma (km 260), taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi hizo zinaendelea.

27. Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa barabara ya **Wazo Hill – Bagamoyo – Msata** sehemu ya **Tegeta – Bagamoyo (km 46.9)**, **Mbegani – Bagamoyo (km 7.2)** na **Makofia – Mlandizi (km 36.7)** kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika na Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi.

Mkataba wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za **TAMCO – Vikawe – Mapinga (km 24)** umesainiwa na maandalizi ya kuanza ujenzi yanaendelea. Kuhusu ujenzi wa barabara ya **Bagamoyo – Saadani – Tanga (km 246)**, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imeonyesha nia ya kutoa fedha za ujenzi. Ujumbe kutoka Benki hiyo ulitembelea mradi

tarehe 13/02/2019 kwa ajili ya kuandaa taarifa itakayowasilishwa kwenye Bodi ya Wadhamini ya Benki hiyo ili kuidhinisha fedha za mkopo nafuu wa ujenzi wa barabara hiyo. Kuhusu ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za **Kisarawe - Maneromango (km 54)** na **Kisarawe - Mlandizi (km 119)**, mradi huu ulikuwa katika hatua ya manunuzi ya kumpata Mkandarasi wa kujenga barabara hiyo.

28. Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Usagara - Geita - Buzirayombo - Kyamyorwa**, ujenzi umekamilika kwa sehemu ya **Uyovu - Bwanga (km 45)** na **Bwanga - Biharamulo (km 67)**. Aidha, usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami umekamilika kwa sehemu ya **Geita - Bulyanhulu Junction (km 58.3)** na **Bulyanhulu Junction - Kahama (km 61.7)** na taratibu za manunuzi ya kuwapata Makandarasi wa ujenzi wa barabara hizi zinaendelea.

29. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara ya **Kigoma - Kidahwe - Uvinza - Kaliua - Tabora**, hadi kufikia Machi 2019, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Urambo - Kaliua (km 28)** umefikia asilimia 35, zabuni kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri atakayesimamia kazi za ujenzi wa barabara ya **Uvinza - Malagarasi (km 51.1)** zimetangazwa na atakapopatikana Mhandisi Mshauri ujenzi utaanza mara moja. Idhini ya kuendelea na taratibu nyingine za manunuzi ilitolewa na Mfuko wa Abu Dhabi (Abu Dhabi Fund) mwishoni mwa Februari, 2019. Aidha, taratibu za kutangaza zabuni za ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Chagu - Kazilambwa (km 36)** zinaendelea.

30. Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa barabara ya **Marangu - Tarakea - Rongai - Kamwanga na Bomang'ombe - Sanya Juu**, hadi Machi, 2019 ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya **Sanya Juu - Elerai (km 32.2)** umekamilika kwa asilimia 92, mkataba wa ujenzi kwa kiwango cha lami mita 800 za barabara ya **Kiboroloni - Kiharara - Tsuduni - Kidia (km 10.8)** umesainiwa na maandalizi ya ujenzi yanaendelea. Kuhusu barabara ya **Kwa Sadala - Masama - Machame**

Junction (km 16), mkataba wa ujenzi wa kilometra 1.4 kati ya kilometra 3.5 zilizobaki umesainiwa na maandalizi ya ujenzi yanaendelea. Aidha, ujenzi wa **Arusha Bypass (km 42.4)** na upanuzi wa barabara ya **Sakina – Tengeru (km 14.1)** umekamilika kwa kiwango cha lami. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa kilometra 2.6 unaendelea katika barabara ya **Kijenge – Usa River (Nelson Mandela AIST: km 14)**.

31. Mheshimiwa Spika, kwa sehemu ya upanuzi wa barabara ya **Arusha – Moshi – Himo – Holili (sehemu ya Tengeru – Moshi – Himo (km 105.0) pamoja na mizani ya Himo)**, Serikali ya Japan kupitia Shirika la Maendeleo la JICA wameonyesha nia ya kugharamia upanuzi wa barabara hii na mazungumzo kati ya Serikali na JICA yako katika hatua za mwisho kabla ya kutangaza zabuni za ujenzi.

32. Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya **Nangurukuru – Mbwemkuru**, hadi Machi, 2019 taratibu za kukamilisha malipo ya Mkandarasi wa ujenzi wa barabara hii zinaendelea. Aidha, **mradi** wa ujenzi wa barabara ya **Ndundu – Somanga** umekamilika. Hata hivyo, kazi za marekebisho kwa sehemu zilizoanza kuharibika zinaendelea.

33. Mheshimiwa Spika, mradi wa barabara ya **Dodoma – Manyoni** unahusisha ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja (One Stop Inspection Station - OSIS) cha Muhalala (Manyoni) pamoja na ujenzi wa mizani inayopima uzito wa magari yakiwa kwenye mwendo (WIM) eneo la Nala Mkoani Dodoma. Hadi Machi, 2019 kazi ya ujenzi wa OSIS zimefikia asilimia 57. Hata hivyo, Mkandarasi amesitisha Mkataba wa ujenzi kutokana na kuchelewa kuidhinishwa kwa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT). Kuhusu Mizani inayopima uzito wa magari yakiwa kwenye mwendo (WIM) eneo la Nala – Dodoma, kazi ya ufungaji wa mizani hiyo imefikia asilimia 32.

34. Mheshimiwa Spika, mradi wa ukarabati wa barabara ya **Nelson Mandela** ulitengewa fedha kwa ajili ya maandalizi ya upanuzi wa sehemu ya **Dar es Salaam Port – TAZARA (km 6)** chini ya awamu ya pili ya mradi wa *Dar es Salaam Maritime*

Gateway ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia. Utekelezaji wa mradi huu haujaanza kwa kuwa utajumuishwa kwenye mradi wa Mabasi Yaendayo kwa Haraka Awamu ya Tano ambao uko kwenye maandalizi ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya usanifu.

35. Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa barabara ya **Dumila – Kilosa**, kazi ya ujenzi kwa sehemu ya **Dumila – Rudewa (km 45)** ilikamilika Desemba, 2013. Kwa sehemu ya **Rudewa – Kilosa (km 24)**, hadi Machi, 2019 mkataba umesainiwa na Mkandarasi yuko kwenye maandalizi ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami. Aidha, kazi ya ujenzi wa mizani ya kupima magari yakiwa kwenye mwendo (Weigh in Motion - WIM) eneo la Dakawa imekamilika.

36. Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Sumbawanga – Matai – Kasanga Port**, kilometra 76.6 zimejengwa kwa kiwango cha lami na kazi za ujenzi zinaendelea. Aidha, hadi Machi, 2019, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya **Matai – Kasesya (km 50)** zinaendelea.

37. Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa **madaraja makubwa**, hadi Machi, 2019 ujenzi wa madaraja ya Mlalakuwa, Momba, Lukuledi na Sibiti ulikuwa umekamilika. Madaraja ambayo ujenzi wake unaendelea ni pamoja na Mara (asilimia 85), Ruhuhu (asilimia 75) na Magara (asilimia 48). Aidha, maandalizi ya ukarabati wa daraja la Kirumi na kuanza ujenzi wa madaraja ya Selander, Wami, Simiyu, Kigongo/Busisi, Sukuma, Mkundi, Msingi, Mtera pamoja na ununuzi wa vyuma vya madaraja ya dharura (Steel Bridge Emergency Parts/ Mabey 200 Compact Bridge Parts) yako katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

38. Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa barabara ya **New Bagamoyo (Morocco Junction - Mwenge – Tegeta: km 17.2)** hadi Machi, 2019, mkataba wa upanuzi wa sehemu ya **Morocco – Mwenge (km 4.3)** ulikuwa umesainiwa kwa ufadhilli wa Serikali ya Japan.

39. Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa barabara ya **Kyaka – Bugene** umekamilika na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa sehemu ya **Bugene – Kasulo (km 124)** na **Omugakorongo – Kigarama – Murongo (km 105)** umekamilika. Mapitio ya taarifa ya uthamini wa mali zitakazoathiriwa na ujenzi wa barabara zinafanyiwa marekebisho kabla ya kuwasilishwa kwa Mthamini Mkuu wa Serikali. Aidha, mapitio ya usanifu wa kina kwa sehemu ya **Bugene – Kasulo (km 124)** na sehemu ya **Kyaka – Mutukula (km 30)** ili kukidhi viwango vya Jumuiya ya Afrika Mashariki yanaendelea.

40. Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya **Isaka – Lusahunga – Rusumo**, hadi Machi, 2019, kazi ya ukarabati wa sehemu ya **Ushirombo – Lusahunga (km 110)** inaendelea ambapo kilometra 91 zimekarabatiwa kwa kiwango cha lami. Kazi ya matengenezo ya dharura katika sehemu korofii kwenye sehemu ya **Lusahunga – Rusumo (km 92)** inaendelea. Aidha, kazi ya mapitio ya usanifu wa kina ili kukidhi viwango vinavyotakiwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki imekamilika. Benki ya Dunia imeonyesha nia ya kugharamia ukarabati wa barabara hii kwa kiwango cha lami kupitia mradi wa *Development Corridors Transport Project (DCTP)*. Kuhusu ujenzi wa mizani ya kupima uzito wa magari yakiwa kwenye mwendo (WIM) na ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja (OSIS) cha Nyakanazi, hadi Machi, 2019 kazi za ujenzi wa kituo cha ukaguzi wa pamoja (OSIS) cha Nyakanazi chini ya ufadhili wa Jumuiya ya Ulaya (EU) zilikuwa zimefikia asilimia 60. Hata hivyo, Mkandarasi amesitisha Mkataba wa ujenzi kutokana na alichokiita ucheleweshaji wa malipo kutokana na kuchelewa kuidhinishwa kwa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT).

Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya **Nyakahura – Kumubuga – Murusagamba/Rulenge – Murugarama** na barabara ya **Rulenge – Kabanga Nickel** zenye jumla ya kilometra 141 unaendelea chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

41. Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa barabara ya **Manyoni – Itigi – Tabora**, hadi kufikia Machi, 2019 ujenzi wa sehemu za

Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.35) na Tabora – Nyahua (km 85) umekamilika. Aidha, sehemu ya **Chaya – Nyahua (km 85.4)** hadi Machi, 2019 kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami imefikia asilimia 26.

42. Mheshimiwa Spika, barabara ya **Korogwe – Handeni** ilikamilika Novemba, 2013. Fedha iliyo tengwa ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi wa ujenzi wa barabara hii. Serikali inaendelea na maandalizi ya kukamilisha malipo ya Mkandarasi wa ujenzi wa barabara hii.

43. Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa ukarabati wa barabara ya **Mwanza/ Shinyanga Border – Mwanza**, hadi Machi, 2019, taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami zilikuwa zinaendelea.

44. Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa **barabara za kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam**; kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami zimekamilika kwa barabara ya **Mbezi (Morogoro Road) – Malamba Mawili – Kinyerezi – Banana (km 14)**, **Kimara Baruti – Msewe – Changanyikeni (km 2.6)**, **Ardhi – Makongo – Goba; sehemu ya Goba – Makongo (km 4)**, **Kimara – Kilungule – External/ Mandala Road (km 9)** sehemu ya External/Mandala Road – Maji Chumvi (km 3). Kazi za ujenzi zinaendelea kwa sehemu ya **Kimara Korogwe – Maji Chumvi (km 6)**, **barabara ya Tegeta Kibaoni – Wazo – Goba – Mbezi Mwisho (km 20)** sehemu ya Goba – Madale (km 5), **Banana – Kitunda – Kivule – Msongola (km 14.7)** na **Maji Chumvi – Chang’ombe – Barakuda (km 2.5)**. Aidha, taratibu za manunu zi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi kwa sehemu ya Mloganzila – Kisopwa (km 1) katika barabara ya **Kibamba – Kisopwa – Kwembe – Makondeko (km 14.66)** zinaendelea.

45. Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya **Mwai Kibaki (km 9.1)** na **Kawe round about – Garden Road Junction (km 2.9)** taratibu za kutangaza zabuni kwa mradi huu zinaendelea. Aidha, taratibu za kutangaza zabuni za ujenzi wa barabara ya **Kongowe – Mjimwema – Kivukoni (km 25.1)** kwa kiwango

cha lami zinaendelea.

Kwa upande wa barabara ya **Mjimwema – Kimbiji (km 27)**, kazi ya usanifu wa kina na utayarishaji wa Nyaraka za Zabuni zinaendelea. Aidha, zabuni za ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami zinatarajiwa kutangazwa mara baada ya kukamilika kwa kazi hii.

46. Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya **Ifakara – Lupiro – Mahenge/ Malinyi – Londo – Songea**, kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Kidatu – Ifakara (km 66.9)** inaendelea na Serikali imeendelea kulipa fidia kwa watakaoathirika na utekelezaji wa mradi huu. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Ifakara – Lupiro – Malinyi – Londo – Lumecha (km 396)**.

47. Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa barabara ya **Tabora – Ipole – Koga – Mpanda**, hadi kufikia Machi, 2019, kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya **Tabora – Sikonge (Usesula) (km 30)** zimekamilika. Kwa sehemu ya **Sikonge (Usesula) – Ipole – Koga – Mpanda (km 359)**, ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Usesula – Komanga (km 108) na barabara ya kuingia mji wa Sikonge, (km 7.5) umefikia asilimia 12.91, Komanga – Kasinde (km 108) na barabara ya kuingia mji wa Inyonga (km 4.8) umefikia asilimia 18.26, na Kasinde – Mpanda (km 108) na barabara ya kuingia mji wa Urwira (km 3.7) umefikia asilimia 15.94.

48. Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya **Makutano – Natta – Mugumu – Loliondo na Loliondo – Mto wa Mbu**, hadi kufikia Machi, 2019 ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya **Makutano – Sanzate (km 50)** umefikia asilimia 74 ambapo kilomita 22 zimekamilika. Kuhusu sehemu ya **Sanzate - Natta – Mugumu (km 85)**, hadi Machi 2019, taratibu za kutangaza zabuni za kumpata Mkandarasi wa ujenzi zilikuwa zinaendelea na ujenzi wa barabara ya **Loliondo – Mto wa Mbu** (sehemu ya Waso – Sale: km 49) ulikuwa umefikia asilimia 25.15.

49. Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya **Ibanda – Itungi/ Kiwira**, hadi Machi, 2019 kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Kikusya – Ipinda –Matema Beach (km 39), sehemu ya Tenende – Matema (km 34.6)**, imefikia asilimia 96 ambapo kilometra 32.3 zimekamilika. Kwa upande wa ujenzi wa sehemu ya **Bujesi –Mbambo (km 10.0) na** kilometra saba (7) za **Tukuyu – Mbambo (km 25)**, Wizara iko katika hatua za manunuzi kwa ajili ya kuwapata Makandarasi wa sehemu hizo.

50. Mheshimiwa Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Nzega – Tabora (km 115)** umekamilika. Aidha, hadi Machi, 2019, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya **Shelui – Nzega (km 110)** zilikuwa zinaendelea ambapo tangazo la zabuni lilitolewa tarehe 17 Februari, 2019.

51. Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya **Sumbawanga – Mpanda – Kanyani – Nyakanazi**, hadi Machi, 2019 ujenzi wa sehemu ya **Sumbawanga – Kanazi (km 75), Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 76.6) na Sitalike – Mpanda (km 36.9)** ulikuwa umekamilika. Kuhusu barabara ya **Mpanda – Mishamo (km 100)** sehemu ya Mpanda – Ifukutwa – Vikonge (km 35), ujenzi umefikia asilimia 66.3 ambapo kilometra 15.22 zimekamilika kwa kiwango cha lami. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya **Kibaoni – Sitalike (km 71)**. Aidha, ujenzi wa barabara ya **Vikonge – Magunga – Uvinza (km 159)** na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya **Namanyere – Katongoro – New Kipili Port (km 64)** umejumuishwa kwenye mradi wa *Lake Tanganyika Transport Project (LTTP)* chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia.

52. Mheshimiwa Spika, mradi wa ukarabati wa barabara ya **Nyanguge – Musoma** unahusisha pia ujenzi wa barabara ya Usagara – Kisera (Mwanza Bypass: km 17), Nyamuswa – Bunda – Bulamba (km 55), Bulamba - Kisorya (km 51) na barabara ya Musoma – Makojo – Busekela (km 92). Mradi huu unahusisha pia ukarabati wa barabara ya Makutano – Sirari (km 83).

Kwa upande wa ukarabati wa sehemu ya **Nyanguge-Simiyu/Mara Border (km 100.4)** mradi huu umejumuishwa kwenye Mradi wa “Lake Victoria Transport Programme” (LVTP) chini ya ufadhilli wa Benki ya Dunia ambapo hadi Machi, 2019 taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ukarabati zilikuwa zinasubiri kukamilika kwa taratibu za mkopo kutoka Benki ya Dunia. Aidha, kazi za ujenzi wa barabara ya **Usagara - Kisesa (km 16.35)** na **daraja la Nyashishi** zimekamilika.

Kuhusu barabara ya **Nansio - Kisorya - Bunda - Nyamuswa; sehemu ya Bulamba - Kisorya (km 51)**, kazi za ujenzi zimekamilika kwa asilimia 55. Aidha, Benki ya Dunia kuitia programu ya *Lake Victoria Transport Project* (LVTP) imeonyesha nia ya kugharamia ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu **Nyamuswa - Bulamba (km 55)**. Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya mapitio ya usanifu wa kina zilikuwa zinasubiri kukamilika kwa taratibu za mkopo kutoka Benki ya Dunia.

Vilevile, upanuzi wa **barabara ya kwenda Kiwanja cha Ndege cha Mwanza (km 12)** umekamilika na kazi ya ukarabati wa barabara ya **Makutano - Sirari (km 83)** zimekamilika. Aidha, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi sehemu yenye urefu wa kilometra 5 zinaendelea kwa barabara ya **Musoma - Makojo - Busekela (km 92)**.

53. Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa barabara ya **Magole - Turiani - Mziha**, ujenzi wa sehemu ya **Magole - Turiani (km 45.2)** umekamilika. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya **Turiani - Mziha - Handeni (km 104)**.

54. Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa ujenzi wa barabara za juu (flyovers/ interchange) na maboresho ya makutano ya barabara katika jiji la Dar es Salaam hadi Machi, 2019, ujenzi wa **barabara ya juu (Flyover) katika makutano ya TAZARA** umekamilika na ujenzi wa barabara za juu (*Interchange*) katika makutano ya **Ubungo** umefikia asilimia

28. Aidha, kazi za upembuzi yakinifu zimekamilika na usanifu wa kina unaendelea katika makutano ya barabara maeneo ya *Fire* (Morogoro/United Nations), Magomeni (Morogoro/Kawawa), Mwenge (Sam Nujoma/New Bagamoyo), Tabata/Mandela, Morocco (Ali Hassan Mwinyi/Kawawa), Buguruni (Mandela/Uhuru), Kinondoni (Ali Hassan Mwinyi/ Kinondoni) na Selander (Ali Hassan Mwinyi/ United Nations).

55. *Mheshimiwa Spika*, barabara ya **Mwigumbi – Maswa - Bariadi – Lamadi**, sehemu za **Mwigumbi – Maswa (km 50.3)** na **Bariadi - Lamadi (km 71.8)** zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu iliyobaki ya **Maswa – Bariadi (km 49.7)** umefikia asilimia 40. Kuhusu barabara ya **Tabora - Ipole – Rungwa (km 172)**, hadi Machi, 2019 kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zimekamilika.

56. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu barabara ya **Kidahwe – Kibondo – Nyakanazi**, hadi Machi, 2019 kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya **Kidahwe – Kasulu (km 63)** zilikuwa zimefikia asilimia 70 ambapo kilometa 34.8 zimekamilika. Aidha, ujenzi wa barabara ya **Nyakanazi – Kibondo (km 50)** umefikia asilimia 60 ambapo kilometa 11 zimekamilika kwa kiwango cha lami. Aidha, Mhandisi Mshauri amewasilisha taarifa ya mwisho ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya **Kabingo – Kibondo – Kasulu – Manyovu (km 260)** na **Barabara ya kupitia Kibondo mjini (km 25.6)**. Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kupitia makubaliano yaliyosainiwa kati yake na Serikali tarehe 5 Machi, 2019 imekubali kutoa fedha za ujenzi wa barabara ya **Kabingo – Kibondo – Kasulu – Manyovu (km 260)**. Zabuni za ujenzi zimeshatangazwa na zitafunguliwa tarehe 9 Mei, 2019. Aidha, uchambuzi wa zabuni za ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Njia panda ya Nduta - Kibondo mjini (km 25.6)** ulikuwa unaendelea.

57. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu mradi wa **barabara ya kwenda Uwanja wa Ndege wa Mafia** (Mafia Airport Access Road (km 16), hadi Machi, 2019 taratibu za kukamilisha malipo ya Mkandarasi wa ujenzi wa barabara hii zinaendelea. Kwa

upande wa mradi wa barabara ya **Chuo Kikuu cha Dodoma (km 12)**, hadi Machi, 2019, kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara hii zimekamilika. Ujenzi wa **Daraja la Nyerere (Kigamboni) (mita 680)** umekamilika. Aidha, kazi za ujenzi wa barabara unganishi kutoka Daraja la Nyerere – Vijibweni zimefikia asilimia 90 na ujenzi wa sehemu ya Tungi – Kibada unaendelea.

58. Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa **njia za magari mazito na maegesho ya dharura katika Ushoroba wa Kati** una lengo la kuimarisha na kuboresha barabara pamoja na kuongeza usalama kwa watumiaji wa barabara katika ushoroba huo. Mradi huu umepangwa kujumuishwa kwenye Usanifu wa Kina kabla ya kufanya ukarabati wa barabara za ushoroba wa katи zilizopangwa kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ambazo ni **Morogoro - Dodoma (km 260), Singida - Shelui (km 108) na** Shelui – Nzega (km 110).

59. Mheshimiwa Spika, mradi wa barabara ya **Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA)** hadi Pugu (**km 8**) unalenga kuipanua barabara hii kuwa njia sita. Mradi huu utajumuishwa kwenye ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tatу. Hadi Machi, 2019, Usanifu wa Kina wa miundombinu ya Mabasi yaendayo Haraka Awamu ya Tatу ulikuwa unaendelea chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia.

60. Mheshimiwa Spika, mradi wa barabara ya **Kimara – Kibaha (km 25.7)** unahusisha upanuzi wa sehemu ya Kimara – Kiluvya (km 19.2) kuwa njia nane ikijumuisha **upanuzi wa madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji**. Hadi Machi, 2019 ujenzi wa barabara hii ulikuwa unaendelea.

61. Mheshimiwa Spika, kuhusu kuijenga kwa njia sita barabara ya mzunguko ya **Pugu – Kifuru - Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 34)**, hadi Machi 2019, taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri atakayefanya kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ujenzi kwa njia sita zilikuwa zinaendelea. Aidha, mradi wa ujenzi wa **mizani mpya karibu na bandari ya Dar es Salaam** unatekelezwa ili magari

makubwa yapime uzito kabla ya kuanza safari na hivyo kudhibiti uzidishaji wa uzito. Hadi Machi, 2019 utekelezaji wa mradi huu ulikuwa umekamilika.

62. Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Tunduma – Sumbawanga**, ujenzi kwa sehemu ya **Tunduma - Ikana (km 63.7)**, **Ikana - Laela (km 64.2)**, **Laela - Sumbawanga (km 95.31)** na **Tunduma - Ikana (eneo la Tunduma mjini - km 1.6)** umekamilika. Aidha, hadi Machi, 2019 kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Mpemba - Isongole (km 51.2)** zilikuwa zimefikia asilimia 28.5.

63. Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa barabara ya **Kagoma – Lusahunga**, ujenzi wa barabara hii umekamilika. Aidha, kazi za ujenzi wa barabara za **Muhutwe – Kamachumu – Muleba (km 54)** na kilometra 5 za barabara ya **Muleba – Kanyambogo – Ruby (km 18.5)** zilikuwa zinaendelea.

64. Mheshimiwa Spika, mradi wa ukarabati kwa kiwango cha lami barabara ya **Arusha – Namanga (km 105)** ulikamilika Desemba, 2012. Aidha, kazi ya ujenzi wa Kituo cha Kutoa Huduma kwa Pamoja Mpakani (One Stop Border Post - OSBP) imekamilika. Hadi Machi, 2019 Serikali iliendelea kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri.

65. Mheshimiwa Spika, ujenzi na ukarabati wa barabara ya **Arusha – Minjingu – Babati – Singida** umekamilika. Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya **Singida – Shelui (km 108)** zinaendelea ambapo tangazo la zabuni lilitolewa tarehe 17 Februari, 2019 na Kampuni 19 zimeonesha nia ya kutekeleza mradi huu.

66. Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya **Dar es Salaam – Mbagala (Kilwa Road)** na **daraja la Gerezani**, upanuzi wa sehemu ya **Bendera Tatu – KAMATA (km 1.3)** utajumuishwa kwenye mradi wa ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili. Mkataba wa ujenzi wa daraja la Gerezani ulisainiwa tarehe 22 Januari, 2019 na

maandalizi ya ujenzi yanaendelea chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Japan (JICA). Aidha, hadi Machi, 2019 kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni kwa sehemu ya ***Mbagala Rangi Tatu – Kongowe*** pamoja na ***Daraja la Mzinga*** zilikuwa zinaendelea.

67. Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya ***Msimba – Ruaha / Ikokoto – Mafinga – Igawa***, hadi Machi, 2019, kazi za ukarabati kwa sehemu ya ***Mafinga – Nyigo (km 74.1) na Nyigo – Igawa (km 63.8)*** zilikuwa zimekamilika. Aidha, kwa upande wa barabara ya ***Rujewa – Madibira – Mafinga (km 152)***, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi.

68. Mheshimiwa Spika, kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya ***Njombe – Moronga – Makete (km 107.4)*** sehemu za Njombe – Moronga (km 53.9) na Moronga – Makete (km 53.5) zimefikia asilimia 25.85. Aidha, kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya ***Njombe – Lupembe – Madeke (km 125)*** zimekamilika na Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi. Kazi za ujenzi wa barabara ya ***Igawa – Mbarali – Ubaruku (km 16)***; sehemu ya ***Mbarali – Ubaruku (km 8.9)*** zinaendelea ambapo kilometra 6.3 zimekamilika kwa kiwango cha lami. Kuhusu barabara ya ***Iringa – Ruaha National Park (km 104)*** mradi huu umeainishwa katika miradi itakayofadhiliwa na Benki ya Dunia kupitia mradi wa *Development Corridors Transport Project*. Mapitio ya tathmini ya athari za mazingira pamoja na mali zitakazoathirika na –ujenzi wa barabara hii yanaendelea. Aidha, taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya ***Mafinga – Mgololo (km 78)*** zinaendelea. Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya ***Igawa – Songwe – Tunduma (km 218)*** ikijumuisha barabara ya ***mchepuo ya Mbeya (Uyole – Songwe: km 40)*** inaendelea chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia.

69. Mheshimiwa Spika, Benki ya Dunia imeonyesha nia ya kugharamia ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara ya ***Makambako – Songea*** chini ya programu ya *Development Corridor Transport Program (DCTP)*. Hadi Machi, 2019

maandalizi ya utekelezaji wa programu hii yalikuwa yanaendelea. Kuhusu barabara ya **Mbeya – Makongolosi (km 115)**, kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya **Chunya – Makongolosi (km 43)** zimefikia asilimia 20.6. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya **Makongolosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa** (km 413).

70. Mheshimiwa Spika, mradi wa ukarabati wa barabara ya **Korogwe – Mkumbara – Same (km 172)** umekamilika. Serikali inaendelea na taratibu za kulipa madai ya Mkandarasi aliyetekeleza mradi huu. Kuhusu mradi wa barabara ya **Chalinze – Segera – Tanga**, Serikali inaendelea na taratibu za kumtafuta Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya **Amani – Muheza (km 36)** ambapo zabuni za ujenzi zimefunguliwa na uchambuzi unaendelea.

71. Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya **Handeni – Kibereshi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboloti – Mrrijochini – Dalai – Bicha – Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro – Singida (km 460)**, mradi huu umepitishwa na Wakuu wa Nchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kama mradi wa kipaumbele kutokana na umuhimu wa barabara hii kwa ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Tanga hadi Hoima (Uganda) na hivyo unatafutiwa fedha kupitia Jumuiya hiyo. Aidha, kuhusu barabara ya **Dodoma – Mtera – Iringa (km 260)**, malipo ya fidia yamefanyika na eneo la ujenzi wa barabara ya mchepuo wa Iringa (km 7.3) limetambuliwa. Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa barabara hii kutoka kwa Washirika mbalimbali wa Maendeleo. Aidha, taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya **Mchepuo wa Babati (Babati Bypass: km 12)** zinaendelea kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

72. Mheshimiwa Spika, mradi wa barabara ya **Itoni – Ludewa – Manda** unalenga kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami na zege. Hadi Machi, 2019, kazi ya ujenzi kwa kiwango cha zege kwa sehemu ya **Lusitu – Mawengi (km 50)** imefikia asilimia 20.14. Kuhusu ujenzi wa barabara ya **Masasi – Songea – Mbamba Bay** na **Masasi – Newala – Mtwara**, ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya **Mbinga – Mbamba Bay (km 66)** umefikia asilimia 8.2 na barabara ya **Mtwara – Newala – Masasi (km 210)**, sehemu ya Mtwara – Mnivata (km 50) kwa kiwango cha lami umefikia asilimia 42.7. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya **Masasi – Nachingwea – Nanganga (km 91)** imekamilika na Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii. Aidha, kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya **Nanganga – Ruangwa – Nachingwea (km 107)** zimekamilika. Kwa upande wa ujenzi wa barabara ya **Likuyufusi – Mkenda (km 122.5)**, taratibu za kufanya mapitio ya usanifu wa kina na nyaraka za zabuni zilizotayarishwa mwaka 2013 zinaendelea kabla ya kutangaza zabuni. Mkataba wa ujenzi wa barabara ya **Kitahi – Lituhi (km 90)** umesainiwa. Benki ya Dunia imeonyesha nia ya kugharamia ukarabati wa barabara ya **Mtwara – Mingoyo – Masasi (km 200)** kwa kiwango cha lami chini ya programu ya *Development Corridor Transport Program (DCTP)* ambapo maandalizi ya utekelezaji wa programu hii yanaendelea. Kwa barabara ya **Nachingwea – Liwale (km 130)** hadi Machi, 2019 mkataba kwa ajili ya kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ulikuwa umesainiwa.

73. Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa barabara ya mchepuo kutoka barabara ya Bagamoyo kuingia kwenye **Chuo cha Uongozi cha Bagamoyo** pamoja na barabara za ndani ya Chuo hicho, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenziwa barabara hizo. Kuhusu ujenzi wa **Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili hadi ya Tano**, hadi Machi, 2019, mkataba wa ujenzi wa barabara za Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili ulikuwa umesainiwa kwa *Lot 1* (barabara) na *Lot 2* (majengo) chini ufadhlili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Aidha, usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni unaendelea kwa mradi wa

BRT Awamu ya Tatu chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia na Serikali inaendelea na maandalizi ya ujenzi wa Mradi wa BRT awamu ya nne na tano.

74. Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) pamoja na Ofisi za Mikoa ya Dar es Salaam, Katavi, Geita, Simiyu, Njombe, Lindi na Songwe, hadi Machi, 2019 ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Wakala wa Barabara Njedengwa, Dodoma ulikuwa unaendelea. Aidha, utekelezaji wa miradi ya majengo ya Ofisi za TANROADS katika mikoa ya Dar es Salaam, Katavi, Geita, Simiyu, Njombe na Lindi unasubiri upatikanaji wa fedha.

75. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya barabara kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Kazi zillzopangwa kutekelezwa katika Barabara Kuu kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ni kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa **kilometra 3,586.8** za barabara ambapo hadi Machi, 2019 utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

i) Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo/ Benaco (km 183.1) – Sehemu ya Bugene– Kasulo/Benaco (km 124)

Kazi za Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina zilikuwa zimekamilika. Aidha, Mhandisi Mshauri anaendelea kufanya mapitio ya usanifu chini ya Benki ya Maendeleo ya Afrika kuititia Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa sehemu ya Kumunazi – Kasulo (km 9), Kasulo – Bugene (km 124) na Kyaka – Mutukula (km 30) ili iweze kugharamia ujenzi wake kuititia Jumuiya ya Afrika Mashariki.

ii) Barabara ya Handeni – Kiberashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboloti – Mrijo Chini – Dalai – Bicha – Chambalo – Chemba – Kwamtoro – Singida (km 460)

Kazi ya usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni imekamilika. Serikali kuititia Jumuiya ya Afrika Mashariki inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii.

iii) Kufanya Mapitio na Kuandaa Miongozo (Standards and

Specifications)

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri atakayefanya mapitio ya miongozo mbalimbali ya kufanya Usanifu wa barabara zilizoandaliwa miaka ya 1999 na 2000 zimekamilika. Aidha, maandalizi ya kupata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi hiyo yanaendelea.

iv) Barabara ya Musoma – Makojo – Busekela (km 92)

Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika na taratibu za manunuzi za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya barabara hii kwa kiwango cha lami zinaendelea.

v) Barabara za Juu (TAZARA na Ubungo)

Kazi ya uhamishaji wa miundombinu iliyoathiriwa na mradi wa *Ubungo Interchange* imekamilika na Mkandarasi anaendelea na kazi za ujenzi wa barabara za makutano.

vi) Barabara ya Kolandoto – Lalago – Mwanhuzi – Matala – Oldeani Junction (km 328)

Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika.

vii) Barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Mto Sibiti – Lalago – Maswa (km 389)

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa barabara hii zinaendelea na zinatarajiwaa kukamilika Juni, 2019.

viii) Barabara ya Isyonje – Kikondo – Makete (km 96.2)

Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zinaendelea.

ix) Kuimarisha Uwezo wa Maabara (Central Material Laboratory – CML) katika Kupima Vifaa vya Ujenzi na Kuanzisha Teknolojia ya Kisasa ya ‘Asphalt Mix Design’

Ununuzi wa vifaa vya maabara unaendelea na Mwongozo wa Uchanganyaji Lami umekamilika na umeanza kutumika.

x) Barabara ya Nyamirembe Port – Katoke (km 50)

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zimekamilika.

xii) Daraja la Kigongo/Busisi katika Barabara ya Usagara - Geita

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika. Mradi huu uko kwenye taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi.

xiii) Mpanda - Ugalla - Kaliua - Ulyankulu - Kahama (km 457)

Taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

xiv) Barabara ya Ipole - Rungwa (km 172)

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika.

xv) Barabara ya Mtwara Pachani - Lusewa - Lingusenguse - Nalasi (km 211)

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

xvi) Barabara ya Arusha - Kibaya - Kongwa (km 430)

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

xvii) Barabara ya Kibada - Tundwisongani/ Kimbiji Junction - Kimbiji (km 40.4) Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

xviii) Barabara ya Chekeni Mwasonga - Kimbiji/ Tundwisongani Junction (km 8.3)

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

xix) Barabara ya Kibada - Mwasonga - Kimbiji (km 19.2)

Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inaendelea.

xx) Barabara ya Nanganga - Ruangwa - Nachingwea (km 91):

Kazi za upembuzi yakinifu na Usanifu wa Kina imekamilika.

xxi) Daraja la Mlalakuwa

Ujenzi wa daraja la Mlalakuwa ulikuwa umekamilika.

xxii) Kuboresha Eneo la Mlima Kitonga (km 10)

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

xxiii) Barabara ya Shabiby – Arusha/Dodoma Round About (km 1.6)

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

xxiv) Barabara ya Chimwaga – Chinyoya – Kikuyu (Dodoma Roundabout) (km 6.5)

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

xxv) Barabara ya Dar es Salaam Road (Nanenane) – Miyuji (Arusha Road) – Mkonze (km 23)

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

xxvi) Barabara ya Emmaus – Mlimwa – Wajenzi (km 5)

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

xxvii) Dodoma Outer Ring Road / Dodoma Bypass (Mtumba - Veyula - Nala - Matumbulu - Mtumba: km 104)

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

xxviii) Barabara ya Ngaresh – Enguik (Monduli Juu) (km 104)

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

xxix) Uchunguzi wa Kina wa Chanzo cha Mafuriko Eneo la Kibaigwa katika Barabara ya Morogoro - Dodoma

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya uchunguzi wa kina wa chanzo cha mafuriko eneo la Kibaigwa zinaendelea.

xxx) Uchunguzi wa Kina Kuhusu Chanzo cha Mafuriko na Kupata Ufumbuzi wa Kudumu Kwenye Daraja la Mkundi

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi

Mshauri wa kufanya kazi hii zinaendelea.

xxxij) Barabara ya Dareda - Dongobeshi (km 60)

Taratibu za manunuzi kwa ajili kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

xxxii) Barabara ya Soni – Bumbuli - Dindira - Korogwe (km 70)

Taratibu za manunuzi kwa ajili kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

xxxiii) Barabara ya Kibaoni – Majimoto - Inyonga (km 152)

Taratibu za manunuzi kwa ajili kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

xxxiv) Barabara ya Kiranjeranje – Namichiga - Ruangwa (km 120)

Mkataba kwa ajili ya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umesainiwa.

xxxv) Barabara ya Masaninga – Matandu – Nangurukuru – Kilwa Masoko (km 55)

Mkataba kwa ajili ya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa Kina umesainiwa.

xxxvi) Barabara za Mwambao wa Ziwa Tanganyika (km 275)

Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Dunia. Taratibu za manunuzi ya Mhandisi Mshauri wa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinasubiri idhini (No Objection) ya Benki ya Dunia ya kuanza kazi hiyo.

xxxvii) Barabara za Mwambao wa Ziwa Victoria (km 44.6)

Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Dunia. Taratibu za manunuzi ya Mhandisi Mshauri wa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinasubiri idhini (No Objection) ya Benki ya Dunia ya kuanza kazi hiyo.

xxxviii) Barabara ya Sabasaba – Sepuka – Ndago – Kizaga

(km 77)

Taratibu za manunuzi kwa ajili kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

xxxix) Barabara ya Singida Urban – Iliongero – Haydom (km 93)

Taratibu za manunuzi kwa ajili kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

xl) Daraja la Mpiji Chini na Barabara za Maingilio (km 1.7)

Taratibu za manunuzi ya Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko, Maegesho ya Vivuko na Matengenezo ya Magari

76. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara kupitia Wakala wa Ufundu na Umeme (TEMESA) ilipanga kuendelea na ujenzi wa maegesho mbalimbali nchini ikiwemo upanuzi wa eneo la maegesho ya Kigamboni katika kivuko cha Magogoni - Kigamboni; maegesho ya Bwina, Bukondo na Zumacheli katika kivuko cha Chato – Nkome; maegesho ya kivuko cha Nyamisati - Mafia na ujenzi wa jengo la abiria na ofisi katika kivuko cha Lindi – Kitunda. Kazi nyiningine zilizopangwa ni manunuzi ya vivuko vipyta vya Kigongo - Busisi, Nyamisati - Mafia na kukamilisha manunuzi ya kivuko cha Magogoni – Kigamboni (MV Kazi). Aidha, Wakala ulipanga kuendelea na ukarabati wa vivuko MV Pangani II, MV Sengerema, MV Kigamboni, MV Misungwi pamoja na manunuzi ya vitendea kazi vya karakana za TEMESA kwa ajili ya kuboresha huduma ya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo ya Serikali.

77. Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2019 miradi ya upanuzi wa eneo la maegesho ya Kigamboni (awamu ya kwanza inayohusisha upanuzi wa jengo la abiria) na ujenzi wa maegesho ya Bwina katika kivuko cha Chato – Nkome

imekamilika. Ujenzi wa jengo la abiria, ofisi na vyoo katika kivuko cha Lindi – Kitunda Mkoani Lindi umefikia asilimia 80. Aidha, nyumba tano (5) zimebomolewa kwa ajili ya upanuzi wa maegesho ya Kigamboni baada ya watusika kulipwa fidia. Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa kujenga maegesho ya Nyamisati - Mafia zinaendelea.

78. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu miradi ya ujenzi wa vivuko, kazi za ujenzi wa kivuko kipyä cha Magogoni – Kigamboni na kivuko kipyä cha Kigongo – Busisi imekamilika, vivuko hivyo vinatoa huduma katika maeneo husika. Aidha, Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa Kivuko kipyä cha Nyamisati – Mafia amepatikana na anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi.

79. *Mheshimiwa Spika*, , kwa upande wa ukarabati wa vivuko, ukarabati wa MV Pangani II umekamilika; ukarabati wa MV Sengerema umefikia asilimia 40, ukarabati wa MV Kigamboni umefikia asilimia 40 na ukarabati wa Kivuko MV Utete umefikia asilimia 90. Aidha, Wizara kuititia TEMESA ipo katika hatua za mwisho za kumpata Mkandarasi wa kufanya ukarabati mkubwa wa MV Misungwi.

Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali

80. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara kuititia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ilipanga kuendelea na ujenzi na ukarabati wa majengo ya Serikali nchi nzima. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa Ikulu ya Chamwino, nyumba 50 kwa ajili ya makazi ya Viongozi na nyumba 4 za Majaji katika mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Kilimanjaro na Shinyanga na Ukarabati wa nyumba 150 za Serikali. Kazi nyingine ni ununuzi wa samani kwa ajili ya nyumba za Viongozi wa Serikali; ujenzi wa nyumba katika kambi ya mradi wa kufua umeme Mto Rufiji; ujenzi wa nyumba 644 za makazi eneo la Magomeni (Magomeni Quarters); ukarabati wa nyumba 512 za watumishi zilizohamishiwa TBA kutoka CDA na TAMISEMI; ujenzi wa karakana mpya ya TEMESA ya kisasa mkoani Dodoma; ujenzi wa karakana mpya

za TEMESA katika mikoa ya Songwe, Simiyu, Geita, Katavi na Njombe; ukarabati wa karakana 5 za kanda za TEMESA katika mikoa mitano ya Dar es Salaam-M.T Depot, Mbeya, Mtwara, Arusha na Mwanza; pamoja na kuwajengea uwezo wataalam wa fani za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi.

81. *Mheshimiwa Spika*, hadi Machi, 2019, miradi iliyotekelizwa na Wizara kupitia Wakala wa Majengo Tanzania ni pamoja na Ujenzi wa Ikulu ya Chamwino, ambao unaendelea; ujenzi wa nyumba za Majaji nne (4) katika mikoa ya Dar es Salaam (1), Kilimanjaro(1), Mtwara (1), na Shinyanga (1) ambao upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji; Ujenzi wa nyumba katika kambi ya kufua umeme ya Mto Rufiji uliendelea ambapo jumla ya nyumba 21 kati ya 28 zimekamilika na kukabidhiwa na nyumba 7 zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji; Ujenzi wa nyumba 644 za makazi eneo la Magomeni (Magomeni Quarters) unaendelea. Miradi mingine ni ukarabati wa majengo na nyumba kwa ajili ya makazi ya Viongozi mkoani Dodoma na Watumishi wa Serikali ambayo inaendelea kutekelezwa.

82. *Mheshimiwa Spika*, hadi kufikia Machi, 2019 Wizara pia kupitia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) imesimamia Ujenzi wa ofisi za Wizara 21 na Taasisi za Umma 3 katika Mji Mpya wa Serikali – Mtumba jjini Dodoma ambao upo katika hatua za mwisho za ukamilishaji.

Usalama Barabarani na Mazingira

83. *Mheshimiwa Spika*, Wizara inaendelea kuratibu shughuli za usalama barabarani na kudhibiti uzito wa magari yanayotumia barabara. Kazi zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2018/19 ni ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi katika maeneo ya Nyakanazi na Manyoni, Ukaguzi wa usalama wa barabara, ujenzi wa mizani ya kisasa ya kupima magari yakiwa kwenye mwendo mdogo Dar es Salaam (Slow Weigh in Motion Weighbridge), ujenzi wa miundombinu na uwekaji wa mfumo wa Upatikanaji na Utoaji Taarifa za Ajali Barabarani katika vituo vya Polisi nichini pamoja na kuweka mfumo wa kudhibiti mwendokasi kwa vyombo vya usafiri

barabarani katika barabara kuu nchini.

84. Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2019 ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi (One Stop Inspection Station – OSIS), Wizara imekamilisha malipo ya fidia katika Ushoroba wa Kati (Central Corridor) katika maeneo ya Manyoni na Nyakanazi na kazi ya ujenzi katika vituo hivi imeanza na imefikia asilimia 60. Kwa upande wa ujenzi wa mizani ya kisasa ya upimaji wa magari yakiwa kwenye mwendo mdogo mijini, kazi ipo kwenye taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa kujenga mizani ya aina hiyo kwa mkoaa wa Dar es Salaam. Aidha kazi ya uwekaji wa kamera za udhibiti mwendo barabarani katika maeneo ya Bwawani na Ubena Zomozi imekamilika kwa asilimia 95.

Kwa upande wa mazingira, Wizara inaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 katika Sekta ya Ujenzi. Ukaguzi wa mazingira umefanyika kwa miradi ya barabara katika mikoa ya Songwe, Rukwa, Kilimanjaro, Tanga, Geita na Mwanza na kujiridhisha na utekelezaji wa sheria hiyo na kanuni za Tathmini ya Athari kwa Mazingira za mwaka 2005 zinazingatiwa na Wahandisi, Wataalam Washauri na Makandarasi. Aidha, maandalizi ya Mfumo wa TEHAMA wa ukusanyaji wa Taarifa za usimamizi wa mazingira katika sekta ya Ujenzi yanaendelea kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

MIRADI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA VIWANJA VYA NDEGE

85. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/19, utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu ya viwanja vya ndege ni kama ifuatavyo:

i) Katika miradi ya ujenzi wa **Viwanja vya Ndege vya Kigoma, Sumbawanga, Tabora na Shinyanga**, Wahandisi Washauri wa kusimamia kazi hizo wamepatikana. Mikataba kwa ajili ya ujenzi wa Viwanja vya Ndege vya Sumbawanga, Tabora na Shinyanga imeshasainiwa na Serikali inasubiri idhini (No Objection) kutoka kwa Benki ya Uwekezaji ya Ulaya

(European Investment Bank – EIB) kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa miradi hiyo. Aidha, Wizara inasubiri idhini kutoka EIB kwa ajili ya kukamilisha taratibu za manunuzi ya kumpata Mkandarasi atakayetekeliza kazi zilizopangwa katika mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kigoma.

ii) Katika mradi uliokamilika wa ujenzi wa **Kiwanja cha Ndege cha Mpanda** Serikali inaendelea na taratibu za kulipa madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa mradi huu.

iii) Kuhusu mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Songwe**, kazi zilizopangwa zilikuwa ni kuendelea na ujenzi wa jengo la abiria pamoja na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege. Kazi nyingine ni ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka ndege na barabara ya kiungio pamoja na ukarabati wa eneo la usalama kwenye barabara ya kutua na kuruka ndege (Runway End Safety Area – RESA).

Zabuni za manunuzi ya Mkandarasi kwa ajili ya ukarabati wa tabaka la juu la barabara ya kutua na kuruka ndege zimefunguliwa na uchambuzi unaendelea. Aidha, Mkandarasi kwa ajili ya kazi ya usimikaji wa taa za kuongozea ndege amepatikana na utekelezaji wa mradi huo unatarajiwu kuanza mwishoni mwa mwezi Mei, 2019. Kuhusu ujenzi wa jengo la abiria, Serikali imesitisha mkataba na Mkandarasi aliyekuwa anatekeleza mradi huu kutoptera na kushindwa kutekeleza matakwa ya mkataba wa kazi. Taratibu za kumpata Mkandarasi mwingine atakayemalizia ujenzi wa jengo hilo zinaendelea.

iv) Katika mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Mwanza**, kazi zilizopangwa ni kuanza ujenzi wa jengo jipya la abiria, kuendelea na upanuzi wa njia ya kutua na kuruka ndege, maegesho ya ndege, ujenzi wa jengo la mizigo, uzio wa kiwanja pamoja na maegesho ya ndege za mizigo. Aidha, kazi nyingine ni ujenzi wa jengo la kuongozea ndege, kituo cha kupozea umeme, maegesho ya magari, kusimika taa za kuongozea ndege na ujenzi wa mfumo wa kuondoa maji ya mvua kiwanjani.

Hadi Machi 2019, kazi za ukarabati na upanuzi wa njia ya

kuruka na kutua ndege, maegesho ya ndege, ujenzi wa jengo la mizigo (Cargo Terminal) pamoja na maegesho ya ndege za mizigo, jengo la kuongozea ndege, kituo cha kupooza umeme, maegesho ya magari, kusimika taa za kuongozea ndege na mfumo wa maji safi, maji taka na maji ya mvua zimetekelawa kwa asilimia 87. Aidha, Serikali inaendelea na majadiliano na Washirika wa Maendeleo mbalimbali ili kupata fedha za ujenzi wa jengo la abiria.

v) Kuhusu mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Arusha** kazi zilizopangwa ni kukamilisha usanifu wa kina kwa ajili ya upanuzi wa jengo la abiria, maandalizi ya usanifu wa kazi ya kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege kwa mita 200 na ujenzi wa maeneo ya kugeuzia ndege (Turning Pads). Kazi nyine ni ujenzi wa uzio wa kiwanja cha ndege, barabara mpya ya kuingilia kiwanjani pamoja na kukarabati maegesho ya magari. Hadi Machi, 2019, kazi ya Usanifu wa Kina kwa ajili ya uboreshaji wa jengo la abiria ilikuwa imekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kawa ajili ya kutekeleza kazi nyine zilizopangwa.

vi) Kuhusu mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Mtwara**, kazi zilizopangwa ni kufanya ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, viungio pamoja na maegesho ya ndege. Kazi nyine ni kusimika taa na mitambo ya kuongozea ndege pamoja na ujenzi wa barabara ya kuingilia kiwanjani na maegesho ya magari. Kazi za ukarabati wa kiwanja hicho zimeanza.

vii) Kwa upande wa mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro**, kazi zilizopangwa ni kufanya usanifu wa kina na kuanza ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, ujenzi wa barabara mpya ya kiungio, usimikaji wa taa za kuongozea ndege na ukarabati wa maegesho ya magari. Taratibu za manunuzi ya Mhandisi Mshauri kwa ajili ya usanifu wa kina wa ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka ndege zinaendelea.

viii) Kuhusu mradi wa **Uendelezaji wa Viwanja** vya Ndege vya **Mikoa** kazi zilizopangwa ni pamoja na ujenzi wa viwanja vya ndege vya mikoa vya Geita, Iringa, Ruvuma, Lindi, Tanga, Mara, kiwanja kipyä cha Mkoa wa Simiyu pamoja na kiwanja cha Lake Manyara. Aidha, kazi nyingine ni kuendelea na ukarabati wa viwanja vya ndege katika mikoa mingine na kukarabati jengo la abiria pamoja na kumalizia ulipaji wa fidia kwenye kiwanja cha ndege cha Dodoma.

Hadi Machi, 2019, ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, barabara ya kiungio, maegesho ya ndege kwenye kiwanja cha ndege cha Geita umefikia asilimia 72. Taratibu za manunuzi ya Mkandarasi kwa ajili ya ukarabati wa kiwanja cha Musoma zipo kwenye hatua za mwisho. Mkataba kwa ajili ya ukarabati wa kiwanja cha Songea umesainiwa na maandalizi ya ukarabati yanaendelea. Taratibu za manunuzi ya makandarasi kwa ajili ya viwanja vya Iringa, Lake Manyara na Tanga zinasubiria mkopo kutoka Benki ya Dunia. Hata hivyo, Serikali imeamua kuanza ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Iringa kwa fedha za ndani wakati taratibu za kupata mkopo kutoka Benki ya Dunia zikiendelea. Zabuni ya manunuzi ya Mkandarasi kwa ajili ya ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Iringa inatarajiwा kutangazwa mwishoni mwa mwezi Aprili, 2019. Aidha, ukarabati wa jengo la abiria la kiwanja cha ndege cha Dodoma ulikuwa umekamilika.

ix) Kwa upande wa ujenzi wa **Kiwanja cha Ndege cha Msalato**, kazi zilizopangwa ni kuendelea na usanifu wa kina na kuanza maandalizi ya ujenzi wa kiwanja kipyä cha Msalato mkoani Dodoma. Aidha, kazi nyingine ni kulipa fidia kwa mali zitakazoathiriwa na utekelezaji wa mradi huu.

Hadi Machi, 2019, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zinaendelea na zimefikia asilimia 75. Aidha, Mhandisi Mshauri anafanya mapitio ya usanifu wa kina uliofanyika awali ili kujumuisha maoni ya Benki ya Maendeleo ya Afrika ambayo imeonyesha nia ya kufadhili awamu ya kwanza ya mradi huo. Kazi zitakazofanyika zinahusisha ujenzi wa njia ya kuruka na kutua ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege na kituo cha uangalizi wa hali ya hewa, ujenzi wa kituo cha kupooza umeme na uzio.

x) Kuhusu **Kiwanja cha Ndege cha Bukoba**, kazi zilizopangwa zilikuwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la watu mashuhuri (VIP Lounge), usanifu wa kina kwa ajili ya kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege pamoja na ufungaji wa taa za kuongozea ndege. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

xi) Utekelezaji mradi wa ujenzi wa **Jengo la Tatu la Abiria (Terminal III)** katika **Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA)** umefikia asilimia 96 na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Mei, 2019.

UTENDAJI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA SEKTA YA UJENZI

Bodi ya Mfuko wa Barabara

86. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/19, Mfuko wa Barabara ulitarajia kukusanya jumla ya Shilingi **908,800,000,000** kwa ajili ya matengenezo ya barabara nchini. Kati ya fedha hizo, Shilingi **636,166,000,000** ni kwa ajili ya matengenezo ya barabara za kitaifa (Barabara Kuu na Barabara za Mikoa) ambazo husimamiwa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Shilingi **272,642,000,000** zilitengwa kwa ajili ya kugharamia barabara za Wilaya ambazo husimamiwa na Ofisi ya Rais -TAMISEMI. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019, Bodi ilikuwa imekusanya na kugawanya kiasi cha jumla ya Shilingi **577,164,474,585.16**. Kati ya hizo Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ilipokea Shilingi **40,054,085,391.94**, TANROADS ilipokea Shilingi **360,486,768,527.44**; Ofisi ya Rais- TAMISEMI ilipokea Shilingi **17,166,000,618.44**; TARURA Shilingi **154,494,005,565.93** na Bodi ya Mfuko wa Barabara ilipokea Shilingi **4,963,614,481.41**.

87. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha usimamizi wa mapato ya Mfuko, Bodi ya Mfuko wa Barabara kwa kushirikiana na TANROADS na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imekamilisha kuweka mfumo wa kieletroniki wa ukusanyaji mapato yatokanayo na faini kwa magari yanayozidisha uzito (ePayment System for Overloading Fees). Mfumo huu ni wa pili kukamilika baada ya ule wa kutoa vibali

vya mizigo isiyo ya kawaida (ePermit) ambayo imeunganishwa kwenye Mfumo wa malipo wa Serikali (GePG). Aidha, ili kuimarisha uwajibikaji na kuongeza uwazi katika shughuli zinazofanyika kwenye vituo vya mizani, Bodii kwa kushirikiana na TANROADS na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imeendelea na uwekaji mfumo wa kielektroniki na kamera za CCTV kwenye vituo 13 vya mizani vya kupimia uzito wa magari. Vituo hivyo ni Vigwaza (2), Mikese (2), Makuyuni (1), Nala (1), Njuki (1), Usagara (1), Himo (2), Mikumi (1), Mingoyo (1) na Mutukula (1). Mfumo huo utawezesha Taasisi husika kufutilia moja kwa moja, kwa wakati husika (real time) jinsi upimaji wa magari unavyoendelea kwenye vituo vya mizani nchini. Pamoja na kujua magari yaliyozidisha uzito na faini iliyotozwa muda ule ule.

88. *Mheshimiwa Spika*, Bodii imemteua Mtaalam Mshauri kufanya utafiti na kuangalia uwezekano wa kurekebisha mgawanyo wa fedha za Mfuko (Allocation Formula) kati ya zile zinazopelekwa kwenye mtandao wa barababara za Kitaifa na zile za Wilaya. Kazi hiyo inatarajiwaa kukamilika Juni, 2019. Vilevile, Bodii ilifanya ukaguzi wa ubora wa kazi za matengenezo ya barabara katika mikoa yote Tanzania Bara pamoja na kufanya ufuutiliaji wa mapato ya Mfuko na kutathmini ubora wa njia zinazotumiwa kukusanya mapato.

Wakala wa Majengo Tanzania

89. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2018/19, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ulipanga kuendelea na ujenzi na ukarabati wa majengo ya Serikali katika mikoa mbalimbali nchi nzima. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa lkulu ya Chamwino jijini Dodoma, ujenzi wa nyumba 50 kwa ajili ya makazi ya Viongozi na nyumba 4 za Majaji katika mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Kilimanjaro na Shinyanga; ujenzi wa nyumba katika Kambi ya mradi wa kufua umeme Mto Rufiji na ujenzi wa nyumba 644 za makazi eneo la Magomeni (Magomeni Quarters). Kazi nyingine ni ukarabati wa nyumba 150 za Serikali, nyumba 431 zilizohamishiwa TBA kutoka CDA na nyumba 81 za TAMISEMI, na Ukarabati wa Shule Kongwe 10 za Sekondari.

90. Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2019, miradi iliyotekelizwa na Wakala wa Majengo ni pamoja na Ujenzi wa Ikulu ya Chamwino-Dodoma ambao unaendelea; ujenzi wa nyumba za Majaji nne (4) katika mikoa ya Dar es Salaam (1), Kilimanjaro(1), Mtwara (1), Shinyanga (1) ambapo ujenzi wa nyumba hizi upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji; ujenzi wa nyumba katika kambi ya kufua umeme ya Mto Rufiji uliendelea ambapo jumla ya nyumba 21 kati ya 28 zimekamilika na kukabidhiwa na nyumba 7 zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na ujenzi wa nyumba 644 za makazi eneo la Magomeni Kota (Magomeni Quarters) unaendelea. Miradi mingine ya ukarabati wa majengo na nyumba kwa ajili ya makazi ya Viongozi mkoani Dodoma na Watumishi wa Serikali inaendelea kutekelezwa.

91. Mheshimiwa Spika, Wakala wa Majengo Tanzania pia umeendelea na ujenzi wa miradi ya majengo ya ofisi za Halmashauri ya Mji wa Handeni, Halmashauri ya Butiama, Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu; ujenzi katika Mkoa wa Njombe wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, makazi ya Mkuu wa Mkoa na makazi ya Katibu Tawala; ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe; ujenzi wa makao makuu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) Dodoma; na ujenzi wa jengo la Wakala wa Misitu Tanzania mkoa wa Dodoma.

92. Mheshimiwa Spika, Vile vile Wakala wa Majengo Tanzania uliendelea kutekeleza Miradi mbalimbali ya Washitiri ikiwemo Mradi wa Ujenzi wa jengo la Maabara ya Tanzania *Atomic Energy Commission* Njiro, Arusha, Ujenzi wa Jengo la Maktaba ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), ujenzi wa Chuo cha Muhimbili Kampasi ya Mloganzila (MUHAS) na Ukumbi wa kisasa wa Mihadhara wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ambao ulikamilika na kukabidhiwa kwa Mshiti. Aidha Wakala ulifanya ukarabati wa majengo ya shule kongwe nchini za Tosamaganga, Azania, Malangali, Jangwani, Kibaha, Minaki, Nangwa, Mirambo, Shule ya wasichana Songea, pamoja na shule ya sekondari Kigoma. Kazi katika mradi huu umekamilika kwa takribani asilimia 80.

93. Mheshimiwa Spika, Wakala pia ulifanya usanifu na ujenzi wa majengo mbalimbali ya Tasisi za afya kama vile, ujenzi wa jengo la x-ray katika Hospitali ya Rufaa Mbeya, ujenzi wa wodi ya upasuaji (theatre na surgical) katika hospitali ya Mkao wa Mbeya, ujenzi wa Hospitali ya Mkao Geita, ujenzi wa jengo la utawala /OPD hospitali ya Sekou Toure, Mwanza pamoja na ujenzi wa Hospitali ya Chato ambapo ujenzi wa majengo haya unaendelea vizuri na upo katika hatua mbalimbali. Aidha, mradi wa ujenzi wa Jengo la utawala/OPD hospital ya Mkao wa Simiyu ulikamilika na kukabidhiwa kwa mshitiri.

94. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2018/19, Wakala wa Majengo Tanzania ulifanya pia Usanifu na kusimimia Ujenzi wa ofisi za Wizara 21 na Taasisi za Umma 3 za Serikali katika Mji Mpya wa Serikali eneo la Mtumba jijini Dodoma ambazo ujenzi wake umekamilika.

Wakala wa Ufundu na Umeme Tanzania

95. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/19, Wakala wa Ufundu na Umeme Tanzania (TEMESA) ulipanga kufanya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo ya Serikali; kusimika na kufanya matengenezo ya mifumo ya umeme, elektroniki, majokofu na viyoyozi kwenye majengo ya Serikali na kutoa ushauri wa kihandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozi na majokofu katika nyumba za Serikali.

96. Mheshimiwa Spika, kuhusu vivuko, Wakala ulipanga kuendelea na upanuzi wa eneo upande wa Kigamboni kwa ajili ya kivuko cha Magogoni – Kigamboni; ujenzi wa maegesho ya Bwina, Bukondo na Zumacheli kwa ajili ya kivuko cha Chato - Nkome; ujenzi wa maegesho ya Mafia na Nyamisati kwa ajili ya kivuko cha Mafia – Nyamisati. Kazi nyingine ni ujenzi wa miundombinu (jengo la abiria, ofisi na uzio) kwa ajili ya kivuko cha Lindi - Kitunda, maegesho ya Kayenze na Bezi kwa ajili ya kivuko cha Kayenze - Bezi pamoja na maegesho ya Mlimba – Malinyi katika eneo la Kikove kwenye Mto Kilombero.

Wakala vilevile ulipanga kukamilisha malipo ya Kivuko MV Kazi kinachotoa huduma ya usafiri kati ya Magogoni - Kigamboni; kukamilisha ujenzi wa kivuko kipyä kitakachotoa huduma ya usafiri kati ya Kigongo-Busisi; ujenzi wa kivuko kipyä kitakachotoa huduma ya usafiri kati ya Nyamisati - Mafia; ujenzi wa kivuko kipyä kitakachotoa huduma ya usafiri kati ya Kayenze na Kisiwa cha Bezi mkoani Mwanza; ujenzi wa kivuko kipyä kitakachotoa huduma ya usafiri kati ya Chato, Nkome na Muhamamba Mkoani Geita; manunuzi ya vitendea kazi kwa ajili ya karakana za TEMESA na ujenzi wa karakana tano (5) mpya katika mikoa ya Songwe, Simiyu, Katavi, Geita na Njombe na kuanza ujenzi wa karakana ya kisasa Jijini Dodoma.

97. Mheshimiwa Spika, TEMESA pia ilipanga kukamilisha ukarabati wa vivuko vya MV Pangani II, MV Sengerema, MV Kigamboni, MV Utete na MV Misungwi pamoja na ukarabati wa karakana tano (5) za kanda katika mikoa ya Mwanza, Arusha, Mtwara, Mbeya na M.T. Depot.

98. Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2019 kazi zilizokamilika ni pamoja na awamu ya kwanza ya upanuzi wa maegesho ya Kigamboni, upanuzi wa jengo la kupumzikia abiria Kigamboni na ujenzi wa maegesho ya Bwina kwa ajili ya kivuko cha Chato-Nkome. Aidha, ujenzi wa miundombinu (jengo la kupumzikia abiria, ofisi na uzio) kwa ajili ya kivuko cha Lindi-Kitunda umefikia asilimia 80, Mkandarasi kwa ajili ya maegesho ya Mlimba - Malinyi anaendelea na kazi na maegesho ya Kayenze na Bezi ambayo yapo katika hatua ya usanifu. Kazi za ukarabati wa Kivuko MV Pangani umekamilika na ukarabati wa Vivuko MV Sengerema na MV Kigamboni zimefikia asilimia 40 na ukarabati wa Kivuko MV Utete umefikia asilimia 90.

99. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kivuko cha Kigongo - Busisi (MV Mwanza) umekamilika na kivuko hicho kinaendelea kutoa huduma ya usafiri tangu Julai, 2018; Makandarasi wa ujenzi wa vivuko vitakavyotoa huduma za usafiri kati ya Nyamisati - Mafia na Chato - Nkome wamepatikana na maandalizi ya kuanza kazi yanaendelea na ujenzi wa kivuko

kitakachotoa huduma ya usafiri kati ya Kayenze na Bezi unaendelea.

TEMESA imeendelea kutekeleza majukumu ya matengenezo ya magari ambapo hadi Machi, 2019 jumla ya magari **11,174** yalifanyiwa matengenezo. Aidha miradi **371** ya umeme, miradi **587** ya viyoyozi na miradi **37** ya kieletroniki imetekelozwa.

Bodi ya Usajili wa Wahandisi

100. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2018/19 hadi Machi, 2019, Bodi imesajili wahandisi **3,283** na Kampuni za ushauri wa kihandisi **17** na kufikisha jumla ya wahandisi waliosajiliwa katika ngazi mbalimbali kuwa **25,263** ambapo Wahandisi **23,157** ni wa ndani na **2,106** ni wa nje. Jumla ya kampuni za ushauri wa kihandisi zilizosajiliwa ni **338** ambapo kampuni za ndani ni **236** na za nje ni **102**. Katika kipindi hicho, Bodi ilifuta usajili kwa Wahandisi Watalaamu **407** ambapo, kati ya hao, wa ndani ni **180** na wa nje ni **227**. Jumla ya kampuni za ushauri wa kihandisi **66** zilifutiwa usajili kwa kukiuka Sheria ya Usajili wa Wahandisi ambapo kampuni za ndani ni **27** na kampuni za nje ni **39**. Aidha, katika kipindi hiki, jumla ya miradi **203** ilikaguliwa. Wahandisi wa kigeni **130** walibainika kufanya kazi bila usajili ambapo kati yao **110** walikuwa na sifa na hivyo walisajiliwa na **20** walikosa sifa hivyo hawakusajiliwa na wakarejeshwa kwao.

101. Mheshimiwa Spika, Bodi pia iliandaa warsha **4** katika kanda **4** kwa Wahandisi Wataalam wanaosimamia mafunzo kwa vitendo kwa wahandisi wahitimu. Vilevile, Bodi iliendelea kuwaapisha Wahandisi Wataalam Kiapo cha Utii kwa Taaluma (Professional Oath) ambapo jumla ya wahandisi **2,876** waliapishwa.

Aidha, Bodi iliendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo kwa Vitendo kwa wahandisi wahitimu **2,681**. Jumla ya wahandisi wahitimu **6,400** wameshapitia Mpango huu tangu uanzishwe mwaka 2003. Bodi iliandaa na kuadhimisha Siku ya Wahandisi 2018 (Annual Engineers' Day 2018) ambayo

ilihudhuriwa na wahandisi zaidi ya **3,500**. Mada ilijojadiliwa katika siku ya wahandisi ilikuwa ni *Miaka 50 ya Mchango wa Wahandisi kwenye Taifa letu pamoja na Mafanikio, Changamoto na Mikakati ya baadaye.*

Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi

102. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/19, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ilipanga kusajili Wataalamu **267** katika fani za Ubunifu Majengo, Ukadiriaji Majenzi na fani zinazoshabihiana nazo, ambapo wataalam **184** wamesajiliwa kufikia Machi, 2019. Aidha, Bodi ilipanga kusajili kampuni **17** za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi ambapo kampuni **9** zimesajiliwa. Vilevile, Bodi ilipanga kusajili miradi ya majengo **920** ambapo miradi ya majengo **522** imesajiliwa kufikia Machi, 2019. Bodi pia ilipanga kuwajengea uwezo wahitimu **132** katika fani za ubunifu majengo, ukadiriaji majenzi na fani zinazoshabihiana nazo kupitia mafunzo kwa vitendo ambapo wahitimu **112** wamepatiwa mafunzo hadi kufikia Machi, 2019.

103. Mheshimiwa Spika, Bodi ilipanga kufanya ukaguzi wa miradi ya ujenzi **2,300** katika mikoa yote ya Tanzania Bara ambapo miradi ya ujenzi **757** imekaguliwa kufikia Machi, 2019. Aidha, katika kutangaza huduma zake, Bodi iliendesha mashindano ya insha kwa wanafunzi wa kidato cha pili na mashindano ya kubuni nyumba zenye gharama nafuu kwa wananchi wenyе kipato cha chini.

Bodi ya Usajili wa Makandarasi

104. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/19, Bodi ilisajili makandarasi wapya **562** hivyo kufanya jumla ya makandarasi waliosajiliwa kufikia **10,072**. Aidha jumla ya miradi **3,262** ilikaguliwa. Miradi **764** sawa na asilimia **23** ilipatikana na mapungufu mbalimbali yakiwemo, kutozingatia afya na usalama kazini, kutosajili miradi na kufanya kazi za thamani inayozidi kiwango kinachoruhusiwa kwa daraja husika. Makandarasi waliokutwa na mapungufu walichukuliwa hatua mbalimbali kwa mujibu wa sheria

ikiwemo kutozwa faini, kupewa onyo, kusimamishwa kufanya biashara ya ukandarasi na kufutiwa usajili.

Bodi iliendesha kozi nne (4) za mafunzo kupitia Mpango Maalum wa Mafunzo Endelevu kwa Makandarasi (Sustainable Structured Training Programme – SSTOP) katika mikoa ya Morogoro, Arusha, Mwanza na Njombe. Jumla ya makandarasi **434** walishiriki katika mafunzo hayo. Bodi pia iliendelea kuendesha mfuko wa kusaidia makandarasi (CAF) unaotoa dhamana za zabuni na malipo ya awali kwa makandarasi wa ndani wa madaraja ya chini na ya kati ili kuwezesha ushiriki wa makandarasi wa ndani katika zabuni na utekelezaji wa miradi mbalimbali. Mfuko huu umeendelea kuwa na mtaji wa **Shilingi bilioni 3.6** kwa mwaka 2018/19. Aidha idadi ya wanachama wa Mfuko iliongezeka kutoka **1,667** mwaka 2017/18 hadi kufikia **1,711** mwaka 2018/19.

Baraza la Taifa la Ujenzi

105. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/19 Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC) lilitokeleza majukumu mbalimbali ikiwemo:

- i. Kuendelea na mapitio ya Sheria iliyoanzisha Baraza hilo (Cap 162, Revised Edition (R.E.) 2008) kwa lengo la kulihuisha Baraza hilo;
- ii. Kuratibu utekelezaji wa mfumo wa kukuza uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi ya umma (Construction Sector Transparency Initiative - CoST);
- iii. Kuratibu mafunzo mbalimbali kwa wadau wa sekta ya ujenzi kuhusu usuluhishi wa migogoro ya ujenzi, usimamizi wa mikataba na manunuzi ya huduma ya ushauri wa kiutaalam;
- iv. Kuendelea na tafiti kuhusu upimaji wa tija na ubora wa kazi katika Sekta ya Ujenzi na changamoto za ushindani wa makandarasi wa ndani katika kutekeleza miradi ya ujenzi ukilinganisha na makandarasi wa kigeni. Tafiti nyingine zililhusu kanuni za mikataba katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa

miundombinu na usimamizi wa miradi ya ujenzi wa miundombinu kwa utaratibu wa Sanifu na Jenga (Design and Build);

v. Kutoa ushauri wa kiufundi na kitaalam kwa wadau mbalimbali wa sekta ya ujenzi katika maeneo yanayohusu uimara wa majengo ya magorofa, mikataba ya ujenzi, madai (claims), mabadiliko ya bei, manunuzi na sheria zake kuhusiana na masuala ya ujenzi, usuluhishi wa migogoro, thamani ya mradi ikilinganishwa na gharama za ujenzi (value for money) na makadirio ya gharama za ujenzi;

vi. Kufanya tathmini ya gharama za ujenzi wa barabara za lami (Unit cost per km) baada ya kufanya mapitio ya miradi 21 iliyoteklezwa na TANROADS kati ya mwaka 2013 na 2017;

vii. Kuendelea kuandaa Viwango (Specifications) vya Ujenzi wa Nyumba za Serikali na Samani;

viii. Kufanya ukaguzi wa kiufundi wa miradi **186** ya ujenzi na ukarabati wa barabara kwenye mikoa ya Mbeya, Tabora na Arusha. Aidha, Baraza lilifanya ukaguzi wa kiufundi wa miradi **28** ya ujenzi wa majengo yenye thamani ya takribani ya **Shilingi bilioni 13.5**;

ix. Kuendelea kukusanya takwimu za Sekta ya Ujenzi kwa mwaka 2018/2019 kwa matumizi ya wadau wa sekta ya ujenzi na kufuatilia ukuaji wa sekta pamoja na kukusanya na kuandaa bei za vifaa vya ujenzi na "indices" kwa ajili ya matumizi ya mabadiliko ya bei (Price Fluctuation Formula). Ukusanyaji wa taarifa stahiki ulifanyika katika mikoa ya Mwanza, Dodoma na Dar es Salaam.

Vilevile, Baraza limeendelea kukusanya taarifa muhimu ili kuwezesha uchapishaji wa jarida la "Construction Business Journal" na "Directory of Construction Materials".

Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia Katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji (Tanzania Transportation Technology Transfer Centre)

106. Mheshimiwa Spika, Kituo hiki kilianzishwa kwa lengo la kuimarisha/ kuboresha sekta ya ujenzi na uchukuzi kwa ujumla kwa kutumia mbinu ya ukusanyaji na usambazaji wa teknolojia katika sekta ya ujenzi na uchukuzi kwa wadau.

Katika mwaka wa fedha 2018/19, Kituo kilifanya kazi zifuatazo:

- i) Kuandaa na kushiriki katika Mkutano wa Kimataifa kuhusu Mikakati ya uwekezaji katika Miundombinu katika sekta ya Barabara na Usafirishaji uliofanyika Arusha. Mkutano huo ullihudhuriwa na washiriki wapatao **190** kutoka nchi **22** duniani.
- ii) Kuendesha kozi mbili (**2**) za mafunzo ya muda mfupi yaliyofanyika Dodoma kwa wahandisi wa Wizara ya Ujenzi, Mfuko wa Barabara, TANROADS na TARURA.
- iii) Kuandaa nakala **300** za jarida la kituo lenye mada mbalimbali zinazohusu teknolojia, usalama barabarani na agenda mbalimbali za Serikali ya Awamu ya Tano katika kukuza miundombinu ya usafirishaji.
- iv) Kushiriki katika maandalizi ya mafunzo ya kimataifa kuhusu *International Training on Road Safety Engineering and Audit* iliyofanyika Dar es Salaam Agosti, 2018.
- v) Kuendelea kutoa huduma za maktaba ya kituo kuhusu Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji na kutekeleza mradi unaolenga kuboresha mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu na upashanaji wa habari za teknolojia.
- vi) Kuanza kwa utekelezaji wa kufundisha programu zinazohamasisha watoto wa shule za msingi na sekondari kupenda sayansi na masomo ya Uhandisi na Usafirishaji mashuleneni.

B.2 SEKTA YA UCHUKUZI

107. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Sekta ya Uchukuzi iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 2,387,031,678,278 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

108. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, Sekta ya Uchukuzi ilitengewa **Shilingi 86,292,678,278** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 57,828,541,000** ni fedha za Mishahara na **Shilingi 28,464,137,278** ni fedha za Matumizi Mengineyo kwa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Uchukuzi. Hadi kufikia Machi, 2019, kiasi cha fedha za Matumizi ya Kawaida kilichotolewa kwa Sekta ya Uchukuzi na Taasisizake ni **Shilingi 54,920,905,599** sawa na asilimia 63.6 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Bajeti ya Maendeleo

109. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Sekta ya Uchukuzi ilitengewa **Shilingi 2,300,739,000,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hadi Machi, 2019 Sekta ya Uchukuzi illikuwa imepokea **Shilingi 485,084,462,824.16** sawa na asilimia 21.08 ya fedha zote za Maendeleo. Aidha, mradi wa Ujenzi wa Reli ya *standard gauge* uliendelea kutumia fedha za Akaunti ya Amana (Deposit) zilizobaki katika mradi huo kwa mwaka 2017/2018 ambapo **Shilingi 556,561,013,252** zilitolewa kutoka kwenye Akaunti hiyo. Hivyo, kwa ujumla fedha zilizotumika katika utekelezaji wa miradi ni **Shilingi 1,041,645,476,076**.

HUDUMA ZA USAFIRI MIJINI NA VIJIJINI

Udhibiti wa Usafiri kwa Njia ya Barabara

110. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2018, usafiri na uchukuzi kwa njia ya barabara umeendelea kuimarika katika kufanikisha shughuli za kiuchumi na kijamii nchini. Huduma hizo zimeendelea kutolewa kwa kiasi kikubwa na sekta binafsi ambapo katika mwaka 2018/2019 usajili wa leseni za

usafirishaji wa abiria uliongezeka kutoka leseni 53,784 hadi 58,933 na leseni za malori kutoka 99,377 hadi 111,345 ikilinganishwa na mwaka 2017/2018. Ongezeko hili la leseni limetokana na mkakati wa kutoa leseni za muda mfupi.

111. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia SUMATRA imeendelea kudhibiti utoaji wa huduma za usafiri kwa njia ya barabara ili kupunguza ajali za magari yanayotoa huduma za usafiri wa Umma. Udhibiti huu ulihusu mwendokasi wa mabasi, ukaguzi wa leseni, faini kwa makosa ya madereva, elimu kwa umma na kutoa leseni za dharura katika kipindi cha msongamanowa abiria wa mikoani. Kuimarika kwa usimamizi wa huduma za usafiri kwa nchi kavu kwa kiasi kikubwa kumechangia kupungua kwa ajali za barabarani. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 kulikuwa na ajali za mabasi 15 ikilinganishwa na ajali 23 zilizotokea katika kipindi kama hicho katika mwaka 2017/2018 zilizohusisha mabasi ya mikoani. Aidha, SUMATRA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani imeendelea kusimamia na kudhibiti mwendokasi wa mabasi ya mikoani kwa kutumia Mfumo wa Ufuutiliaji Mwenendo wa Mabasi ya Masafa Marefu (Vehicle Tracking System - VTS). Hadi Machi, 2019, jumla ya mabasi 3,083 yaendayo mikoani yalikuwa yameunganishwa kwenye mfumo huo ikilinganishwa na mabasi 1682 yaliyokuwa yanatumia mfumo huu Machi, 2018.

112. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019, SUMATRA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi nchini imefanikiwa kupunguza ajali zinazotokana na mabasi ya abiria, magari ya mizigo na pikipiki kutoka ajali 1,471 hadi 1,001. Upungufu huu ni sawa na asilimia 32. Katika kipindi hicho, vifo vilivytokana na ajali za mabasi, malori na pikipiki pia vilipungua kwa asilimia 41 kutoka vifo 880 hadi vifo 520. Hata hivyo, asilimia 76 ya vyanzo vya ajali za barabarani ni makosa ya kibinadamu. Kwa kutambua hili, Wizara kupitia SUMATRA kwa kuanzia inaandaa mfumo rasmi wa kuwadhibiti madereva wa vyombo vya usafiri wa abiria na mizigo. Mfumo huu utahusisha kutoa vyeti vya weledi kwa madereva kwa kutumia mfumo wa TEHAMA na kuhakikisha kuwa ujuzi na mwenendo wa madereva unasimamiwa ipasavyo.

Udhibiti wa Usafiri kwa Njia ya Treni

113. Mheshimiwa Spika, SUMATRA imeendelea kudhibiti utoaji wa huduma za usafiri kwa njia ya reli kwa lengo la kuboresha huduma na usalama katika usafiri huo. Katika mwaka 2018/2019, SUMATRA imefanya kaguzi za usalama wa mabehewa na madaraja ya treni, ufuatiliaji wa vyanzo vya ajali za treni na umwagikaji wa mafuta katika njia za reli. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019, jumla ya ajali 3 za treni zilitokea maeneo ya Lumba, Mbeya na Kigoma. SUMATRA ilifuatilia vyanzo vya ajali hizo na kutoa maelekezo kwa Shirika la Reli (TRC) na Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) kuchukua hatua za kurekebisha kasoro zilizobainika. Kufikia Septemba 2018, TRC na TAZARA zilikuwa zimerekebisha kasoro hizo.

Usafiri wa Reli Jijini Dar es Salaam

114. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendela kuboresha huduma za usafiri wa reli katika Jiji la Dar es Salaam ili kupunguza msongamano wa magari barabarani. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi Februari, 2019, jumla ya abiria 1,524,381 walisafirishwa kwa njia ya reli kati ya stesheni za Dar es salaam na Mwakanga kwa kutumia reli za TAZARA. Aidha, katika kipindi kama hicho 2018 jumla ya abiria 1,603,256 walisafirishwa. Upungufu huu umechangiwa na kupungua kwa mabehewa na kufunguliwa kwa daraja la Mfugale. Kwa upande wa TRC, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019, abiria waliohudumiwa kati ya Stesheni - Ubungo - Pugu ni 5,431,037 ikilinganishwa na abiria 5,786,360 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2017/2018. Upungufu huu umetokana na mabadiliko ya mara kwa mara ya vituo vya treni ili kuruhusu ujenzi wa reli ya Standard Gauge (SGR). Aidha, ukamilishwaji wa daraja la Mfugale ulisaidia kupunguza msongamano wa magari kwenye barabara za Mandela na Nyerere.

Shirika la Reli Tanzania (TRC)

115. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa awamu ya kwanza ya Mradi

wa Reli ya kati kwa *Standard Gauge* kutoka Dar es salaam hadi Mwanza (Km 1,219), hususan kwenye vipande viwili vya awali, Dar es Salaam hadi Morogoro (Km 300) na Morogoro hadi Makutupora (Km 422) unaendelea kutekelezwa. Ujenzi wa kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro umekamilika kwa asilimia 45.8. Ujenzi wa kipande hiki unatarajiwa kukamilika Novemba, 2019 kulingana na mkataba. Kazi zilizotekeliza ni pamoja na:

- (i) Kutandika kilomita 30 za reli;
- (ii) Ujenzi wa makalvati kwa asilimia 55;
- (iii) Ujenzi wa madaraja kwa asilimia 42;
- (iv) Ujenzi wa daraja refu katikati ya Jiji la Dar es Salaam lenye urefu wa kilomita 2.54 ambaa umekamilika kwa asilimia 63;
- (v) Kazi ya ukataji wa miinuko na ujazaji wa mabonde (earthworks) umekamilika kwa asilimia 66;
- (vi) Kazi ya uwekaji wa nguzo za mfumo wa umeme kwa ajili ya kuendeshea treni inaendelea;
- (vii) Ujenzi wa stesheni za Dar es Salaam, Pugu na Soga unaendelea; na
- (viii) Kazi ya utwaaji wa ardhi imekamilika.

116. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu ujenzi wa reli sehemu ya Morogoro hadi Makutupora (km 422), kazi imekamilika kwa asilimia 7.12 na inatarajiwa kukamilika Februari, 2021. Kazi zinazoendelea kwa sasa ni pamoja na uthamini na uhakiki wa wananchi watakaopisha mradi, ukataji wa miinuko na ujazaji wa mabonde, usanifu wa njia na ujenzi wa kambi za Kilosa na Ihumwa. Aidha, zabuni za ununuzi wa vichwa vya treni, mabehewa na mitambo itakayotumika kutoa huduma ya usafiri kwenye reli ya *Standard Gauge* zimefunguliwa tarehe 7 Machi, 2019. Kazi ya kuchambua zabuni hizo imekamilika na majadiliano (negotiation) na mzabuni

yanaendelea. Kuhusu ujenzi wa mfumo wa umeme wa SGR, Desemba, 2018, Serikali kuititia TRC na TANESCO ilisaini Mkataba wa miezi 11 na Kampuni ya Larsen & Tourbo (L&T) Construction kwa ajili ya kuanza kazi hiyo. Hivi sasa Mkandarasi huyo anaendelea na kazi.

117. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuendelea na awamu ya kwanza ya ujenzi wa Reli ya Kati kwa sehemu iliyosalia ya Makutupora – Tabora (km 295), Tabora – Isaka (km 133) na Isaka – Mwanza (km 250). Juhudi zinazofanywa na Serikali zimesaidia kupata wawekezaji mbalimbali ambao wameonyesha nia ya kufanikisha upatikanaji wa fedha na kushiriki katika ujenzi wa reli ya Makutupora – Mwanza.

118. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutambua umuhimu wa Reli ya Kati inayotumika sasa (Meter Gauge Railway - MGR) katika kusafirisha bidhaa na abiria. Aidha, reli hii inatumika kwa ajili ya ujenzi wa reli ya SGR unaoendelea. Mkataba wa ukarabati wa njia ya reli kwa kuondoa reli zote nyepesi na kuweka reli mpya zenyenzo wa ratili 80 kwa yadi kati ya Dar es Salaam na Isaka ulisainiwa Julai, 2018. Ukarabati wa njia ya reli kutoka Dar es Salaam - Kilosa (Km 283) umekamilika kwa asilimia 10 na unatarajiwa kukamilika Juni, 2020. Aidha, ukarabati wa sehemu ya Kilosa-Isaka (Km 687) umekamilika kwa asilimia 10.8 na unatarajiwa kukamilika Januari, 2020.

119. Mheshimiwa Spika, kazi zinazoendelea kutekelezwa katika mwaka 2018/2019 ni pamoja na:

- (i) Kukamilisha kazi ya usanifu wa kina wa kuinua kiwango cha njia ya reli kati ya Tabora - Kigoma na Kaliua – Mpanda. kazi hii inatarajiwa kukamilika Juni, 2019;
- (ii) Kukamilisha usanifu wa awali kwa ajili ya ujenzi wa reli ya Uvinza na Musongati (Burundi) yenye urefu wa Km 200 kwa Standard Gauge. Kazi hii inategemea kukamilika Juni, 2019;
- (iii) Kuendelea na kazi ya kufufua njia ya reli ya Tanga hadi

Arusha kwa ajili ya usafiri wa abiria na mizigo. Kazi ya ukarabati wa reli hii kwa kipande cha Tanga – Same (km 199) imekamilika;

(iv) Kuboresha eneo la treni la kupakia/ kupakua mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam na kukarabati vituo vya kuhudumia mizigo vya llala na Isaka;

(v) Upembuzi Yakinifu wa ujenzi wa njia mpya za reli kutoka katikati ya Jiji la Dar es Salaam kwenda maeneo ya Pugu, Mbagala/Chamazi, Luguruni/ Kibaha na Bunju/Kerege; na

(vi) Ukarabati wa vitendea kazi yakiwemo mabehewa ya mizigo na abiria.

120. *Mheshimiwa Spika*, Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa reli ya *Standard Gauge* kati ya Mtwara – MbambaBay na matawi ya Mchuchuma na Liganga na reli ya Tanga – Arusha – Musoma kwa *Standard Gauge*. Kazi za Upembuzi yakinifu na Usanifu wa Awali wa ujenzi wa reli katika maeneo hayo imekamilika. Kwa upande wa reli ya Mtwara – MbambaBay na matawi ya Mchuchuma na Liganga, mkataba na Mshauri Mwelekezi (Transaction Advisor) ulisainiwa Februari, 2019. Kuhusu reli ya Tanga – Arusha – Musoma, Serikali inaendelea na majadiliano na Mshauri Mwelekezi (Transaction Advisor). Kazi itayofanywa na Washauri Waelekezi hawa ni kuandaa andiko la kunadi miradi hii ili kupata wawekezaji kwa utaratibu wa ubia (PPP) na kuandaa makabrasha ya zabuni.

121. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imekusudia kuboresha usafiri wa abiria na kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam kwa kutumia usafiri wa treni. Kazi ya kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa njia mpya za reli Jijini Dar es Salaam zikiwemo zile za kwenda maeneo ya Pugu kuitia Kiwanja cha Ndege cha Julius Nyerere, Mbagala/Chamazi, Luguruni/ Kibaha na Bunju/Bagamoyo itakamilika Juni, 2019.

122. *Mheshimiwa Spika*, Kazi ya kukarabati reli ya Tanga – Arusha (km

439) kwa ajili ya usafiri wa abiria na mizigo inaendelea. Kazi ya ukarabati wa reli hii sehemu ya Tanga – Same (km 199) imekamilika. Kazi inayoendelea ni ujenzi wa madaraja 6. Aidha, Sehemu ya Same – Arusha (Km 186), kazi ya ukarabati wa njia, ujenzi wa madaraja na makalvati inaendelea. Kwa ujumla mradi huu unatarajiwa kukamilika Desemba, 2019.

123. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utoaji wa huduma za usafiri, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 TRC ilisafirisha tani 311,978 za shehena ikilinganishwa na tani 277,561 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2017/2018. Hili ni ongezeko la asilimia 36.9. Kwa upande wa abiria, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019, abiria 370,981 walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 380,177 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2017/2018. Huu ni upungufu wa asilimia 24. Sababu za upungufu huu zinatokana na kupisha ujenzi wa reli ya SGR na ukarabati wa njia ya *meter gauge* unaondelea.

Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)

124. Mheshimiwa Spika, Serikaliza Tanzania na Zambia kwa pamoja zimeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha utendaji wa TAZARA. Hatua hizo ni pamoja na kuboresha miundombinu na huduma za reli na Serikali kuchangia uendeshaji wa Mamlaka upande wa Tanzania. Hadi Machi, 2019 TAZARA ilikuwa imefanya matengenezo makubwa ya njia kwenye sehemu zilizowekewa katazo la mwendokasi (speed restricted areas) ya jumla ya kilometa 82.5 kati ya kilometa 150 zilizowekewa katazo la mwendokasi. Kazi nyingine zilizotekelizwa katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019, ni pamoja na ukarabati wa mabehewa ya mizigo 85, mabehewa ya abiria 4; kubadilisha mataruma ya zege 12,827 na mataruma ya mbao 2,704; kufanya matengenezo ya kawaida ya injini, mabehewa ya abiria na mizigo, mtambo wa kunyoosha reli na matengenezo ya njia ya reli. Aidha, ujenzi wa miundombinu wezeshi katika stesheni ya Fuga kwa ajili ya kuhudumia vifaa vyta ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme katika maporomoko ya maji ya Mto Rufiji (Stiegler's Gorge) ulitekelezwa. Kazi zilizotekelizwa katika

stesheni hiyo ni pamoja na kukamilika kwa taratibu za ununuzi wa mitambo ya kupakia na kupakua mizigo, ujenzi wa jukwaa la kushushia na kuhifadhi mizigo, na ukarabati wa nyumba za watumishi na njia ya reli.

125. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/2018, Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya kununua vipuri vya Injini (Traction Motors)42 na mitambo ya kusaidia uzalishaji wa mataruma ya zege (Dumper Truck, Excavator and Drill Rig) katika mgodi wa kokoto ulioko Kongolo, Mbeya. Vifaa hivi viliagizwa na vitaanza kuwasili nchini mwishoni mwa Aprili, 2019. Vifaa vyote vitakuwa vimepokelewa ifikapo Septemba, 2019.

126. Mheshimiwa Spika, Serikali ilikamilisha utekelezaji wa miradi iliyoinishwa katika Itifaki ya 15 ya ushirikiano wa kiuchumi na kiufundi kati ya Serikali za Tanzania na Zambia kwa upande mmoja na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa upande mwingine. Miradi iliyokamilika ni pamoja na ununuzi wa vichwa vya treni vya njia kuu vinne (4), Injini za sogeza nne (4), Mashine za uokoaji mbili (2), Forklift sita (6), winchi 4, mabehewa ya abiria 18, Mataruma ya mbao 30,000, Viberenge Vitano (5), saruji ya kutengeneza mataruma ya zege kwenye kiwanda cha Kongolo, mafunzo kwa watumishi 42 na vipuri vya injini na mabehewa ya mizigo. Hivi sasa Serikali inaendelea na taratibu za kukamilisha makubaliano ya Itifaki ya 16. Miradi itakayokuwa kwenye Itifaki ya 16 ni pamoja na ununuzi wa vipuri vya kuimarisha njia ya reli, injini na mabehewa.

127. Mheshimiwa Spika, uboreshaji uliofanyika TAZARA umesaidia kuboresha huduma zake kwa kupunguza muda wa kusafirisha shenena kati ya Dar es Salaam na New Kapiri Mposhi kutoka wastani wa siku 6.5 mwaka 2017/2018 mpaka wastani wa siku 6.2 Machi, 2019. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019, TAZARA ilisafirisha tani 134,743 za shehena ikilinganishwa na tani 176,858 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2017/2018. Huu ni sawa na upungufu wa asilimia 23.8. Upungufu huu umetokana na idadi ndogo ya injini zilizopo kwa sasa. Kwa upande wa abiria, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019, TAZARA ilisafirisha

abiria 599,061 ikilinganishwa na abiria 574,311 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2017/2018. Hili ni ongezeko la asilimia 4.3.

USAFIGI NA UCHUKUZI MAJINI

128. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kusimamia utoaji wa huduma za usafiri na uchukuzi majini kupitia taasisi zake ikiwemo Kampuni inayomilikiwa kwa pamoja kati ya Tanzania na China (SINOTASHIP), Kampuni ya Huduma za Meli katika Maziwa (MSCL) pamoja na sekta binafsi. Aidha, huduma za bandari zimeendelea kutolewa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) pamoja na sekta binafsi.

Huduma za Uchukuzi Baharini

129. Mheshimiwa Spika, Uchukuzi wa masafa marefu baharini umeendelea kutolewa na SINOTASHIP. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019, Kampuni hii ilisafirisha jumla ya tani 598,000 za shehena ya mizigo ikilinganishwa na jumla ya tani 580,000 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2017/2018. Hili ni ongezeko la asilimia 3.1 ya shehena ya mizigo iliyosafirishwa. Aidha, SINOTASHIP iliongeza njia kuu za meli za kusafirisha mizigo kutoka Mashariki ya mbali hadi Tanzania kutoka njia mbili na kufikia njia tatu.

Huduma za Uchukuzi Katika Maziwa

130. Mheshimiwa Spika, huduma za uchukuzi wa abiria na mizigo katika maziwa makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa zimeendelea kutolewa na Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) pamoja na vyombo vya watu binafsi. Aidha, Serikali kupitia MSCL imeendelea kuboresha usafiri wa abiria na mizigo katika Maziwa hayo kwa kuanza kutekeleza mradi wa ununuzi wa meli mpya na ukarabati wa meli zilizopo. Hadi Machi, 2019, kazi zilizotekeliza ni pamoja na:

- i. Mikataba ya Ujenzi wa meli mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo katika ziwa Victoria; ujenzi

wa chelezo; pamoja na ukarabati wa meli ya MV Victoria na MV Butiama ilisainiwa Septemba, 2018 na kazi zinaendelea. Mikataba kwa ajili ya ukarabati wa meli za MV. Umoja na MV. Serengeti zilizopo katika Ziwa Victoria inatarajiwa kusainiwa kabla ya Julai, 2019; na

ii. Kwa upande wa Ziwa Tanganyika, Mikataba ya ujenzi wa meli mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 600 na tani 400 za mizigo pamoja na ukarabati mkubwa wa meli ya MV. Liemba imekamilishwa na inatarajiwa kusainiwa kabla ya Julai, 2019.

131. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2018 hadi Machi, 2019, Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) ilisafirisha abiria 64,709 ikilinganishwa na lengo la kusafirisha abiria 82,159 na kusafirisha shehena ya mizigo tani 15,421 ikilinganishwa na lengo la kusafirisha tani 68,352. Kushuka kwa utendaji huo kultitokana na kuharibika mara kwa mara kwa mell ya MT. Sangara, MV Umoja, MV Serengeti na MV Songea.

Huduma za Bandari

132. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ilihudumia shehena za mizigo tani milioni 6.658 katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2017 ikilinganishwa na tani 6.952 milioni zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2018/2019. Aidha, katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2018, Vitengo vya Makasha (TPA) na TICTS katika Bandari ya Dar es Salaam vilihudumia makasha (TEUs) 363,145 ikilinganishwa na makasha (TEUs) 361,430 yaliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2017/2018. Hili ni ongezeko la makasha (TEUs) 1,715 sawa na asilimia 0.5.

133. Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kupanua soko la bandari zetu, kuongeza shehena na kukabiliana na ushindani kutoka bandari za nchi jirani. Hatua hizo ni pamoja na kusogea huduma za kibandari karibu na wateja kwa kufungua ofisi katika miji ya Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DR Congo); Lusaka, Zambia; Kigali, Rwanda; Bujumbura, Burundi; pamoja na kuanzisha ofisi

inayosimamiwa na wakala (Agent) Mjini Kampala, Uganda.

134. *Mheshimiwa Spika*, katika hotuba yangu kwa mwaka wa fedha 2018/19, nililiahidhi Bunge lako Tukufu kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari itatekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo yenye lengo la kuboresha utendaji wa bandari za Mwambao na Maziwa Makuu. Miradi iliyokamilika ni pamoja na:

- i. Uboreshaji wa gati Na. 1 katika bandari ya Dar es Salaam ulikamilika Desemba, 2018 na limeanza kutumika;
- ii. Ukarabati wa jengo la kuhifadhi mizigo katika bandari ya Kilwa ulikamilika Septemba, 2018; na
- iii. Awamu ya kwanza ya ujenzi wa bandari kavu ya Kwala, Ruvu Vigwaza iliyohusu ujenzi wa uzio na kusawazisha eneo kwa kiwango cha changarawe ilikamilika Septemba, 2018.

135. *Mheshimiwa Spika*, Miradi mingine ya uboreshaji wa bandari za bahari kuu na kwenye maziwa inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na:

- i. Uboreshaji wa gati Na. 1-7 na ujenzi wa gati jipya la kushusha magari katika Bandari ya Dar es Salaam. Kazi hii iliyanza Juni, 2017 inatarajiwa kukamilika Desemba, 2020. Ujenzi wa gati namba 1 ulikamilika Desemba, 2018. Kazi ya ujenzi wa gati la kushushia shehena ya magari (RoRo Berth) ikiwa ni pamoja na ujazaji wa kifusi na kuongeza kina (dredging along the quay side) umefikia asilimia 45;
- ii. Ujenzi wa gati moja (multipurpose terminal) katika Bandari ya Mtwara kwa ajili ya kuhudumia shehena mchanganyiko. Ujenzi huu ulioanza Machi, 2017 unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2019. Hadi sasa kazi ya ujenzi imekamilika kwa asilimia 35;
- iii. Ujenzi wa gati la Nyamisati, Rufiji. Ujenzi huu umekamilika kwa asilimia 32 na unatarajiwa kukamilika Mei, 2019;

- iv. Ujenzi wa gati la Kalya (Sibwesa) katika Ziwa Tanganyika unaojumuisha ujenzi wa gati na miundombinu mingine kama ghala la kuhifadhi mizigo na jengo la abiria umekamilika kwa asilimia 91 na unatarajiwa kukamilika Juni, 2019;
- v. Ukarabati wa *Control Tower* katika Bandari ya Dar es salaam unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Aprili, 2019;
- vi. Ukarabati wa Bandari ya Tanga unaojumuisha upanuzi wa eneo la kuhifadhi mizigo na ukarabati wa miundombinu umekamilika kwa asilimia 83 na unatarajia kukamilika Juni, 2019;
- vii. Ujenzi wa gati la Nyamirembe katika ziwa Victoria ulioanza Agosti, 2018 umefikia asilimia 30 na unatarajiwa kukamilika Julai, 2019;
- viii. Mradi wa ujenzi wa Gati mbili (2) za Majahazi (two dhow wharves) Mwigobelo katika Ziwa Victoria utakaowezesha majahazi na vyombo vidogo vya usafirishaji wa abiria na uvuvi kutia nanga kwa usalama umefikia asilimia 42. Mradi huu unatarajiwa kukamilika Mei, 2019;
- ix. Ujenziwa Bandari ya Magarine katika Ziwa Victoria umefikia asilimia 54 na unatarajiwa kukamilika Juni, 2019;
- x. Ujenzi wa Bandari ya Lushamba katika Ziwa Victoria umefikia asilimia 80 na unatarajiwa kukamilika Juni, 2019;
- xi. Ujenzi wa gati la Lagos katika Ziwa Tanganyika umefikia asilimia 25 na unatarajiwa kukamilika Juni, 2019;
- xii. Ujenzi wa gati la Kabwe, Nkasi katika Ziwa Tanganyika umefikia asilimia 28 na unatarajiwa kukamilika Mei, 2020;
- xiii. Ujenzi wa magati ya MbambaBay, Manda na Matema katika Ziwa Nyasa upo katika hatua za mwisho za ununuzi wa kuwapata Wataalam Waelekezi kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa uboreshaji wa magati hayo. Kazi hii inatarajiwa kuanza Juni 2019; na

xiv. Ujenzi wa meli mpya ya abiria na mizigo yenye uwezo wa kusafirisha abiria 200 na tani 200 za mizigo katika Ziwa Nyasa umekamilika kwa asilimia 86. Kazi hii inatarajiwa kukamilika Desemba, 2019.

136. Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa Bandari mpya inayotarajiwa kujengwa eneo la Mbegani, Bagamoyo. Ujenzi wa Bandari hii utasadia kuimarisha ujenzi wa Tanzania ya viwanda na kuchangia katika kufikia uchumi wa Kati. Majadiliano na wawekezaji waliokuwepo yaani kampuni ya China Merchant Holdings International Limited (CMHI) na State General Reserve Fund (SFRF) ya Serikali ya Oman yamesitishwa baada ya wawekezaji hao kuweka masharti yasiyokuwa na maslahi kwa Taifa. Masharti hayo ni pamoja na wawekezaji kudai kuachiwa jukumu la kupanga viwango vya tozo na kutoruhusu wawekezaji wengine katika eneo la kati ya Bagamoyo na Tanga. Majadiliano hayo yanaweza kuendelea iwapo wawekezaji hao wataondoa masharti yasiyo na maslahi kwa taifa.

137. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuimarisha ulinzi na usalama kwenye mipaka ya nchi yetu na kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato. Hatua hizo ni pamoja na kudhibiti bandari bубу nchini. Serikali kuititia taasisi zake za TPA, TASAC na Halmashauri za Miji na Wilaya, ilifanya kazi ya kubainisha bandari bубу nchini ambapo jumla ya bandari bубу 437 zimebainishwa. Hatua inayoendelea ni kufanya tathmini ya bandari zinazofaa kurasimishwa au kufungwa. Tathmini hiyo itakamilika Juni, 2019.

138. Mheshimiwa Spika, Mradi wa ujenzi wa Bandari Kavu eneo la Kwala, Ruvu unatekelezwa katika awamu mbili. Awamu ya kwanza ya kujaza kokoto na kushindilia imekamilika kwa asilimia 100 katika eneo lenye ukubwa wa Hekta 20.8. Awamu ya pili ya mradi inahusisha kazi ya kujenga reli ya kuunganisha bandari hiyo inayofanywa na Shirika la TRC. Kazi hii imefikia asilimia 70 na inatarajiwa kukamilika Mei, 2019.

Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Majini

139. Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (Tanzania Shipping Agency - TASAC) kwa mujibu wa Sheria ya Uwakala wa Meli Namba 14 ya Mwaka 2017, kupitia Tangazo la Serikali Na. 53 la tarehe 16 Februari, 2018. Lengo la kuanzisha Shirika hili ni pamoja na kudhibiti ulinzi na usalama wa vyombo vya usafiri majini; kudhibiti uchafuzi wa mazingira katika maji utokanao na meli; kuendeleza na kupanua sekta ndogo ya usafiri majini; kudhibiti huduma za bandari na usafiri majini; kuhimiza ufanisi na ushindani mionganoni mwa watoa huduma katika sekta ya usafiri majini na kulinda maslahi mapana ya Taifa ikiwa ni pamoja na kuondosha na kusafirisha madini na mazao yake, mafuta, mitambo na vipuri vitumikavyo migodini, bidhaa zenyeh maslahi ya Taifa, nyara za Serikali na wanyama. Aidha, TASAC immeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usafiri Majini ya mwaka 2003 (Merchant Shipping Act, 2003). Pia, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Bahari Zanzibar (Zanzibar Maritime Authority - ZMA), huduma na usalama wa usafiri majini umeendelea kusimamiwa katika eneo lote la maji ya Tanzania kwa kuzingatia matakwa ya Shirika la Bahari Duniani (IMO).

140. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, TASAC ilitekeleza yafuatayo:

i. Kufanya ukaguzi wa usalama wa vyombo vikubwa na vidogo vya usafiri majini. Jumla ya kaguzi 130 kwa vyombo vikubwa zilifanyika ambapo asilimia 57.7 ya vyombo vilivyofanyiwa kaguzi hizo vilikidhi viwango vya usalama wa uendeshaji wa vyombo hivyo baharini. Aidha, Shirika lilifanya kaguzi 3,430 kwa vyombo vidogo, ambapo asilimia 71.43 ya vyombo vilivyofanyiwa kaguzi hizo vilikidhi viwango vya usalama wa uendeshaji wa vyombo hivyo baharini. Msisitizo uliwekwa katika kuhakikisha kuwa, vyombo hivyo vinakidhi viwango vya ubora;

ii. Kufanya kaguzi za meli saba (7) ambazo zilihitaji matengenezo na marekebisho makubwa. Meli hizo ni MV.

Mwanza, Meli ya Chuo cha Bahari Dar es Salaam, MV. Njombe, MV Ruvuma, MV. Bijli, MV. Umoja na MV. Rafiki;

iii. Kutoa elimu ya ulinzi na usalama wa usafiri majini kwa kujumuisha wadau katika maeneo mbalimbali. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019, jumla ya mikutano 101 ilifanyika;

iv. Kusajili Meli zilizokidhi viwango vya ubora ambapo hadi Machi, 2019, jumla ya meli nne (4) za Tanzania zilisajiliwa na kupewa vyeti vya usajili baada kukaguliwa na kukidhi viwango vya usajili. Aidha, Shirika lilitoa leseni kama ifuatavyo:

- Leseni 29 za uwakala wa meli;
- Leseni 578 za mawakala wa uondoshaji shehena bandarini;
- Leseni 25 za wakusanyaji mizigo (cargo consolidators/deconsolidators);
- Leseni 34 za watoa huduma ndogo ndogo bandarini (miscellaneous port services); na
- Leseni 42 za wapimaji wa makasha (gross mass verifiers).

v. Kukagua utendaji wa bandari za Mwanza, Nansio, Geita, Bukoba, Kemondo, Mtwara, Tanga, Ndumbi, Mbamba Bay, Dar es Salaam, Lindi, Kilwa, Kasanga, Kipili, Itungi na Kiwira;

vi. Kukagua utendaji wa Mawakala wa Meli katika mikoa ya Kigoma, Mwanza, Mtwara na Dar es Salaam; Mawakala wa Uondoshaji na Uingizaji wa shehena bandarini 176, wakusanyaji mizigo 16, wapimaji wa makasha 12 na watoa huduma ndogo Bandarini 5; na

vii. Kuandaa miongozo ya ndani 11 inayohusu shughuli za biashara za usafirishaji majini (Internal Operating Procedures Manual for Shipping Business) na rasimu za Kanuni zinazohusiana na ulinzi na usalama wa usafiri majini.

141. Mheshimiwa Spika, katika kaguzi zilizofanyika, mkazo uliwekwa katika kuhakikisha kuwa wadau wote wanaohusika na masuala ya bandari wanatoa huduma kwa saa 24 kila siku na kuhakikisha matakwa ya Kanuni yanazingatiwa ili kusaidia katika kuongeza ufanisi wa bandari. Aidha, Shirika limeweka mkakati wa kuhakikisha kuwa cheti cha ubora cha Kimataifa kwa huduma zitolewazo na Shirika (ISO 9001:2015) kinapatikana ifikapo Juni, 2019.

USAFIRI NA UCHUKUZI KWA NJIA YA ANGA

Udhhibitit wa Huduma za Usafiri wa Anga

142. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, Wizara kuititia Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) imeendelea kudhibiti utoaji wa huduma za usafiri wa anga nchini kwa kuzingatia viwango vya Kimataifa vinavyosimamiwa na Shirika la Usafiri wa Anga Duniani (International Civil Aviation Organisation-ICAO).

143. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2018 hadi Machi, 2019, ndege 15 zilipewa usajili wa mara ya kwanza hapa nchini na kupewa vyeti vya ubora (Certificate of Airworthiness) na ndege 6 ziliondolewa kwenye orodha ya usajili baada ya kumalizika kwa mikataba ya ukodishaji. Aidha, ndege nyingine 49 zilikaguliwa na kupewa vyeti vya ubora na kuruhusiwa kuendelea kutoa huduma.

144. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, Mamlaka ya Usafiri wa Anga iliendelea kutekeleza mradi wa ufungaji wa Rada nne (4) za kuongozea ndege za kiraia. Rada hizi zitafungwa katika viwanja vya ndege vya JNIA, KIA, Mwanza na Songwe, Hadi Machi, 2019, utekelezaji wa Mradi huu ulikuwa katika hatua mbalimbali. Katika Kiwanja cha ndege cha JNIA, ujenzi wa jengo la mnara wa rada umekamilika kwa asilimia 100, ufungaji wa mtambo wa rada umekamilika kwa asilimia 90 na mradi huu utakamilika mwishoni mwa Aprili, 2019; Kuhusu Kiwanja cha ndege cha Mwanza, ujenzi wa jengo la mnara na mitambo ya rada umekamilika kwa asilimia 50 na mtambo utaanza kufungwa Mei, 2019; Kuhusu Kiwanja cha

ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro, ujenzi wa jengo la mnara wa rada na jengo la mtambo wa rada umekamilika kwa asilimia 90. Kazi hii itakamilika Julai, 2019. Aidha, kuhusu Kiwanja cha ndege cha Songwe, majadiliano ya kupidisha michoro ya majengo ya eneo itakapofungwa rada yamekamilika. Mtambo wa Rada umeshawasili nchini na kazi ya ufungaji inatarajiwa kukamilika ifikapo Septemba, 2019.

145. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Mamlaka ililenga kufanya ununuzi na ufungaji wa mtambo wa kuwezesha ndege kutua kwa usalama (Instrument landing System - ILS) katika Kiwanja cha Ndege cha Zanzibar. Mkataba wa ufungaji wa mtambo huu ulitiwa saini Agosti, 2018. Mradi huu unatekelezwa na kampuni ya PEJA East Africa ya Uholanzi na unatarajiwa kukamilika Agosti, 2019. Aidha, Mradi wa ukarabati wa mnara wa kuongozea ndege katika kituo cha Pemba ullkamilika Januari, 2019 na kuzinduliwa rasmi wakati wa sherehe za miaka 55 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

146. Mheshimiwa Spika, sekta ya usafiri wa anga nchini imeendelea kukua. Idadi ya abiria wanaosafiri kwenda na kutoka nje ya nchi imeongezeka kutoka abiria 2,461,528 mwaka 2017/18 hadi abiria 2,661,528 mwaka 2018/19. Kuongezeka kwa idadi ya abiria kunatokana na kuongezeka kwa huduma za usafiri wa anga baada ya kusaini Mikataba ya Usafiri wa Anga (Bilateral Air Services Agreements) kati ya Tanzania na nchi zingine; uimarishaji wa huduma na miundombinu ya usafiri wa anga vikiwemo viwanja vyatundege; ukuaji wa uchumi na kuongezeka kwa shughuli za utalii nchini. Aidha, idadi ya abiria wanaosafiri ndani ya nchi imeongezeka kutoka abiria 2,786,852 mwaka 2017/18 hadi abiria 2,926,195 mwaka 2018/2019, hii ni sawa na ongezeko la asilimia 5.0. Sababu ya ongezeko la abiria wa ndani ni pamoja na Kampuni ya Ndege Tanzania kuimarisha huduma zake; kukua kwa shughuli za kiuchumi nchini; kuongezeka kwa utalii nchini na kuanzishwa kwa safari za ndege katika maeneo mapya. Kwa upande wa mizigo, jumla ya tani 27,910.3 zilizosafirishwa ikilinganishwa na tani 24,574.5 zilizosafirishwa katika mwaka wa fedha 2017/18. Hili ni

ongezeko la asilimia 3.5. Ongezeko hili linatokana na kukua kwa shughuli za kibashara na kiuchumi ndani na nje ya nchi pamoja na jitihada za Serikali za kukuza usafirishaji wa mizigo kupitia usafiri wa anga hapa nchini.

147. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuhakikisha kuwa sekta binafsi inaimarika na kuendelea kukua katika utoaji wa huduma za usafiri wa anga, katika mwaka 2018/2019, Serikali ilisaini Mikataba mipy ya Usafiri wa Anga kati yake na nchi nyingine (Bilateral Air Services Agreements – BASA) mbili (2) za Malaysia na Hispania. Vile vile, Tanzania ilipitia upya mikataba yake ya BASA na nchi tisa (9) ambazo ni Zambia, Uturuki, Oman, Sri Lanka, Uingereza, Zimbabwe, Ethiopia, Afrika Kusini na Rwanda. Hatua hii imeifanya Tanzania kuingia mikataba ya usafiri wa anga (BASA) na jumla ya nchi 72, ikilinganishwa na nchi 70 mwaka 2017/2018.

148. Mheshimiwa Spika, miradi mingine iliyokamilishwa ni pamoja na:

(i) Ufungaji wa mtambo wa kuboresha mtandao wa mawasiliano ya simu na radio za kuongozea ndege (*Voice Communication Control Switch - VCCS*) katika viwanja vya Ndege vya JNIA na KIA;

(ii) Mradi wa Mfumo wa Kuandaa Hati za Madai (billing system on invoices) kwa ndege zote zinazofanya safari katika anga la Tanzania; na

(iii) Ujenzi wa mitambo ya kisasa ya kutuma na kupokea taarifa za usafiri wa anga (Aeronautical Message Handling System- AMHS).

149. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019, Mamlaka ya Usafiri wa Anga iliendelea kufanya kaguzi za viwanja vyote vya ndege nchini ili kuhakikisha kuwa viwanja hivi vinakidhi vigezo, masharti na kanuni zilizowekwa na Mamlaka. Viwanja vya ndege vilivokaguliwa na kupewa vyeti vya ubora baada ya kukidhi vigezo vya kimataifa kwa ajili ya kupokea ndege kubwa ni pamoja na Viwanja vya

kimataifa vya Julius Nyerere; Amani Abedi Karume na Kilimanjaro. Viwanja vingine vilivyokaguliwa ni pamoja na Dodoma, Songwe, Iringa, Mtwara, Lindi, Mwanza, Musoma, Shinyanga, Kigoma, Tabora, Bukoba, Tanga, Sumbawanga, Mpanda, Nachingwea, Kilwa Masoko na Songea. Aidha, Mamlaka imeendelea kusimamia viwango vya ubora katika viwanja vinavyomilikiwa na Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa (TANAPA), Wizara ya Maliasili na Utalii na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) ili kuimarisha utoaji huduma na kukuza utalii nchini.

150. *Mheshimiwa Spika*, Mamlaka imeendelea kufanya kaguzi za mara kwa mara za kupangwa na za kushtukiza ili kudhibiti usalama wa usafiri wa anga katika viwanja vya ndege, mashirika ya ndege pamoja na watoa huduma za usafiri wa anga. Lengo ni kuhakikisha kwamba viwanja vyetu havitumiki katika vitendo vya kihalifu. Kazi zilizotekelzwani pamojanakudhibitiuingizaji na usafirishaji wa bidhaa haramu, bidhaa zisizo na ubora na bidhaa zenye maslahi kwa Taifa. Pia, Mamlaka ya Usafiri wa Anga kwa kushirikiana na Jeshi la Wananchi Tanzania kuititia kamati ya Kitaifa ya Usalama wa Usafiri wa Anga, imeunda timu ya wataalam ya kufanya Uhakiki nchi nzima kwa lengo la kujua viwanja vilivyopo nchini na mahitaji ya kiusalama katika viwanja hivyo. Tayari uhakiki umefanywa kwa Arusha, Manyara, Moshi, Tanga, Mwanza, Shinyanga, Kagera, Simiyu, Geita na Mara. Uhakiki katika maeneo ya Kigoma, Katavi, Rukwa, Mbeya, Iringa, Njombe, Songwe, Lindi, Ruvuma, Mtwara, Dodoma, Singida, Tabora, Mkoa wa Pwani na Morogoro unaendelea.

Huduma za Viwanja vya Ndege

151. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kuititia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) imeendelea na ununuzi wa mitambo, matengenezo ya miundombinu na mitambo mbalimbali katika viwanja inavyoendesha ili kuboresha huduma na kuimarisha usalama.

152. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/2019, Mamlaka

ya Viwanja vya Ndege ililenga kununua vifaa vya ulinzi, usalama na mawasiliano katika viwanja vya ndege. Hadi Machi, 2019, kazi ya kununua mitambo 2 ya ukaguzi wa abiria na mizigo (X-ray machines) kwa viwanja vya ndege vya Iringa na Songea imekamilika. Aidha, taratibu za ununuzi wa mitambo hiyo kwa ajili ya viwanja vya ndege vya Mwanza, Kigoma, Dodoma, Musoma, Songwe, Mtwara, Kilwa Masoko, Lindi, Nachingwea, Moshi na Bukoba zinaendelea. Mkataba wa ununuzi wa magari ya zimamoto matatu (3) kwa ajili ya viwanja vya ndege Mpanda, Shinyanga na Iringa upo katika hatua za mwisho kusainiwa. Vile vile, taratibu za ununuzi zinakamilishwa kwa ajili ya ununuzi wa Kamera (CCTV) kwa Viwanja vya Ndege vya Dodoma na Mtwara na vifaa vya mawasiliano vya Viwanja vya ndege vya Arusha, Songea, Kahama, Mafia na Iringa.

153. *Mheshimiwa Spika*, eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanja Kipywa cha Ndege cha Mkoa wa Manyara limekwisha bainishwa. Kazi inayoendelea sasa ni manunuzi ya Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Kazi hii inatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka 2019/2020.

Huduma za Usafiri wa Anga

154. *Mheshimiwa Spika*, utoaji wa huduma ya usafiri wa anga ndani ya nchi umeendelea kuimarika. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, huduma hiyo imeendelea kutolewa na ndege zenye ratiba maalum (scheduled flight) kupililia Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL), Precision Air, Auric Air, Coastal Air na Fastjet Air. Pia, huduma ya usafiri wa anga kwa ratiba zisizo maalum (general aviation) zimeendelea kutolewa kupililia mashirika kama Auric Air, Coastal Air, Zanair, Air Excel, Tanzanair, Sky aviation na Tropical air.

155. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019, Serikali ilipokea ndege tatu (3) mpya. Ndege moja kubwa ya masafa marefu aina ya Boeing 787 – 8 Dreamliner yenye uwezo wa kubeba abiria 262 iliwasili Julai, 2018. Ndege mbili za masafa ya kati aina ya Airbus A220 –

300 zenye uwezo wa kubeba abiria 132 kila moja, moja iliwasili Desemba, 2018 na nyingine iliwasili Januari, 2019. Ongezeko hili la idadi ya ndege limesababisha ATCL kutoa huduma za usafiri wa anga katika vituo 9 vya ndani ya nchi na vituo 5 vya kikanda. Vituo vya ndani ya nchi ni pamoja na Dar es Salaam, Mwanza, Bukoba, Kigoma, Kilimanjaro, Tabora, Dodoma, Mbeya na Zanzibar. Vituo vya Kikanda ni Entebbe, Uganda; Bujumbura, Burundi; Harare, Zimbabwe; Lusaka, Zambia na Hahaya, Comoro. Aidha, ATCL inatarajia kuanza kutoa huduma za usafiri wa anga katika mijji ya Bangkok, Thailand; Mumbai, India; Johannesburg, Afrika Kusini na Guangzhou, China. Kwa sasa maandalizi yanaendelea na safari hizi zinatarajiwa kuanza kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha wa 2018/2019.

156. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/2019, Serikali ililenga kununua ndege mbili (2) mpya. Ndege moja alina ya *Bombardier Dash 8 Q400* yenye uwezo wa kubeba abiria 76 na ndege kubwa moja (1) ya masafa marefu aina ya *Boeing 787-8 Dreamliner* yenye uwezo wa kubeba abiria 262. Hadi Machi, 2019, asilimia 36 ya malipo ya ununuzi wa ndege aina ya *Boeing 787-8 Dreamliner* yalifanyika na ndege hiyo inatarajiwa kuwasili nchini mapema Januari 2020. Kuhusu ndege moja (1) mpya aina ya *Bombadier Dash 8 Q400*, malipo ya asilimia 30 ya ununuzi wa ndege hiyo yalifanyika na ndege hiyo inatarajiwa kuwasili Novemba, 2019.

157. *Mheshimiwa Spika*, katika juhudzi za kuendelea kuboresha huduma zake, hadi Machi, 2019, ATCL imewapeleka mafunzoni marubani (51), wahandisi (14) na wahudumu wa ndani ya ndege (66). Aidha, ATCL imeendelea kuboresha miundombinu ya biashara kwa kuijunga kwenye mfumo wa uuzaaji wa tiketi ulimwenguni (Global Distribution System – GDS), ambapo hadi Machi, 2019 ATCL imeweza kuuza tiketi zake katika nchi 25 (twenty five GDS). Pia, ATCL imerejea katika mfumo wa usuluhisho wa mauzo ya tiketi (IATA Clearing House – ICH). Mafanikio mengine ni pamoja na kuanza ukarabati wa Karakana ya ndege (Hangar) iliyoko katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro lijulikanalo kama *Kilimanjaro Maintenance Facilities – KIMAF*; kuboresha

Mifumo ya TEHAMA na tovuti yake ambapo kwa sasa inawapa wateja urahisi wa kukata tiketi; kufanya usajili wa kuingia katika ndege kwa njia ya mtandao (on line check in); na kuboreshwa mfumo wa ufuatiliaji wa mzigo (cargo tracking) kutoka kituo kimoja hadi kingine.

158. Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa utendaji na utoaji huduma umeiwezesha ATCL kumiliki soko la usafiri wa anga la ndani kwa asilimia 40.8 kutoka asilimia 2.5 za mwaka 2017. Aidha, ATCL imeongeza idadi ya abiria kutoka abiria 216,798 katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 hadi abiria 307,192 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Hili ni ongezeko la asilimia 41.69.

HUDUMA ZA HALI YA HEWA

159. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, Wakala wa Hali ya Hewa (TMA) uliendelea kutoa tahadhari dhidi ya hali mbaya ya hewa na majanga yanayohusiana na hali ya hewa. Huduma zilizotolewa na Wakala ni pamoja na utabiri wa hali ya hewa; utabiri mahsus kulingana na hitaji la sekta au wadau na tahadhari juu ya matukio ya hali mbaya ya hewa. Taarifa hizi zimesaidia kupunguza athari za matukio ya hali mbaya ya hewa, ukuaji wa sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii pamoja na kupunguza athari zitokanazo na mabadiliko ya tabia nchi.

160. Mheshimiwa Spika, Desemba 2018, Wakala ulifanyiwa tena ukaguzi wa kimataifa na kufanikiwa kuendelea kumiliki cheti cha utoaji wa huduma bora za hali ya hewa kwa sekta ya usafiri wa anga (ISO 9001:2015 certified). Aidha, katika mwaka 2018/2019, viwango vya usahihi wa utabiri wa hali ya hewa viliongezeka kutoka asilimia 81 na kufikia asilimia 87.5; jumla ya vifaa vya hali ya hewa 20 vinavyopima halijoto visivyotumia zebaki vilinunuliwa na kufungwa katika maeneo mbalimbali nchini. Vilevile, vifaa vya kupima mgandamizo wa hewa (Barometers) vinavyotumia zebaki katika vituo saba (7) vya hali ya hewa vinavyotekeleza mfumo wa kimataifa wa utoaji wa huduma bora kwa sekta ya usafiri wa anga vilibadilishwa na kufungwa vifaa visivyotumia zebaki. TMA

itaendelea kubadilisha vifaa vinavyotumia zebaki ili kukidhi matakwa ya makubaliano ya kimataifa yanayoweka ukomo wa matumizi ya zebaki ifikapo mwaka 2020.

161. Mheshimiwa Spika, ili kuendelea kuboresha huduma za hali ya hewa na kuimarisha utendaji kazi wa Wakala, katika mwaka 2018/2019, Wakala umefanya ukarabati mkubwa wa vituo vya hali ya hewa vya Chukwani (Zanzibar), Dodoma, Handeni, Morogoro, Mtwara na Kilwa Masoko. Aidha, mikataba kwa ajili ya ununuzi wa Rada (3) tatu za hali ya hewa zitakazofungwa katika mikoa ya Mtwara, Mbeya na Kigoma imesainiwa na kazi za ujenzi wa rada hizo inaendelea. Pia, kazi za ujenzi wa barabara, jengo la rada, kibanda cha mlinzi, uzio pamoja na uwekaji wa umeme katika maeneo yatakayofungwa rada hizo zinaendelea.

MAFANIKIO YALIYOFIKIWA KATIKA SEKTA YA UCHUKUZI KWA MWAKA 2018/2019

162. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Sekta ya Uchukuzi iliweza kufikia mafanikio yafuatayo:

- (i) Kukamilika ujenzi wa gati Na. 1 katika mradi wa uboreshaji wa gati Na. 1 – 7 na kuanza kutumika;
- (ii) Kukamilisha ununuzi wa Ndege tatu (3) na kuanzisha ununuzi wa ndege mbili (2); kutoa mafunzo ya marubani (51), wahandisi (14) na wahudumu (66),
- (iii) Ujenzi wa reli kati ya Dar es Salaam na Morogoro (km 300) kufikia asilimia 45.8 na sehemu ya Morogoro hadi Makutupora (km 422) kufikia asilimia 7.12;
- (iv) Kazi ya ukarabati wa miundombinu ya reli kutoka Dar es Salaam – Isaka (km 970) imefikia asilimia 13;
- (v) Kurejeshwa kwa huduma ya usafirishaji wa shehena za mizigo kwenye mabehewa (wagon ferry) kutoka Mwanza hadi bandari ya Port Bell, Uganda baada ya kusimama kwa takriban miaka 10;

- (vi) Ukarabati wa reli ya Tanga hadi Arusha (km 439) ambapo kilomita 199 zimekamilika;
- (vii) Ukarabati wa Gati namba 2 katika Bandari ya Tanga umefikia asilimia 86;
- (viii) Ujenzi wa meli mpya ya abiria na mizigo katika Ziwa Nyasa yenye uwezo wa kusafirisha abiria 400 na tani 200 za mizigo umefikia asilimia 86;
- (ix) Kiwango cha usahihi wa utabiri wa hali ya hewa kimeongezeka kutoka asilimia 81 hadi 87.5;
- (x) Ununuzi wa Rada 4 za kuongozea ndege za kiraia;
- (xi) Kusainiwa kwa mikataba ya ujenzi wa Rada tatu (3) za hali ya hewa na kaazi ya ujenzi inaendelea;
- (xii) Kuanza ujenzi wa meli mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo, ujenzi wa chelezo, pamoja na ukarabati wa meli za MV Victoria na MV Butiama katika Ziwa Victoria;
- (xiii) Kukamilika kwa ukarabati wa Jengo la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro (KIA); na
- (xiv) Kutungwa kwa Sheria mpya za kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.

B.3 SEKTA YA MAWASILIANO Ukusanyaji wa Mapato

163. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2018 hadi Machi, 2019 Sekta ya Mawasiliano imekusanya jumla ya **Shilingi 99,032,658,238.7** kwa mchanganuo ufuatao: TCRA imekusanya Jumla ya **Shilingi 58,938,941,951.71** ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 15,057,228,047.45** zinatokana na asilimia 15 ya pato ghafi la Mamlaka, **Shilingi 12,282,213,906.26** ni kutokana na Mfumo wa TTMS, **Shilingi 22,339,500,000.00** ni kutokana na mauzo ya masafa (Frequency Spectrum

Dividend II) na **Shilingi 9,260,000,000.00** ni rejesho la mtaji uliozidi. Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) umechangia kiasi cha **Shilingi 8,000,000,000.00** na fedha kupelekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, **Shilingi 32,093,716,287.09** zilikusanywa na Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) na kuhifadhiwa katika akaunti maalum ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

164. Mheshimiwa Spika, Taasisi za Sekta ya Mawasiliano katika mwaka wa fedha 2016/17 zilipata faida na hivyo zimetoa gawio Serikalini la jumla ya **Shilingi 81,558,042,398.00** kwa mchanganuo ufuatao; Mamlaka ya Mawasiliano imetoa **Shilingi 79,808,042,398.00**; Shirika la Mawasiliano limetoa **Shilingi 1,500,000,000.00** na Shirika la Posta limetoa **Shilingi 250,000,000.00**

Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

165. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Sekta ya Mawasiliano ilitengewa kiasi cha **Shilingi 3,856,423,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,930,485,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 1,925,938,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 **Shilingi 2,728,316,826.97** zilikuwa zimetolewa na Hazina. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,096,153,572.00** zimetolewa kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 1,632,163,254.97** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Bajeti ya Maendeleo

166. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Sekta ya Mawasiliano ilitengewa jumla ya **Shilingi 15,000,000,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo zikiwa ni fedha za ndani. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 **Shilingi 3,670,500,020.00** zilikuwa zimetolewa na Hazina.

Ukuaji wa Sekta ya Mawasiliano

167. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mawasiliano imeendelea kuwa moja ya sekta zinazochangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba,

2018 Sekta ya Mawasiliano ilikua kwa **asilimia 14.7** ikilinganishwa na **asilimia 13.1** kwa kipindi kama hicho mwaka 2017/2018. Aidha, kuna ongezeko kubwa la huduma kwa wananchi zinazotolewa na Serikali na pia sekta binafsi kuitia mawasiliano ya simu za kiganjani kama vile kutuma na kupokea pesa, kununua umeme, kulipia huduma za maji na ving' amuzi. Ni wazi huduma za mawasiliano zimechangia kurahisisha utendaji kazi na kuboresha maisha ya wananchi kijamii na kiuchumi kutokana na kupata huduma mbalimbali kwa uwazi, urahisi, haraka na pasipo na ubaguzi. Vilevile, ukuaji wa sekta ya mawasiliano umesaidia Serikali kuimarisha ukusanyaji wa kodi na maduhuli kwa kutumia mifumo ya TEHAMA.

168. Mheshimiwa Spika, laini za simu za viganjani zimeongezeka kutoka **40,080,954** mwaka 2017 hadi **43,621,499** mwaka 2018 na idadi ya watumiaji wa intaneti iliongezeka kutoka **22,995,109** mwaka 2017 hadi kufikia **23,142,960** mwaka 2018. Vituo vya kurusha matangazo ya redio vimeongezeka kutoka vituo 156 mwaka 2017 hadi kufikia vituo 158 mwaka 2018 na vituo vya kurusha matangazo ya luninga kwa kutumia mitambo iliyosimikwa ardhini vimeongezeka kutoka vituo 34 mwaka 2017 hadi kufikia vituo 37 mwaka 2018. Pia, watoa huduma za mawasiliano ya simu na posta wameongezeka na kuleta ushindani wenye tija na ufanisi nchini kwa sekta zote.

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

169. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mawasiliano imeendelea na maandalizi ya utekelezaji wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa awamu ya III sehemu ya II kwa lengo la kuboresha matumizi ya miundombinu hiyo na kuwezesha upanuzi wa Mkongo hadi kwenye makao makuu ya wilaya zote nchini. Katika kipindi cha mwaka 2018/2019, Wizara imewezesha ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za Mkongo wa Taifa katika maeneo ya Tukuyu, Kibaha, Kahama, Ifakara, Kidatu na Mafinga. Hii imepelekea kuongeza maeneo na kuboresha

upatikanaji wa huduma ya Mkongo wa Taifa ili kuendelea na jitihada za kuhakikisha wananchi wanapata huduma za mawasiliano katika ngazi za wilaya kwa gharama nafuu. Aidha, kwa mwaka 2018/2019 Wizara imeendelea na programu ya kuunganisha taasisi za Serikali kwenye Mkongo wa Taifa ambapo Halmashauri kumi (10) za Katesh, Sikonge, Mbulu, Monduli, Kaliua, Urambo, Kiteto, Simanjiro, Uvinza na Wanging'ombe zimeunganishwa na Mkongo wa Taifa na hatua ya mwisho ya uhakiki wa maunganishohayoinaendelea. Kuunganishwa kwa taasisi hizi kunaboresha upatikanaji wa huduma bora za mawasiliano hivyo kuongeza ufanisi wa mifumo inayotumiwa na halmashauri ikiwemo ya ukusanyaji fedha, rasilimali watu, ya mawasiliano ndani ya serikali (Electronic Office, Government Mailing System) na mingine inayotumiwa kwenye ngazi ya halmashauri.

170. *Mheshimiwa Spika*, kuongezeka kwa kasi ya matumizi ya TEHAMA kumeleta uhitaji mkubwa wa kuendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kupitia ujenzi wa mifumo mbalimbali ya TEHAMA nchini. Kwa mwaka 2018/2019 Wizara imepanua na kuboresha mfumo wa kuwezesha mikutano kwa njia ya mtandao yaani 'Video Conferencing' katika maeneo yafuatayo:- Ofisi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ofisi ya Rais wa Serikali ya Mapinduzi - Zanzibar, Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi – Zanzibar, Ofisi ya Waziri Mkuu, Makao makuu ya OR-TAMISEMI na Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa ambapo kwa sasa Wizara na Ofisi hizo zinaweza kufanya mikutano na kuongea kwa wakati mmoja kwa kupitia ama 'Audio/Video' au 'Web Conference' kuliko ilivyokuwa awali.

171. *Mheshimiwa Spika*, Wizara inaendelea na taratibu zitakazowezesha kufikisha huduma ya Mkongo wa Taifa katika ofisi ambazo hazina huduma ya mkongo. Ofisi hizo ni pamoja na Halmashauri za Siha, Ngorongoro, Nyang'hwale, Bukombe, Mbogwe, Kyerwa, Nsimbo, Mlele, Buhigwe, Malinyi, Buchosa, Kalambo, Ushetu, Busokelo, Momba na kituo cha Manyovu. Aidha, uunganishwaji huu utahusisha vituo vya

afya, polisi, posta, mahakama na taasisi nyingine ili kuboresha huduma kwa wananchi zitakazotolewa na taasisi hizo. Utekelezaji huu unafanyika kulingana na upatikanaji wa fedha za maendeleo.

172. *Mheshimiwa Spika*, kituo cha Taifa cha Kutunza Data cha Dar es Salaam (Internet Data Centre) kimeendelea kutoa huduma bora kwa taasisi za Serikali na taasisi binafsi. Kituo kimeweza kuongeza kutoka wateja 52 mwaka 2017/2018 hadi wateja 79 mwezi Desemba, 2018.

Huduma za Mawasiliano kwa Wote

173. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) imepeleka huduma za mawasiliano katika kata 530 zenye vijiji 2,132 na wakazi zaidi milioni 3.6. Aidha, tarehe 13 Desemba, 2018, Mfuko umesaini mikataba ya kipeleka huduma za mawasiliano katika kata 173 nchini ambapo utekelezaji wake unatarajiwaa kukamilika Septemba, 2019. Kata hizi zina vijiji 369 na wakazi zaidi ya milioni 1.8

174. *Mheshimiwa Spika*, Serikali iliingia mkataba na Kampuni ya simu ya Viettel kufikisha huduma ya mawasiliano vijijini mwaka 2014. Kupitia makubaliano hayo, kampuni ya simu ya Viettel ilipewa jukumu la kufikisha huduma ya mawasiliano kwenye vijiji 4,000. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 tayari huduma ziliikuwa zimefika katika maeneo husika.

Mpango wa Anwani za Makazi na Postikodi

175. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI na wadau wengine inatekeleza Mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi nchini ikiwa ni utekelezaji wa Sera ya Posta ya mwaka 2003 inayoelekeza kuwepo kwa Anwani za kitaifa zitakazorahisisha utoaji wa huduma mbalimbali za kijamii pamoja na ufikishaji wa barua, nyaraka na vipeto majumbani na maofisini. Mfumo huu unatoa anwani ya makazi hivyo kurahisisha na kuongeza wigo wa kukusanya mapato, utoaji/ufikishaji wa huduma mahali alipo mwananchi na kuwezesha kufanyika kwa biashara mtandao. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kila mwananchi anakuwa na anwani za makazi.

176. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/19 viongozi na watendaji katika Halmashauri mbalimbali wamejengewa uelewa na uwezo katika kusimamia na kutekeleza mfumo huu. Sambamba na elimu inayotolewa, uwekaji wa miundombinu unaendelea katika Kata 48 za Halmashauri za majiji ya Mwanza, Tanga na Dodoma; Manispaa za Illemela, Shinyanga, Morogoro na Moshi; Wilaya za Chato, Bahi na Chamwino; na Miji ya Geita na Kibaha.

177. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2018/19, kazi ya uwekaji wa nguzo zinazoonyesha majina ya mitaa na namba za nyumba unakamilishwa katika kata 48 za Majiji ya Dodoma, Mwanza na Tanga; Manispaa za Illemela, Shinyanga, Morogoro na Moshi; Wilaya za Chamwino, Chato, Bahi, na miji ya Geita na Kibaha. Aidha, maandalizi ya kuweka miundombinu yanaendelea katika Mji wa Serikali, Dodoma na Kata 63 katika Halmashauri nyingine 11. Halmashauri hizo zipo katika mikoa ya Lindi, Mbeya, Kagera, Arusha, Mtwara, Ruvuma, Kigoma, Simiyu, Katavi, Mara na Tabora.

UTENDAJI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA SEKTA YA MAWASILIANO Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

178. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imeendelea kusimamia Mfumo wa Kuhakiki na Kusimamia Huduma za Mawasiliano (TTMS) kwa ufanisi ili kuhakikisha kuwa mapato yanayopatikana yanawasilishwa Hazina. Mapato ya TTMS yaliyotokana na idadi ya dakika za mawasiliano ya simu za kimataifa zilizoingia hapa nchini, kuanzia mwezi Oktoba, 2013 hadi mwezi Februari, 2019 ni **Shilingi 97,169,479,672.66**

179. Mheshimiwa Spika, Mfumo wa TTMS umewezesha: Kuhakiki ubora wa huduma za Mawasiliano; Kutoa takwimu za mawasiliano yanayofanyika ndani na nje ya nchi (international and local traffic); Kutambua mapato na takwimu za miamala ya fedha mtandao (mobile money transaction); Kugundua mawasiliano ya ulaghai (fraudulent traffic); Kubaini na kufungia simu zenye namba tambulishi zilizonakiliwa (Duplicate IMEIs) ambapo taarifa hii inapatikana kwenye rajisi ya namba tambulishi ya simu; Kutambua taarifa

za laini ya simu (SIM Card profile) na namba tambulishi za kifaa cha mawasiliano, "Central Equipment Identification Register" (CEIR) pamoja na utambuzi wa mapato.

180. Mheshimiwa Spika, Moduli ya Utambuzi wa Mapato yatokanayo na Huduma za Mawasiliano ya Simu (Telecommunication Revenue Assurance System - TRAS) ni Mfumo wenge uwezo wa kuhakiki mapato yatokanayo na huduma za mawasiliano pamoja na huduma nyingine zinazotumia mitandao ya Makampuni ya simu za mkononi kufanya miamala ya kifedha au kulipia huduma nyingine. TRAS pia inatupatia takwimu mbalimbali zinazotoa taswira halisi juu ya matumizi ya huduma za mawasiliano katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Mfumo huu unasaidia kuongeza ufanisi katika kusimamia Sekta ya Mawasiliano pamoja na kwenda sambamba na kasi ya mabadiliko yanayotokea katika sekta ya mawasiliano duniani kote.

181. Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa mfumo huu ulijengwa pasipo gharama za ziada kwa Serikali kufuatia maagizo yaliyotolewa na Mhe. Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli mwaka 2016.

182. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia TCRA inaendelea kusimamia kwa ufanisi uendeshaji wa Mfumo wa Rajisi wa Namba Tambulishi za simu za kiganjani (CEIR) hivyo kuwezesha kudhibiti matumizi ya simu ambazo hazina ubora (bandia). Simu bandia haziwezi tena kuunganishwa na mtandao wowote wa simu hapa nchini. Tangu mfumo uanze kufanya kazi mwezi Oktoba, 2013 hadi kufikia mwezi Februari, 2019 idadi ya namba tambulishi (IMEIs) zilizofungiwa zilikuwa takribani 2,160,682. Mfumo wa CEIR umepunguza kwa kiasi kikubwa wizi wa simu za mkononi kwani mara mteja anapoibowi simu yake na kutoa taarifa simu hiyo inafungiwa mara moja. Aidha, TCRA kwa kushirikiana na wadau wengine inatekeleza mfumo utakaowawezesha watakaopoteza simu au laini za simu kupata ripoti ya polisi kwa njia ya mtandao (online).

183. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya

Mawasiliano imeendelea na zoezi la kuzitambua na kuzifungia namba za simu ambazo zimekuwa zikiingiza mawasiliano ya simu za kimataifa kwa njia za ulaghai. Kabla ya udhibiti huu, mawasiliano kwa njia ya ulaghai yamepelekea watoa huduma kukosa mapato na hivyo kama nchi kupoteza mapato. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Februari, 2019, TCRA imefanikiwa kupunguza mawasiliano ya simu za kimataifa kwa njia ya ulaghai kutoka asilimia 15 (Julai 2018) hadi kufikia chini ya asilimia 5 (Februari 2019).

184. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mawasiliano imeendelea kukua kwa kwa kasi kutoptera na mabadiliko ya Teknolojia. Mabadiliko haya yamekuja na changamoto mbalimbali za usalama na uhalifu katika mitandao. Changamoto hizi ni pamoja na ulaghai, utapeli, wizi n.k. Serikali kupitia TCRA inaendelea kudhibiti vitendo hivi kwa kujenga uwezo kwa watumishi wake pamoja na kushirkiana kwa karibu na vyombo vya ulinzi na usalama. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2018, TCRA iliratibu na kuwezesha mafunzo ya uchunguzi wa vifaa vya kielektroniki na mawasiliano kwa kuvishirkisha vyombo vingine vya ulinzi na usalama kwa lengo la kukabiliana na ongezeko la uhalifu katika mitandao.

185. Mheshimiwa Spika, naomba nitoe wito kwa wananchi watumie vizuri huduma za mawasiliano kwa kuwa zinachangia ukuaji wa uchumi na maendeleo ya taifa letu na tuepuke matumizi yasiyo sahihi ya huduma hizo kwa kutoitumia katika kufanya uhalifu na wizi kwa njia ya mtandao; vitendo vinavyo kuka maadili, mila na desturi zetu na uvunjifu wa amani. Aidha, nawahimiza wananchi tuendelee kulinda miundombinu ya Mawasiliano kwa kuwa ni muhimu katika kukuza uchumi wetu.

Shirika la Posta Tanzania (TPC)

186. Mheshimiwa Spika, Shirika la Posta limeendelea kusambaza barua, nyaraka, na vipeto kupitia masanduku ya barua na huduma ya Posta Mlangoni kwenye maeneo yenye miundombinu ya Misimbo ya Posta na Anwani za Makazi. Jitihada za Serikali zinaendelea ili kuwezesha huduma za

Posta kuwafikia wananchi wengi zaidi kuititia miundombinu hiyo.

187. Mheshimiwa Spika, Shirika limeendelea kuimarisha huduma za Duka Mtandao kuititia maduka yake mawili yaliyoanzishwa kuititia tovuti: <http://www.stamps.tz.post> kwa ajili ya wakusanyaji na biashara za stempu na <http://www.postashoptz.post> kwa ajili ya kutangaza na kuuza bidhaa mtambuka hapa nchini na hata nje ya nchi. Bidhaa hizo ni pamoja na sanaa za kazi za mikono na bidhaa za viwandani.

188. Mheshimiwa Spika, Shirika la Posta limeunganisha ofisi 158 katika mfumo wa uendeshaji wa kielektroniki ambao huwezesha huduma zote kutolewa kimtandao. Shirika pia limeunganisha mikoa ya Dar es Salaam na Pwani katika Mifumo ya Malipo ya Kielektroniki ya Serikali (GePG) na EFD. Vilevile, Shirika linaendelea kuimarisha vituo vya kutolea intaneti kwa wananchi ambavyo vinasaidia jamii kupata huduma kuititia mtandao kama vile matokeo ya mitihani, nafasi za kozi mbalimbali na nafasi za ajira.

189. Mheshimiwa Spika, Shirika linaendelea kuendesha Kituo cha Huduma Pamoja/Jamii Centre katika Posta Kuu ya Dar es Salaam ambacho kinawezesha upatikanaji wa huduma za kiserikali mahali pamoja. Upanuzi wa kituo hiki unaendelea kufanywa. Aidha, Shirika linaendelea kuboresha majengo na kuweka muonekano mzuri. Katika mwaka 2018/19, Shirika limeboresha majengo yake katika mikoa ya Dodoma, Mwanza, Arusha, Morogoro, Kigoma na Mjini Magharibi kwa upande wa Zanzibar. Vilevile katika kuimarisha usalama wa mali za wateja kamera za ulinzi (CCTV) zimenunuliwa na kufungwa katika Ofisi za mikoa ya Dodoma, Kigoma, Kagera, Mwanza na Mjini Magharibi.

Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL)

190. Mheshimiwa Spika, Shirika limeongeza idadi ya wateja hai (Active Customers) wa huduma mbalimbali za mawasiliano (voice na data) kutoka wateja 488,537 mwaka 2017/18 hadi kufikia wateja 1,074,642 mwezi Februari, 2019.

Ongezeko hili limepelekea shirika kufikia asilimia 2 ya soko la wateja wa mawasiliano Tanzania kutoka asilimia 0.8 mwaka 2017/18. Aidha, Kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote Shirika linatekeleza mradi wa kupeleka mawasiliano vijiji ni awamu ya tatu (Special Zone) ambapo kata 12 zitafikiwa na huduma hii. Pia Shirika limepata zabuni nyingine ya kupeleka mawasiliano katika kata 64 ambapo mradi huo unatarajia kukamilika mwezi Septemba,2019.

191. Mheshimiwa Spika, Shirika kwa mwaka wa pili mfululizo limeendelea kupata faida na kuondoka katika Mashirika yaliyokuwa yakijiendesha kwa hasara. Kwa mwaka wa fedha 2018/19, Shirika limepata faida baada ya kodi ya Shilingi bilioni 8.3 na hivyo linataraja kutoa gawio la shilingi bilioni 2.1. Aidha, Shirika limejiunga katika Mfumo wa Malipo wa kielektroniki wa Serikali (GePG) ili kurahisisha ukusanyaji wa mapato. Vilevile, Shirika limeendelea kusimamia Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano nchi nzima kwa Ufanisi ambapo makampuni ya Simu, sekta binafsi, Serikali na taasisi zake zinanufaika na huduma hizo za Mkongo.

192. Mheshimiwa Spika, Shirika limeendelea kutoa huduma za fedha kwa njia ya mtandao kupitia TTCL Pesa (T-PESA) ambapo tangu ilipoanzishwa mwezi Julai, 2017 hadi mwezi Machi, 2019 ilikuwa na jumla ya watumiaji wa huduma hiyo 351,000 na jumla ya mawakala 10,000. Ili kutanua wigo wa biashara T-PESA imeunganishwa kwenye mfumo wa malipo wa serikali wa GePG, benki na watoa huduma zamawasiliano wengine. Katika kuboresha huduma hii, T PESA inatarajia kuanzisha miamala ya fedha kwa njia ya kadi (Cashless Transaction).

Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)

193. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote iliendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya kupeleka huduma za mawasiliano katika kata 530 zenye vijiji 2,132 na wakazi zaidi milioni 3.6 ambayo imekamilika. Aidha, tarehe 13 Desemba, 2018, Mfuko umesaini mikataba ya kupeleka huduma za mawasiliano katika kata 173 zingine

nchini ambapo utekelezaji wake unatarajiwa kukamilika mwaka wa fedha 2019/20. Kata hizi zina vijiji 369 na wakazi zaidi ya milioni 1.8.

194. Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imetoa fedha (Shilingi Milioni 165.3) kwa ajili ya ukarabati wa vyumba katika ofisi za Shirika la Posta vitakavyotumika kama vituo vya TEHAMA katika ofisi za posta pamoja na ununuzi wa vifaa vya mtandao na samani.

195. Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imetoa mafunzo ya TEHAMA kwa waalimu 569 wa shule za umma. Aidha, Mfuko umetoa jumla ya fedha Shilingi milioni 57.9 kwa ajili ya ukarabati wa vyumba viliviyotengwa kwa ajili ya mitambo ya kutolea huduma ya tiba mtandao katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Taasisi ya Mifupa (MOI).

Tume ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICTC)

196. Mheshimiwa Spika, Tume imefanya utafiti wa kubaini utayari wa sekta juu ya Mfumo wa usajili na utambuzi wa wataalam wa TEHAMA nchini. Utafiti unaonyesha kuwa, wataalam wa TEHAMA hawajasajiliwa na Bodi za utaalam. Kutokana na kuongezeka kwa mifumo ya TEHAMA na ukuaji wa Viwanda vinavyotumia teknolojia ya TEHAMA (automation), kuna uhitaji mkubwa wa wataalamu. Idadi ya wataalam wa TEHAMA inaonekana ni ya kuridhisha japokuwa uwezo na maadili yao ya utaalam yanahitaji udhibiti. Aidha, Matokeo haya ya utafiti kuhusu uhitaji wa kusajili wataalam katika TEHAMA, yanafanyiwa kazi ili kupata sheria itakayosimamia jambo hili. Vilevile Mfumo wa Kielektroniki wa kusajili wataalam wa TEHAMA nchini (Online ICT Professional Registration System), umeandaliwa ili kuwezesha kukusanya takwimu za wataalamu hao.

197. Mheshimiwa Spika, Tume imeendelea kutekeleza programu ya kuwajengea uwezo na kukuza utaalam wa TEHAMA kwa kuandaa kongamano la mwaka la wataalam wa TEHAMA mwezi Oktoba 2018 na kongamano la usalama mtandaoni mwezi Machi, 2019. Aidha, Tume imefanya

mikutano ya vijana ya kuhamasisha TEHAMA katika vyuo vya elimu ya juu mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Dodoma.

198. Mheshimiwa Spika, Tume inaendelea kufanya upembuzi yakinifu wa kuanzisha kituo cha kufanya maboresho vifaa vya TEHAMA (value addition of used ICT equipment) ili kulinda mazingira na kuongeza mchango wa TEHAMA katika uchumi wa viwanda nchini.

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA CCC)

199. Mheshimiwa Spika, Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA CCC) ni taasisi yenye jukumu la kulinda na kutetea maslahi ya watumiaji wa huduma za mawasiliano zinazodhibitiwa kisheria na TCRA. Katika mwaka 2018/2019 Baraza limeendelea kutoa elimu na kuhamasisha watumiaji wa huduma na bidhaa za mawasiliano juu ya fursa na masuala muhimu kwa watumiaji wakiwemo vijana, wajasiriamali, viongozi wa serikali za mitaa, Asasi za Kiraia, viongozi wa dini na watumiaji wenyewe mahitaji maalum mfano wenyewe changamoto ya kusikia na kuona. Aidha, Baraza kupitia Kamati za Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano zilizopo katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Morogoro, Iringa, Lindi, Mtwara, Mwanza, Tanga, Mbeya na Mjini Magharibi – Zanzibar linaendelea na jukumu lake la kuelimisha na kuhamasisha watumiaji kuanzia ngazi ya chini kabisa kwenye jamii.

B.4 TAASISI ZA MAFUNZO

200. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inasimamia vyuo vya mafunzo vifuatavyo:

Chuo cha Ujenzi Morogoro

201. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/19, Chuo cha Ujenzi kiliendelea kutoa mafunzo ya ufundi katika fani mbalimbali ikiwemo umeme, uashi, magari, bomba, barabara na madaraja, uchomeaji (welding), mitambo, uchoraji wa ramani za majengo pamoja na udereva wa magari na mitambo.

Hadi Machi, 2019 Chuo kimetoa mafunzo kwa jumla ya wanafunzi **1,186** wa fani mbalimbali. Kazi nyingine zilizotekelawa ni ununuzi wa vitendea kazi na vifaa vya kufundishia, ukarabati wa zana za kufundishia, ukarabati wa majengo ya Chuo pamoja na ujenzi wa karakana ya mafunzo ya barabara.

Chuo cha Matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi Mbeya (Appropriate Technology Training Institute - ATI)

202. Mheshimiwa Spika, Chuo hiki kilianzishwa kwa lengo la kuratibu, kutoa na kuendeleza matumizi stahiki ya teknolojia ya nguvukazi katika ukarabati na matengenezo ya barabara nchini.

203. Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2019 Chuo kimetekeliza majukumu mbalimbali ikiwemo kutoa mafunzo ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi ya ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe kwa wasimamizi wa barabara kutoka Taasisi na sekta binafsi; kuendesha mafunzo ya ujenzi wa barabara za lami pamoja na kutoa mafunzo kwa njia ya vitendo kupitia barabara za mafunzo ambapo kilomita 0.5 zilikarabatiwa katika Halmashauri ya Rungwe na kilomita 21 zilizo chini ya Wakala wa Barabara (TANROADS) Mbeya zilifanyiwa matengenezo ya kawaida kwa ajili ya mafunzo kivitendo. Chuo pia kimefanya uhamasishaji kwa kutangaza huduma na mafunzo yatolewayo na Chuo kupitia makongamano na maonyesho ya Nanenane pamoja na kuhamasisha matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika Halmashauri za Mikoa ya Iringa, Njombe, Morogoro, Mbeya, Songwe, Lindi, Tabora, Shinyanga, Dodoma, Rukwa, Ruvuma, Singida na Mwanza. Kazi nyingine ni kuwaendeleza kitaaluma watumishi wa Chuo; kufanya ukarabati wa miundombinu ya Chuo ili kuboresha huduma kwa watendaji wake na washiriki wa kozi pamoja na kufanya matengenezo ya magari na mitambo ya mafunzo.

Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI)

204. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, DMI

imeendelea kutoa mafunzo katika taaluma mbalimbali za uchukuzi baharini. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019, DMI ilitekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kukamilisha ukarabati wa meli ya mafunzo ambayo kwa sasa ipo kwenye majaribio;
- (ii) Kupata Hati miliki ya eneo lenye ekari 500 lilitopo Mkuranga;
- (iii) Kukamilisha kazi ya kupitia mitatu (3) kwa lengo la kuiboresha na kuandaa Mitaala mitano 5 mipyä;
- (iv) Kuthibitishwa kwa Mtaala wa Shahada ya Uzamili katika taaluma ya Uchumi wa Bahari na Usafirishaji Shehena; na
- (v) Kupeleka Walimu watano (5) nchini China kwa ajili ya masomo ya juu kwenye fani ya Bahari.

Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)

205. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) ili kiwe kituo bora kinachokidhi mahitaji ya Sekta ya Uchukuzi. Katika mwaka 2018/2019, Chuo kilitoa kozi ndefu 21 ambapo jumla ya wanafunzi 2,877 walidahiliwa ikilinganishwa na lengo la wanafunzi 2,500. Hili ni ongezeko la asilimia 15. Kwa sasa, Chuo kina jumla ya wanafunzi 6,688. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya wanafunzi 1,550 walihitimu mafunzo ya kozi ndefu ikilinganishwa na wanafunzi 1,125 waliohitimu katika mwaka wa masomo 2017/2018. Hili ni ongezeko la asilimia 38.

206. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, Chuo kilianza rasmi kutoa mafunzo ya kozi ya Uhudumu wa Ndani ya Ndege (Cabin crew course) baada ya kupata ithibati kutoka Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA). Jumla ya wanafunzi 24 walidahiliwa na kuhitimu mafunzo hayo. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya Wanafunzi 16 walihitimu kwa mara ya kwanza kozi ya Uhandisi wa Matengenezo ya Ndege. Chuo kinaendelea kufuatilia ithibati (Approved Training Organisation - ATO) ya kutoa mafunzo ya urubani kutoka TCAA.

207. Mheshimiwa Spika, Chuo kimeendelea kukagua magari katika kituo chake cha ukaguzi wa magari kilichoko katika eneo la Chuo, Mabibo. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019, Chuo kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kilikagua jumla ya magari 2,656 ikilinganishwa na lengo la magari 1,500. Hili ni ongezeko la asilimia 77. Chuo kinaendelea kukamilisha upembuzi yakinifu kuhusu kikipandisha hadhi Chuo cha NIT kuwa Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Usafirishaji. Utafiti huo unafanywa na Timu ya wataalam kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. Aidha, Chuo kimepata kiwanja chenye ukubwa wa hekta 60 katika Kiwanja Cha Ndege Cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA) kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kufundishia urubani pamoja na kiwanja chenye ukubwa wa ekari 150 katika eneo la Kikwetu mkoani Lindi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya uanzishwaji wa mafunzo ya Sayansi ya Bahari.

Chuo cha Usafiri wa Anga Dar es Salaam (CATC)

208. Mheshimiwa Spika, mafunzo ya shughuli za usafiri wa anga na uendeshaji wa viwanja vya ndege yameendelea kutolewa na Chuo cha Usafiri wa Anga Dar es Salaam. Aidha, Chuo kimeendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi wanaotoka katika nchi za Uganda, Botswana, Namibia, Swaziland, Zambia, Burundi, Rwanda, Somalia, Nigeria, Liberia, Sierra Leone na Guinea. Mazungumzo na nchi za Sudan na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo yanaendelea ili Chuo kianze kutoa mafunzo kwa wataalam wa usafiri wa anga kutoka katika nchi hizo. Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2000 hadi Machi, 2019, Chuo kimeshatoa wahitimu 6,163. Kati yao, wazawa ni 5,183 na waliotoka nje ya nchi ni 980.

Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma

209. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma ili kuweka mazingira bora ya ufundishaji. Katika mwaka 2018/2019, jumla ya wanafunzi 58 walidahiliwa. Kati ya hao, wanafunzi 30 walikuwa ngazi ya cheti na 28 ngazi ya diploma. Aidha, jumla ya wanafunzi 43 walihitimu mafunzo yao ambapo wanafunzi 26 walihitimu mafunzo ya hali ya hewa katika ngazi ya cheti

na 17 walihitimu mafunzo ya hali ya hewa katika ngazi ya Diploma.

B. 5 MASUALA MTAMBUKA

Ushirikishwaji wa Wanawake Katika Kazi za Barabara

210. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza ushiriki wa wanawake katika kazi za barabara. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kuchapisha nakala 450 za miongozo ya ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za barabara kuzisambaza kwa wadau na kufanya ukaguzi, ufuatiliaji na tathmini ya kazi zilizofanywa na makandarasi pamoja na vikundi vya wanawake katika mikoa ya Mara, Geita, Simiyu, Mwanza, Shinyanga, Songwe, Njombe na Rukwa. Kazi nyingine ni kutoa elimu kwa wadau kuhusu Mwongozo wa Ushirikishwaji Wanawake katika kazi za barabara kuititia Warsha mbalimbali pamoja na kutoa mafunzo kwa makandarasi wanawake hamsini (50) katika mkoa mpya wa Songwe ili kuwapa ujzi wa kushiriki katika kazi za barabara kwa kutumia teknolojia ya nguvukazi. Aidha, Wizara ilifanya uhamasishaji katika shule za Sekondari za wasichana katika mikoa ya Manyara na Dodoma ili kuwahamasisha wasichana kusoma masomo ya sayansi na hisabati.

Maboresho ya Sheria Za Kisekta

211. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha na kutunga sheria za kisekta ili kuendana na sera na mwelekeo wa uchumi wa soko unaolenga kuipeleka Tanzania katika uchumi wa Kati. Tarehe 30 Januari, 2019, Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini Namba 3 ya mwaka 2019 (Land Transport Regulatory Authority – LATRA Act, No. 3, 2019) na sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania ya mwaka 2018 (The Tanzania Meteorological Authority Act, 2018). Sheria ya LATRA ilitungwa ili kuboresha udhibiti wa huduma za usafiri ardhini baada ya kutungwa kwa Sheria ya Uwakala wa Meli Na. 14 ya mwaka 2017.

206. Aidha, Sheria ya Hali ya Hewa ilitungwa ili kuratibu, kuthibiti na kudhibiti utoaji wa huduma za hali ya hewa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sheria hizi zitaanza kutumika katika mwaka 2019/2020.

Ushiriki wa Wizara Katika Jumuiya Mbalimbali za Kimataifa

212. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara imeendelea kushiriki katika masuala yanayohusu Sekta ya Ujenzi katika Jumuiya za Kimataifa na Kikanda hususan Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

213. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Wizara kupitia Sekta ya Ujenzi imeendelea kushiriki katika majadiliano kuhusu utekelezaji wa miradi ya barabara inayotekelzeza chini ya Jumuiya hiyo. Kutokana na ushiriki huo, Serikali imefanikiwa kupata fedha za kutekeleza miradi mbalimbali ambapo mapitio ya usanifu wa barabara ya Lusahunga – Rusumo (km 92) kwa upande wa Tanzania inayounganisha Tanzania na Rwanda yamekamilika chini ya ufadhili wa NEPAD-IPPF/AfDB. Aidha, Benki ya Dunia imeonyesha nia ya kugharamia ukarabati wa barabara hii. Vilevile, Benki ya Maendeleo ya Afrika imetoa fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Nyakanazi – Kasulu – Manyovu (km 260) kwa upande wa Tanzania na Rumonge – Rutunga – Bujumbura (km 45) kwa upande wa Burundi. Vilevile, mapitio ya usanifu wa kina wa barabara za Kumnazi – Kasulo – Bugene pamoja na Kyaka – Mutukula – Masaka zinazounganisha Tanzania na Uganda yanaendelea chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika.

214. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu ushiriki katika Jumuiya ya Maendeleo Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Wizara imeendelea kufuatilia makubaliano ya masuala yafuatayo;

(i) Uwianishaji wa Sheria, Kanuni, Miongozo na Viwango kuhusu usafirishaji wa mizigo mizito kwa magari makubwa kwa njia ya barabara. Majadiliano hayo yamepanuliwa na kuhusisha Jumuiya za Utatu (*COMESA*

– EAC – SADC *Tripartite Free Trade Area*) ambapo lengo kuu ni kurahisisha ufanyaji wa biashara katika Jumuiya hizo tatu kwa kuwianisha viwango vya usafirishaji wa mizigo pamoja na ujenzi wa Vituo vya Ukaguzi wa Pamoja (One stop Inspection Station – OSIS).

(ii) Majadiliano ya Biashara ya Huduma (*Negotiations on Trade in Services*) kwa Nchi Wanachama wa SADC ambayo yamelenga kufungua na kukuza fursa za utoaji huduma kwa Sekta ya Ujenzi zikiwemo kazi za ujenzi, huduma za kihandisi pamoja na huduma za ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi. Majadiliano hayo yanatarajiwaka kumamilika Juni, 2019.

(iii) Utekelezaji wa miradi ya barabara iliojumuishwa katika Mpango Kamambe wa Uendelezaji wa Miundombinu kwa Nchi Wanachama wa SADC. Miradi hiyo ni Kidatu – Ifakara – Lupiro – Malinyi – Lumecha (km 396), Matai – Kasesya (km 50), Kazilambwa – Chagu (km 36) na Makambako – Songea (Sehemu ya Lwangu - Makambako: km 87).

Rasilimali watu na Maendeleo ya Watumishi

215. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wizara, katika mwaka wa fedha 2018/2019 jumla ya watumishi 123 wa Sekta ya Uchukuzi walipatiwa mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi na watumishi 10 walipatiwa mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi. Kazi nyingine zilizotekelizwa katika kipindi hicho ni pamoja na kuandaa Mpango wa miaka mitatu (3) wa Rasilimali watu (Human Resources Plan) na Mpango wa Urithishanaji Madaraka (Succession Plan). Lengo la mipango hii ni kukabiliana na changamoto za uhaba wa watumishi walioandaliwa vizuri kulingana na mahitaji ya Sekta. Aidha, katika mwaka 2018/2019, Sekta ya Uchukuzi ilianza kazi ya kuboresha Muundo wa Utumishi wa kada za Maafisa Usafiri ili kuendana na mahitaji ya wataalam wa fani hiyo katika masuala ya uchukuzi na usafirishaji. Muundo huu utakamilika katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Masuala ya mapambano dhidi ya Rushwa

216. Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha azma ya Serikali ya awamu ya tano ya kuzuia na kupambana na Rushwa, Sekta

ya Uchukuzi kwa kushirikiana na taasisi zilizo chini yake imeandaa Mkakati wa Wizara wa miaka mitano (5) wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa (2017/2018 hadi 2021/2022). Aidha, Watumishi wameendelea kupata mafunzo yanayohusu madhara ya rushwa na umuhimu wa kuzuia vitendo vya rushwa kupitia semina na mabaraza ya wafanyakazi.

Udhibiti wa UKIMWI na Magonjwa yasiyoambukiza.

217. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu mapambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI na magonjwa yasiyoambukiza (Non Communicable diseases), katika mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kutoa elimu, mafunzo na misaada ya mahitaji muhimu kwa watumishi wote waliojitekeza kuwa wameathirika na UKIMWI.

B.6 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WIZARA NA MIKAKATI YA KUZITATUA

218. *Mheshimiwa Spika*, katika utekelezaji wa majukumu yake, Wizara ilikabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na **uwezo mdogo wa Mfuko wa Barabara kukidhi mahitaji ya matengenezo ya barabara.** Katika mwaka wa fedha 2018/19, fedha za Mfuko unatosheleza asilimia 34 tu ya mahitaji halisi ya matengenezo ya barabara nchini ikilinganishwa na asilimia 45 katika mwaka wa fedha 2017/18. Ili kukabiliana na changamoto hii, Serikali inaendelea kushirikiana na taasisi za ndani na za kimataifa kufanya tafiti za teknolojia rahisi ya matengenezo ya barabara. Aidha, Bodi ya Mfuko wa Barabara inaandaa mapendekezo ya kuongeza wigo wa vyanzo vya mapato ya Mfuko.

219. *Mheshimiwa Spika*, vilevile, Wizara ilikabiliwa na changamoto ya **mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya miundombinu.** Ili kukabiliana na changamoto hii, Wizara imeendelea kutenga fedha katika bajeti ya kila mwaka pamoja na kutafuta mikopo yenye masharti nafuu ili kutekeleza miradi ya maendeleo. Aidha, Serikali itaendelea kushawishi sekta binafsi kuwekeza katika uendelezaji na uboreshaji wa miradi ya uchukuzi;

220. Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni **uzidishaji wa uzito wa magari unaofanywa na wasafirishaji na hivyo kusababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu ya barabara**. Wizara inakabiliana na changamoto hii kwa kudhibiti uzito wa magari barabarani kuitia usimamizi wa mizani ambapo jumla ya mizani 68 zimebekwa katika Mikoa yote hapa nchini. Jitihada nyingine ni ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi (One Stop Inspection Stations - OSIS) ambavyo vinajengwa katika Ushoroba wa Kati na Ushoroba wa Dar es Salaam (TANZAM). Aidha, Wizara inaendelea na usimamizi wa utekelezaji wa Sheria ya Udhibiti wa Uzito wa Magari ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2016 na Kanuni zake ambayo imeanza kutekelezwa Machi, 2019.

221. Mheshimiwa Spika, vilevile, kuna changamoto ya **ushiriki hafifu wa Makandarasi wa ndani katika miradi mikubwa ya ujenzi**. Hii ni kutokana na kuwa na uwezo mdogo wa mitaji, utaalam na mitambo. Wizara kuitia Bodi ya Usajili wa Makandarasi, Baraza la Taifa la Ujenzi na Bodi ya Usajili wa Wahandisi imeendelea kutoa mafunzo kwa Wahandisi Washauri na Makandarasi wa Ndani ili wasimamie na kutekeleza miradi kikamilifu hususan mikataba ya ujenzi na matengenezo ya barabara. Jitihada nyingine ni kuendeleza Mfuko Maalum wa Kutoa Dhamana ya Kusaidia Makandarasi Wadogo na wa Kati unaoratibiwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi pamoja na kuhamasisha makandarasi wa ndani kujiunga ili kuomba zabuni kwa utaratibu wa ubia. Aidha, Wizara imeendelea kuwahamasisha Makandarasi wa ndani wajunge ili kupatiwa miradi maalum ambayo inatengwa kwa ajili ya kuwajengea uwezo. Miradi hiyo ni pamoja na barabara ya Makutano – Sanzate (km 50), Rudewa – Kilosa (km 24), Urambo – Kaliua (km 28) na daraja la Mlalakuwa ambalo limekamilika.

222. Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni **uharibifu/hujuma zinazofanywa na wananchi katika miundombinu ya barabara** pamoja na **wizi wa alama za barabarani**. Wizara itaendelea kusimamia Sheria zilizopo kuhusu uharibifu huo pamoja na kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa

kutunza miundombinu ya barabara kwa lengo la kupunguza uharibifu/hujuma ya miundombinu hiyo.

223. *Mheshimiwa Spika*, kuna changamoto ya mabadiliko ya hali ya hewa (Climate Change) yanayosababisha mifumo ya hali ya hewa kubadilika mara kwa mara na kusababisha **uharibifu wa miundombinu.** Kwa kutambua hili, Wizara imeendelea kupanua mtandao wa rada za hali ya hewa na kuongeza vifaa kwa lengo la kuboresha utabiri na tahadhari juu ya matukio ya hali mbaya ya hewa.

224. *Mheshimiwa Spika*, utoaji wa huduma za reli umeendelea kukabiliwa na changamoto ya **uvamizi, uharibifu na hujuma kwa miundombinu ya reli,** hususan reli zenyewe, mataruma, vifungio na madaraja. Kuhusu uvamizi wa maeneo, elimu imeendelea kutolewa kwa wananchi walijenga kwenye hifadhi ya reli kupisha utekelezaji wa miradi pamoja na wale wenye nia ya kujenga kwenye maeneo ya hifadhi ya miundombinukutofanya hivyo. Aidha, Serikali itaendelea kufanya tathmini kwa ajili ya fidia kwa wale ambao maeneo yao yatatwaliwa. Vile vile, ushirikishaji wa vyombo vyta dola pamoja na jamii inayozunguka miundombinu ya reli umeendelea kuzingatiwa ili kupambana na watu wachache wanaohujumu miundombinu ya uchukuzi.

225. *Mheshimiwa Spika*, changamoto nyingine ni ucheleweshwaji katika **upatikanaji wa makandarasi wa Ujenzi na Ukarabati wa Meli** katika Maziwa kutokana na kukosekana kwa wazabuni wanaokidhi **vigezo na sifa zinazostahili** na hivyo kusababisha taratibu za zabuni kurudiwa. Katika hili, Wizara imeendelea kushirikisha Balozi zetu zilizoko nje ya nchi kuelezea miradi ya maendeleo ili wazabuni wenye kidhi vigezo waweze kujitokeza kwa wingi katika zabuni zitakazotangazwa.

C. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA SEKTA ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20

226. *Mheshimiwa Spika*, vipaumbele vyta miradi ya Wizara

itakayotekelawa katika mwaka wa fedha 2019/20 ni miradi inayoendelea kutekelezwa ambayo ipo kwenye llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015, miradi inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo, miradi iliyoainishwa katika Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021) na Ahadi za Viongozi Wakuu wa Serikali. Aidha, Wizara itaendelea kuweka kipaumbele kwenye miradi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara na viwanja vya ndege sehemu za mipakani mwa nchi yetu na nchi jirani ili kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi.

227. Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea na juhudzi za kupunguza umaskini kwa kushirikisha vikundi vya wananchi katika kazi za ujenzi kwa kampuni na vikundi maalum kwa kutumia teknolojia ya matumizi ya nguvu kazi (Labour Based Technology - LBT). Juhudi nydingine za Serikali ni kuwashirikisha makundi maalum na makandarasi wadogo kwenye kazi za ujenzi ambazo zinatekelezwa kwa kutumia teknolojia ya matumizi ya nguvu kazi. Aidha, Wizara itaendelea na juhudzi za kuwajengea uwezo Makandarasi wa ndani ili waweze kushiriki kwenye miradi ya ujenzi.

228. Mheshimiwa Spika, katika kuongeza fursa za ajira kwa wananchi, Wizara itaendelea kuzingatia utekelezaji wa Sera ya Uwezeshaji wa Wananchi ambapo makundi maalum (wanawake, watu wenyewe mahitaji maalum na vijana) na makandarasi wadogo wa ndani watashirikishwa kikamilifu kwenye miradi ya ujenzi. Kupitia Sera hii, Wizara itaendelea na jitihada za kutenga miradi maalum ambayo itawezesha makandarasi wa ndani kutekeleza miradi hii. Aidha, Wizara imeazimia kuwa miradi yote mikubwa ya ujenzi inakuwa na mpango mahususi wa mafunzo kwa Wataalam wazawa lengo likiwa ni kuwaongeza utaalam ili hatimaye waweze kusimamia wenyewe miradi ya aina hiyo.

229. Mheshimiwa Spika, kuhusu uwazi wakati wa manunuzi na utekelezaji wa miradi ya ujenzi, Wizara itaendelea kutekeleza miradi yote kwa uwazi kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Manunuzi ya Umma ili kuepusha kuwepo kwa vitendo vya rushwa. Aidha, Wizara itachukua hatua stahiki

dhidi ya watakaobainika kukiuka sheria na taratibu zilizopo.

C.1 SEKTA YA UJENZI

Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo

230. Mheshimiwa Spika, bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Sekta ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2019/20 ni Shilingi **36,142,664,000.00**. Aidha, Sekta ya Ujenzi imetengewa jumla ya **Shilingi 1,294,051,604,268.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyo tengewa fedha ni kama inavyoonyeshwa katika **Kiambatisho Na.1**. Maeleo kuhusu Miradi ya Maendeleo ni kama ifuatavyo:

MIRADI WA KUJENGA UWEZO (INSTITUTIONAL CAPACITY BUILDING)

231. Mheshimiwa Spika, lengo la mradhi huu ni kujenga uwezo wa watumishi wa Sekta ya Ujenzi kwa kuwapatia mafunzo na vitendea kazi vya ofisi kwa ajili ya kuboresha utendaji wa Sekta ya Ujenzi. Katika mwaka wa fedha 2019/20, mradhi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 275.00** fedha za ndani.

MIRADI YA VIVUKO, UJENZI WA NYUMBA NA MAJENGZO YA SERIKALI

232. Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti usalama wa vivuko na kuepusha ajali za vyombo vya usafiri majini, Wizara inaendelea na taratibu za kuandaa Mfumo wa Usimamizi na Ufuatiliaji wa Vivuko (Ferry Management System - FMS). Mfumo huu utawezesha kufuatilia na kudhibiti mienendo ya vivuko ikiwa ni pamoja na kuangalia uzito wa mizigo pamoja na idadi ya abiria waliopakiwa kwenye vivuko vyote nchini. Mfumo huu utakapokamilika utaunganishwa katika mfumo wa ufuatiliaji na usimamizi wa utekelezaji wa miradi ya Wizara na taasisi zake ujulikanao kama *Integrated Infrastructure Management System – IIMS*. Lengo la mfumo huo ni pamoja na kurahisisha ufuatiliaji na usimamizi wa utendaji kazi katika Sekta ya Ujenzi pamoja na Taasisi zake. Mifumo mingine

itakayo jumuishwa kwenye mfumo huu ni pamoja na Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Mizani ya Kupima Uzito wa Magari (Weighbridge Data Management System), Mfumo wa Usimamizi wa Nyumba na Majengo ya Serikali (Government Real Estate Management System - GRMS), Mfumo wa Ukataji Tiketi za kwenye Vivuko Kielektroniki (e-Ticket system), Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa (Computerized Integrated Management Information System - CIMIS), Mfumo wa Utoaji Vibali via Kusafirisha Mizigo Isiyo ya Kawaida Kielektroniki (e-Permit), Mfumo wa Taarifa za Ajali za Barabaran (Roads Accident Information System) pamoja na Mfumo wa Usimamizi na Matengenezo ya Barabara (Road Maintenance and Management System - RMMS).

Ujenzi wa Vivuko na Maegesho ya Vivuko

233. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 9,574.09** kwa ajili ya miradi ya vivuko kama ifuatavyo:

i) Ujenzi wa Maegesho ya Vivuko

234. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2019/20 jumla ya **Shilingi milioni 1,551.35** zimetengwa kwa ajili ya upanuzi wa maegesho ya Kigamboni; ujenzi wa maegesho ya Bukondo na Zumacheli; ujenzi wa maegesho ya Nyamisati – Mafia; ujenzi wa maegesho ya kivuko cha Lindi – Kitunda pamoja na ujenzi na ukarabati wa maegesho ya Bugolora – Ukara, Rugezi – Kisorya, Kilambo – Namoto na Utete – Mkongo. Lengo ni kuwezesha abiria na magari kupanda na kushuka kwenye vivuko nyakati zote za mwaka.

ii) Ununuzi wa Vivuko Vipyta

235. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa **Shilingi milioni 5,922.07** kwa ajili ya manunuzi ya kivuko kipyta cha Nyamisati – Mafia, kivuko kipyta cha Bugolora – Ukara, boti moja (1) ya uokozi kwa ajili ya Lindi – Kitunda, boti nne (4) kwa ajili ya kisiwa cha Ukerewe (Ilugwa, Nafuba na Ghana) na Magogoni - Kigamboni pamoja na ununuzi wa vifaa vya karakana za TEMESA.

iii) Ukarabati wa Vivuko

236. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,100.67** kwa ajili ya kazi mbalimbali za ukarabati wa MV Tegemeo, MV Musoma, MV Mara, MV KIU, MV Sengerema, MV Ujenzi, MV Kigamboni, MV Kome II na MV Misungwi.

Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali

237. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 43,542.91** kwa ajili ya kutekeleza miradi ifuatavyo:

i) Ujenzi wa Nyumba za Viongozi na Ofisi za Serikali

238. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20 jumla ya **Shilingi milioni 13,650.52** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za viongozi wa Serikali. Fedha hizi ni kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa nyumba 50 za Viongozi, Ikulu ya Dodoma pamoja na nyumba za Majaji katika Mikoa ya Dar es Salaam(1), Kilimanjaro (1), Mtwara (1) na Shinyanga (1).

ii) Ujenzi wa jengo la ofisi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

239. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20 jumla ya **Shilingi milioni 4,255.15** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ofisi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano katika Mji mpya wa Serikali Mtumba, Dodoma.

iii) Ujenzi wa Nyumba za Makazi Eneo la Magomeni (Magomeni Quarters)

240. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20 jumla ya **Shilingi milioni 12,765.44** zimetengwa kwa ajili ya umalizaji wa nyumba za Makazi za *Magomeni Quarters*.

iv) Ukarabati wa Nyumba na Manunuzi ya Samani kwa Ajili ya Nyumba za Viongozi

241. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2019/20 jumla ya **Shilingi milioni 6,552.93** zimetengwa kwa ajili ya kukarabati nyumba za viongozi, manunuzi ya samani za Viongozi na kwenye lkulu Ndogo za Serikali, ukarabati wa nyumba zilizokuwa zinamilikiwa na Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA) pamoja na ukarabati wa nyumba zilizokuwa zinamilikiwa na TAMISEMI na NHC.

v) Kujenga Uwezo wa Wabunifu Majengo, Wakadiriaji Majenzi na Huduma za Ushauri

242. *Mheshimiwa Spika*, jumla ya **Shilingi milioni 510.61** zimetengwa kwa ajili ya kuwajengea uwezo Wabunifu Majengo (Architects) na Wakadiriaji Majenzi (Quantity Surveyors) kupitia Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB) na huduma za ushauri, usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa nyumba za Serikali zinazotolewa na Wakala wa Majengo Tanzania.

vi) Ujenzi wa Karakana za TEMESA na TBA

243. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2019/20 karakana za TEMESA zimetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,127.57** kwa ajili ya ujenzi wa karakana mpya ya kisasa ya magari jijini Dodoma; ukarabati wa karakana tano (5) zilizopo Mwanza, Arusha, Mtwara, Mbeya na MT. Depot Dar es Salaam pamoja na kuanza ujenzi wa karakana katika Mikoa mipyaya Songwe, Simiyu, Geita, Njombe na Katavi. Aidha, **Shilingi milioni 3,191.36** zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa karakana za TBA katika mikoa ya Arusha, Mwanza, Dodoma, Mbeya, Tabora na Dar es Salaam.

MIRADI YA BARABARA NA MADARAJA

244. *Mheshimiwa Spika*, miradi ya barabara na madaraja itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2019/20 ni kama ifuatavyo:

Barabara za Kuelekea Kwenye Mradi wa Kufua Umeme Katika Maporomoko ya Mto Rufiji

245. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 145.00** kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya barabara ya Bigwa – Kisaki (km 50).

Barabara ya Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro – Dodoma

246. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,605.00** kwa ajili ya kuendelea na ukarabati (*overlay*) wa barabara ya Mlandizi – Chalinze (km 44.24). Aidha, kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi wa barabara ya Kwa Mathiasi (Morogoro Road) – Msangani (km 8.3) na barabara ya Ubena Zomozi –Ngerengere (km 11.6). Kazi nyingine ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuanza ukarabati wa barabara ya Morogoro – Dodoma (km 260).

Barabara ya Wazo Hill – Bagamoyo – Msata

247. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,240.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za TAMCO – Vikawe – Mapinga (km 24) na Kisarawe – Maneromango (km 54). Aidha, kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara ya Bagamoyo (Makurunge) – Saadani – Tanga (km 246), sehemu ya Tanga – Pangani (km 50), kuendelea na maandalizi ya upanuzi wa sehemu ya Tegeta – Bagamoyo (km 46.9), ujenzi wa barabara ya Mbegani – Bagamoyo (km 7.2) na kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Makofia – Mlandizi (km 36.7).

Barabara ya Usagara – Geita – Buzirayombo - Kyamyorwa

248. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,180.00** fedha za ndani kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha

lami wa barabara za Geita – Bulyanhulu Junction (km 58.3), Bulyanhulu Junction – Kahama (km 61.7) na kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Nyamirembe Port – Katoke (km 50).

Barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora

249. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 8,542.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Urambo – Kaliua (km 28) na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu za Uvinza – Malagarasi (km 51.1) na Kazilambwa – Chagu (km 36).

Barabara ya Marangu – Tarakea – Rongai - Kamwanga/ Bomang'ombe – Sanya Juu

250. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 33,185.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kwa Sadala – Masama – Machame Junction (km 16), Kiboroloni – Kikarara – Tsuduni – Kidia (km 10.8), Kijenge – Usa River (Nelson Mandela AIST: km 14), kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Mianzini – Ngaramtoni (km 18) na upanuzi wa barabara ya Arusha – Moshi – Himo – Holili (sehemu ya Tengeru– Moshi – Himo (km 105) pamoja na mizani ya Himo.

Barabara ya Dodoma – Manyoni na Barabara ya Mchepuo kuingia Manyoni Mjini

251. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 4,320.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (One Stop Inspection Station – OSIS) cha Muhalala (Manyoni) na kununua mizani ya kupima magari yakiwa kwenye mwendo (Weigh in Motion – WIM) itakayojengwa kwenye eneo la Nala (Dodoma). **Ukarabati wa Barabara ya Port Access (Nelson Mandela)**

252. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20

mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 50.00** kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili kuifanyia upanuzi sehemu ya barabara hii hadi TAZARA (km 6) kutoka njia nne za sasa kuwa njia sita.

Barabara ya Dumila – Kilosa - Mikumi

253. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,020.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Rudewa – Kilosa (km 24).

Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port

254. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, jumla ya **Shilingi milioni 8,100.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na kazi za ujenzi wa barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112) na kuanza ujenzi wa barabara ya Matai – Kasesya (km 50).

Ujenzi wa Madaraja Makubwa

255. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 13,400.00** kwa ajili ya maandalizi ya ukarabati wa Daraja la Kirumi (Mara); kuendelea na ujenzi wa barabara unganishi katika Daraja la Sibiti (Singida); kuendelea na ujenzi wa Daraja la Ruhuhu (Ruvuma), Daraja la Jipyala Wami (Pwani), Daraja la Magara (Manyara) na Daraja la Kitengule (Kagera). Aidha, kazi nyiningine ni kuanza ujenzi wa Daraja la Sukuma (Mwanza), Daraja la Kigongo/Busisi (Mwanza), Daraja la Msingi (Singida) pamoja na kuanza maandalizi ya ujenzi wa Daraja la Mkenda (Ruvuma), Daraja la Mzinga (Dar es Salaam) na Daraja la Simiyu (Mwanza). Fedha hizi pia zitatumika kuanza usanifu na ujenzi wa Daraja la Godegode (Dodoma), kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Daraja la Mtera, Daraja la Mkundi (Morogoro), Daraja la Malagarasi Chini (Kigoma), Daraja la Ugalla (Katavi), Daraja Mitomoni (Ruvuma) na ununuzi wa Vipuri vyaa Daraja la Dharura (*Emergency Steel Bridge Parts*).

Barabara ya New Bagamoyo (Kawawa Junction – Tegeta)

256. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2019/20 jumla ya **Shilingi milioni 11,260.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza upanuzi wa sehemu ya Morocco – Mwenge (km 4.3) na kuboresha mifereji ya maji ya mvua kwenye sehemu ya Mwenge – Tegeta (km 14).

Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo

257. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2019/20, jumla ya **Shilingi milioni 735.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya fidia kwa barabara ya Bugene – Kasulo (km 124) na Omugakorongo – Kigarama – Murongo (km 105) kabla ya kuanza ujenzi wa barabara hizi kwa kiwango cha lami. Kazi nyingine ni kuendelea na mapitio ya usanifu wa kina kwa sehemu ya Kumunazi – Kasulo (km 9), Bugene – Kasulo (km 124) na Kyaka – Mutukula (km 30).

Barabara ya Isaka – Lusahunga

258. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2019/20, jumla ya **Shilingi milioni 10,660.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa sehemu ya Ushirombo – Lusahunga (km 110) na ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (One Stop Inspection Station – OSIS) cha Nyakanazi. Kazi nyingine ni kuanza ukarabati wa barabara ya Lusahunga – Rusumo (km 92) na kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Nyakahura – Kumubuga – Murusagamba/Rulenge – Murugarama na barabara ya Rulenge – Kabanga Nickel (km 141).

Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora

259. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2019/20, jumla ya **Shilingi milioni 11,330.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Nyahua – Chaya (km 85.4).

Barabara za Mikoa

260. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2019/20, jumla ya **Shilingi milioni 40,000.00** zimetengwa kwa ajili ya barabara za mikoa na madaraja katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara pamoja na programu ya kuwajengea uwezo

wahandisi wahitim (Structured Engineers Apprenticeship Programme – SEAP) kuitia Bodi ya Usajili wa Wahandisi. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ukarabati wa jumla ya kilometra **486.07** kwa kiwango cha changarawe, kujenga kilometra **40.81** kwa kiwango cha lami na ujenzi wa madaraja **12**. Orodha ya miradi ya barabara za Mikoa itakayotekelawa kwa kutumia fedha za Bajeti ya Maendeleo kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali imeonyeshwa katika Kiambatisho Na. 2.

Barabara ya Mwanza/Shinyanga Border – Mwanza

261. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, jumla ya **Shilingi milioni 290.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza upembizi yakinifu na usanifu wa kina ili kuifanya ukarabati barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mradi wa Kuondoa Msongamano Barabara za Dar es Salaam

262. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 33,120.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kilometra 4 kwenye barabara ya Kibamba – Kisopwa – Kwembe – Makondeko (km 14.66), Banana – Kitunda – Kivule – Msongola (km 14.7), Mjmwema – Kimbiji – Pembamnazi (km 30), Goba – Makongo (km 4) na Wazo Hill – Madale (km 9). Kazi nyininge ni kuanza maandalizi ya upanuzi wa barabara za Mwai Kibaki (km 9.1) na Kongowe – Mjmwema – Kivukoni (km 25.1).

Kidatu – Ifakara – Lupiro – Malinyi – Londo – Lumecha - Songea

263. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi 12,135.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu za Kidatu – Ifakara (km 68), kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Ifakara – Kihansi – Mlimba
– Taweta/Madeke (km 220.22) sehemu ya Ifakara – Kihansi (km 126.74) na sehemu ya barabara ya Ifakara – Lupiro – Malinyi – Londo – Lumecha (km 396).

Barabara ya Tabora – Ipole – Koga – Mpanda

264. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 61,560.01** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa

sehemu za Usesula – Komanga (km 115), Komanga – Kasinde (km 120) na Kasinde – Mpanda (km 118).

Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/ Loliondo – Mto wa Mbu

265. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 7,050.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu za Makutano – Sanzate (km 50) na Waso – Sale Junction (km 50). Aidha, kazi nytingine ni kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu za Sanzate – Natta (km 40), Natta – Mugumu (km 45) na Karatu – Mbulu - Hydom – Sibiti River – Lalago – Maswa (km 389): sehemu ya Mbulu – Hydom (km 50).

Barabara ya Ibanda – Itungi/Kajunjumele – Kiwira Port

266. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 6,370.00** kwa ajili ya ukarabati wa sehemu ya Ibanda – Itungi (km 27.8) na kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kikusya – Ipinda – Matema Beach (km 39: sehemu ya Tenende – Matema: km 34.6). Kazi nytingine ni kuanza ujenzi wa kilometra 7 za sehemu ya Tukuyu – Mbambo na Bujesi – Mbambo (km 10).

Barabara ya Nzega – Tabora

267. Mheshimiwa Spika, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 310.00** katika mwaka wa fedha 2019/20 kuanza kwa ajili ya kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara ya Shelui – Nzega (km 110).

Barabara ya Sumbawanga – Mpanda – Nyakanazi

268. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi 7,950.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Mpanda – Ifukutwa – Vikonge (km 35) na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa

sehemu za Kibaoni – Sitalike (km 71), Kizi – Lyambalyamfipa – Sitalike (km 86.31) na kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Vikonge – Magunga – Uvinza (km 159) pamoja na kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu ya Namanyere - Katongoro - New Kipili Port (km 64.8).

Barabara ya Nyanguge – Musoma, Mchepuo wa Usagara – Kisesa na Bulamba - Kisorya

269. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 6,350.00** katika mwaka wa fedha 2019/20 kwa ajili ya kuweka taa za barabarani katika mradi wa upanuzi wa barabara ya kwenda uwanja wa ndege wa Mwanza (km 12). Aidha, fedha hizi zitatumika kuendelea na ujenzi wa barabara za Nansio – Kisorya – Bunda – Nyamuswa (sehemu ya Kisorya – Bulamba: km 51). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara za Nyamuswa – Bulamba (km 55), Musoma – Makojo – Busekela (km 92) na kuendelea na maandalizi ya ukarabati wa barabara ya Nyanguge – Simiyu/Mara Border (km 100.4) na Makutano – Sirari (km 83).

Barabara ya Magole – Mziha – Handeni

270. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,170.00** katika mwaka wa fedha 2019/20 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu ya barabara ya Turiani – Mziha – Handeni (km 104).

Ujenzi wa Barabara za Juu (Flyovers) Jijini Dar es Salaam na Barabara Unganishi

271. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 21,953.00** katika mwaka wa fedha 2019/20 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa *Interchange* ya Ubungo pamoja na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuboresha makutano ya barabara katika maeneo ya *Fire*, Magomeni, Mwenge, Tabata/Mandela, Morocco, Buguruni pamoja na makutano ya barabara za Kinondoni/Ali Hassan Mwinyi na Selander (Ali Hassan Mwinyi/UN Road Junction). Aidha, kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi

wa *Mabey Flyovers* katika jiji la Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza.

Barabara ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi

272. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 4,830.00** katika mwaka wa fedha 2019/20 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Maswa – Bariadi (km 50). Aidha, Wizara imepanga kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Kolandoto – Mwanhuzi (km 10), Lalago – Ng’oboko – Mwanhuzi (km 74) na barabara ya Isabdula (Magu) - Bukwimba - Ngudu - Ng’hungumalwa (km 10) .

Barabara ya Tabora – Ipole – Rungwa (Sehemu ya Ipole – Rungwa)

273. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,050.00** katika mwaka wa fedha 2019/20 kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi

274. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 24,230.00** katika mwaka wa fedha 2019/20 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Kidahwe – Kasulu (km 63), Nyakanazi – Kakonko (km 50) pamoja na kuanza ujenzi wa sehemu ya Kakonko (Kabingo) – Kibondo - Kasulu - Manyovu (km 260) na barabara ya Nduta Junction - Kibondo mjini (km 25.6).

Barabara ya Dodoma University na Barabara ya Mzunguko wa Dodoma

275. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 9,040.00** katika mwaka wa fedha 2019/20 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya kutoka Ihumwa kuelekea Chuo Kikuu cha Dodoma (km 12) na Barabara za lkulu ya Chamwino pamoja na kuanza ujenzi wa barabara ya mzunguko ya Dodoma

(Dodoma Outer Ring Road: Mtumba – Veyula – Nala – Matumbulu – Mtumba: km 104). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kongwa Jct – Ng’ambi – Mpwapwa - Gulwe- Kibakwe (km 98).

Daraja la Nyerere (Kigamboni) na Barabara Uganishi

276. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2019/20 mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 60,740.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara uganishi ya Daraja la Nyerere – Vijibweni (km 1.5) na kuanza ujenzi wa barabara ya Kibada – Mwasonga – Tundwisongani Jct/ Tundwisongani – Kimbiji (km 41). Kazi nyingine ni kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Tungi – Kibada (km 3.8).

Fedha za Matengenezo na Ukarabati wa Barabara

277. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 587,389.00** kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa barabara, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, udhibiti wa uzito wa magari, usalama barabarani na mazingira, matengenezo na ukarabati wa Vivuko pamoja na kujenga uwezo wa Wizara na Taasisi zinazosimamia masuala ya Barabara na Vivuko. Fedha hizi zinasimamiwa na Bodi ya Mfuko wa Barabara.

278. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara pia itaendelea na

206. utekelezaji wa miradi ifuatayo:

Ujenzi wa Njia za Magari Mazito na Maegesho ya Dharura Katika Barabara Kuu za Ushoroba wa Kati: Jumla ya **Shilingi milioni 145.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2019/20 kwa ajili ya kuanza kazi ya usanifu wa kina wa maeneo ya kujenga njia za magari mazito kwenye miinuko na kujenga maegesho ya dharura katika barabara kuu ya Ushoroba wa Kati.

Upanuzi wa Barabara ya Kimara – Kibaha ikijumuisha Upanuzi wa Madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji: Jumla ya **Shilingi milioni 7,920.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na upanuzi wa barabara ya Kimara – Kibaha (km 25.7) kuwa njia nane pamoja na upanuzi wa madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji kwa utaratibu wa kusanifu na kujenga (*Design and Build*).

Ujenzi wa Barabara ya Kisarawe – Mlandizi: Jumla ya **Shilingi milioni 580.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2019/20 kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

Ujenzi wa Barabara ya Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju: Jumla ya **Shilingi milioni 20.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2019/20 kwa ajili ya kuanza maandalizi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu za Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho (km 12.7) na Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 21.3).

279. Mheshimiwa Spika, miradi mingine ya maendeleo ya barabara itakayoteklezwa katika mwaka wa fedha 2019/20 ni pamoja na:

Barabara ya Tunduma – Sumbawanga: Jumla ya **Shilingi milioni 4,070.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2019/20 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mpemba – Isongole (km 51.2) pamoja na kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Ruanda – Iyula - Nyimbili (km 21).

Barabara ya Kagoma – Lusahunga: Kiasi cha **Shilingi milioni 2,155.00** kimetengwa katika mwaka wa fedha 2019/20 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu za Muhutwe – Kamachumu – Muleba (km 54) na Muleba – Kanyambogo – Rubya (km 18.5). Aidha, kazi nydingine ni kuanza maandalizi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Mutukula – Bukoba – Muhutwe – Kagoma (km 136) ili kuifanya ukarabati barabara hii.

Barabara ya Singida – Babati – Minjingu: Katika mwaka wa

fedha 2019/20, kiasi cha **Shilingi milioni 240.00** zimetengwa kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Singida – Shelui (km 110).

Barabara ya Dar es Salaam – Mbagala (Kilwa Road) sehemu ya KAMATA – Bendera Tatu: Jumla ya **Shilingi milioni 4,580.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daraja la Gerezani na kuendelea na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa upanuzi wa sehemu ya Mbagala Rangi Tatu – Kongowe (km 3.8) pamoja na daraja la Mzinga.

Barabara ya Msimba – Ruaha Mbuyuni/ Ikokoto Mafinga: **Shilingi milioni 19,930.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu za Njombe – Moronga (km 53.9), Moronga – Makete (km 53.5) na Mbarali – Ubaruku (km 8.9). Kazi nyine ni kuanza ujenzi wa barabara za Rujewa – Madibira – Mafinga (km 152), Njombe – Lupembe – Madeke (km 100) na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Iringa – Msembe - Ruaha National Park (km 104). Aidha, kazi nyine ni kuendelea na mapitio ya usanifu wa kina na kuanza ukarabati wa barabara ya Makambako – Songea (km 295), kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara za Mafinga – Mgololo (km 78.0), Igawa – Songwe – Tunduma (km 218) na barabara ya mchepuo ya Uyole – Songwe (Mbeya Bypass: km 40).

Barabara ya Same – Mkumbara – Korogwe: **Shilingi milioni 1,740.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ukarabati wa sehemu za Same – Himo (km 76), Mombo – Lushoto (km 32) na kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Lushoto – Magamba – Mlola (km 34.5) na Soni – Bumbuli – Dindira – Korogwe (km 74).

Barabara ya Mbeya – Makongolosi: **Shilingi milioni 6,140.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Chunya – Makongolosi (km 43) na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Mkiwa – Itigi – Noranga (km 56.9) na Mbalizi – Makongolosi (km 50).

Barabara ya Chalinze – Segera – Tanga: Shilingi milioni 1,450.00 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Amani – Muheza (km 36).

Barabara ya Itoni – Ludewa – Manda: Shilingi milioni 4,300.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha zego sehemu ya Lusitu – Mawengi (km 50).

Daraja Jipyia la Selander: Shilingi milioni 11,020.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Daraja Jipyia la Selander (km 1.03) na barabara unganishi zenyе jumla ya urefu wa kilometra 5.2.

Barabara ya Handeni – Kiberashi – Kibaya

- **Singida: Shilingi milioni 1,450.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Handeni – Kiberashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboloti
- Mrojo Chini – Dalai – Bicha – Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro – Singida (km 460) kwa kuanzia na sehemu ya Handeni – Kiberashi (km 50).

Barabara ya Dodoma – Iringa: Shilingi milioni 950.00 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya mchepuo ya Iringa (Iringa Bypass: km 7.3).

Barabara ya Dodoma – Babati: Shilingi milioni 1,050.00 zimetengwa kwa ajili ya kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya mchepuo wa Babati (Babati Bypass: km 12).

Barabara ya Masasi – Songea – Mbamba Bay: Shilingi milioni 30,350.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za Mbanga – Mbamba Bay (km 66) na Masasi – Newala-Mtwara(sehemu ya Mtwara-Mnivata (km 50). Aidha, kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara za Masasi – Nachingwea (km 45), Mtwara – Newala – Masasi (Sehemu ya Mnivata – Tandahimba (km 50), Likuyufusi – Mkenda (km 122.5) na Kitai – Lituhi (km 90) pamoja na kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Nanganga – Ruangwa – Nachingwea (km 100), ukarabati wa barabara

ya Mtwara – Mingoyo – Masasi (km 200). Vile vile, mradi huu unahusisha kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Nachingwea – Liwale (km 130).

Barabara ya Kwenda Chuo cha Uongozi: Shilingi milioni 455.00 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ndani ya eneo la Chuo cha Uongozi Bagamoyo.

Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili hadi ya Nne: Shilingi milioni 28,797.22

280. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20 mradi huu umetengewa **Shilingi milioni 28,797.22** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka awamu ya pili inayohusisha barabara ya Kilwa (kutoka Katikati ya Jiji hadi Mbagala), Chang'ombe (kutoka makutano ya barabara ya Kilwa/Chang'ombe hadi makutano ya barabara ya Nyerere/ Chang'ombe), Kawawa (kutoka makutano ya barabara ya Nyerere/Kawawa hadi makutano ya barabara ya Morogoro/ Kawawa) na sehemu ya Sokoine Drive. Barabara hizo zina urefu wa jumla ya kilometra **20.3**. Kazi nyingine ni ujenzi wa flyovers mbili katika makutano ya barabara za Mandela/Kilwa na Nyerere/ Kawawa na ujenzi wa vituo (*depots, terminals na feeder stations*).

Kuhusu Awamu ya Tatu na Nne ya BRT, kazi zitakazofanyika ni kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara zilizopo kwenye awamu hizo. Barabara zilizopo kwenye Awamu ya tatu ni Uhuru, Nyerere, Bibi Titi na Azikiwe zenye urefu wa jumla ya kilometra **23.6**. Aidha, Awamu ya nne yenye urefu wa kilometra **25.9** itahusisha ujenzi wa barabara ya kupitia Ali Hassan Mwinyi hadi Morocco na kuendelea hadi Tegeta kupitia Mwenge. Vilevile itahusisha barabara ya Sam Nujoma na kuungana na mradi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Kwanza katika kituo kikuu cha Ubungo. Katika mwaka wa fedha 2019/20 kazi zitakazofanyika ni mapitio ya usanifu na ujenzi mradi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tatu na usanifu wa kina pamoja na ujenzi wa mradi

wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Nne. Aidha, Awamu ya Tano na Sita ya mradi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka zitafanyiwa usanifu wa kina.

Ujenzi wa Makao Makuu ya Wakala wa Barabara (TANROADS) na Ofisi za Mikoa: Jumla ya **Shilingi milioni 8,906.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Wakala wa Barabara (TANROADS) pamoja na Ofisi za Mikoa ya Dar es Salaam, Katavi, Geita, Simiyu, Njombe, Lindi na Songwe.

MIRADI YA USALAMA BARABARANI NA MAZINGIRA

281. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara itaendelea kutekeleza majukumu yanayohusu kuratibu na kuimarisha shughuli za usalama barabarani, mazingira na kudhibiti uzito wa magari yanayotumia barabara zetu. Mradi wa **Usalama Barabarani** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,700.00** kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi; uanzishwaji wa mfumo wa usimamizi wa usalama wa vivuko; ukaguzi wa usalama wa barabara; mapitio ya Sera ya Usalama Barabarani; kuendelea na ujenzi wa mizani ya kisasa ya kupima magari yakiwa kwenye mwendo mdogo (Slow Weigh in Motion Weighbridge) Mkoani Dar es Salaam pamoja na ujenzi wa miundombinu na uwekaji wa Mfumo wa Upatikanaji na Utoaji Taarifa za Ajali Barabarani katika vituo vya Polisi nchini. Kazi nyingine ni kujenga uwezo na uelewa wa masuala ya usalama barabarani kwa umma.

282. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi wa **Menejimenti ya Utunzaji wa Mazingira** umetengewa **Shilingi milioni 100.00** kwa ajili ya kuandaa mpango wa kukabili mabadiliko ya tabia nchi kwa sekta ya Ujenzi; kutoa mafunzo kuhusu kukabili mabadiliko ya tabia nchi katika sekta ya Ujenzi kwa wahandisi na mafundi sanifu; kufanya ukaguzi wa mazingira katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo; kuandaa mfumo wa TEHAMA wa ukusanyaji wa taarifa za mazingira; kutoa elimu ya usimamizi wa mazingira katika

barabara na kuandaa programu za udhibiti wa uchafuzi wa mazingira (Pollution Control Programme).

MIRADI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA VIWANJA VYA NDEGE

283. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20 miradi ya ujenzi wa miundombinu ya viwanja vya ndege imetengewa kiasi cha **Shilingi milioni 102,192.375**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 40,000.00** ni za ndani na **Shilingi milioni 62,192.375** ni za nje. Miradi ifuatayo itatekelezwa:

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kigoma

284. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20 mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 690.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 120.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 570.00** ni fedha za nje kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB). Fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Abiria pamoja na miundombinu yake (maegesho ya ndege, maegesho ya magari na barabara ya kuingia na kutoka), usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege, ujenzi wa uzio, ujenzi wa jengo la kuongozea ndege na ujenzi wa jengo la uangalizi wa hali ya hewa (OBS).

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mpanda

285. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 500.00** kwa ajili ya ujenzi wa uzio.

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Tabora

286. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20 mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 6,102.38**. Kati ya hizo, **Shilingi milioni 902.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 5,200.38** ni fedha za nje kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) kwa ajili ya ujenzi wa jengo la abiria na jengo la kuongozea ndege. Kazi nyingine ni ujenzi wa barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari pamoja na jengo la uangalizi wa hali ya hewa.

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe

287. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20 mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,700.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo la abiria, usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege, ukarabati wa tabaka la juu la barabara ya kutua na kuruka ndege, barabara ya kiungio pamoja na ukarabati wa eneo la usalama kwenye barabara ya kutua na kuruka ndege.

Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza

288. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 8,070.00**. Kati ya hizo, **Shilingi milioni 5,110.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 2,960.00** ni fedha kutoka BADEA na OFID kwa ajili ya kusimika taa za kuongozea ndege, ujenzi wa jengo jipya la abiria, maegesho ya magari, uzio wa usalama pamoja na mfumo wa maji safi, maji takaa na maji ya mvua, ujenzi wa jengo jipya la abiria, na maegesho ya magari.

Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Arusha

289. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 698.00** fedha za ndani kwa ajili ya kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege kwa meta 200 na ujenzi wa maeneo ya kugeuzia ndege. Kazi nyiningine ni ujenzi wa uzio wa usalama, ujenzi wa barabara mpya ya kuingilia kiwanjani pamoja na kukarabati maegesho ya magari.

Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara

290. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20, mradi huu umetengewa kiasi cha **Shilingi milioni 4,500.00** kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, viungilio pamoja na maegesho ya ndege. Kazi nyiningine ni kusimika taa na mitambo ya kuongozea ndege pamoja na ujenzi wa barabara ya kuingilia kiwanjani na maegesho ya magari.

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga

291. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 7,200.00**. Kati ya hizo, **Shilingi milioni 100.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 7,100.00** ni fedha za nje kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB). Kazi zitakazotekelawa ni pamoja na ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege, viungio, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uangalizi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari. Kazi nyingine ni pamoja na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege na uzio wa kiwanja cha ndege.

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga

292. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 8,850.00**. Kati ya hizo, **Shilingi milioni 100.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 8,750.00** ni fedha za nje kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB). Fedha hizo zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege, viungio, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uangalizi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege pamoja na kujenga uzio wa usalama.

Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro

293. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 100.00** fedha za ndani kwa ajili ya kufanya usanifu wa kina na maandalizi ya kuanza ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, usimikaji wa taa za kuongozea ndege na ukarabati wa maegesho ya magari.

Uendelezaji wa Viwanja vya Ndege vya Mikoa

294. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 36,282.00**.

Kati ya hizo, Shilingi milioni **16,875.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 19,407.00** fedha za nje kutoka Benki ya Dunia (WB). Fedha hizi ni kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vya ndege katika mikoa ya Geita na Simiyu pamoja na upanuzi na ukarabati wa viwanja vya ndege vya Iringa, Ruvuma (Songea), Lindi, kiwanja cha *Lake Manyara*, Tanga na Mara (Musoma). Aidha, kazi nyingine ni kumalizia ulipaji wa fidia kwa wananchi walioathirika na mradi wa kiwanja cha ndege cha Dodoma pamoja na kuanza ukarabati wa kiwanja cha Ndege cha Moshi na viwanja vingine vya mikoa.

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Msalato

295. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 11,600.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 3,100.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 8,500.00** ni fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Kazi zitakazotekelawa ni kulipa fidia kwa mali zitakazoathiriwa na utekelezaji wa mradi huu pamoja na kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mradi huu.

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Bukoba

296. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa kiasi cha **Shilingi milioni 100.00** kwa ajili ya usanifu wa kina kwa ajili ya kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege pamoja na ufungaji wa taa za kuongozea ndege.

Ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria Katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA)

297. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 13,800.00** kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo jipya la abiria (Terminal Building III). Kati ya hizo, **Shilingi milioni 4,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 9,705.00** ni fedha za nje kutoka Benki ya HSBC ya Uingereza. Kazi nyingine ni kulipa fidia kwa wakazi wa Kipunguni na Kigilagila waliohamishwa kupisha utekelezaji

wa mradi huu. Aidha, **Shilingi milioni 95.00** za ndani zimetengwa kwa ajili ya kufanya usanifu wa kina kwa ajili ya upanuzi na ukarabati wa jengo la pili la abiria (Terminal Building II).

FEDHA ZA MFUKO WA BARABARA

298. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20 jumla ya **Shilingi 587,389,000,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kufanya kazi za matengenezo na ukarabati wa barabara kuu na za mikoa. Kati ya fedha hizo, TANROADS imetengewa **Shilingi 524,103,620,000.00** kwa ajili ya matengenezo ya barabara na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Ujenzi) imetengewa **Shilingi 58,233,735,546.00** kwa ajili ya kazi za ukarabati wa barabara, upembusi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara, ukarabati na ununuzi wa vivuko, usalama barabarani pamoja na usimamizi na ufuatilajji wa miradi hiyo. Aidha, **Shilingi 5,051,644,454.00** zitatumika kugharamia uendeshaji wa Bodi ya Mfuko wa Barabara.

299. Mheshimiwa Spika, kiasi cha **Shilingi 58,233,735,546.00** ni fedha za maendeleo kutoka Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa ajili ya Wizara (Ujenzi). Kati ya hizo, **Shilingi 14,919,483,000** ni kwa ajili ya kufanya upembusi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara zenye urefu wa kilometa **5,602.73**. Kiasi cha **Shilingi 4,740,226,000.00** ni kwa ajili ya manunuzi na ukarabati wa vivuko pamoja na ujenzi wa maegesho ya vivuko; **Shilingi 2,585,578,000.00** ni kwa ajili ya miradi ya Usalama Barabarani na Mazingira na **Shilingi 4,978,984,546.00** ni kwa ajili ya kazi za usimamizi na ufuatilajji wa miradi inayotekelozwa na Wizara (Ujenzi) pamoja na kujenga uwezo wa watumishi. Aidha, miradi ya barabara za mikoa imetengewa **Shilingi 31,009,464,000.00** kwa ajili ya kufanya ukarabati wa jumla ya kilometra **407.01** kwa kiwango cha changarawe na kujenga kilometra **31.20** kwa kiwango cha lami pamoja na ujenzi na ukarabati wa madaraja **15** katika mikoa mbalimbali nchini.

Mchanganuo wa miradi itakayotekelozwa kwa fedha za Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi,

Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi) umeonyeshwa katika **Viambatisho Na. 3** na **4**.

300. Mheshimiwa Spika, jumla ya **Shilingi 524,103,620,000.00** ni fedha za Mfuko wa Barabara ambazo zimetengwa kwa ajili ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS). Fedha hizo zitatumika kufanya matengenezo ya barabara kuu na barabara za mikoa, madaraja na uendeshaji wa mizani.

Mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo umeoneshwa katika **Viambatisho Na. 5, 5A - 5D**.

MPANGO WA UTEKELEZAJI KAZI KATIKA TAASISI ZILIZO CHINI YA SEKTA YA UJENZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20

Wakala wa Barabara

301. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Wakala wa Barabara Tanzania umepanga kujenga barabara zenye urefu wa **kilometra 432.30** kwa kiwango cha lami, ujenzi wa madaraja **13** pamoja na ukarabati wa **kilometra 56** kwa kiwango cha lami katika barabara kuu. Aidha, Wakala umepanga kufanya matengenezo ya barabara kuu na barabara za mikoa ambayo yatahusisha matengenezo ya kawaida (routine and recurrent maintenance) kwa **kilometra 32,944.31** matengenezo ya muda maalum na sehemu korofi ya **kilometra 5,031.14** na matengenezo ya madaraja **3,376**. Mpango huu pia unajumuisha shughuli za udhibiti wa uzito wa magari na hifadhi za barabara, kazi za dharura pamoja na mradi wa matengenezo ya barabara kwa mikataba ya muda mrefu.

Kwa upande wa barabara za mikoa, Wakala utajenga kwa kiwango cha lami barabara zenye urefu wa **kilometra 72.01** ambapo **kilometra 40.81** zitajengwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometra 31.20** zitajengwa kwa fedha za Mfuko wa Barabara. Aidha, **kilometra 893.04** zitakarabatiwa kwa kiwango cha changarawe ambapo kati ya hizo **kilometra 486.03** na madaraja **12** yatakarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometra 407.01**

pamoja na madaraja **15** yatajengwa/yatakarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara.

302. *Mheshimiwa Spika*, vilevile, Wakala utaendelea na jukumu la kusimamia miradi ya ujenzi na ukarabati wa Viwanja vya Ndege ambapo kazi zitakazoteklezwa ni kukamilisha ujenzi wa jengo la Tatu la Abiria (Terminal Building III) katika kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA) na kuendelea na ujenzi wa kiwanja kipyä cha Ndege cha Geita. Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa jengo la Pili la Abiria (Terminal Building II) katika kiwanja cha Ndege cha Mwanza, kuanza ujenzi wa kiwanja kipyä cha Ndege cha Simiyu pamoja na maandalizi ya ujenzi wa Kiwanja kipyä cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato. Aidha, Wakala utaendelea na ukarabati wa jengo la Pili la Abiria (Terminal Building II) katika kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA), kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA) pamoja na viwanja vya Ndege vya Lindi, Arusha, Musoma, Bukoba, Moshi, Tanga, Sumbawanga, Kigoma, Tabora, Iringa, Shinyanga, Mtwara, Nachingwea, Songea, Songwe, Dodoma na viwanja vingine mikoani.

Wakala wa Majengo Tanzania

303. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2019/20 Wakala wa Majengo Tanzania umepanga kumalizia ujenzi wa nyumba 6 za majaji katika mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Kagera, Mtwara, Shinyanga na Tabora; kuendelea na ujenzi wa nyumba za Makazi, Magomeni Kota, ujenzi wa nyumba 50 za Viongozi Dodoma, nyumba 5 za watumishi mikoa ya Katavi, Simiyu, Songwe, Njombe na Geita pamoja na ujenzi wa nyumba za makazi kwenye Ikulu ya Chamwino, Dodoma.

Wakala vilevile umepanga kufanya ukarabati wa nyumba za iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA); ukarabati na matengenezo ya nyumba za viongozi Jijini Dodoma; ukarabati wa Karakana za Wakala katika mikoa ya Dar es salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya na Dodoma pamoja na ununuzi wa samani kwa nyumba 55 za

viongozi mkoani Dodoma na Mikoa mipya. Aidha, Wakala utaendelea kutoa huduma ya ushauri katika ujenzi wa majengo ya Serikali pamoja na kuendesha programu za kuwajengea uwezo Wataalam wa Ujenzi na Ushauri.

Wakala wa Ufundu na Umeme Tanzania.

304. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20, Wakala wa Ufundu na Umeme umepanga kuendelea na kazi zifuatazo: Upanuzi wa maegesho upande wa Kigamboni kwa ajili ya kivuko cha Magogoni – Kigamboni; ujenzi wa maegesho ya vivuko kati ya Bukondo na Zumacheli kwa ajili ya kivuko cha Chato – Nkome; ujenzi wa maegesho ya Nyamisati na Mafia kwa ajili ya kivuko cha Nyamisati – Mafia, ujenzi wa maegesho ya Kayenze na Bezi kwa ajili ya kivuko cha Kayenze – Bezi, ujenzi wa maegesho ya Mlimba na Malinyi kwa ajili ya kivuko cha Mlimba – Malinyi na maegesho ya Itungi *Port*. Kazi nyingine ni ujenzi na ukarabati wa maegesho ya Kigongo na Busisi kwa ajili ya kivuko cha Kigongo – Busisi, maegesho ya Kilambo na Namoto kwa ajili ya kivuko cha Kilambo – Namoto pamoja na maegesho ya Utete na Mkongo kwa ajili ya kivuko cha Utete – Mkongo pamoja na Magogoni na Kigamboni kwa ajili ya kivuko cha Magogoni - Kigamboni.

Wakala vilevile umepanga kuendelea na ujenzi wa vivuko vipyta vitakavyotoa huduma ya usafiri kati ya Nyamisati - Mafia, Bugorola – Ukara, Kayenze – Bezi na Chato – Nkome. Aidha, Wakala utafanya manunuzi ya boti tano (5) zitakazotoa huduma ya usafiri kati ya Lindi – Kitunda, Ukerewe (Ilungwa, Nafuba na Ghana) na Magogoni – Kigamboni pamoja na manunuzi ya vitendea kazi kwa ajili ya karakana za TEMESA.

305. Mheshimiwa Spika, vilevile Wakala umepanga kukarabati MV Tegemeo, MV Mara, MV Ujenzi, MV Ruhuhu na MV KIU. Aidha, Wakala unatarajia kukamilisha ukarabati wa MV Sengerema, MV Kigamboni na MV Misungwi. Wakala pia umepanga kujenga karakana tano (5) katika mikoa ya Songwe, Simiyu, Geita, Njombe na Katavi; kujenga karakana mpya ya kisasa makao makuu ya Serikali (Dodoma) pamoja na kukarabati karakana tano (5) ambazo ni karakana ya Dar

es Salaam (MT. Depot), Mtwara, Mbeya, Mwanza na Arusha. Aidha, Wakala utaendelea na jukumu lake la msingi la kufanya matengenezo ya magari ambapo magari **46,604** yatafanyiwa matengenezo. Kazi nyingine zitakazotekelezwa ni usimikaji na matengenezo ya mifumo ya umeme, elektroniki, viyoyozi na majokofu.

Bodi ya Mfuko wa Barabara

306. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Mfuko wa Barabara unatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 839,127,000,000** zitakazotumika kufanya kaziza matengenezo ya barabara nchini. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 587,389,000,000** zitatumika kufanya matengenezo ya barabara kuu na za mikoa zinazosimamiwa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na **Shilingi 251,738,000,000** zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Wilaya zilizo chini ya Ofisi ya Rais –TAMISEMI.

307. Mheshimiwa Spika, ili kuandaa mkakati endelevu wa matengenezo ya barabara nchini Bodi kwa ufadhili wa Benki ya Dunia itaendelea kufanya tathmini ya mtandao wa barabara (Road Inventory and Condition Survey) ili kubaini thamani, urefu na hali ya barabara nchini. Tathmini hiyo itawezesha kufanyika kwa mapitio ya mgawanyo wa fedha za Mfuko kati ya barabara kuu na za mikoa zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na zile za wilaya ambazo zinazosimamiwa na Ofisi ya Rais –TAMISEMI. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Ujenzi), Ofisi ya Rais – TAMISEMI, TANROADS na TARURA inatarajia kuandaa mfumo mmoja wa matengenezo na usimamizi wa barabara (Road Management & Maintenance System) utakaokidhi mahitaji ya taarifa kwa taasisi zote za Serikali zinazoshugulika na barabara. Lengo ni kuongeza ufanisi katika kutoa na kupata taarifa zinazohusu hali ya barabara na mahitaji ya matengenezo ya barabara pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji wa mifumo iliyopo (RMMS, MIS na DROMAS).

308. Mheshimiwa Spika, vilevile Bodi itaendelea kufanya utafiti wa vyanzo vipya vyta mapato ya Mfuko kwa kuzingatia

uzoefu wa kikanda na kimataifa. Aidha, Bodi itaimarisha ufuatiliaji wa ukusanyaji wa mapato ya Mfuko na kufanya tafiti juu ya maeneo ambayo yanaweza kusababisha kuvuja mapato na kuishauri Serikali ipasavyo. Bodi pia itaendelea kushirikiana na taasisi za kitafiti ili kupata teknolojia nafuu ya matengenezo ya barabara kwa lengo la kupunguza gharama na kuongeza ufanisi katika matumizi ya fedha za Mfuko. Aidha, Bodi itaendelea na ukaguzi wa ubora wa kazi za matengenezo ya barabara katika mikoa yote nchini.

Bodi ya Usajili wa Wahandisi

309. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Bodi imepanga kusajili wahandisi **2,422**, mafundi sanifu **300** na kampuni za ushauri wa kihandisi **20**. Pia Bodi imepanga kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo kwa vitendo kwa wahandisi wahitimu **3,527**. Aidha, Bodi itaendelea kufanya kaguzi za shughuli za kihandisi nchini kwenye miradi **200** na kusajili miradi **700** ili shughuli zote za kihandisi zifanywe na wahandisi waliosajiliwa na kwa kufuata maadili ya utendaji kazi za kihandisi. Bodi imepanga kutembelea na kukagua miradi yote ya ujenzi wa barabara Tanzania Bara, ikiwa ni pamoja na barabara za Halmashauri.

Bodi vilevile itaendelea kusimamia mafunzo ya kujienda kitaluma kwa wahandisi watalaam na washauri, kwa ajili ya kuwaendeleza wahandisi kwa ujumla pamoja na kuwashawishi wahandisi watalaam ili waanzishe kampuni za ushauri wa kihandisi mikoani na hivyo kusogezza huduma hii muhimu karibu na watumiaji.

Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi

310. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Bodi imepanga kusajili Watalaam **280**, katika fani za ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi. Aidha, Bodi imepanga kusajili kampuni **15** za ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi. Vilevile, Bodi imepanga kuendelea na mafunzo kwa vitendo kwa wahitimu **140** katika fani za ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi.

Bodi pia imepanga kufanya ukaguzi wa miradi ya ujenzi **2,000** katika mikoa yote, Tanzania Bara na kusajili miradi ya majengo **950**. Aidha, Bodii imepanga kuendesha mashindano ya kubuni mchoro wa jengo la zahanati la gharama nafuu ambao utatolewa kwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ili litumike katika ujenzi wa zahanati katika maeneo mbali mbali nchini. Bodii pia itaendeleza mashindano ya insha kwa wanafunzi wa sekondari, ikiwa ni njia ya kuwahamasisha kusoma masomo ya sayansi na hatimaye kusomea taaluma za ubunifu majengo, ukadiriaji majenzi na taaluma zinazoshabihiana nazo.

Bodi ya Usajili wa Makandarasi

311. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Bodii imepanga kusajili jumla ya Makandarasi **900**, kukagua jumla ya miradi ya ujenzi **3,100** pamoja na kusajili miradi **3,200**. Aidha, Bodii inataraja kuendesha kozi tatu (3) za mafunzo katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Njombe. Vilevile, Bodii imepanga kuendesha warsha mbili (2) za mafunzo ya ubia (Joint Venture) katika mikoa ya Arusha na Mwanza. Bodii pia itaendeleza mfuko maalum wa kutoa dhamana ya kusaidia makandarasi wa ndani wadogo na wa kati. Aidha, Bodii itaendelea na jitihada za kuhamasisha makandarasi wa ndani kujinga ili kupata uwezo wa kuomba zabuni kwa utaratibu wa ubia.

Baraza la Taifa la Ujenzi

312. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Baraza litaendelea na ukamilishaji wa taratibu za kulihuisa na kuliimarishe kwa kufanya mabadiliko Sheria iliyolanzisha ili liweze kutekeleza ipasavyo majukumu ya kuratibu shughuli za ujenzi nchini. Aidha, Baraza litashiriki kuanda Kanuni za Utekelezaji wa Sheria iliyolanzisha pamoja na maboresho yatakayofanyika.

313. Mheshimiwa Spika, Baraza pia litaendelea kuratibu mfumo wa kukuza uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi ya umma; kuratibu na kutoa mafunzo kwa

wadau mbalimbali katika sekta ya ujenzi; kutoa ushauri wa kiufundi na wa kitaalam kwa wadau mbalimbali wa sekta na kuratibu na kuwezesha utatuzi wa migogoro ya mikataba ya miradi ya ujenzi. Aidha, Baraza litaendelea kufanya kaguzi za kiufundi za miradi ya ujenzi; kuboresha ukusanyaji, uwekaji na utoaji wa takwimu na taarifa za Sekta ya Ujenzi kwa kuanzisha kituo maalum cha taarifa za sekta ya Ujenzi (Construction Industry Information and Data Centre) pamoja na kuandaa taarifa mbalimbali za kiufundi na kitaalam kuhusu Sekta ya ujenzi.

314. Mheshimiwa Spika, vilevile, Baraza litaendelea kuboresha uratibu wa mfumo wa kutoa taarifa muhimu za miradi ya ujenzi pamoja na kuratibu utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa kutumia teknolojia ya nguvu kazi yenye lengo la kukuza vipato nya wananchi katika maeneo husika ya miradi.

Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia Katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji Tanzania (Tanzania Transportation Technology Transfer Centre)

315. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Kituo kitaendelea na jukumu lake la kusambaza teknolojia katika sekta ya ujenzi na usafirishaji hapa nchini. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na kuandaa na kusambaza majorida ya teknolojia mbalimbali katika sekta hizo; kutoa huduma ya maktaba ya Kituo. Aidha, Kituo kwa kushirikiana na TANROADS, TARURA, Mfuko wa Barabara, taasisi za mafunzo, wataalamu binafsi na taasisi zisizo za Serikali kitaendesha mafunzo, warsha na semina kwa wadau yanayolenga kutatua changamoto za kiteknolojia zinazoikabili sekta ya ujenzi na usafirishaji.

Vikosi vya Ujenzi

316. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Vikosi vya Ujenzi vitaendelea kutekeleza miradi inayohusu; ujenzi na ukarabati wa majengo ya ofisi na nyumba za Viongozi wa Serikali, ujenzi wa maegesho ya vivuko pamoja na ukarabati wa nyumba za watumishi wa Serikali mkoani

Dodoma. Aidha, Vikosi vinatarajia kuimarisha mradi wa utengenezaji na uuzaaji wa vifaa vya ujenzi (Buildings Materials Centre) Dar es salaam na Dodoma pamoja na kuendeleza viwanja 38 vinavyomilikiwa na Vikosi vya Ujenzi Dodoma. Pamoja na kutekeleza miradi hiyo, Vikosi vitaendelea na maboresho ya kiutendaji kwa kufanya ukarabati wa karakana za Vikosi zilizopo Dar es Salaam na Dodoma.

C.2 SEKTA YA UCHUKUZI

Makadirio ya Ukusanyaji wa Mapato, Matumizi ya Kawaida na Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

317. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Sekta ya Uchukuzi (Fungu 62) imetengewa jumla ya **Shilingi 3,629,130,373,895** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 85,408,131,000** zimetengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 3,543,722,242,895** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyo tengewa fedha ni kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 6**

318. Mheshimiwa Spika, Mgawanyo wa fedha za maendeleo kwa kila mradi na kazi zitakazotekelawa kwa mwaka 2019/2020 ni kama ifuatavyo:

319. Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha uendeshaji wa Jengo la Tatu la Abiria (TB III) katika Kiwanja cha Ndege cha JNIA kwa kulipia gharama za uendeshaji na kuweka miundombinu wezeshi katika jengo hilo, TAA imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 26,000.00** kwa ajili ya kugharamia umeme, maji, matengenezo ya mitambo na mifumo ya ulinzi na usalama, mifumo ya TEHAMA, vifaa vya zimamoto, viyoyozi, *elevators*, daraja la kupandia na kushukia abiria, vyoo, mfumo wa maegesho ya magari na kuboresha mazingira ya nje ya jengo.

320. Mheshimiwa Spika, Kazi nyingine zitakazotekelawa na Mamlaka ya Viwaja vya Ndege ni pamoja na:

(i) Ujenzi wa uazio wa Usalama kwa Viwanja vya Ndege vya JNIA, Mwanza, Geita, Sumbawanga na Kigoma;

(ii) Kuendelea na taratibu za utwaaji wa maeneo mapya kwa ajili ya viwanja vipyta vya ndege vya Bagamoyo (Pwani), Kisumba (Sumbawanga), Msalato (Dodoma), Mwada (Manyara) na Igegu (Simiyu);

(iii) Kuendelea kuboresha mitambo na mifumo ya kufuatilia mienendo ya shughuli za usalama na uendeshaji wa viwanja (CCTV) kwa viwanja vya JNIA, Mtwara, Songwe, Lake Manyara na Iringa;

(iv) Kufunga mitambo ya ulinzi na usalama katika viwanja vya ndege vya Tanga na Moshi;

(v) Kuimarisha huduma za zimamoto katika viwanja vya ndege pamoja na ununuzi wa magari matatu ya Zimamoto na vifaa mbalimbali vya uokoaji;

(vi) Kuendelea kuboresha huduma zinazotolewa katika viwanja vya ndege ili kukidhi viwango vya kimataifa;

(vii) Kuboresha na kufunga mifumo ya maegesho ya magari katika Viwanja vya ndege vya JNIA, Arusha na Mwanza;

(viii) Kuendelea kuboresha na kuunganisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato katika Viwanja vya Ndege vya JNIA, Mwanza na Arusha;

(ix) Kujenga jengo la kuhifadhia mizigo (cold room) katika kiwanja cha ndege cha KIA.

321. *Mheshimiwa Spika*, Mfuko wa Maendeleo ya Reli (Railway Fund) umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 255,700.00** kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa reli mpya ya *standard gauge*, kukarabati reli iliyopo, ununuzi wa injini na mabehewa ya mizigo na abiria na upembuzi yakinifu kwa ajili ya miradi ya reli. Miradi hiyo ni pamoja na Kaliua – Mpanda – Karema, Tabora – Kigoma, Tanga – Arusha – Musoma na Mtwara – Mbamba Bay na matawi ya Mchuchuma – Liganga.

322. Mheshimiwa Spika, jumla ya Shilingi **milioni 216,005.642** zimetengwa kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya reli iliyopo kutoka Dar es Salaam hadi Isaka. Kazi zitakazofanya na:

- (i) Ujenzi/ukarabati wa madaraja na makalvati katika eneo la Dar es Salaam – Itigi (Km 626);
- (ii) Ukarabati wa njia ya reli kutoka Itigi – Isaka (Km 344);
- (iii) Huduma za ushauri katika eneo la Dar es Salaam hadi Isaka (Km 970);
- (iv) Ukarabati wa majengo ya stesheni;
- (v) Ujenzi wa njia za kupishana katika stesheni za llala na Isaka;
- (vi) Ununuzi wa vifaa na mitambo (*Track recording car, injini* (3), mabehewa ya mizigo (44), *Train control system, Train modelling software, na management accounting Information Software*); na
- (vii) Kutoa Mafunzo kwa Watumishi wa Shirika la Reli (TRC), Wizara na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini (LATRA).

323. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa reli mpya ya *Standard Gauge* kati ya Dar es Salaam – Tabora – Isaka - Mwanza na Isaka - Rusumo umetengewa **Shilingi milioni 2,476,016.6**. Kati ya fedha hizo, Shilingi milioni 2,446,016.6 ni kwa ajili ya ujenzi wa *Standard Gauge* sehemu ya Dar es Salaam hadi Makutupora; Shilingi milioni 10,000 ni kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa reli kati ya Isaka – Rusumo na Shilingi milioni 20,000 ni kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa reli ya Makutupora – Tabora – Isaka. Kazi zitakazoteklezwa ni pamoja na:

- (i) Kukamilisha ujenzi wa reli ya kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro (Km 300) ikiwa ni pamoja na miundombinu ya umeme;
- (ii) Kuendelea na ujenzi wa reli na miundombinu ya umeme ya reli ya Morogoro hadi Makutupora (Km 422);

(iii) Kuanza utekelezaji wa mradi wa reli ya Makutupora – Tabora – Isaka - Mwanza (Km 676) kwa kufanya tathmini ya ardhi, kulipa fidia na kulipa malipo ya awali;

(iv) Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa reli ya Isaka hadi Rusumo (Km 371) kwa kufanya tathmini ya ardhi, kulipa fidia na malipo ya awali ya ujenzi;

(v) Kuendelea na taratibu za upatikanaji wa fedha kwa maeneo ya ujenzi wa reli kwa sehemu za Makutupora hadi Tabora (Km 294), Tabora hadi Isaka (Km 133) na Isaka hadi Mwanza (Km 249); na

(vi) Kuendelea na ulipaji wa fidia ya ardhi kwa maeneo yatakayohitajika kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya reli. Kazi nyingine zitakazotiezwa ni pamoja na:

- Kuanza hatua muhimu za ujenzi wa reli ya Jijini Dar es Salaam (DSM Commuter Trains) baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinfu na usanifu wa awali;

- Kuendelea na ukarabati wa mitambo muhimu na matengenezo ya vichwa na mabehewa, karakana ya kukarabati reli na mataruma yake, machimbo ya uzalishaji kokoto;

- Kuanza kuboresha njia ya reli kutoka Kaliua hadi Mpanda kwa kutumia mataruma yanayotolewa kutoka Mradi wa ukarabati wa reli ya kutoka Dar es Salaam hadi Isaka (Km 970);

- Kuanza kutoa huduma ya usafiri wa treni iliyosimama kwa takriban miaka 10 kutoka Tanga hadi Arusha.

324. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Serikali imetenga jumla ya **Shilingi milioni 500,000** ili kuendelea kuboresha utendaji wa ATCL. Fedha hizo zitatumiika kutekeleza kazi zifuatazo:

(i) Kukamilisha malipo ya Ndege ya pili aina ya Boeing 787 Dreamliner na ndege ya nne aina ya Bombardier Q400;

- (ii) Kufanya malipo ya awali ya ununuzi wa ndege mbili (2) mpya aina ya A220-300;
- (iii) Ununuzi wa ndege moja aina ya Bombardier Q400 na injini ya akiba kwa ajili ya ndege aina ya Bombardier Q400;
- (iv) Kuendelea kuboresha karakana ya matengenezo ya ndege iliyo kia; na
- (v) Kulipa madeni yaliyohakikiwa pamoja na gharama za kuanzia kwa ndege mpya zitakazopokelewa katika kipindi hicho.

325. Mheshimiwa Spika, ili kuboresha huduma za uchukuzi wa abiria na mizigo katika Maziwa Makuu, katika mwaka 2019/2020, Serikali imetenga **Shilingi milioni 70,000** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa meli mpya na kukarabati mellizopo katika Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika. Kazi zilizopangwa ni pamoja na:

- (i) Kuendelea na ujenzi wa meli moja mpya; chelezo na ukarabati wa meli za MV Victoria na MV Butiama katika Ziwa Victoria;
- (ii) Kuanza ujenzi wa meli moja mpya, tishari (Barge) moja na ukarabati wa meli ya MV Liemba na MT. Sangara katika Ziwa Tanganyika;
- (iii) Kuanza ujenzi wa *Wagon Ferry* moja na ukarabati wa meli za MV.Umoja na MV Serengeti katika Ziwa Victoria;
- (iv) Kuendelea kufanya matengenezo ya kinga (preventive maintenance) kwa meli za MV Clarias na ML. Wimbi;
- (v) Kuendelea kufunga mfumo wa kielektroniki wa kukata tiketi melini (Electronic Ticketing Systems) na mfumo wa kielecronic wa uendeshaji (Fleet Management Systems) kwenye bandari ya Kigoma;
- (vi) Kuendelea kufunga *flow scanners* kwenye bandari ya

Kigoma ili kudhibiti matumizi ya mafuta katika meli za Kampuni; na

(vii) Kuboresha muundowa kiutumishi pamoja na mazingira ya kazi na kujenga uwezo wa rasilimali watu kuititia mafunzo na ajira.

326. *Mheshimiwa Spika*, mbali na fedha zilizotengwa katika bajeti kuu ya Serikali, taasisi mbalimbali chini ya Sekta ya Uchukuzi zitaendelea kutekeleza mipango yao kwa kutumia makusanyo ya ndani (own sources).

327. *Mheshimiwa Spika*, wakati taratibu za kuunganisha majukumu ya TAA na KADCO zikiendelea, katika mwaka 2019/2020, Kampuni ya KADCO itatekeleza majukumu yafuatayo:

(i) Kuweka mfumo mpya wa taa za kuongozea ndege wakati wa kutua na kuruka (Aeronautical Ground Lighting) katika kiwanja cha KIA;

(ii) Kujenga jengo la kuhifadhi mizigo (cargo building) na kukarabati jengo liliopo kwa ajili ya ofisi za utawala;

(iii) Kuimarisha ulinzi na usalama wa Kiwanja kwa kununua vifaa nya kisasa;

(iv) Kuimarisha njia ya kutua na kuruka ndege kwa kuweka tabaka la juu;

(v) Kuboresha maegesho ya magari na njia za waenda kwa miguu; na

(vi) Kuendelea kushughulikia suala la kuhakiki mipaka ya kiwanja cha KIA, kuweka alama za mipaka, kufanya tathmini ya kulipa fidia wananchi katika maeneo hayo.

328. *Mheshimiwa Spika*, ili kuendelea kuboresha miundombinu ya Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), katika mwaka wa fedha 2019/2020, Mamlaka itatekeleza malengo yafuatayo:

- (i) Kununua mtambo wa kunyoosha reli na kushindilia kokoto (Tamping Machine);
- (ii) Kufanya upembuzi yakinifu wa tawi la reli lenye urefu wa kilometra 20 kutoka Mlowo hadi machimbo ya Makaa ya Mawe ya Magamba mkoani Songwe;
- (iii) Kununua mtambo wa kusaga kokoto (Secondary Crusher) pamoja na mtambo wa kubeba mawe (Dumper Track);
- (iv) Ukarabati na uimarishaji wa miundombinu ya njia kuu ya reli iliyopo;
- (v) Matengenezo na ukarabati wa vichwa vya treni vilivyopo, mitambo, mabehewa ya mizigo na ya abiria;
- (vi) Ukarabati wa majengo ya karakana ya Dar es Salaam, mitambo, vifaa na mashine mbalimbali ikijumuisha Karakana ya Mbeya, kiwanda cha kokoto na uzalishaji wa mataruma ya zege cha Kongolo; na
- (vii) Kuboresha mazingira ya kufanya kazi, na kujenga uwezo wa rasilimali watu kupitia mafunzo na ajira.

329. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Mamlaka ya Usafiri wa Anga imetenga fedha zake za ndani ili kutekeleza miradi mbalimbali ya kuboresha shughuli za udhibiti wa usafiri wa anga. Miradi hiyo inahusu:

- (i) Kuendelea na ufungaji wa Rada za kuongozea ndege za kiraia katika viwanja vya KIA, Mwanza na Songwe na kuziendesha;
- (ii) Ununuzi wa mfumo wa usambazaji taarifa za ndege kmtandao (AIXM - Aeronautical Information Exchange Model);
- (iii) Kufunga mitambo ya umeme wa juu (solar) katika vituo vya Dodoma, Mtwara, Tanga, Iringa, Kigoma, Pemba, Arusha, Mpanda na Songwe;

- (iv) Kufunga vifaa vya mawasiliano ya sauti kati ya Marubani na waongozaji wa ndege katika kiwanja cha ndege cha JNIA;
- (v) Kuanza ujenzi wa Chuo cha Usafiri wa Anga kiwanja cha ndege cha JNIA;
- (vi) Kufanya uhakiki wa vifaa vya kuongozea mienendo ya ndege katika vituo vya KIA, JNIA, Zanzibar na Mwanza;
- (vii) Kufunga vifaa vya kuongozea ndege katika jengo jipya la kuongozea ndege kituo cha Mwanza; na
- (viii) Kufanya utafiti wa masoko/huduma katika sekta ndogo ya usafiri wa anga.

330. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imetenga jumla ya **Shilingi milioni 548,653** kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi milioni 452,153 ni fedha za ndani na Shilingi milioni 96,500 ni fedha za nje za mkopo kutoka Benki ya Dunia (International Development Agency - IDA) na Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (Department for International Development – DFID). Kazi zitakazotekeliza katika mwaka 2019/2020 ni pamoja na:

- (i) Kuhudumia shehena ya tani za mapato milioni 15.175, katika Bandari zinazoendeshwa na Mamlaka. Aidha, Kitengo cha TICTS katika Bandari ya Dar es Salaam kitahudumia makasha (TEUs) 563,000;
- (ii) Kuendelea na mradi wa uboreshaji wa gati Na. 2 -7 na ujenzi wa gati jipya la kushusha shehena ya magari katika Bandari ya Dar es Salaam. Gati Na. 1 limekamilika katika mwaka 2018/2019;
- (iii) Kukamilisha ujenzi wa gati moja (multipurpose terminal) lenye urefu wa mita 300 katika bandari ya Mtwara;
- (iv) Kukamilisha ukarabati na uboreshaji wa magati yaliyopo

kwenye Bandari ya Tanga kwa kuimarisha sakafu ngumu na kuongeza kina cha gati Na. 1 – 2 na maandalizi ya ujenzi wa magati mawili yenye urefu wa mita 300;

(v) Kuendelea na ununuzi wa mitambo na vifaa mbalimbali kwa Bandari zote;

(vi) Kuendelea na ujenzi wa Chelezo katika Bandari ya Dar es Salaam;

(vii) Kukamilisha ujenzi wa magati ya Nyamisati, Mafia, Kilwa, Lindi na Rusungi katika mwambao wa bahari ya Hindi;

(viii) Kuendelea na ujenzi wa magati ya Nkome, Nyamirembe, Magarine, Lushamba na Mwigobero katika ziwa Victoria;

(ix) Kuendelea na ujenzi wa magati ya Lagosa, Kalya (Sibwesa), Kasanga, Kagunga, Ujiji, Kabwe na ujenzi wa Bandari ya Karema katika Ziwa Tanganyika;

(x) Kuendelea na ujenzi wa Chelezo katika Bandari ya Kigoma;

(xi) Kuendelea na ujenzi wa magati ya Kiwira, Ndumbi na Itungi katika Ziwa Nyasa;

(xii) Kuendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA na mfumo wa usalama bandarini (Port Integrated Security System - ISS);

(xiii) Kuendelea na ujenzi wa Bandari Kavu za Kwala, Ruvu na kuanza ujenzi wa bandari kavu ya Katosho, Kigoma; na

(xiv) Kukamilisha mpango wa utwaaji wa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa Bandari mpya na Bandari Kavu katika maeneo ya Katosho, Kibirizi, Chongoleani, Ruvu na Ihumwa.

331. *Mheshimiwa Spika*, Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (Tanzania Shipping Agencies Corporation – TASAC) ni Shirika jipya lililoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Uwakala wa Meli Namba 14 ya Mwaka 2017. Kupitia Tangazo la Gazeti la Serikali Na. 53 la tarehe 16 Februari, 2018. TASAC ilianza rasmi kutekeleza majukumu yake tarehe 23 Februari, 2018. Katika

mwaka 2019/2020, TASAC imepanga kutekeleza kazi mbalimbali za udhibiti na usimamizi wa usafiri kwa njia ya maji. Kazi hizo ni pamoja na:

(i) Kuweka mifumo ya kielektroniki ya kuainisha shehena inayostahili kuondoshwa (clearing and forwarding) na Shirika ikiwa ni pamoja na madini na mazao yake, mitambo na vipuri vitumikavyo katika migodi, mafuta, bidhaa zenyе maslahi ya Taifa, nyara za Serikali na viumbe hai kwa mujibu wa Kifungu cha saba (7) cha Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania Na. 14 ya mwaka 2017;

(ii) Kuweka mifumo ya kielektroniki ya kufuatilia na kupokea taarifa na nyaraka za shehena kutoka kwa wenge meli na mawakala wao;

(iii) Kuweka mifumo ya kielektroniki ya kuandaa na kuwasilisha taarifa za uhakiki wa shehena iingiayo na itokayo nchini;

(iv) Kusajili meli za Tanzania ambazo zimekidhi viwango vyatubora;

(v) Kuendelea kufanya ukaguzi wa ubora na usalama wa meli zifanyazo kazi nchini na zinazotoka nje ya Nchi (flag and port State Control Inspection);

(vi) Kuendelea kusimamia ubora wa elimu ya mabaharia inayotolewa na Chuo cha Bahari Dar es Salaam (Dar es Salaam Maritime institute - DMI) kulingana na Mkataba wa Kimataifa wa Ufundishaji na Utoaji vyeti vyatubora (International Convention on Standards of Training, Certification and Watchkeeping 78 as amended - STCW) ili waendelee kupata ajira kwa meli za ndani na nje ya Nchi;

(vii) Kuendelea na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira utokanao na shughuli za uendeshaji wa meli;

(viii) Kusimamia ujenzi salama wa meli mpya na ukarabati wa meli zilizopo;

(ix) Kuendelea kutoa elimu kwa wadau wa sekta ndogo ya

usafiri majini pamoja na umma kwa ujumla kuhusu masuala ya ulinzi na usalama wa vyombo vyaa majini;

(x) Kuendelea kudhibiti huduma za bandari na usafiri majini kwa kuweka vigezo na viwango vya ubora wa huduma na kufanya kaguzi kwa watoa huduma za bandari na usafiri wa majini kwa kuzingatia viwango vya ubora;

(xi) Kuendelea kuimarisha mifumo ya kielektroniki ya kukusanya mapato ya Shirika (Manifest Billing System);

(xii) Kukuza ushindani mionganoni mwa watoa huduma katika sekta ya usafiri majini;

(xiii) Kufungua na kuimarisha ofisi ya Makao Makuu na kufungua ofisi za mikoa katika mikoa yote ya Tanzania Bara yenye shughuli za usafiri majini; na

(xiv) Kuandaa Kanuni za Usimamizi wa Vivuko nchini.

332. Mheshimiwa Spika, SUMATRA ipo katika kipindi cha mpito kufuatia kupitishwa kwa sheria ya kuanzishwa Mamlaka mpya itakayosimamia huduma za usafiri wa Ardhini Januari, 2019. Lengo la kufanya mabadiliko haya ni kutenganisha huduma za udhibiti wa usafiri wa ardhini na majini na hivyo kuanzishwa Mamlaka mpya itakayosimamia huduma za usafiri wa Ardhini pekee. Taasisi hiyo itajulikana kwa jina la Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini (LATRA) na inatarajiwa kuanza kutekeleza majukumu yake katika mwaka 2019/2020 kwa kufanya yafuatayo:

(i) Kuimarisha udhibiti wa usalama, na ubora wa huduma za usafiri wa ardhini;

(ii) Kuimarisha matumizi ya teknolojia katika usimamizi wa ubora wa usafirishaji wa mizigo na abiria na kudhibiti upotevu wa mapato;

(iii) Kuchochaea maendeleo ya Sekta ya Usafiri kwa kushawishi wawekezaji wakubwa katika Sekta ya Usafiri wa Ardhini;

- (iv) Kuboresha Kanuni na miongozo ya utendaji na usimamizi wa huduma za usafiri wa nchi kavu;
- (v) Kutoa leseni kwa watoa huduma zinazodhibitiwa na kusimamia masharti ya leseni hizo ikiwemo kuhakikisha utunzaji wa mazingira;
- (vi) Kudhibiti gharama na tozo mbalimbali kwa kuzingatia Sheria na Kanuni ili kuhakikisha kuwa tozo hizo zinaendana na gharama za uzalishaji na pia zinaleta ufanisi katika soko; na
- (vii) Kutoa elimu kwa umma kuhusu mabadiliko ya Sheria, Kanuni mpya na miongozo ya udhibiti wa sekta.

333. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/2020, Mamlaka ya Hali ya Hewa imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kukamilisha kazi ya kuandaa Kanuni kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa Sheria mpya ya Mamlaka ya Hali ya Hewa ya mwaka 2018;
- (ii) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa rada tatu (3) za hali ya hewa pamoja na miundombinu yake;
- (iii) Kuanza kutekeleza mfumo wa kudhibiti ubora wa huduma za hali ya hewa zinazotolewa (QMS) sekta ndogo ya usafiri majini;
- (iv) Kuendelea kuboresha huduma za hali ya hewa kwa sekta ya usafiri wa anga kulingana na matakwa ya Shirika la Viwango Duniani (ISO 9001:2015);
- (v) Ukarabati wa vituo vya hali ya hewa na uendeshaji wa mtandao wa vituo vya hali ya hewa;
- (vi) Kufanya tafiti mbalimbali zikiwemo za mabadiliko ya hali ya hewa;
- (vii) Kuboresha miundombinu ya mawasiliano ya hali ya hewa ikiwa pamoja na kuunganisha vituo kwenye Mkongo wa Taifa;

(viii) Kutoa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa kutumia huduma za hali ya hewa;

(ix) Kupanua mtandao wa vituo vya hali ya hewa kwa kununua na kufunga mitambo ya kupima hali ya hewa inayojiendesha yenye (Automatic Weather Stations);

(x) Kuendesha karakana ya kutengeneza baadhi ya vifaa vya hali ya hewa iliyopo JNIA.

(xi) Utekelezaji wa programu ya kukabiliana na kuendana na mabadiliko ya hali ya hewa yanayopelekea kutokea kwa mabadiliko ya tabia nchi; na

(xii) Kujenga uwezo wa wafanyakazi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa.

C.3 SEKTA YA MAWASILIANO

334. *Mheshimiwa Spika*, Kwa mwaka wa fedha 2019/20, bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Sekta ya Mawasiliano ni **Shilingi 3,973,197,000.**

335. *Mheshimiwa Spika*, Sekta ya Mawasiliano imepanga kutekeleza Mpango wa Muda wa Kati na Muda Mrefu ambao umetilia mkazo katika maeneo yafuatayo:

TEHAMA

i. Kusimamia utekelezaji na uendelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili kufikisha huduma za Mkongo hadi Makao Makuu ya Wilaya na kuongeza uunganishaji wa taasisi za Serikali kwenye Mkongo wa Taifa zikiwemo Ofisi za Halmashauri, Hospitali, Shule, Mahakama na vituo vya polisi. Kuunganishwa kwa taasisi hizi kwenye Mkongo wa Taifa kutawezesha mifumo mbalimbali iliyopo kufanya kazi kwa ufanisi ikiwemo mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya serikali (GePG);

ii. Kuratibu ukamilishaji wa Sheria ya kulinda taarifa binafsi (Personal Data Protection Act);

iii. Kusimamia utekelezaji wa mkakati wa mtandao wa TEHAMA wenyе kasi zaidi (National Broadband Strategy); na

iv. Kusimamia utekelezaji wa mkakati wa kitaifa wa usalama wa mitandao (National Cyber security strategy)

MAWASILIANO

i. Kukamilisha uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Posta ya Mwaka 2003 na kuhuisha Sheria ya Posta ya mwaka 1993 ili iendane na ukiasi wa Teknolojia na kiuchumi;

ii. Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA 2016;

iii. Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Anwani za Makazi nchini; na

iv. Kuimarisha mashirikiano na mashirika ya kimataifa na kikanda.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

336. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania itatekeleza masuala yafuatayo:

i) Kwa kushirikiana na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA CCC) kuendelea kuelimisha watumiaji wa huduma za mawasiliano kuhusu Sheria, haki na wajibu wa watumiaji, kuhusu matumizi ya Mfumo mpya wa anwani za makazi na misimbo ya Posta, uhakiki wa usajili wa laini za simu za kiganjani, wajibu wa watumiaji katika masuala ya tahadhari dhidi ya uhalifu kuititia mtandao na kufanikisha ufumbuzi wa malalamiko kati ya watumiaji na watoa huduma za Mawasiliano;

ii) Kuendelea kutekeleza usimamizi wa usalama wa mitandao ya mawasiliano kuititia TZ- CERT;

iii) Kuendelea kusimamia na kuboresha mfumo wa usimamizi

wa huduma za mawasiliano, TTMS, ili uendane na mahitaji pamoja na mabadiiliko ya Teknolojia;

iv) Kuandaa Muongozo juu ya matumizi ya utangazaji wa kidigit kwa redio.

v) Kujenga Miundombinu ya kitaifa ya kuhakikisha usalama wa miamala inayofanyika kwa njia za kielektroniki “National Public Key Infrastructure (NPKI)”

vi) Kuendelea kutekeleza mifumo ya utendaji kazi (Quality Management System) ili kuongeza ufanisi wa udhibiti wa Mawasiliano ya simu, Posta na Utangazaji;

vii) Kuendelea kusimamia Sekta ya mawasilino na kuhakikisha kuwa watoa huduma wote wanatoa huduma kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo;

viii) Kuendelea kufanya utafiti juu ya matumizi ya Masafa ambayo hayatumiki katika bendi ya (470MHz- 694MHz);

ix) Kuendelea kujenga uwezo wa kukabiliana na uhalifu wa matumizi mabaya ya mtandao kwa Taasisi za Ulinzi na Usalama; na

x) Kuendelea kuboresha mfumo wa utoaji wa leseni za huduma za mawasiliano.

Shirika la Posta Tanzania (TPC)

337. *Mheshimiwa Spika*, Katika mwaka wa fedha 2019/20, Shirika la Posta linatarajia kutekeleza majukumu yafuatayo:

i) Shirika litaanzisha ujenzi wa Jengo la kutolea huduma katika kiwanja chake eneo la Mji wa Serikali Dodoma, kukamilisha upatikanaji wa hatimiliki kwa viwanja vyake 43 ambavyo havijapata hatimiliki na kufanya matengenezo na kuboresha majengo yake ya kutolea huduma;

ii) Shirika litaimarisha huduma ya ‘Posta Pesa’ kwa uwakala

na kuifanya huduma hiyo kuwafikia wananchi wengi zaidi ili kuboresha vyanzo vya mapato yake; na

iii) Shirika litakamilisha uunganishaji wa Ofisi zake zote katika Mfumo wa Serikali wa Malipo (Government Payment Gateway-GePG).

Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL)

338. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2019/20 Shirika la Mawasiliano Tanzania litatekeleza majukumu yafuatayo: -

i) Upanuzi na uboreshaji wa Mifumo ya Mtandao Mhimili Usafirishaji wa Data na Simu za Mkononi;

ii) Uboreshaji wa Mifumo ya Usalama wa Mtandao kwa wateja wa Shirika;

iii) Kupanua na kuiongezea uwezo Idara ya biashara na masoko pamoja na kuimarisha kitengo cha makusanyo;

iv) Kuongeza idadi ya wateja hai (Active Customers) wa huduma mbalimbali za mawasiliano (simu na data) kutoka 1,074,642 Februari, 2019 hadi 1,800,000 mwaka 2019/20;

v) Kuimarisha mkakati wa kuuza muda wa maongezi na kuendelea kubuni njia mbalimbali za kuhakikisha huduma za muda wa maongezi zinawafikia watumiaji wa mtandao wa TTCL katika ngazi zote;

vi) Kuendelea kusimamia na kuendesha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Kituo cha Data cha Taifa (National Data Centre); na

vii) Kuendesha TTCL Pesa kwa ufanisi zaidi.

Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)

339. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2019/20, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) utatekeleza kazi zifuatazo:

- i. Kukamilisha utekelezaji wa miradi ya kufikisha huduma ya mawasiliano vijiji ni katika kata 200 ili kuhakikisha kuwa huduma zinaflia asilimia 95 ya vijiji vyote nchini;
- ii. Kukamilisha utekelezaji wa miradi ya kufikisha huduma ya mawasiliano katika maeneo ya kata 20 kwenye maeneo ya mipakani na yenyе uhitaji maalum;
- iii. Kufikisha matangazo ya luninga ya kidigitali katika mikoa 2;
- iv. Kuendelea kutoa vifaa vya TEHAMA na kuunganisha mtandao wa intaneti katika shule za sekondari 150 zaidi;
- v. Kuendelea kutekeleza mradi wa kuanzisha vituo 10 vya TEHAMA;
- vi. Kuendelea kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa walimu 1,000;
- vii. Kuendelea kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa Wanafunzi wasichana 700;
- viii. Kuendeleza ushirikiano na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika uunganishwaji wa mtandao wa mawasiliano katika hospitali za Serikali ili kuleta ushirikiano wa kitabibu kwa njia ya mtandao na kuondoa tatizo sugu la uhaba wa madaktari bingwa; na
- ix. Kuanza ujenzi wa Ofisi za Mfuko jijini Dodoma.

Tume ya TEHAMA (ICTC)

340. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Tume ya TEHAMA itatekeleza mambo yafuatayo:

- i. Kukamilisha mpango mkakati wa kutengeneza vifaa vya TEHAMA nchini na kusimamia utekelezaji wake;
- ii. Kusajili na kuendeleza wataalam wa TEHAMA kupitia programu mbalimbali za mafunzo ili kujenga uwezo wa kitaalam na ubunifu;

iii. Kukua uwekezaji katika TEHAMA kwa kushirikiana na sekta binafsi ikiwemo kuendeleza wajasiriamali wadogo wadogo wa TEHAMA hapa nchini pamoja na kushirikiana na makampuni ya TEHAMA nchini na nje ya nchi; na

iv. Kuandaa majukwaa ya kitaalam na Biashara (ICT Professionals and Business Forums) kama mkakati wa kukuza ufahamu wa masuala ya TEHAMA kwa wataalam, kuvutia zaidi shughuli za ubunifu na biashara za TEHAMA kutoka nje ya nchi pamoja na kukuza zile za hapa nchini.

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA CCC)

341. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/2020 Baraza litaendelea kufanya yafuatayo:

i. Kuelimisha umma kuhusu matumizi sahihi ya huduma na bidhaa za mawasiliano;

ii. Kupokea taarifa na maoni kutoka kwa watumiaji wa huduma na bidhaa za mawasiliano na kuziwasilisha kwa taasisi husika ili kuboresha ufanisi na kupunguza changamoto kwa watumiaji;

iii. Kuimarisha na kujenga uwezo wa Kamati za Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Lindi, Iringa, Tanga, Mwanza, Kagera na Mjini Magharibi – Zanzibar; na

iv. Kuanzisha Kamati zingine katika mikoa ya Katavi, Kigoma, Manyara na Singida.

C. 4 TAASISI ZA MAFUNZO Chuo cha Ujenzi Morogoro

342. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Chuo cha Ujenzi Morogoro kimepanga kufundisha jumla ya wanafunzi **1,200** katika fani za ufundis sanifu na ufundis stadi wa fani za barabara, madaraja, majengo, magari na mitambo; kompyuta; udereva wa magari ya umma na magari ya abiria pamoja na uendeshaji wa mitambo. Aidha,

Chuo kimepanga kununua vifaa vya maabara ya barabara na majengo; kuendelea kufanya ukarabati wa mitambo mitatu ya ujenzi wa barabara itakayotumika katika mafunzo kwa vitendo pamoja na kumalizia ujenzi wa karakana ya ufundu magari na eneo la kisasa la kuoshea magari (car wash bay). Chuo pia kimepanga kufanya tathmini ya mafunzo inayotoa katika Wilaya zote za Tanzania Bara na Visiwani.

Chuo cha Matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi (Appropriate Technology Training Institute – ATI) - Mbeya

343. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2019/20, Chuo kimepanga kutoa mafunzo kwa Wahandisi **30**, Mafundi Sanifu **30**, wasimamizi wa barabara **30** na vikundi vya wanawake, vijana na wasimamizi wa barabara wapatao **150**. Kazi nyingine ni kufanya tathmini ya matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi nchini na kuendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia hiyo katika ujenzi, matengenezo na ukarabati wa barabara. Chuo kitatembelea na kutoa ushauri wa matumizi ya teknolojia Stahiki ya Nguvukazi kwa kada na wadau mbalimbali katika mikoa kumi (10) ya Kilimanjaro, Katavi, Rukwa, Bukoba, Kigoma, Musoma, Arusha, Pwani, Manyara na Tanga.

Chuo vilevile kimepanga kuimarisha na kuboresha mtaala wa utoaji wa mafunzo ya lami kwa barabara za vijiji na mijini; kuboresha miundombinu ya Chuo ili kuboresha huduma kwa watendaji wake na washiriki wa kozi, pamoja na kufanya matengenezo ya magari na mitambo ya mafunzo na kuongeza vifaa na huduma mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya mafunzo; kuboresha utendaji wa Chuo kwa kuongeza watumishi wa kada ya kufundisha pamoja na utawala na kuwaongezea uwezo na kuboresha utendaji wao wa kazi kwa kushiriki mafunzo mbali mbali pamoja na kuimarisha makusanyo na mapato ya ndani ili kujenga uwezo wa Chuo kujitegemea.

Chuo kimepanga kuendelea kusimamia ukarabati na matengenezo ya barabara kwa kuitia barabara za mafunzo katika utoaji wa mafunzo kwa jamii ili kuendelea kuhamasisha

matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi kwa umma. Aidha Chuo kitashiriki kwenye mikutano, maonyesho na makongamano ya kitaifa na kikanda ili kujenga na kuimarisha uwezo wa watendaji wa Chuo na kueneza Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi.

Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)

344. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimejiwekea malengo yafuatayo:

- (i) Kuhuisha Mitaala ya ufundishaji ili kukidhi matakwa;
- (ii) Kukamilisha taratibu za kupata ithibati ya kufundisha marubani;
- (iii) Kununua magari matatu (3), vitabu vya ziada na kiada na vifaa vya kufundishia mafunzo ya usafiri wa reli ili kuboresha mafunzo yanayotolewa na Chuo;
- (iv) Kukamilisha ujenzi wa jengo la mafunzo ya usafiri wa anga (Aviation Complex) na upanuzi wa jengo la utawala;
- (v) Kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Ukaguzi wa Magari;
- (vi) Kuendelea na ujenzi wa Awamu ya Nne (4) wa Kituo cha Rasilimali Mafunzo;
- (vii) Kuendelea na ukarabati wa Majengo ya Chuo;
- (viii) Uandaaji wa Matumizi Bora ya Ardhi - Eneo la Kikwetu Mkoani Lindi kwa ajili ya uanzishwaji wa mafunzo ya Sayansi ya Bahari;
- (ix) Uandaaji wa matumizi bora ya ardhi Kilimanjaro – KIA kwa ajili ya uanzishwaji wa mafunzo ya usafiri wa anga;
- (x) Kuanzisha Kituo cha Utafiti wa Mafunzo ya usafiri wa reli; na

(xi) Kuendelea na maandalizi ya uanzishwaji wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Usafirishaji.

345. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Chuo cha Bahari Dar es Salaam kitatkeleza miradi ifuatayo:

- (i) Kufanya upembuzi yakinifu na kutafuta wadau/wabia kwa ajili ya uendelezaji wa miundombinu ya chuo katika eneo la Mkuranga na lile la Barabara ya Sokoine;
- (ii) Ununuzi wa vifaa vya mafunzo ili kuboresha miundombinu ya kusoma na kujifunzia;
- (iii) Kukamilisha ukarabati wa meli ya mafunzo ili kutoa mafunzo kwa vitendo (on board training); na
- (iv) Kuendeleza utafiti na Ushauri elekezi kwenye sekta ya Bahari.

C.5 MASUALA MTAMBUKA

Ushirikishwaji wa Wanawake katika Kazi za Barabara

346. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendesha programu mbalimbali zenyе lengo la kuongeza idadi ya wanawake wanaoshiriki katika kazi za barabara. Katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara imepanga kutoa mafunzo kwa makandarasi wanawake juu ya namna ya kuomba zabuni na kujaza zabuni kwa usahihii pamoja na kuwasaidia kusajili kampuni zao za ujenzi. Vilevile, Wizara itatoa mafunzo kwa wanawake na vikundi vya wanawake kuhusu matengenezo na ukarabati wa barabara kwa kutumia teknolojia ya nguvu kazi pamoja na kufuutilia kwa karibu kazi za barabara zinazofanywa na makandarasi wanawake. Aidha, Wizara imepanga kutembelea vyuo vya elimu ya juu ili kufanya ufuutiliaji kuhamasisha wasichana wanaosoma masomo ya sayansi na hisabati pamoja na kuendelea kusambaza nakala za miongozo ya ushirikishaji wa wanawake katika kazi za barabara.

Rasilimali Watu

347. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara itaendelea kuwaendeleza kitaaluma watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi kulingana na mpango wa mafunzo ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

348. Mheshimiwa Spika, kuhusu kupambana na ugonjwa hatari wa UKIMWI, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa watumishi kuhusu mbinu za kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo ikiwa ni pamoja na upimaji kwa hiari. Wizara pia itaendelea kuhamasisha watumishi ili washiriki katika mashindano mbalimbali ya michezo kwa lengo la kuboresha afya zao pamoja na kujenga mahusiano mazuri kazini.

D. SHUKRANI

349. Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati viongozi wenzangu katika Wizara ninayoiongoza nikianza na Mheshimiwa **Elias John Kwandikwa (Mb.)**, **Naibu Waziri Ujenzi**); Mheshimiwa **Mhandisi Atashasta Justus Nditiye(Mb.)**, Naibu Waziri (Uchukuzi na Mawasiliano); Makatibu Wakuu **Arch. Elius Asangalwisyen** Mwakalinga (Ujenzi); **Mhandisi Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho** (Uchukuzi); **Mhandisi Dkt. Maria Leticia Sasabo** (Mawasiliano) na **Dkt. Jim James Yonaz**, Naibu Katibu Mkuu (Mawasiliano). Aidha, nawashukuruwatendaji wote wa Wizara kwa juhudi walizofanya kuhakikisha kwamba tunatimiza majukumu tulyokabidhiwa na Taifa ipasavyo. Napenda pia kuwashukuru Viongozi na Watumishi wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano mzuri amba wamekuwa wakinipa. Ushirikiano wao ndio uliowezesha kutekeleza majukumu ya Wizara yetu katika mwaka uliopita. Naomba waendelee na juhudi hizo katika kipindi kijacho ili tuweze kutimiza malengo tuliojiwekea.

350. Mheshimiwa Spika, nchi na washirika mbalimbali wa maendeleo wamechangia katika utekelezaji wa programu

na mipango mbalimbali ya Wizara. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwatambua washirika hao wa maendeleo ambao ni pamoja na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Majini (IMO), Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO), Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (BADEA), OPEC Fund, Umoja wa nchi za Ulaya, "Third World Organization for Women in Science (TWOWS)", UNESCO, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Japan (JICA), Korea Kusini (KOICA), Abu Dhabi Fund, Ujerumani (KfW), Uingereza (DFID), Uhlanzi (ORIO), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Kuwait (KFAED), Uturuki, HSBC, TMEA, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za SADC, Nchi za Urusi, Afrika Kusini, Uingereza, Marekani, Uhlanzi, Japan, India, China, Denmark, Norway, Ubelgiji, Ujerumani, Taasisi za fedha za CRDB, NSSF, PSSSF na TIB, Asasi zisizokuwa za Kiserikali, Sekta Binafsi pamoja na wengine wengi.

351. Mheshimiwa Spika, mwisho, nakushukuru tena wewe binafsi na Naibu Spika. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara (www.mwtc.go.tz).

**E. MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA YA UJENZI,
UCHUKUZI NA MAWASILIANO KATIKA MWAKA WA FEDHA
2019/2020**

352. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wafedha 2019/20, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 4,963,297,839,163.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,330,194,268,268.00** ni kwa ajili ya Sekta ya Ujenzi, **Shilingi 3,629,130,373,895.00** ni kwa ajili ya Sekta ya Uchukuzi na **Shilingi 3,973,197,000.00** ni kwa ajili ya Sekta ya Mawasiliano. Mchanganuo wa fedha zinazoombwa kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:

SEKTA YA UJENZI (FUNGU 98)

353. Mheshimiwa Spika, jumla ya **Shilingi 1,330,194,268,268.00** za Fungu 98 (Ujenzi) zinajumuisha **Shilingi 36,142,664,000.00**

kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara (Ujenzi) na Taasisi ambapo **Shilingi 33,788,265,000.00** ni za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 2,354,399,000.00** ni za Matumizi Mengineyo. Bajeti ya Maendeleo ni Shilingi **1,294,051,604,268.00** ambazo zinajumuisha **Shilingi 990,000,000,000.00** fedha za ndani na **Shilingi 304,051,604,268.00** fedha za nje. Fedha za ndani zinajumuisha **Shilingi 587,389,000,000.00** za Mfuko wa Barabara na **Shilingi 402,611,000,000.00** za Mfuko Mkuu wa Serikali.

SEKTA YA UCHUKUZI (FUNGU 62)

354. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Uchukuzi imetengewa jumla ya **Shilingi 3,629,130,373,895** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya hizo, **Shilingi 85,408,131,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 58,337,187,000** ni za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 27,070,944,000** ni za Matumizi Mengineyo. Aidha, miradi ya maendeleo imetengewa **Shilingi 3,543,722,242,895**, kati ya fedha hizo, **Shilingi 3,327,716,600,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 216,005,642,895** ni fedha za nje.

SEKTA YA MAWASILIANO (FUNGU 68)

355. Mheshimiwa Spika, **Shilingi 3,973,197,000** za Fungu 62 (Mawasiliano) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara (Mawasiliano) na Taasisi ambapo **Shilingi 2,047,259,000** ni za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 1,925,938,000** ni za Matumizi Mengineyo.

356. Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii, nimeambatanisha Miradi ya Wizara itakayotekelawa katika mwaka wa fedha 2019/20 (**Kiambatisho Na. 1-6**) ikiwa ni pamoja na kiasi cha fedha kilichotengwa kutekeleza miradi hiyo. Naomba viambatisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja hii.

357. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati iliyo shughulikia bajeti hii.

MHE. MOSHI S. KAKOSO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ifuatayo ni taarifa kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na maoni na ushauri kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia Kanuni ya 123 ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari 2016, taarifa hii imegawanyika katika sehemu tatu zifuatazo: Sehemu ya Kwanza inahusu utangulizi. Sehemu hii inabainisha mpangilio wa taarifa inayowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi unaojikita katika masuala makubwa mawili. Mapitio ya taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya mwaka 2018/2019. Mapitio yanajielekeza zaidi katika makusanyo ya mapato, upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo, ukaguzi wa miradi ya maendeleo na utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Uchambuzi huu upo katika maeneo makuu manne ambayo ni makisio ya ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha 2019/2020, makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha

2019/2020 na mambo mengine muhimu yaliyojitekeza wakati wa kujadili, kuchambua na kuitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu imejielekeza katika maoni na ushauri wa Kamati kuhusiana na masuala yote yaliyofanyiwa uchambuzi katika Fungu 62 (Sekta ya Uchukuzi), Fungu 98 (Sekta ya Ujenzi) na Fungu 68 (Sekta ya Mawasiliano).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2018/2019. Sehemu hii inabainisha upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo kwa sekta zote za Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2018/2019 (kama inavyooneshwa katika Jedwali Namba 1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Ujenzi - Fungu 98. Mwenendo wa utolewaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa sekta hii ni wakuridhisha kwani hadi mwezi Machi, 2019 asilimia 55 ya fedha za ndani za miradi ya maendeleo zilikuwa zimetolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekta ya Uchukuzi - Fungu 62, bado kumeendelea kuwapo na changamoto ya kutokutolewa fedha kwa wakati na hivyo, kusababisha baadhi ya miradi kuchelewa kuanza na kutokukamilika kwa wakati kama ilivyopangwa. Kama Jedwali Na.1 linavyoonesha, kati ya fedha zote za ndani za miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 fedha zilizotolewa hadi kufika mwezi Machi, 2019 ni asilimia 17 tu. Baadhi ya miradi ambayo hadi mwezi Machi, 2019 haikupata fedha yoyote ni reli ya kisasa kati ya Mtwara-Mbambabay, Mchuchuma & Liganga (kilometra 1,092), ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Tanga-Arusha - Musoma (kilometra 1,108) na mradi wa usafiri wa treni abiria Jijini Dar es Salaam. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Sekta ya Mawasiliano - Fungu 68, Kamati imebaini kuwa fedha za miradi ya maendeleo zilizopokelewa hadi mwezi Machi 2019, ni shilingi 3,670,500,020 ambapo kati ya fedha hizo, fedha zilizotumika ni shilingi 1,531,406,388.91 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa miradi iliyotekelawa kwa mwaka 2018/2019. Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi kwa baadhi ya miradi ya maendeleo iliyokuwa imetengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Ziara hii ilifanyika kuanzia tarehe 13 hadi 20 Machi, 2019 katika Mikoa ya Dodoma, Morogoro, Pwani, Dar es Salaam na Mtwara. Miradi iliyotembelewa ni ifuatavyo:-

Viwanja vya Ndege vya Dodoma na Msalato; ujenzi wa reli ya kati sehemu ya Dar es Salaam- Morogoro; ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria (*Terminal III*); ujenzi wa rada ya kuongozea ndege Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere; Chuo cha Usafirishaji Tanzania-NIT; ujenzi wa barabara ya Mtwara - Newala - Masasi (km 210); ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara na ujenzi wa Bandari ya Mtwara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara hiyo, Kamati imebaini katika mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Msalato, changamoto imekuwa ni upatikanaji wa fedha za ujenzi pamoja na ulipaji fidia kwa wananchi waathirika wapatao 1,926 ambao wanatarajiwa kulipwa fidia kiasi cha shilingi bilioni 14.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa, maendeleo ya mradi sehemu ya Dar es Salaam hadi Morogoro ni mazuri kwani fedha kwa ajili ya malipo mbalimbali ya mradi zinatolewa kwa wakati na hakuna madai yoyote kwa mkandarasi. Aidha, fidia mbalimbali kwa ajili ya maeneo yaliyotwaliwa ili kupisha ujenzi wa reli zinaendelea kutolewa kadiri mradi unavyoendelea na ujenzi wa sehemu hii umefikia asilimia 45 na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Novembra, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa ujenzi wa Jengo la Tatu la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere, kazi zote za ujenzi wa jengo zimefikia asilimia 96 na mradi unatarajiwa kukamilika kukamilika ifikapo tarehe 31 Mei, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji-NIT, katika ziara Kamati ilibaini changamoto mbalimbali ambazo kimsingi zikifanyiwa kazi zitasaidia Chuo hiki kufanya kazi vizuri na kuzalisha wataalam wengi watakaosaidia kusimamia na kuendeleza miundombinu nchini. Baadhi ya changamoto hizo ni; Upungufu wa Watumishi 133 wanataaluma 87 na watumishi wa kawaida 46. Hali hii imesababisha chuo kutumia watumishi kwa muda kutoka nje hasa wanataaluma jambo lenye gharama kubwa na kuelemea chuo. Madeni ya Chuo ya Mwaka 2015/16 yanayofikia Shilingi Bilioni 2.29 yanashuburi kuhakikiwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani Serikali. Upungufu wa Vifaa vya kujifunzia na kufundishia hasa mafunzo ya uhandisi na hosteli za wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa ujenzi wa barabara ya Mtwara- Newala- Masasi; kasi ya tekelezaji wa mradi huu si yakuridhisha kwani kati ya Kilomita 210, za barabara hii, zimejengwa Kilomita 50 tu tangu Mwaka 2017 ambazo ujenzi wake umefikia asilimia 38 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa ujenzi wa bandari ya Mtwara; katika ziara Kamati ilijionea maendeleo na kasi nzuri ya utekelezaji wa mradi huu japo kuhikiwa yapo mapungufu yaliyofanya mwanzoni mwa mradi ambapo mradi ulianza bila ya kuwa na Mshauri Mwelekezi; hivyo kusababisha kujenga/kuchimba kina cha Mita 13 badala ya 15 na upana wa mita 5 badala ya mita 5.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Anuani za Makazi unalenga uhakiki kila mwananchi anakuwa na anwani ya mahali alipo, hivyo kuwezesha mwananchi kupata huduma kwa uhakika na urahisi. Katika ziara, Kamati imebaini changamoto kubwa inayokabili utekelezaji wa mradi huu ni

ni ufinyu wa Bajeti; hakuna fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu, na hata kiasi kidogo kinachotengwa hakitolewi chote ama kutotolewa kwa wakati. Kwa mfano katika mwaka wa fedha 2017/2018 kati ya Shilingi Billioni 3 zilizoidhinishwa, hadi kufikia mwezi Juni, 2018 zilitolewa jumla ya shilingi 1, 292,279,295.67 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jumla, katika ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati imebaini changamoto kubwa iliyopo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni kutopatikana kwa fedha za miradi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Naomba kufanya marekebisho kwenye Jedwali Na. 2, kwamba fedha za miradi ya maendeleo kiasi cha bilioni 15 zilizoandikwa kwenye Sekta ya Mawasiliano zifutwe badala yake isomeke 0, kwamba hakuna fedha zilizotengwa kwa miradi ya maendeleo ya Sekta ya Ujenzi. Hivyo, jumla ya fedha zinazombwa ni Shilingi Triliioni 4.8 ambazo zimewasilishwa na Waziri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi triliioni 4.8 Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza fedha kwa ajili ya kuimarisha miundombinu nchini. Mchanganuo wa Fedha hizo unaonekana katika jedwali namba 2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za miradi ya maendeleo kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kutoka shilingi triliioni 4.2 kwa mwaka 2018/2019 hadi Shilingi triliioni 4.8 kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ongezeko la Fedha la takribani asilimia 14, fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Sekta ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kuna upungufu wa shilingi 772,404,748,873.38 ambayo ni sawa na asilimia 39.08 ya fedha za miradi ya

Maendeleo za Sekta ya Ujenzi zilizokuwa zimeidhinishwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kamati inashauri Serikali kutafuta fedha hizo ambazo zimekuwa pungufu shilingi billioni 772.4. Fedha hizi zitasaidia kuongeza kasi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara nchini ambayo bado imekuwa na changamoto ya kutokupitika wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo kwa Sekta ya Mawasiliano, hakuna fedha yoyote iliyotengwa. Hata hivyo, Kamati ilielezwa kuwa fedha hizo za miradi ya maendeleo zitatolewa toka katika fedha za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Kamati inasisitiza kuwa ni muhimu fedha hizo zitolewe ili kuendeleza miradi muhimu iliyokuwa inaendelea, kama vile, Mradi wa Anuani za Makazi na misimbo ya posta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uchukuzi kuhusu ujenzi wa reli nchini Kamati inashauri yafuatayo; Kamati bado inaendelea kusisitiza ushauri wake kuwa mradi wa ujenzi wa Reli ya Kati kipaumbele kiwe kwenye reli yenye matarajio ya mzigo mkubwa ili kutengeneza mazingira ya Serikali kurudisha fedha zitakazokuwa zimewekezwa. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kwamba reli hii ijengwe kwa kuzingatia faida za kiuchumi na kipaumbele zaidi ziwekwe kwenye tawi la Tabora – kigoma -Uvinza- Msongati; Kaliua – Mpanda – Kalema; na Tabora- Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa reli ya Kati uende sambamba na ununuzi wa vichwa na mabehewa ya treni, ili mradi utakapokamilika kwa sehemu ya Dar es Salaam hadi Morogoro huduma za usafirishaji zianze mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo mbalimbali ya uendeshaji wa treni, pamoja na uratibu wa matumizi ya reli mpya yatolewe ili mradi utakapokamilika pawepo na wataalam wa ndani ambao watakuwa tayari kuupokea na kuusimamia mradi huu. Serikali ihakikishe mradi wa sehemu ya Dar es Salaam hadi Morogoro unakamilika kwa wakati mwezi Novemba, 2019 kama Mkataba na Mkandarasi unavyoonesha ili kuepuka gharama zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuepusha uvamizi wa maeneo ya reli, ni vema Shirika la Reli Tanzania-TRC liweke alama zinazoonesha mwisho wa eneo la reli ili kuondoa usumbufu na migogoro isiyokuwa na lazima kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Reli lianze kuijendesha kisasa kwa kufunga vyombo vya kielektroniki ili kuweza kutunza kumbukumbu zote za kiutendaji, ufatiliaji wa mizigo kwa wateja, udhibiti wa mafuta, udhibiti wa mwendo na usalama. Hii italifanya Shirika hili kuweza kuijendesha kisasa na kupunguza gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujenzi wa reli ya kisasa ni wa gharama kubwa, na kwa kuwa pamoja na ujenzi wa reli ya kati unaoendelea sasa, pia tunatarajia kuanza kujenga reli nyingine za Tanga – Arusha – Musoma kilometra 1108, Mtware- Mbambabay na Mchuchuma-Liganga kilometra 1092 na Isaka – Rusumo 371. Kamati inashauri Serikali kujenga reli hizi kwa awamu kwa kufuata kipaumbele na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie uwezekano wa kushirikisha sekta binafsi na kupata mikopo yenye gharama nafuu ili kuharakisha zoezi zima la ujenzi wa reli nchini. Kwa kufanya hivyo, Serikali itaweza kuweka fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mingine ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bandari Kamati inashauri yafuatayo; Serikali kuona uwezekano wa kubakisha angalau asilimia 40 ya makusanyo ya Mamlaka ya Bandari Tanzania ili Mamlaka hii iweze kuendeleza baadhi ya miradi katika bandari zake zinafanyiwa kazi.

Pamoja na kuwa shughuli za upanuzi na ukarabati wa bandari ya Dara es Salaam unaendelea, Kamati inasisitiza, ili kuongeza ufanisi na mapato katika bandari ya Dar es Salaam, ni vema juhudzi za makusudi zifanyike ili kuweza kuhamisha gati la mafuta liliopo Kurasini (KOJ) na kujenga gati namba 13 na 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau wote wa bandari waunganishwe kwenye mfumo wa kielektroniki unaotumiwa na bandari ili kuweza kuharakisha uondoshwaji wa mizigo bandarini kwani wakati mwингine mizigo inachelewa kutokana na wadau wengine kama Mkemia Mkuu, Shirika la Viwango Tanzania - *TBS*, Wizara ya Nishati na Madini na wengine wengi kutokuwemo kwenye mfumo huo kutokutumia mfumo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iharakishe ujenzi wa bandari za nchi kavu ili kupunguza gharama kwa wateja kusafiri mpaka Dar se salaam kwa ajili ya kutoa mizigo. Ni muda mrefu sasa tangu Serikali imeanza mipango ya kujenga bandari kavu katika maeneo ya Kwala -Pwani, Ihumwa - Dodoma, Fela-Mwanza, Katosho-Kigoma, King'ori-Arusha, Isaka-Kahama, na Inyala- Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iharakishe kutafuta mwekezaji ili ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo uweze kuanza kwa kuwa bandari hii ni muhimu na itatoa fursa za kiuchumi katika ukanda huo. Vile vile, Serikali ilipe fidia kwa wananchi walibakia ndani ya eneo linalotarajiwa kujengwa bandari hii ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima wakati mradi huu utakapoanza;

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iharakishe mchakato wa kupata *flow meter* mpya kwa ajili ya upimaji wa mafuta yanayoingia Bandari ya Dar es Salaam kwani kutokuwepo na mtambo wa kupima kiasi cha mafuta (*flow meter*) kunasababisha kutokujua kwa uhakika kiwango cha mafuta kinachoingia bandari ya Dar es Salaam.

Mwenyekiti Mwenyekiti, Kuhusu Bandari ya Mtwara, kasi ya uanzishwaji wa bandari ya hii iende sambamba na ujenzi wa njia ya treni. Mamlaka ya Bandari Tanzania- *TPA* ishirikiane kwa karibu na Shirika la Reli Tanzania- *TRC* kuona namna ya kuimarisha mtandao wa reli, kwa kuwa bandari hii ikiunganishwa na reli itazalisha mapato makubwa kwa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kampuni ya Huduma za Meli-*MSCL*; Kamati inashauri yafuatayo; Kampuni ya Huduma za Meli-*MSCL* kufunga teknolojia ya kufatilia matumizi ya mafuta kwenye meli (*Flow Scanner*) na kuweka mfumo wa kufatilia mahali meli ilipo kila wakati (*trucking system*). Kufanya haya kutasaidia kuweza kuziba mianya ya upotevu wa fedha za Kampuni. Aidha, Kamati inashauri Serikali ijipange kutengeneza Meli zote kumi na nne (14) zilizopo katika Maziwa Makuu ili kuiwezesha Kampuni ya Meli Tanzania kumudu kuijiendesha kibashara na hata kuweza kulipa madeni yote inayodaiwa;

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kutohama uwekezaji unaofanyika sasa wa ukarabati na ujenzi wa meli mpya katika Maziwa Makuu, ni vema Serikali iendelee kulipa mishahara ya kwa wafanyakazi wa Kampuni ya Meli Tanzania hasa kwa kipindi hiki cha mpito mpaka Kampuni hii itakapoweza kuijiendesha. Serikali iharakishe kukamilisha zoezi la kurasisimisha bandari bubu zilizopo katika mwambao wa bahari ya Hindi na katika maziwa makuu ili kuongeza mapato katika halmashauri na bandari kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli ya *TAZARA*, Kamati inashauri Serikali iharakishe mazungumzo baina ya nchi wabia wa reli ya *TAZARA* kuhusu kuimarisha reli hii kutohama na umuhimu wake katika kukuza uchumi. Nchi Serikali kwa kushirikiana na nchi wabia wa *TAZARA* ikamilishe itifaki ya 16 kuhusu mkopo kutoka China kwa ajili ya kusaidia kuiboresha *TAZARA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikamilishe manunuzi ya injini na vipuri pamoja na mitambo ya kusaidia kuzalisha kokoto na mataluma ya zege kwenye mgodi wa kokoto uliopo Kongolo- Mbeya na kusaidia viweze kuingia nchini kwa haraka ili vianze kutumika kwa ajili ya kuongeza pato la *TAZARA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania Kamati inaendelea kushauri Serikali kuipatia Mamlaka hii angalau asilimia 50 ya maduhuli

yatokanayo na viwanja vya ndege ili Mamlaka ya Viwanja vya Ndege- (*TAA*) iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuongeza kasi ya ujenzi na ukarabati; pamoja na, uendeshaji wa viwanja vya ndege nchini. Aidha, Mamlaka izitumie vizuri fedha za mapato ya ndani zinazotokana na utuaji wa ndege, uegeshaji wa ndege na magari katika maegesho ya viwanja ili ziweze kutumika katika shughuli za uendeshaji wa viwanja vya ndege. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihakikishe Viwanja vyote vya Ndege na mali zake zote zinazomilikiwa zipate Hati Miliki; Aidha, kuhakikisha Viwanja vya Ndege vyote vinawekewa uzio kwa ajili ya kuepusha hatari zinazotokana na wanyama au binadamu wanaokatiza katika maeneo ya viwanja vya ndege pamoja na kuepuka migogoro ya ardhi na wananchi wanaoishi pembezoni mwa viwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Kampuni ya Ndege Tanzania-*ATCL*; *ATCL* ijitangaze kwenye vyombo rasmi vya Kimataifa ambavyo huonesha safari za ndege dunia nzima. Aidha, Kampuni hii sasa iijipange kuingia katika soko kwa kujitangaza katika vyombo vya habari, majarida na vipeperushi mbalimbali, kujali wateja na kuwa na bei nafuu ili kuhakikisha abiria wengi wanatumia ndege hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wafanyakazi wa Kampuni ya Ndege Tanzania- *ATCL* kupewa mafunzo ya huduma kwa wateja, mara kwa mara, ili kuweza kutoa huduma nzuri wakati wote. Hii itasaidia Kampuni kushindana na makampuni mengine yanayofanya biashara ya usafiri wa anga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Ujenzi kuhusu Wakala wa Barabara- *TANROADS*, Kamati inashauri yafuatayo; Serikali itekeleze Sera yake ya kuunganisha Mikoa yote kwa barabara za lami kama vile, Lindi -Morogoro, Morogoro-Mlimba-Madeke Njombe, Lindi -Songea, Kigoma -Katavi-Tabora-Kagera, Mbeya-Makete-Njombe, Arusha-Mara. Aidha, miradi ya barabara inaendelea ipewe kipaumbele na ile ambayo haijaanza ifanyiwe upembuzi yakini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vilevile, Serikali kujenga kwa kiwango cha lami barabara zifuatazo:- Barabara zinazounganisha nchi yetu na nchi nyigine hususani Mikoa ya Kagera, Kigoma, Katavi, Ruvuma na Mtwara; Barabara zinazounganisha Makao Makuu ya Mikoa kama vile Kigoma-Kasulu-Kagera, Katavi – Kigoma – Tabora; Barabara za Kiuchumi, kama vile, Mtwara – Newala – Masasi, ambayo ni barabara inayopita katika maeneo ambayo yanazalisha korosho kwa wingi, ukizingatia kwamba zao la korosho linachangia kwa kiasi kikubwa uchumi wa mikoa ya kusini na nchi kwa ujumla. Na barabara ya Singida – Chemba – Handeni – Tanga ambayo ni barabara yenye tija kiuchumi kutokana na kuwapo kwa bomba la mafuta linalounganishwa na nchi ya Uganda. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, umuhimu wa makuballiano ya nchi ya Rwanda kutaka kutumia bandari ya Tanga; na Barabara nyingine ni zile zilizohaidiwa za Marais waliostaafu na Rais aliyeo madarakani tunaomba zitekelezwe ahadi hizo kwa wakati. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Bodi ya Usajili wa Wahandisi na Bodi ya Usajili wa Makandarasi kuchukulia hatua kali kwa wakandarasi wanaofanya kazi chini ya kiwango. Sekta ya Ujenzi isimamie ipasavyo Sheria ya barabara kwa kutoa elimu kwa wananchi kwa kutumia vyombo vyahabari, kama runinga, magazeti, redio na simu za mkononi. Aidha, vyombo vinavyohusika na usimamizi wa sheria ya barabara kuwa macho wakati wote na endapo kutaonekana mtu anajenga ndani ya hifadhi ya barabara kuzuiwa na kubomolewa mapema. Aidha, Wakala wa Barabara iendelee na zoezi la kuweka alama za mipaka katika maeneo ya barabara. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya mawasiliano kuhusu mradi wa Anuani Makazi na Misimbo ya Posta, Kamati inashauri yafuatayo; Serikali itoe kipaumbele kwa mradi wa anwani za makazi na misimbo ya posta kwani mradi huu ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu. Aidha, Kamati inashauri Wizara husika ikiwemo Ardhi, Nyumba na

Maendeleo ya Makazi; TAMISEMI na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano zikae na kuona namna nzuri ya kuhakikisha mradi huu muhimu unatekelezwa haraka na kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mradi huu uwe wa kisasa na kuendana na wakati, ni vema wataalam wakajifunze nchi zingine na kuona namna nchi nyininge zilivyofanya na kuweza kufanikisha. Vibao vinavyoonesha majina ya mitaa viandikwe kwa lugha ya Kiswahili na Wakati zoezi la kuweka majina ya mitaa linaendelea, ni muhimu Serikali za Mitaa kuhakikisha zinaweka ulinzi wa nguzo dhidi ya wahalifu wanaochukua vyuma chavu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA, ikabiliane na changamoto za kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano, kama vile, uhalifu mitandaoni unaojumuisha kashfa kwa watu, usambazaji wa picha zisizostaili hivyo kuharibu maadili, mila na desturi zetu. Aidha, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA iendelee kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kutekeleza sheria ya uhalifu wa kimtandao na kuwabana wahalifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati inaendelea kusisitiza kuongezwa kasi ya zoezi la usajili wa namba za simu ili kuwa na taarifa za kila mmiliki au mtumiaji wa simu kwa ajili ya usalama na kutekeleza Sheria ya Mawasiliano na Posta. Vilevile, Serikali iongeze kasi ya kutoa vitambulishao vya Taifa ili kila Mtanzania aweze kutambuliwa na kuepuka udanganyifu unaofanywa kwenye mitandao na kuendelea kudhibiti mawasiliano ya ulaghai hatimaye kupunguza vitendo viovu vinavyofanyika kuititia njia ya mtandao na kuimarisha usalama wa watu na mali zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote-UCSAF, Kamati inashauri, Serikali ipitie na kuangalia upya taratibu za umilikishwaji ardhi hasa maeneo ya ardhi yanayojengwa minara ili kuweka utaratibu wa maeneo yaliyokodiwa ama kununuliwa kwa ajili ya ujenzi wa minara kumilikiwa na Serikali za vijiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihakikishe inaweka mabango yanayoonesha ushiriki wake katika ujenzi wa minara ambayo imetoa ruzuku. Hii ni kutokana na ukweli kuwa Serikali za Mikoa, Wilaya hadi ngazi ya chini pamoja na wananchi hawatambui uwepo wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote na kwamba, miradi hiyo ya ujenzi wa minara ni kwa ruzuku ya Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana iliyoko maeneo mengi ni kuwa minara inajengwa na Makampuni ya ya simu yenye; hivyo mchango wa Serikali katika kusambaza mawasiliano hautambuliki kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) iwekee masharti ya kutoa leseni kwa Makampuni ya Simu pamoja na masharti mengine ya kupeleka mawasiliano katika maeneo ya pembezoni kama mchango wa kijamii (*Corporate Social Responsibility*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika la Posta Tanzania, Kamati inashauri yafuatayo; Serikali iharakishe kulipa madeni ya pensheni kwa wafanyakazi wa iliyokuwa Posta ya Jumuia ya Afrika Mashariki ili kuliondolea Shirika mzigo wa kulipa madeni ya kila mwezi, fedha ambazo zingeelekezwa kwenye uendeshaji wa shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Simu (*TTCL*), Shirika la Mawasiliano Tanzania (*TTC*) liweke mikakati madhubuti ya kukusanya madeni kwa Wizara/Taasisi na Mashirika ya Serikali ambayo madeni hayo yameripotiwa hadi Juni 2018 kufika Jumla ya shilingi bilioni 28, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhakikisha kunakuwa na mpango endelevu wa kuulinda na kuuendeleza Mkongo wa Taifa. Hili lifanyike kwa kuangalia upya utaratibu ambao umeruhusu Makampuni ya Simu mengine kumiliki Mikongo yao sambamba na Mkongo wa Serikali kwani Mikongo hii binafsi itafifisha maendeleo ya Mkongo wa Serikali na hata kuhatarisha usalama wa nchi pamoja na kuikosisha Serikali Mapato. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ni muhimu sana katika kuharakisha na kuchochaea maendeleo ya nchi. Miradi ilio ndani ya Sekta hii ni mikubwa na inahitaji fedha nyingi ili yote iweze kukamilika kwa wakati uliopangwa. Hivyo, Kamati inaona ni muhimu Serikali kushirikisha Sekta binafsi katika kutekeleza miradi hii mikubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao waliyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti pamoja na kuandaa taarifa hii. Naomba kuwatambua wajumbe wa Kamati ya Miundombinu walioshiriki mwanzo hadi mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni na Ushauri kwa niaba ya wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Kwa namna ya pekee naomba nimshukuru Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Eng. Isack Kamwelwe, akisaidiana na Manaibu Mawaziri, Mheshimiwa Justus Atashasta Nditiye na Mheshimiwa Elias Kwandikwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati inawashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara hii *Arch. Elius A. Mwakalinga* (Sekta ya Ujenzi), *Eng. Dkt. Leonard Chamuriho* (Sekta ya Uchukuzi), *Eng. Dkt. Maria Sasabo* (Sekta ya Mawasiliano) pamoja na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Jim Yonaz. Kamati pia inawashukuru Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na wafanyakazi wote ambao wameipa Kamati ushirikiano mkubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nachukuwa fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake. Aidha, shukrani za pekee ziende kwa Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Dickson M. Bisile pamoja na Makatibu wa Kamati Ndugu Hosiana John na Ndugu Francisca Haule pamoja na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao uliowezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti baada ya maelezo hayo, naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA
UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO KWA MWAKA WA
FEDHA 2018/2019; PAMOJA NA MAONI NA USHAURI KUHUSU
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO
KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 – KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia Kanuni ya 123 ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari 2016, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu zifuatazo: -

- a) Sehemu ya Kwanza inahusu utangulizi, inabainisha mpangilio wa taarifa inayowasilishwa;
- b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi unaojikita katika masuala makubwa mawili yafuatayo: -

i) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2018/2019. Mapitio yanajielekeza zaidi katika makusanyo ya mapato, Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo, Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo na Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati;

ii) Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Uchambuzi huu upo katika maeneo makuu manne ambayo ni Makisio ya Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na Mambo mengine muhimu yaliyojitekeza wakati wa kujadili, kuchambua na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii.

c) Sehemu ya Tatu imejielekeza katika Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusiana na masuala yote yaliyofanyiwa uchambuzi katika **Fungu 62 (Sekta ya Uchukuzi)**, **Fungu 98 (Sekta ya Ujenzi)** na **Fungu 68 (Sekta ya Mawasiliano)**.

SEHEMU YA PILI

2.0 **MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**
2.1 **Makusanyo ya Mapato**

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 hadi kufika 28 Februari, 2019, Sekta ya Mawasiliano ilikusanya jumla ya **Shilingi 32,094,316,287.09**. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 32,093,716, 287.09** zimetokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na **Shilingi 600,000** zimetokana na mauzo ya nyaraka za zabuni.

Mheshimiwa Spika, fungu 98- Sekta ya Ujenzi ilikadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi 68,827,800.00** kupitia idara zenye vyanzo vya mapato. Hadi kufika mwezi Machi, 2019 jumla ya **Shilingi 23,180,000.00** zilikusanywa sawa na **asilimia 33.68** ya kiwango kilichokadiriwa kukusanywa.

2.2 Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2018/2019

Mheshimiwa Spika, sehemu hii inabainisha upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo kwa Sekta zote za Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Jedwali Na. 1, Upatikanaji Fedha za Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Sekta Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano hadi Kufikia 28 Machi, 2019

SEKTA	Fedha zilizoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2018/19			Fedha zilizotolewa hadi kufikia Machi, 2019		
	Matumizi ya Kawaida	Fedha za Ndani za Miradi ya Maendeleo	Fedha za Nje za Miradi ya Maendeleo	Matumizi ya Kawaida	Fedha za Ndani za Miradi ya Maendeleo	Fedha za Nje za Miradi ya Maendeleo
Uchukuzi	90675,898,235	2300,739,000,000	0	54,920,905,599,40 (60,56%)	391,161,650,000 (17%)	0
Ujenzi	33129,943,796	1,510,514,754,141,38	435,927,599,000	21,078,292,500 (64%)	850,266,153,647,15 (55%)	252,325,455,891 (58%)
Mawasi- iano	3856,423,000	15,000,000,000	0	2,728,316,826,97 (71%)	1,531,406,368,91 (10%)	0

Chanzo: Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano 2018/2019

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Ujenzi (Fungu 98), mwenendo wa utolewaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Sekta hii ni wakuridhisha kwani hadi mwezi Machi, 2019 **asilimia 55** tu ya Fedha za Ndani za Miradi ya Maendeleo zilikuwa zimetolewa.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Uchukuzi (Fungu 62), bado kumeendelea kuwapo kwa changamoto ya kutokutolewa fedha kwa wakati; na hivyo, kusababisha baadhi ya miradi kuchelewa kuanza; hivyo, kutokukamilika kwa wakati uliopangwa. Kama Jedwali Na.1 linavyoonesha, kati ya Fedha zote za Ndani za Miradi ya Maendeleo zilizoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; fedha zilizotolewa hadi kufika mwezi Machi, 2019 ni **asilimia kumi na saba tu (17%)** tu hivyo, baadhi ya miradi haikupata fedha yoyote. Miradi hiyo ni mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa kati ya Mtwara-M/bay, Mchuchuma & Liganga (Km 1092), ujenzi wa reli ya kisasa

kutoka Tanga-Arusha hadi Musoma (Km 1,108) na mradi wa usafiri wa Treni Abiria Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mawasiliano (Fungu 68), Kamati imebaini kuwa Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizopokelewa hadi Mwezi Machi 2019, ni **Shilingi 3,670,500,020.00** ambapo kati ya fedha hizo, Fedha zilizotumika ni **Shilingi 1,531,406,388.91** tu.

2.3 **Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa kwa Mwaka 2018/2019**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa baadhi ya miradi ya maendeleo iliyokuwa imetengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Ziara hii ilifanyika kuanzia tarehe 13 hadi 20 Machi, 2019 katika mikoa ya Dodoma, Morogoro, Pwani, Dar es Salaam na Mtwara. Miradi iliyotembelewa ni; -

- a) Viwanja cha Ndege cha Dodoma na Msalato;
- b) Ujenzi wa reli ya kati sehemu ya Dar es Salaam- Morogoro;
- c) Ujenzi wa jengo la tatu la Abiria (Terminal III), na Ujenzi wa rada ya kuongozea ndege Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere;
- d) Chuo cha Usafirishaji Tanzania-NIT
- e) Ujenzi wa barabara ya Mtwara-Newala- Masasi (km 210)
- f) Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara; na
- g) Ujenzi wa Bandari ya Mtwara.

2.3.1 **Yaliyobainika katika Ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo**

- i) **Mradi wa upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Dodoma na Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Msalato, Dodoma.**

Mheshimiwa Spika, Shughuli za ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Dodoma zilianza rasmi mwezi June, 2018 na unatarajiwa kukamilika Machi 2019 kwa gharama

ya Shilingi **milioni 624**. Mradi huu wa upanuzi na ukarabati wa jengo la abiria umeongeza ukubwa wa jengo hadi kufikia uwezo wa kuhudumia abiria 146 wanaoondoka kwa wakati mmoja ukilinganisha na uwezo wa jengo la zamani liliokuwa na uwezo wa kuhudumia abiria 35 tu.

Katika ziara hiyo, Kamati ilibaini kuwa changamoto inayokabili upanuzi wa Kiwanja cha Ndege Cha Dodoma ni upatikanaji wa fedha na gharama kubwa kwa ajili ya fidia za utwaaji wa eneo liliosalia ili kumalizia kusimika mfumo wa taa za kuongozea ndege, ambapo kwa sasa zimebekwa upande mmoja tu wa barabara ya kuruka na kutua ndege.

Aidha, Kiwanja kutokuwa na uzio huku kimezungukwa na makazi ya watu wenyewe shughuli mbalimbali zisizo rafiki kwa usafiri kwa anga. Jambo hili wakati mwingine linasababisha watu kukatiza Kiwanjani hapo. Juu ya hayo, mara kadhaa wanyama, kama vile, mbwa; hukatiza katika maendeo ya Kiwanja jambo linalodhoofisha usalama wa kiwanja.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu kiwanja cha ndege cha Msalato, Kamati ilijulishwa kuwa mwaka 2017, Serikali kuitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania, iliingia Mkataba na Kampuni ya STUDI International ya nchini Tunisia kwa ajili ya mapitio ya upembusi yakinifu na usanifu wa awali; na pia, kufanya usanifu wa kina katika Kiwanja hiki kwa gharama ya **Dola za Kimarekani 1, 885, 050.00**.

Kazi za usanifu zimelenga kugawa mradi katika awamu mbili; yaani awamu ya kwanza, ambapo Kiwanja kitakuwa daraja (code) 4E chenye uwezo wa kuhudumia ndege kubwa kama, Airbus A 350, Boeng 787 Dreamliner, Boeng 777, Ndege za Mizigo aina ya Antonov (AN-125) kwenye kipindi cha miaka 20 ya awali; na awamu ya pili ambayo itahusu kupanua Kiwanja kufikia daraja (code) 4F lenye uwezo wa kuhudumia Ndege kama Boeng 747 na Airbus A380. Benki ya ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imeonesha nia ya kufadhili ujenzi wa awamu wa kwanza ambao unakadiriwa kugharimu dola za Kimarekani **Milioni 591.266**.

Katika mradi huu wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Msalato, changamoto imekuwa ni upatikanaji wa fedha za ujenzi pamoja na ulipaji fidia kwa wananchi waathirika wapatao 1,926 ambao wanatarajiwa kulipwa fidia kiasi cha **Shilingi bilioni 14.6.**

- ii) **Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge) sehemu ya Dar es Salaam hadi Morogoro**

Mheshimiwa Spika, Kamati imejulishwa kuwa, Ujenzi wa Reli ya Kati sehemu ya Dar es Salaam mpaka Morogoro (Km 300) kinajengwa kwa ubia wa Kampuni ya YAPI MERKEZI ya Uturuki na MOTA-ENGIN ya Ureno. Gharama za Mradi kwa sehemu hii ni **Shilingi Trioni 2.7.**

Shughuli zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa madaraja (42%), ujenzi wa makalvati (55%), ujenzi wa daraja refu katikati ya jiji la Dar es Salaam lenye Km 2.54 (63%), ukataji wa miinuko na ujazaji wa mabonde (66%), kazi za utandikaji wa reli zinaendelea; pamoja na, kazi ya uwekaji wa nguzo za umeme kwa ajili ya kuendeshea treni.

Mheshimiwa Spika, Kwa ujumla, maendeleo ya mradi wa ujenzi kipande cha kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro ni mazuri; kwani fedha kwa ajili ya malipo mbalimbali ya mradi zinatolewa vema na kwa wakati na hakuna madai yoyote kwa Mkandarasi. Aidha, fidia mbalimbali kwa ajili ya maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili ya kupisha ujenzi wa reli zinaaendelea kutolewa kadiri mradi unavyosogea. Ujenzi wa sehemu hii umefikia asilimia 45, na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Mwezi Novemba, 2019.

- iii) **Ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria (Terminal III), Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere**

Mheshimiwa Spika, Kamati imejulishwa kuwa mkandarasi wa ujenzi na mhandisi mshauri walipatikana mwaka 2013 na wameendelea na kazi za ujenzi kwa kuzingatia mikataba yao na Serikali. Hadi mwezi Februari 2019, utekelezaji wa kazi zote

umefikia asilimia 95. Kasi hii imetokana na juhudzi za Serikali kulipa mada ya mkandarasi kwa lengo la kumaliza kazi kwa muda uliopangwa.

Kwa ujumla, mchanganuo wa kazi zote za ujenzi wa jengo zimefikia asilimia tisini na sita (96%), kazi za nje ya jengo – (maegesho ya magari) asilimia tisini na mbili 92%, kazi za nje ya jengo (maegesho ya ndege) asilimia tisini na nane (98%). Kazi za ujenzi zinaendelea vizuri na inatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 31 Mei, 2019.

Kukamilika kwa jengo la tatu la abiria katika Kiwanja hiki kutawezesha kuhudumia abiria 2,800 kwa saa; na abiria milioni sita, kwa mwaka, jambo litakalosababisha kiwanja hiki kuwa kitovu cha usafiri wa anga nchini na Afrika mashariki kwa ujumla.

iv) Ujenzi wa Rada ya Kuongozea Ndege

Mheshimiwa Spika, Katika kuimarisha usafiri wa anga nchini, mwaka 2016/17, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) ilianza mchakato wa ununuzi wa rada nne (4) za kuongozea ndege za kiraia nchini. Mradi huu unatekelezwa na Mzabuni Thales LAS France SAS kutoka Ufaransa kwa thamani ya **Euro 22, 351,248.00** gharama ya mitambo na **Shilingi 5, 865,097,261** gharama ya ujenzi wa miundombinu.

Mradi wa Rada unagharamiwa na Serikali kwa asilimia 100; ambapo asilimia 55 sawa na **Shilingi bilioni 35.1** imegharamiwa na Serikali Kuu. Fedha hizi zimekwishapokelewa na Mamlaka. Aidha, Mamlaka inagharamia asilimia 45 sawa na **Shilingi bilioni 27.3**.

Usimikaji wa rada hizi unahusisha viwanja vya ndege vya JNIA, Mwanza, Kilimanjaro na Songwe-Mbeya. Mpaka mwezi Machi 2019, jumla ya **Shilingi Bilioni 57,322,085,709** zimekwishatumiwa kwa manunuzi ya Rada nne na ujenzi wa jengo la Rada. Hatua za utekelezaji zilizofikiwa ni kukamilika kwa asilimia 100 jengo la mnara wa Rada, kibanda cha Mlinzi,

na jengo la mitambo ya rada. Aidha, Usimikaji wa mtambo unaoendelea umefikia asilimia 90%.

v) **Chuo ha Taifa cha Usafirishaji-NIT**

Mheshimiwa Spika, kwa uwekezaji huu mkubwa unafanywa na Serikali katika Sekta Usafiri na usafirishaji. Hata hivyo, ipo haja ya kuhakikisha uwekezaji mkubwa pia unafanyika katika uandaaji wa rasilimali watu watakaoendesha na kusimamia uwekezaji huo. Kamati ilipotembelea Chuo cha Taifa cha Usafirishaji ilibaini changamoto mbalimbali ambazo kimsingi zikifanyiwa kazi zitasaidia Chuo hiki kufanya kazi vizuri zaidi na kuzalisha wataalam wengi watakaosaidia kusimamia na kuendeleza miundombinu nchini. Changamoto hizo ni; -

- a) Upungufu wa Watumishi 133 (wanataaluma 87 na watumishi wa kawalda 46). Hali hii imesababisha chuo kutumia watumishi wa muda kutoka nje hasa wanataaluma jambo lenye gharama kubwa na kuelemea Chuo;
- b) Madeni ya Chuo ya Mwaka 2015/16 yanayofikia **Shilingi Bilioni 2.29** yanashuburi kuhakikiwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani Serikali;
- c) Upungufu wa Vifaa vyta kujifunzia na kufundishia hasa mafunzo ya uhandisi;
- d) Kutoamiliika kwa wakati kwa ujenzi wa jengo la Rasilimali Mafunzo (Maktaba), chuo kimeshindwa kukamiliisha ujenzi wa awamu ya tatu wa kituo kama ilivyopangwa kutohana na ufinyu wa bajeti; na
- e) Uhaba wa hosteli za wanafunzi, uchakavu wa barabara za ndani ya chuo, uhaba wa miundombinu ya chuo kama vile, madarasa, karakana na ofisi za watumishi;

vi) **Barabara ya Mtwara-Newala Masasi**

Mheshimiwa Spika, barabara hii ni kati ya barabara za kiuchumi Mkoani Mtwara ambayo inaanzia Mtwara Mjini –

Newala – Masasi Km 210) kwa kupitia Wilaya za Tandahimba na Newala. Ni dhahiri kuwa Serikali iliona umuhimu wa kujenga barabara hii kimkakati kutokana na uzalishaji mkubwa wa zao la korosho ambao hufanyika katika maeneo inayopita barabara hii.

Mkataba wa mradi huu ulisainiwa tarehe 19 Januari, 2017 na kazi ilianza kutekelezwa rasmi tarehe 17 Aprili, 2017. Hata hivyo, Kamati haikuridhishwa na kasi ya utekelezaji wa mradi huu kwani kati ya Kilometra 210, za barabara hii zimejengwa Kilometra 50 tu tangu Mwaka 2017 ambazo ujenzi wake umefikia asilimia 38 tu.

vii) **Kiwanja cha Ndege cha Mtwara**

Mheshimiwa Spika, Mkataba kwa ajili ya ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara ulisainiwa tarehe 09 Novemba, 2017 kati ya Serikali ya Tanzania na *M/S Beijingh Construction Engineering Group Company Ltd* kwa gharama ya **Shilingi Bilioni 50.4** kwa muda wa miezi 27. Kwa mujibu wa Mkataba, kazi zinatarajjiwa kukamilika 26 Septemba 2020. Hali ya kiwanja hiki kwa sasa ni chakavu kutokana na kuwepo kwa mashimo na kubonyea kwa tabaka la lami. Serikali imekusudia kupanua kiwanja hiki kutoka daraja la 3C kwenda 4E ili kiweze kuhudumia ndege kubwa zaidi ndani na nje ya nchi kutokana na umuhimu wa hasa wa kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2018/2019, kiwanja hiki kilitengewa jumla ya **Shilingi 12,848,000,000.00**. Mkandarasi amewasilisha ombi la kulipwa malipo ya awali **Shilingi 7,008,497,029.91** ambapo Kamati imejulishwa kuwa Wizara ya Fedha inaendelea kukamilisha taratibu za malipo hayo. Hata hivyo, mradi huu umechelewa kuanza kwani Mkataba wa ujenzi ulisainiwa toka mwaka 2017 ambapo unatakiwa 2020. Kamati inaona ipo haja ya Mkandarasi kuongeza kasi ya ujenzi ili kukamilisha mradi kwa wakati.

viii) **Bandari ya Mtwara**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa, bandari ya Mtwara ilijengwa katika miaka ya 1950 ikiwa na uwezo wa

kuhudumia tani 400,000 za shehena kwa mwaka. Hata hivyo, bandari hii imeendelea kuwa ya umuhimu katika ukanda wa kusini kwa kuitisha shehena za korosho zisizobanguliwa, makasha, saruji, mitambo na bidhaa zinazotumika katika shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi baharini.

Mheshimiwa Spika, Kijiografia bandari ya Mtwara inazo fursa nyingi kutokana na kuwa na kina kirefu cha mita 9.5 hadi mita 12.5 katika baadhi ya maeneo, eneo kubwa la upanuzi ikilinganishwa na Bandari jirani za Nacal, Beira na Durban zinazotumiwa haswa na nchi za Malawi na Msambiji. Fursa hizi zinaweza kuongezeka endapo; -

- a) Bandari itaunganishwa na reli/barabara kutoka Mtwara hadi Mbambabay kwa mizigo ya nchi za Malawi na Zambia; na
- b) Miundombinu ya Bandari itaboreshwa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Gati mpya za nyongeza;

Mheshimiwa Spika, endepo Bandari hii itaimarishwa itasaidia sana kupata mizigo nchi ya Malawi, kwani karibu migodi yote mikubwa ya madini iko Kaskazini mwa nchi hiyo, hivyo bandari ya Mtwara ndiyo itakayokuwa njia fupi zaidi kuliko bandari za Afrika ya Kusini, hususan Durban.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwa na mipango ya kupanua bandari ya Mtwara kwa kujenga gati nne mpya na kuifanya kuwa ya kisasa kwa ajili ya kuhudumia shehena ya gesi na mafuta, madini, na mazao ya kilimo yanayopatikana ukanda wa Mtwara. Ujenzi kamili ulianza mnamo tarehe 27 Mei 2017 ambapo kwa sasa umefikia asilimia 35 na unatarajia kukamilika mwishoni mwa mwaka 2019.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipotembelea mradi huu, ilijionea maendeleo na kasi nzuri ya utekelezaji. Yapo mapungufu yaliyofanyika mwanzoni mwa mradi ambapo mradi ulianza bila ya kuwa na Mshauri Mwelekezi; hivyo kusababisha

kujenga/ kuchimba kina cha Mita 13 badala ya 15 na upana wa mita 5 badala ya mita 5.5.

ix) **Mradi wa Anuani za Makazi**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ziara katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Mtaa wa Uhuru na kuona utekelezaji wa mradi huu unavyoendelea. Kamati ilielezwa kuwa ifikapo mwezi Aprili, 2019 miundombinu itakamilika katika Kata 3 ambapo inatarajiwा Kata husika zianze kutumia anwani za makazi kufikisha huduma mahali alipo mwananchi ama taasisi kupitia huduma za Posta Mlangoni na EMS.

Mheshimiwa Spika, Mfumo huu unalenga kuhakikisha kila mwananchi anakuwa na anwani ya makazi; hivyo, kuwezesha mwananchi kuhudumiwa kiraishi mahali alipo. Manufaa mengine ya mfumo huu ni kama yafuatayo: -

- i) Kuongeza ajira kutokana na fursa za kusambaza bidhaa kwa wateja;
- ii) Kurahisisha biashara mtandao na kukuza uchumi wa Taifa;
- iii) Kurahisisha utoaji wa huduma mbalimbali za kijamii; Kwa mfano, usajili wa mali, biashara, vizazi na vifo n.k
- iv) Kuongeza Usalama wa wananchi kwa kutoa huduma za dharura kwa wakati mfano ajali, moto, ugonjwa na uhalifu;
- v) Kuongeza mapato ya Serikali kwa kuwa mamlaka zinazohusika na ukusanyaji wa mapato zinakuwa na taarifa ya mahali walipa kodi/ wananchi walipo, hivyo kuleta tija na ufanisi katika ukusanyaji wa mapato;
- vi) Kuboresha utendaji wa taasisi mbalimbali kwa mfano, benki kuwa na uhakika wa mahali wanapopatikana wateja wakati wa mikopo n.k
- vii) Kurahisisha utambulisho wa watu wanaoishi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na

viii) Kuwezesha utambuzi wa mwelekeo na eneo ambalo mtu anahitaji kwenda.

Mheshimiwa Spika, licha ya mafanikio yanayotarajiwa kutokana na kuendelezwa kwa mradi wa anuani za makazi; changamoto mbalimbali zifuatazo zimeendelea kukabili utekelezaji wa mradi huu: -

- i) Ufinyu wa Bajeti; hakuna fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu, na hata kiasi kidogo kinachotengwa hakitolewi chote/ ama kutotolewa kwa wakati; kwa mfano katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kati ya **Shilingi Bilioni 3** zilizoidhinishwa, hadi kufikia mwezi Juni, 2018 zilitolewa jumla ya **Shilingi 1, 292,279,295.67** tu;
- ii) Barabara/mitaa mingi kutokuwa na majina yaliyorasimishwa;
- iii) Uharibifu wa miundombinu ya mfumo uliopo katika miradi;
- iv) Kutokuwapo na taarifa za Barabara na Nyumba/ Majengo katika kila Kata na ujenzi holela; na
- v) Baadhi ya halmashauri kutokuwa na mpango kazi wa mfumo; na ushirikishaji hafifu wa wadau katika kuchangia gharama za uwekaji wa miundombinu.

x) **Ujenzi wa Mizani Dakawa Morogoro**

Mheshimiwa Spika, Kamati imejulishwa kuwa mradi huu ulianza tarehe 25 Oktoba, 2017 na kutarajiwa kumalizika tarehe 24 Oktoba, 2018. Kutokana na changamoto zilizojiteza, muda wa kukamilika mradi uliongezwa hadi tarehe 24 Machi 2019. Hadi kufikia tarehe 20 Machi, 2019 kazi ilikuwa imekamilika kwa asilimia 98 ingawa thamani ya kazi iliyoidhinishwa kwa malipo ni asilimia 75. Mradi unagharimu jumla ya **shilingi 14,784,337,526.99** unahusisha ujenzi wa mizani mbili kubwa na za kisasa za kupima uzito wa magari yakiwa katika mwendo; ukiwemo mfumo wa kuchambua magari yaliyozidisha uzito. Mradi huu ni muendelezo wa hatua za

kudhibiti na kupunguza uharibifu wa barabara unaosababishwa na magari kuzidisha uzito.

Mheshimiwa Spika, Kwa jumla, katika ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati imebaini changamoto kubwa iliyopo katika utekelezaji wa miradi hasa ya sekta ya Uchukuzi ni kutopatikana kwa fedha za miradi kwa wakati.

2.4 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua na kupitisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2018/19, Kamati ilitoa maoni na ushauri mbalimbali. Maoni na ushauri huo uligusa masuala muhimu kama vile Bandari, Reli, Viwanja vya Ndege, Barabara na Mawasiliano. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kati ya mambo yaliyoshauriwa, yapo ambayo Serikali imeyazingatia na mengine yanaendelea kuzingatiwa. Baadhi ya ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni pamoja na: -

a) Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam;

Kamati imejulishwa kuwa hatua mbalimbali zimechukuliwa ili kuondoa vikwazo visivyo vya lazima katika bandari zetu; kama vile kuweka vituo vitatu vya ukaguzi wa maroli kwenye ushoroba wa kati; kuiondoa nchi ya DRC Congo kwenye utaratibu wa himaya moja ya forodha, kwa kuwa, nchi hiyo si moja ya mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; kuanzisha vituo vya pamoja mipakani na kuboresha reli na barabara zilizopo bandarini.

i) Uboreshaji wa gati namba 1-7 na ujenzi wa gati jipya la kushushia magari. Ujenzi wa gati namba 1 umekamilika hapo tarehe 8 Disemba, 2018; ujenzi wa gati la kushushia shehena za magari ambao unahusisha kazi za ujazaji wa kifusi na kuchimba kwa ajili ya kuongeza kina imefikia asilimia 45; Kazi za usanifu wa gati namba 4-7; pamoja na, utengenezaji wa vifaa mbalimbali vinavyotumika katika kujenga na kuimarisha gati namba 2-7 zinaendelea.

ii) Kupanua na kuchimba ili kuongeza kina cha lango la kuingilia meli. Kazi ya usanifu wa kina ilianza mwezi Disemba 2018 na inatarajia kukamilika mwezi Juni, 2019. Kazi ya kupanua, kuchimba na kuongeza kina cha lango la kuingilia na kutokea meli zinatarajiwa kuanza mwezi Oktoba, 2019.

b) Kampuni ya Huduma za Meli- MSCL, imezingatia ushauri wa kufunga mfumo wa kukata tiketi kwa njia ya kielektroniki. Mfumo huu uliana rasmi mwezi Januari, 2018 utasaidia kuimarisha njia za ukusanyaji mapato.

c) Ushauri wa kuendelea na ujenzi wa Reli ya Kati na matawi yake yote;

Kamati imefahamishwa kuwa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha Kimataifa ni wa awamu. Awamu ya kwanza utekelezaji wake umefikia asilimia arobaini na na sita (46%) kutoka Dar es Salaam-Morogoro (km 300) na unatarajia kukamilika Novemba, 2019;

Aidha, Awamu ya pili ya kutoka Morogoro-Makutopora (km 336), Mkataba umesainiwa tarehe 29 Septemba, 2017 na ujenzi wake uliana 26 February, 2018 na unatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba 2020. Ujenzi wa reli hii umefikia asilimia saba (7%);

d) Ushauri wa kukarabati na kufufua njia nyingine za reli

Mheshimiwa Spika, kuhusu reli ya Tanga-Arusha- Musoma, ukarabati wa sehemu ya Tanga-Arusha (Km 439), jumla ya Km 253 (Tanga-Mombo-Same), kazi za ukarabati wa njia zmekamilika. Kazi zinazoendelea ni ujenzi wa madaraja na makalavati. Aidha, Kuhusu reli ya Mtwara-Mbambabay na Matawi ya Liganga na Mchuchuma, usanifu wa awali wa njia ya reli kwa kiwango cha *standard gauge* umekamilika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukarabati wa baadhi ya maeneo korofi ya reli, madaraja na mabehewa 40 ya mizigo, Shirika la Reli Tanzania limefanikiwa kusafirisha tani 429.994 za mizigo ikilinganishwa na tani 351,758 zilizosafirishwa kwa kipindi cha mwaka 2017 ikiwa ni ongezeko la **asilimia 22.24**.

e) **Mheshimiwa spika**, Ulipaji wa madeni ya wafanyakazi wa TAZARA; Kamati imejulishwa kuwa kazi ya uhakiki wa madeni ambayo TAZARA inadaiwa ilifanywa na wataalamu kutoka Hazina na kukamilika mwezi February, 2019. Aidha hadi kufikia June 2018 deni la TAZARA liliolahakikiwa ni **shilingi biloni 433.9**. Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kulipa deni linalohusu upande wa Tanzania.

f) **Mheshimiwa Spika**, Kuimarisha usalama wa usafiri wa nchi kavu;

Kamati ilijulishwa kuwa Serikali kupitia SUMATRA imekuwa ikifanya tafiti mbalimbali ili kubaini vyanzo vikuu vya ajali za barabarani. Matokeo ya tafiti hizo yanaonesha asilimia 76 ya ajali zinasababishwa na makosa ya kibinadamu, asilimia 16 ubovu wa magari na asilimia 8 ni miundombinu na mazingira. Katika hatua za kutatua changamoto hizo Serikali ilichukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufunga vifaa vya kutoa taarifa za mwenendo wa mabasi ya abiria yanayofanya safari za mikoani na kuunganishwa na mfumo unaofuatilia mwenendo wa mabasi (*vehicle tracking system*). Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 jumla ya mabasi 3083 yalikuwa yamefunga vifaa hivyo. Aidha, Bunge lilitunga Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini, 2018 ambayo imeweka utaratibu wa kusajili wahudumu wote wa vyombo vya usafiri ardhini; kudhibiti taaluma ya udereva na ubora wa vyombo vya usafiri ardhini ambapo ilianza na magari yanayotumika na abiria.

g) **Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania;

i. Kuhusu kuboresha Kiwanja cha Ndege cha Mwanza. Kamati imejulishwa kuwa kazi ya uboreshaji wa kiwanja hiki inaendelea ikiwa ni pamoja na ujenzi wa jengo la mizigo ambao umekamilika kwa **asilimia 90** na ujenzi wa jengo la kuongozea ndege (*control tower*) umekamilika kwa **asilimia 90**. Mamlaka inaendelea kufanya marejeo ya usanifu wa ujenzi wa jengo la abiria. Pia Serikali tayari imeanza mazungumzo na Serikali ya Rwanda ili Rwanda Air ianze

kusafirisha minofu ya samaki kwenda Ulaya kupitia kiwanja hiki; na

ii. Ulipaji wa fidia ili kumaliza migogoro na wananchi walio kwenye maeneo ya viwanja vya ndege. Kamati ilijulishwa kuwa Serikali imekuwa inalipa fidia kwa wananchi ambao wameathirika kutokana na utwaaji wa ardhi ili kupisha ujenzi na upanuzi wa viwanja vya ndege nchini. Serikali imelipa fidia ya **shilingi bilioni 3.4** kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja cha ndege Dodoma na **bilioni 4.3** katika viwanja vya ndege vya Sumbawanga na Shinyanga. Aidha, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege-TAA kwa kushirikiana na Wakala wa Barabara Tanzania-TANROADS imetayarisha vitabu vya uthamini kwa ajili ya fidia katika viwanja vya ndege vya Songea, Dodoma (awamu ya tatu), Msalato, Simiyu, Lake Manyara, Iringa, Musoma, na Nachingwea. Taratibu za malipo hayo zinaendelea.

h) Kampuni ya Ndege Tanzania-ATCL;

Kampuni imefanikiwa kuingia katika Mfumo wa (*International Air Transport Association-IATA*) na kujunga na Mfumo wa uuzaji wa tiketi ulimwenguni (*Global Distribution System-GDS*). Kwa sasa tiketi za ATCL zinapatikana kwa Wakala wote waliosajiliwa katika Mfumo wa wauzaji wa tiketi duniani.

i) Kuunganisha Makao Makuu ya Mikoa ambayo bado hayajaunganishwa kwa barabara za lami; barabarara zimeendelea kutengenezwa kwa kiwango cha lami kulingana na upatikanaji wa fedha, barabara hizo ni barabara ya Kigoma – Kagera, Katavi – Kigoma, Kigoma – Tabora, Katavi – Tabora, Njombe – Mbeya, Arusha – Mara na Shinyanga – Simiyu – Mwanza na Mara.

j) Uharibifu wa barabara kutokana na uzito mkubwa wa mizigo. Kamati imejulishwa kuwa utafiti uliofanywa na chuo kikuu cha Dar Es Salaam kupitia BICO, M/S COWI, CML pamoja na PADECO kupitia JICA ulionesha kwamba matairi ya *super single* yamekuwa chanzo kikubwa cha uharibifu wa barabara. Ili kutatua changamoto hii Serikali imeanza kutumia

sheria mpya ya udhibiti wa uzito wa mgari ya Afrika Mashariki kuanzia mwezi Machi, 2019 ambapo matairi aina ya *super single* yamepunguziwa uzito wa kubeba mzigo kutoka tani 10 hadi tani 8.5.

Aidha, ujenzi wa mizani bandarini kwa ajili ya kuhakikisha magari yote yaliyozidi uzito hayataruhusiwa kuanza safari kabla ya uzito huo kupunguzwa kwa mujibu wa sheria ya Afrika Mashariki. Kutoa adhabu kali kwa wafanyakazi wa mizani na wasafirishaji wasio waaminifu kwa kuruhusu magari yenye uzito mkubwa kuendelea na safari pale yanapoonekana yamezidisha uzito. Pia ufungaji wa mfumo (*weigh Bridge Management System*) kwa ajili ya kuangalia utendaji wa mizani zetu kwa uwazi zaidi ili kupunguza rushwa na kuongeza ufanisi.

k) Kupunguza msongamano jijini Dar Es Salaam kwa kujenga barabara za juu hasa katika makutano ya barabara kuu zenye msongamano mkubwa kama vile Magomeni, Morocco na Mwenge. Kamati imejulishwa kuwa, Serikali inaendelea na ujenzi wa *interchange* kwenye makutano ya Ubungo na ujenzi wa *flyover* mbili katika maeneo ya makutano ya barabara ya Nyerere na Kawawa pamoja na makutano ya barabara ya Kilwa na Nelson Mandela eneo la uhasibu katika mradi wa BRT II ambapo mkataba wa kuanza ujenzi huu umesainiwa.

l) Kuongeza mizani za kisasa zinazopima uzito wa magari huku yakiwa kwenye mwendo; Kamati imejulishwa Serikali imeendelea na ujenzi wa mizani inayopima magari yakiwa katika mwendo katika maeneo mbalimbali kama vile Dakawa morogoro ambayo ujenzi wake umefikia asilimia 98, Nala (Dodoma), Njuki (Singida), Wenda (Iringa) na Mpemba (Songwe);

m) Serikali kuhakikisha inasimamia kuwepo kwa ushirikiano katika mifumo ya miundombinu (infrastructure sharing) na kuyaelekeza makampuni ya simu kushirikiana katika ujenzi wa minara na kufunga antenna zao katika mnara mmoja ili kuepuka matumizi ya eneo kubwa la ardhi kwa kuwa

mrundikano wa minara eneo moja. Kamati imejulishwa kuwa Serikali kupitia mamlaka ya mawasiliano inaendelea kusimamia kuwepo kwa ushirikiano wa miundombinu baina ya watoa huduma na ili kuhakikisha suala hili linatekelezwa ipasavyo serikali ilitunga kanuni za kieletroniki za mawasiliano na Posta (the electronic and postal communications Access, Co-Location and Infrastructure sharing Regulations, 2018). Aidha watoa huduma za mawasiliano wanashirikiana katika matumizi ya pamoja ya minara.

n) Ushauri wa Kamati kuhusu Serikali kufuta deni la **shilingi bilioni 26** ambalo Shirika la Posta linadaiwa na Mamlaka ya mapato Tanzania. Kamati ilijulishwa kuwa Serikali kupitia Sheria ya Msamaha (*Amnesty*) imekubali kufuta deni la shirika la **shilingi 12,039,071 437** linalotokana na tozo, riba, na adhabu na kubakiwa na deni la msingi la **shilingi 14,840,500,596**. Serikali kupitia wizara ya fedha na mipango inaendelea na taratibu za kuchukua deni hili.

o) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kudhibiti mawasiliano ya ulaghai na kupunguza vitendo viovu vinavyofanyika kupitia njia ya mtandao ili kuimarisha usalama wa watu na mali zao. Kamati imejulishwa kuwa Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano imeendelea na zoezi la kuzitambua na kuzifungia namba za simu ambazo zimekuwa zikiingiza mawasiliano ya simu za kimataifa kwa njia ya ulaghai. Kabla ya udhibiti huu Serikali ilikuwa ikipoteza mapato yake kwa asilimia 100. Katika kipindi cha Julai 2018-Februari, 2019 TCRA imefanikiwa kupunguza mawasiliano ya ulaghai kutoka asilimia 15 hadi kufikia chini ya asilimia 5.

2.5 Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

2.5.1 Makisio ya Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano hususan Sekta ya Ujenzi inatarajia kukusanya jumla ya **shilingi 68,828,000.00** kutoka Idara zenye vyanzo vyaa mapato kama vile Idara ya Rasilimali

Watu, Idara ya Huduma za Kiufundi, Kitengo cha Menejimenti ya Huduma za Ununuzi na Ugavi. Aidha, Sekta ya Mawasiliano inatarajia kukusanya jumla ya **shilingi 22,517,437,400** katika mwaka wa fedha 2019/2020 kutohana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa mawasiliano pamoja na mauzo ya nyaraka za zabuni.

2.5.2 Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi Triliioni 4.8 (4,888,087,065,163)**. Jedwali lifuatalo linaonesha mchanganuo wa fedha zinazoombwua:

Jedwali Na.2, Makadirio ya Matumizi ya Kawaida Na Miradi ya Maendeleo Kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

SEKTA	MATUMIZI YA KAWAIDA	MIRADI YA MAENDELEO	JUMA
Ujenzi (Fungu 98)	36,142,664,000.00	1,204,037,604,268.00	1,240,180,268,268
Uchukuzi (Fungu 62)	85,408,131,000	3,543,722,242,895	3,629,130,373,895
Mawasiliano (Fungu 68)	3,973,197,000	15,000,000,000	18,856,423,000
JUMAKUU	125,523,992,000	4,762,759,847,163	4,888,087,065,163

Chanzo; Taarifa ya Makadirio ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka 2019/2020 kiasi cha **Shilingi Triliioni 4.8** ni ongezeko la **asilimia 14** ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha uliopita 2018/2019 ambayo ilikuwa **Shilingi Triliioni 4.2**.

2.5.3 Mambo Mengine yaliyojitekeza wakati wa Kuchambua na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka 2019/2020

a) Sekta ya Uchukuzi

i. Uimarishwaji wa Mtandao wa Reli Nchini

Mheshimiwa Spika, moja kati ya vipaumbele vikuu kwa upande wa uimarishwaji wa miundombinu ni ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kisasa (*Standard Gauge*). Katika kufanikisha azma hiyo Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya mradi huu mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za ujenzi wa reli ya kati kutoka **shilingi trilioni 1.5** zilizoidhinishwa 2018/2019 hadi **shilingi trilioni 2.4** zilizotengwa kwa mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la **asilimia 60**. Fedha hizi ni kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kisasa kutoka Dar es Salaam- Makutupora - Tabora- Isaka Rusumo.

Mheshimiwa Spika, hii ni hatua nzuri na ya kupongezwa kwani, ujenzi wa reli hii yenye kasi ya km 160 kwa saa itasaidia kurahisisha usafiri hasa wa abiria na na usafirishaji wa mali ghafi hatimaye kuchochaea ukuaji wa viwanda na hata kuongeza Pato la Taifa.

Ni matarajio ya Kamati kuwa reli hii itajengwa na matawi yake kwa kuzingatia faida za kiuchumi na kipaumbele kitawekwa katika maeneo ambayo yana mali ghafi nydingi ili kuleta tija.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati imejulishwa kuwa katika mwaka wa fedha 2019/2020, Mfuko wa Maendeleo ya Reli umetengewa **shilingi bilioni 255.7 (255,700,000,000)** kwa ajili ya kukarabati reli iliyopo, ununuzi wa injini na mabehewa ya mizigo na abiria na kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya reli za ni Kaliua-Mpanda-Karema, Tabora-Kigoma, Tanga-Arusha-Musoma na Mtwara Mbambabay na matawi ya mchuchuma Liganga.

ii. **Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania-TPA**

Mheshimiwa Spika, Mamlaka hii inamiliki na kusimamia Bandari Kuu za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara pamoja na bandari ndogo za Kilwa Masoko, Kilwa Kivinje, Kwale, Lindi, Mikindani, Mafia, Pangani na Bagamoyo. Vilevile, Mamlaka ya Bandari Tanzania inamiliki bandari kadhaa za maziwa makuu kama vile Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa. Majukumu ya Mamlaka hii ni kuendeleza, kuendesha shughuli za bandari, kutangaza huduma za bandari, kushirikisha na kusimamia sekta binafsi katika uendelezaji za uendeshaji wa bandari nchini.

Mamlaka ya Bandari licha ya kutoa huduma kwa mizigo inayoingia na kutoka ndani ya nchi; pia inahudumia nchi za Burundi, Rwanda, DR Congo, Uganda, Zambia, Malawi na Zimbambwe.

Kamati, katika kutekeleza majukumu yake imeelezwa changamoto ambazo zimekuwa zikiikabili Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania-TPA kuwa ni: -

- a) Uwezo mdogo wa kuhudumia meli kubwa na kina kifupi katika bandari ya Dar es Salaam pamoja na Tanga;
- b) Uwepo wa bandari bubu na ushindani wa Bandari zingine kama vile Beira-Msumbiji, Mombasa-Kenya na Durban-Afrika Kusini; na
- c) Uchakavu wa Miundombinu ya bandari na reli inayounganisha bandari na maeneo mengine

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa bandari kavu eneo la Ruvu (Vigwaza), katika Vikao vya Kamati vilivyofanyika mwezi Machi, 2019, imeelezwa kuwa awamu ya kwanza ya mradi huu imeshakamilika na sasa awamu ya pili imefikia asilimia sabini (70%) na inatarajiwaa kukamilika mwezi Mei, 2019.

Aidha, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania, katika mwaka wa fedha 2019/2020 imepanga kukamilisha ukarabati

na uboreshaji wa magati yaliyoko bandari ya Tanga, ujenzi wa magati katika mwambao wa bahari ya Hindi, kukamilisha ujenzi wa magati katika maziwa makuu, kuendelea na kukamilisha mpango wa utwaaji ardhi kwa ajili ya ujenzi wa bandari kavu katika maeneo ya Katosho, Kibirizi, Chongoleani na Ihumwa Dodoma.

Vilevile, ni muhimu pia kwa bandari zilizo katika kipaumbele vya Serikali kama vile Bandari ya Mbegani Bagamoyo na Bandari ya Mwambani Tanga kuanza kutekelezwa.

iii. **Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL)**

Mheshimiwa Spika, japokuwa Serikali imekuwa na dhamira ya kuboresha usafiri wa abiria na mizigo katika Maziwa Makuu yaani (Victoria, Tanganyika na Nyasa), kwa kununua meli mpya na kukarabati meli zilizopo, bado kumeendelea kuwapo na changamoto mbalimbali ambazo zimesababisha katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Februari, 2019, Wakala wa Huduma za Meli kutokufikia malengo ilijojiwekea.

Changamoto kubwa imekuwa kutokutolewa kwa wakati fedha zilizoidhinishwa ambapo katika Mwaka wa fedha 2018/2019 ilitengewa **shilingi bilioni 20**, hadi kufika Machi, 2019 zimetolewa **shilingi bilioni 3** sawa na asilimia 15 ya fedha zote zilizoidhinishwa.

Upungufu huo wa fedha, umesababisha Kampuni ya Huduma ya Meli kufanya kazi chini ya malengo ilichojiwekea Mfano; kusafirisha jumla ya abiria 64,709 ikilinganishwa na lengo la kusafirisha abiria 82,159 ambao ni upungufu kwa abiria 17,450 sawa na asilimia 21.24. Aidha, kwa upande wa mizigo jumla ya tani 15,421 zilisafirishwa katika maziwa yote matatu ikilinganishwa na lengo la kusafirisha tani 68,352 ikiwa ni upungufu wa tani 52,931 sawa na asilimia 77.

iv. **Kampuni ya Ndege Tanzania- ATCL**

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kununua ndege kutoka ndege moja iliyokuwepo

2016 hadi kufikia ndege sita. Katika kuendeleza juhudhi hizo mwaka wa fedha 2019/2020 zimetengwa **shilingi Bilioni 500 (500,000,000,000)** kwa ajili ya kukamilisha malipo ya ndege ya pili aina ya Boing 787 Dreamliner, kukamilisha ndege nyingine aina ya Bombadier Q400 na malipo ya awali ya kununua ndege mbili mpya aina A220-300, ununuzi wa ndege moja Bombadier Q400, ununuzi wa Injini ya akiba kwa ajili ya Bombadier Q400, kuboresha karakana ya KIMAFA na kulipa madeni yaliyohakikiwa.

Mheshimiwa Spika, Kuongezeka kwa ndege kumeiwezesha Kampuni kuongeza idadi ya miruko ili kukidhi mahitaji ya usafiriwa anga katika baadhi ya vituo kikiwepo kituo cha Dodoma ambapo ndege ilikuwa inafanya safari mara tatu kwa wiki na sasa inafanya safari mara nne kwa wiki. Hadi kufika Desemba, 2018 ATCL imefanikiwa kumiliki soko la usafirii wa anga kwa asillimia 40.8 na kuwa Kampuni inayoongoza kwa soko la ndani.

Aidha, ATCL imeongeza safari za kikanda kuelekea Entebbe-Uganda na Bujumbura-Burundi. ATCL imelenga kuongeza safari za Johannesburg, Harare na Lusaka. Vilvile kuanza safari za Kimataifa katika vituo vya Guangzhou, Bangkok na Bombay.

Changamoto zinazoikabili ATCL ni pamoja na uchache wa wataalam hususan marubani, uchache wa nyenzo za kiutendaji hususan magar na madeni ambayo yameendelea kulipwa kulingana na upatikanaji wa fedha.

b) **Sekta ya Ujenzi**

i) **Bajeti ya Miradi ya Maendeleo ya Sekta ya Ujenzi**

Mheshimiwa Spika, sekta ya ujenzi ni sekta muhimu ambayo imekuwa ikitekeleza majukumu mbalimbali ya ujenzi ikiwemo ujenzi ukarabati na matengenezo ya barabara, madaraja na vivuko; Ujenzi ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali; ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege; usimamizi wa masuala ya ufundi na umeme; Usimamizi wa shughuli za

ukandarasi, uhandisi, ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi; Usimamizi wa maabara na vifaa vya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 kuna upungufu wa **shilingi 772,404,748,873.38** ambazo ukilinganisha na mwaka wa fedha uliopita 2018/2019 ni upungufu wa **asilimia (39.08)**. Kutokana na upungufu huu wa fedha za miradi ya maendeleo, Kamati inaona hali hii itaathiri ujenzi wa miundombinu hasa barabara ambazo ndiko kuna watumiaji wengi ukizingatia kwamba barabara ni sekta mtambuka. Vilevile, upungufu wa fedha za miradi ya maendeleo utaathiri miradi iliyoleta imeanza na inayoendelea ikiwa ni pamoja na miradi ya kuunganisha baadhi ya Makao Makuu ya Mikoa, ujenzi wa barabara za kiuchumi na barabara za kiusalama.

ii) Miradi ya ujenzi wa Barabara

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara ina jukumu la kusimamia ujenzi, ukarabati na matengenezo kwenye mtandao wa barabara kuu na za Mikoa zenye urefu wa jumla ya kilomita 35,000 ambapo kati ya hizo kilomita 12,786 ni barabara kuu na kilometa 22,214 ni barabara za mikoa. Lengo ni kuwezesha barabara ziweze kupitika kwa urahisi na hatimaye kusaidia ukuaji wa uchumi wa nchi kama ilivyofafanuliwa katika Mipango Mikakati ya Kitaifa ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2015, Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano na Mikakati ya Kisekta.

Mheshimiwa Spika, barabara ni sekta mtambuka kwa kuwa jamii yote hutegemea miundombinu ya barabara ili kufanikisha masuala mbalimbali ya kijamii na kiuchumi. Miundombinu ya barabara inapokuwa mizuri husaidia jamii kwa kurahisisha watu kutoka sehemu moja hadi nyingine, kuokoa muda, gharama na uchovu. Pamoja na umuhimu huo ujenzi wa barabara umekuwa na changamoto kubwa ya kibajeti kwa kutengewa fedha kidogo na kutotolewa fedha kwa wakati. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2018/2019, hadi kufikia mwezi Machi, 2019 fedha zilizoidhinishwa kwa baadhi ya miradi ya barabara hazikuwa zimetolewa.

Mfano, barabara ya Dar es Salaam-Chalinze-Morogoro express way, Nangurukuru- Mbwemkuru; Dumila- Kilosa-Mikumi; Dumila-Rudewa; Korogwe-Handeni; Singida-Babati-Minjingu; Same- Mkumbara-Korogwe; na Handeni-Kibereshi-Kibaya-Singida.

Aidha, baadhi ya barabara fedha zilitolewa kidogo ukilinganisha na kiasi kilichoidhinishwa na muda uliobaki kabla ya kumaliza mwaka wa fedha 2018/2019. Barabara hizo ni Wazo Hill -Bagamoyo- Msata; Usagara-Geita-Buzirayombo-Kyamyorwa; Dodoma -Manyoni; Sumbawanga -Mpanda-Nyakanazi; Ipole-Rungwa; na Magole-Mziha-Handeni.

Mheshimiwa Spika, lengo mojawapo la Sekta ya Ujenzi ni kuhakikisha Miji yote Mikuu na Mikoa inaunganishwa kwa barabara za lami. Hata hivyo, bado kuna Mikoa mingine ambayo haijaunganishwa kwa barabara za lami hususan Mikoa ya Katavi- Kigoma, Katavi-Tabora, Kigoma-Kagera, Mbeya -Makete- Njombe, Lindi- Morogoro, Lindi-Ruvuma n.k. Aidha, baadhi ya barabara za Mikoa ziko katika hali isiyoridhisha na nyingine hazipitiki wakati wa mvua hivyo kuathiri shughuli za kiuchumi na kijamii.

iii) **Malipo ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri**

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kazi kubwa inayofanywa na Wakandarasi na Wahandisi Washauri katika ujenzi hususan kwenye miradi ya barabara. Kamati imejulishwa kuwa hadi kufikia Machi, 2019 deni la Makandarasi na Wahandisi Washauri wa miradi ya barabara ni **shilingi bilioni 711.13**. Madeni yaliyolipwa ni yale yaliyohakikiwa hadi mwezi Juni, 2016 ambapo kiasi cha **shilingi trilioni 1.6** zimeshalipwa. Aidha, kazi ya kuhakiki madeni ya hadi mwezi Juni, 2017 imekamilika na fedha zinaendelea kutolewa kwa ajili ya malipo ya madai ya miradi ya barabara.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kwa kuona umuhimu wa kuwashirikisha wakandarasi wa ndani katika ujenzi wa miradi ya barabara ambapo kiasi cha **Shilingi milioni 442,005.782** za Mfuko wa Barabara zimetumika kulipa

Makandarasi wa ndani. Hata hivyo, changamoto kubwa imeendelea kuwa uwezo mdogo wa mtaji walionao Makandarasi wa ndani hivyo kushindwa kushiriki kikamilifu katika fursa za kazi kutokana na masharti ya upatikanaji wa dhamana za zabuni, dhamana za ushiriki wa kazi, mitaji ya kuwezesha kufanya kazi kutoka mabenki kuwa ngumu na kutozingatia mahitaji halisi ya shughuli za kuhandisi. Hali hii ya kukosa mitaji kunawafanya Makandarasi kushindwa kukua na kupata fursa ambazo zitawezesha kuwakwamua kutokana na uwezo mdogo.

iv) **Wakala wa Ufundu na Umeme (TEMESA)**

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Ufundu na Umeme Tanzania (*The Tanzania Electrical Mechanical and Electronics Services Agency-TEMESA*) ni Wakala muhimu sana kwani unatoa huduma ya matengenezo ya magari, mitambo, pilipiki, mifumo ya umeme, majokofu na viyoyozi. Vilevile Wakala huu unasimamia ukodishaji wa magari na mitambo ya kusaga kokoto pamoja na kutoa ushauri katika nyanja mbalimbali za kihandisi Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Wakala huu unakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo za ukosefu wa rasilimali watu wenye weledi unaoenda sambabamba na mabadiliko ya teknolojia, vifaa vyta kisasa vinavyoweza kuendana na magari ya kisasa na mitambo ya kisasa ambayo inahitaji kutumia mashine ili kugungua tatizo wakati wa ukarabati. Kutokana na changamoto hizo, magari ya Serikali yanakwenda kutengenezwa kwa waagizaji wakubwa (*dealer*) ambao gharama zao zinatozwa kulingana na muda ambao umetumika kutengeneza gari husika na hivyo kusababisha gharama kuwa kubwa.

v) **Miradi ya Ujenzi wa Viwanja vya Ndege**

Mheshimiwa Spika, miradi mbalimbamli ya ujenzi wa viwanja vya ndege inaendelea katika Mikoa mbalimbali kama vile Kigoma, Mpanda, Mtwara, Mwanza, Arusha, Sumbawanga, Shinyanga, Kilimanjaro, Msalato, Tabora na Songwe. Kazi

kubwa zinazofanyika katika miradi hiyo zinajumuisha ujenzi barabara za ndege, upanuzi wa barabara za ndege, upanuzi na ukarabati wa maegesho ya ndege, ujenzi wa vituo vya uangalizi wa hali ya hewa, ujenzi wa barabara za kuingilia viwanja vya ndege, uboreshaji wa viwanja hivyo pamoja na ujenzi wa majengo ya abiria na mizigo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi 2019, mradi wa kiwanja cha ndege cha Julius nyerere ulikuwa umekamilika kwa asilimia tisini na tano (95%) na viwanja vingine vya ndege miradi bado inaendelea. Hata hivyo, miradi hii inakabiliwa na changamoto kubwa ya ufinyu wa bajeti na kutokutolewa fedha kwa wakati. Mfano; Kiwanja cha Ndege cha Songwe, Arusha na Kilimanjaro vinakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti hali inayosababisha kuchelewa kukamilika kwa miradi hii.

Mheshimiwa Spika, kutokutolewa fedha za miradi hii kwa wakati kunaathiri utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Ujenzi kwani kumekuwa na ongezeko la gharama kutokana na riba, mabadiliko ya bei za vifaa vya ujenzi na mabadiliko viwango vya kubadilisha fedha.

vi) **Sekta ya Mawasiliano**

a) **Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania**

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia TCRA imeweka Mfumo wa kusimamia mawasiliano ya simu (*Tele-Traffic Management System-TTMS*), ambao umechangia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Sheria na Kanuni zillizopo katika udhibiti wa mawasiliano. Mkataba ulikuwa wa miaka mitano ambao ulilingiwa kwa njia ya Kujenga, Kuendesha na Kuhamisha Umiliki (*Build, Operate and Transfer*). Mkataba ulianza 1 Oktoba 2013 na umemaliza muda wake tarehe 30 Septemba, 2018. Toka mfumo huu ulipoanza kufanya kazi mpaka Septemba 2018, Serikali imeweza kupata chanzo kipywa cha mapato yanayotokana na mawasiliano ya simu za Kimataifa zinazoingia nchini ambapo kiasi cha **Shilingi 93,665,645,344.55** ziliwasilishwa Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Mfumo huu umeongeza ufanisi katika usimamizi wa Sheria ikiwa ni pamoja na kwenda sambamba na mabadiliko ya kasi yanayotokea katika Sekta ya Mawasiliano duniani.

b) Mradi wa Postikodi na Misimbo za Posta

Mheshimiwa Spika, mradi huu ni muhimu sana kutohakana na faida zake kiuchumi na kijamii. Hata hivyo, pamoja na umuhimu wa mradi huu, bado kumeendelea kuwapo changamoto ya kutokutolewa fedha za maendeleo kwa wakati hivyo kusababisha mradi kutekelezwa ipasavyo. Kwa miaka mitatu mfululizo mwenendo wa utoaji fedha katika mradi huu sio wa kuridhisha. Katika mwaka wa Fedha 2016/2017 mradi huu uliidihiishiwa **shilingi bilioni 3** ambapo kiasi kilichotolewa kilikuwa **milioni 95** tu; katika mwaka wa fedha wa 2017/18 mradi huu uliidihiishiwa **shilingi billion 3** ambapo hadi kufikia Machi 2018, hakuna kiasi chochote kilichotolewa. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 mradi huu uliidihiishiwa **shilingi bilioni 4** lakini hadi kufikia mwezi Machi, 2019 kiasi kilichopokelewa na kutumika ni **shilingi milioni 796** tu.

c) Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (USCAF)

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*Universal Communication Service Access Fund- UCSAF*) ulianzishwa na Serikali kwa Sheria Na. 11 ya Mwaka 2006 ukiwa na lengo la kupeleka huduma ya mawasiliano maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara. Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kwa kushirikiana na sekta binafsi hususan Makampuni ya simu kama vile TIGO, VODACOM, HALOTEL.

Mheshimiwa Spika, Mnamo mwezi Julai, 2018, Kamati ilifanya ziara ya kutembelea na kukagua minara ya mawasiliano ya simu iliyojengwa kwa ruzuku ya Serikali kuititia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote- UCSAF na kwa ushirikiano na Makampuni binafsi. Lengo la ziara hii lilikuwai kufuatilia kwa karibu upatikanaji wa mawasiliano hasa katika maeneo ya pembezoni ambayo Serikali imetoa fedha zake (ruzuku). Ziara hii ilijumuisha Mikoa kumi na mbili (12) ya Tanzania Bara ambayo ni Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Mara, Simiyu, Shinyanga, Iringa, Njombe, Ruvuma na Lindi.

Mheshimiwa Spika, kufuatia ziara hiyo, yafuatayo ni mambo yaliyobainika katika ziara hiyo: -

- i) Ushiriki wa Serikali katika kuwezesha mawasiliano; Pamoja na Serikali kutoa ruzuku za ujenzi wa minara ili kuhakikisha mawasiliano yanawafikia watu wote, hakuna alama yoyote iliyowekwa katika minara kutambulisha wananchi na jamii mchango wa Serikali. Hili linafanya mchango wa Serikali katika kuwezesha mawasiliano kutojulikana kabisa na badala yake Makampuni husika ndio yanayoonekana na kufahamika kutoa huduma hiyo muhimu.
- ii) Umiliki wa Maeneo yaliyojengwa Minara; Taratibu za upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa minara kutokuwa wazi jambo linalosababisha Serikali za Vijiji husika kutokunufalka kwa namna yoyote na malipo ya pango la eneo liliojengwa mnara. Kamati imebaini kuwa watu binafsi ambao si wakazi wa vijiji husika ndio walionunua maeneo hayo na kupangisha Makampuni ya simu.
- iii) Ushiriki katika Kazi za Maendeleo; Makampuni ya Simu hayashiriki ipasavyo katika shughuli za maendeleo (*Corporate Social Responsibility*) katika maeneo yanayofanya shughuli zake za kibiaresha mathalani maeneo ambayo wamejenga minara.
- iv) Kutokuwepo Mawasiliano wakati Wote; Kamati imebaini pamoja na kuwepo kwa minara, upatikanaji wa huduma ya simu kwa wananchi wa baadhi ya vijiji vilivyotembelewa imekuwa si wakati wote kama ambavyo Serikali imekusudia. Hii ni kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo; minara kuwepo mbali na watoa huduma, minara kujengwa katika vilima ambapo hakuna miundombinu ya barabara za magari kufikisha huduma jambo linalosababisha ucheleweshwaji wa huduma ya matengenezo au mafuta ya *generator* na kusababisha kukosa mawasiliano na uelekeo wa mnara na uwepo wa milima inayozuia za mawasiliano kufika katika vijiji vilivyokusudiwa.

v) Utunzaji wa Mazingira; Kamati imebaini kuwa maeneo yaliyojengwa minara inayomilikiwa na Kampuni ya Tigo (MIC), Vodacom na Halotel hakuna huduma za msingi kama vile chumba cha kulala na choo cha mlinzi. Jambo hili si sahihi na huchangia uchafuzi wa mazingira kwani walinzi hujisaidia vichakani na ikiwa mnara upo jirani na makazi ya watu, hulazimika kuomba huduma katika makazi ya wananchi.

Aidha, kutokuwepo kwa nyumba ya mlinzi kumekuwa ni changamoto kubwa kwani maeneo mengine yapo katika hifadhi au mbuga za wanyama na hivyo kuhatarisha maisha ya walinzi wa minara.

vi) Ujenzi wa Minara katika eneo moja; Ni ukweli usiopingika kuwa wananchi wanahitaji huduma za mawasiliano toka kwa watoa huduma mbalimbali kulingana na uchaguzi wa huduma bora. Hata hivyo, kwa matumizi bora ya ardhii, Kamati inaona si sahihi kwa kila Kampuni kujenga mnara wake kwani baada ya muda nchi yetu itakuwa imetapaka minara ukiachilia mbali miundombinu mingine muhimu.

vii) Uhitaji wa Huduma za “*Internet*”: Katika maeneo yote ya minara ambayo Kamati imetembelea, kumebainika uhitaji mkubwa wa huduma ya *Internet*. Hii ni kutokana na minara mingi iliyojengwa kuititia mradi wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kuwa ya kiwango cha 2G ambayo hutoa huduma ya sauti na ujumbe pekee.

viii) Minara Maeneo ya Mipakani; Kumekuapo na changamoto ya wananchi wanaoishi maeneo ya mipakani kukosa huduma ya mawasiliano au wakati mwengine kupata huduma ya mawasiliano toka nchi jirani jambo ambalo si sawa na ni hatari kwa usalama wa nchi.

ix) Rasilimali watu katika Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote; Kutokana na uwekezaji mkubwa unaofanywa na Serikali wa kujenga minara, imebainika kuwepo kwa wafanyakazi wachache katika Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kumekuwa na changamoto hasa katika kufuatilia miradi hiyo wakati wa ujenzi na hata kufuatilia ufanisi wake.

Mheshimiwa Spika, mradi huu wa kusambaza mawasiliano unakabiliwa na changamoto ya upungufu wa fedha za kutosha kipeleka mawasiliano katika maeneo yenye uhitaji wa huduma hiyo kwa wakati. Hata hivyo, Kamati inaona ipo haja ya Mfuko wa Mawasiliano kutafuta vyanzo vingine vya fedha ili kuhakikisha miradi inatekelezwa kama ilivyopangwa.

d) Shirika la Mawasiliano Tanzania – TTCL

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Shirika la Mawasiliano Tanzania-TTCL, Kamati imejulishwa kuwa Serikali iliruhusu TTCL kukopa **Shilingi Bilioni 96** kwa kutumia dhamana ya rasilimali za Shirika ambapo hadi mwezi Machi 2019, shirika limeshakopa **Shilingi Bilioni 66** na limewasilisha maombi ya kukamilisha mkopo wa kiasi kilichobaki. Fedha hizo zimeiwezesha kampuni kutekeleza majukumu yake kama vile kuendesha huduma ya T-Pesa ambapo hadi mwezi February, 2019 Shirika lilikuwa na wateja 351,000 na jumla ya mawakala 10,000; kuongeza idadi ya wateja hai kutoka wateja 488,537 mwaka 2017/2018 hadi wateja 1,074,642 mwezi February, 2019.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za Serikali bado Shirika la Mawasiliano Tanzania limeendelea kukabiliwa na changamoto kubwa ya madeni ya zamani ambapo hadi kufikia June, 2018, jumla ya **Shilingi Bilioni 28** zilikuwa zinadaiwa kutoka kwa Serikali na Taasisi zake.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI
3.1 Bajeti ya Wizara

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za miradi ya maendeleo kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kutoka **Shilingi trilioni 4.2** kwa mwaka 2018/2019 hadi **Shilingi trilioni 4.8** kwa mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ongezeko la Fedha la takribani **asilimia 14**, fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya

maendeleo ya Sekta ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kuna upungufu wa **shilingi 772,404,748,873.38** ambayo ni sawa na **asilimia (39.08)** ya Fedha za miradi ya Maendeleo za Sekta ya Ujenzi zilizokuwa zimeidhinishwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Kamati inashauri Serikali kutafuta fedha hizo zilizopungua takribani **shilingi bilioni 772.4**. Fedha hizi zitasaidia kuongeza kasi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara nchini ambayo bado imekuwa na changamoto ya kutokupitika wakati wote.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo kwa Sekta ya Mawasiliano, hakuna fedha yoyote iliyotengwa. Hata hivyo, Kamati ilielezwa kuwa fedha hizo za miradi ya maendeleo zitatolewa toka katika fedha za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Kamati inasisitiza kuwa ni muhimu fedha hizo zitolewe ili kuendeleza miradi muhimu iliyokuwa inaendelea, kama vile, mradi wa Anuani za Makazi na misimbo ya posta, mkongo wa taifa wa mawasiliano, na ujenzi wa kituo cha kutengeneza Vifaa vya TEHAMA.

3.2 Sekta ya Uchukuzi

1. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu ujenzi wa reli nchini Kamati inashauri yafuatayo;

a) Kamati bado inaendelea kusisitiza ushauri wake kuwa mradi wa ujenzi wa Reli ya Kati kipaumbele kiwe kwenye reli yenye matarajio ya mzigoto mkubwa ili kutengeneza mazingira ya Serikali kurudisha fedha zitakazokuwa zimetumika kwa muda mfupi. Aidha, Kamati inashauri Serikali kwamba reli hii ijengwe kwa kuzingatia faida za kiuchumi na kipaumbele zaidi kiwekwe katika tawi la Tabora – kigoma -Uvinza-Msongati; Kaliua – Mpanda -Kalema; na Tabora- Mwanza;

b) Ujenzi wa reli ya Kati uende sambamba na ununuzi wa vichwa na mabehewa ya treni, ili mradi utakapokamilika kwa sehemu ya Dar es Salaam hadi Morogoro huduma za usafirishaji zianze;

- c) Mafunzo mbalimbali ya uendeshaji wa treni; pamoja na, uratibu wa matumizi ya reli mpya yatolewe ili mradi utakapokamilika pawepo na wataalam wa ndani ambao watakuwa tayari kuupokea na kuusimamia mradi huu;
- d) Serikali ihakikishe mradi wa sehemu ya Dar es Salaam hadi Morogoro unakamilika kwa wakati mwezi Novemba, 2019 kama Mkataba na Mkandarasi unavyoonesha ili kuepuka gharama;
- e) Ili kuepusha uvamizi wa maeneo ya reli, ni vema Shirika la Reli Tanzania-TRC liweke alama zinazoonesha mwisho wa eneo la reli ili kuondoa usumbufu kwa wananchi;
- f) Shirika la reli lianje kuijendesha kisasa kwa kufunga vyombo vya kielektroniki ili kuweza kutunza kumbukumbu zote za kiutendaji, ufatillaji wa mizigo kwa wateja, uthibiti wa mafuta, udhibiti wa mwendo na usalama. Hii italifanya Shirika hili kuweza kuijendesha kisasa na kupunguza gharama za uendeshaji;
- g) Kwa kuwa ujenzi wa reli ya kisasa ni wa gharama kubwa, na kwa kuwa; pamoja na ujenzi wa reli ya kati unaoendelea sasa, pia tunatarajia kuanza kujenga reli nyingine za Tanga – Arusha –Musoma (1108 km), Mtwara- Mbambabay na Mchuchuma-Liganga (1092 km) na Isaka –Rusumo (371). Kamati inashauri Serikali kujenga reli hizi kwa awamu kwa kufuata kipaumbele; na
- h) Serikali iangalie uwezekano wa kushirikisha sekta binafsi au kupata mikopo yenye gharama nafuu ili kuharakisha zoezi zima la ujenzi wa reli nchini. Kwa kufanya hivyo, Serikali itaweza kuweka fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mingine ya maendeleo.

2. Mheshimiwa Spika, kuhusu Bandari Kamati inashauri yafuatayo;

- a) Serikali kuona uwezekano wa kubakisha angalau **asilimia 40** ya makusanyo ya Mamlaka ya Bandari Tanzania ili

Mamlaka hii iweze kuendeleza baadhi ya miradi katika bandari zake;

- b) Pamoja na kuwa shughuli za upanuzi na ukarabati wa bandari ya Dara es Salaam unaendelea, Kamati inasisitiza, ili kuongeza ufanisi na mapato katika bandari ya Dar es Salaam, ni vema juhudzi za makusudi zifanyike ili kuweza kuhamisha gati la mafuta liliopo kurasini (KOJ) na kujenga gati namba 13 na 14;
- c) Wadau wote wa bandari waunganishwe kwenye mfumo wa kielektroniki unaotumiwa na bandari ili kuweza kuharakisha uondoshwaji wa mizigo bandarini kwani wakati mwingine mizigo inachelewa kutokana na wadau wengine kama Mkemia Mkuu, Shirika la Viwango Tanzania-TBS, Wizara ya Nishati na Madini na wengine wengi kutokuwemo kwenye mfumo huo;
- d) Serikali iharakishe ujenzi wa bandari za nchi kavu ili kupunguza gharama kwa wateja kusafiri mpaka Dar se salaam kwa ajili ya kutoa mizigo. Ni muda mrefu sasa tangu Serikali imeanza mipango ya kujenga bandari kavu katika maeneo ya Kwala -Pwani, Ihumwa -Dodoma, Fela-Mwanza, Katosho-Kigoma, King'ori-Arusha, Isaka-Kahama, na Inyala-Mbeya;
- e) Serikali iharakishe kutafuta mwekezaji ili ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo uweze kuanza kwa kuwa bandari hii ni muhimu na itatoa fursa za kiuchumi katika ukanda huo. Vile vile, Serikali ilipe fidia kwa wananchi waliobakia ndani ya eneo linalotarajiwa kujengwa bandari hii ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima wakati mradi huu utakapoanza;
- f) Serikali iharakishe mchakato wa kupata *flow meter* mpya kwa ajili ya upimaji wa mafuta yanayoingia Bandari ya Dar es Salaam kwani kutokuwepo na mtambo wa kupima kiasi cha mafuta (*flow meter*) kunasababisha kutokujua kwa uhakika kiwango cha mafuta kinachoingia bandari ya Dar es Salaam; na

g) Kuhusu Bandari ya Mtwara, kasi ya uanzishwaji wa bandari ya hii iende sambamba na ujenzi wa njia ya treni. Mamlaka ya Bandari Tanzania- TPA ishirikiane kwa karibu na Shirika la Reli Tanzania- TRC kuona namna ya kuimarisha mtandao wa reli, kwa kuwa bandari hii ikiunganishwa na reli itazalisha mapato makubwa kwa nchi;

3. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Kampuni ya Huduma za Meli-MSCL; Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Kampuni ya Huduma za Meli-MSCL kufunga teknolojia ya kufatilia matumizi ya mafuta kwenye meli (*Flow Scanner*) na kuweka mfumo wa kufatilia mahali meli ilipo kila wakati (*trucking system*). Kufanya haya kutasaidia kuweza kuziba mianya ya upotevu wa fedha za Kampuni;

b) Serikali ijipange kutengeneza Meli zote kumi na nne (14) zilizopo katika Maziwa Makuu ili kuiwezesha Kampuni ya Meli Tanzania kumudu kujiendesha kibiashara na hata kuweza kulipa madeni yote inayodaiwa;

c) Kutokana uwekezaji unaofanyika sasa wa kukarabati na ujenzi wa meli mpya katika Maziwa Makuu, ni vema Serikali iendelee kulipa mishahara ya kwa wafanyakazi wa Kampuni ya Meli Tanzania hasa kwa kipindi hiki cha mpito mpaka Kampuni hii itakapoweza kujiendesha; na

d) Serikali iharakishe kukamilisha zoezi la kurasimisha bandari bubu zilizopo katika mwambao wa bahari ya Hindi na katika maziwa makuu ili kuongeza mapato katika halmashauri na bandari kwa ujumla.

4. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu TAZARA, Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Serikali iharakishe mazungumzo baina ya nchi wabia wa reli ya TAZARA kuhusu kuimarisha reli hii kutokana na umuhimu wake katika kukuza uchumi. Nchi Serikali kwa kushirikiana na nchi wabia wa TAZARA ikamilishe itifaki ya 16 kuhusu mkopo kutoka china kwa ajili ya kusaidia kuiboresha TAZARA.

- b) Seikali ikamilishe manunuzi ya injini na vipuri pamoja na mitambo ya kusaidia kuzalisha kokoto na mataluma ya zege kwenye mgodi wa kokoto uliopo Kongolo- Mbeya na kusaidia viweze kuingia nchini kwa haraka ili vianze kutumika kwa ajili ya kuongeza pato la TAZARA.
- c) Serikali iharakishe mchakato wa ajira za watumishi wa TAZARA ili kupata wafanyakazi wenyewe ujuzi na weledi wa kutosha kuliongezea Shirika uwezo kwani wafanyakazi wengi wamemaliza muda wao na kustaafu;
- d) Serikali ihakikishe inatoa kwa wakati fedha za ujenzi wa kipande cha reli chenye urefu wa kilometra 18 kutoka Chikola kwenda kwenye mgodi wa Magamba ili kuweza kurahisisha usafirishaji wa makaa ya mawe kwani mzigo unaotoka ni mkubwa hivyo unaweza kuipatia TAZARA mapato ya kutosha kujidesha; na
- e) Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kulipa deni lote la TAZARA ambalo uhakiki wake umekamilika na kuendelea kutafuta fedha ili kulipa deni hasa linalohusu upande wa Tanzania.

5. Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania-TAA: -

- a) Kamati inaendelea kushauri Serikali kuipatia Mamlaka hii angalau **asilimia 50** ya maduhuli yatokanayo na viwanja vya ndege ili Mamlaka ya Viwanja vya Ndege- (TAA) iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuongeza kasi ya ujenzi na ukarabati; pamoja na, uendeshaji wa viwanja vya ndege nchini. Aidha, Mamlaka izitumie vizuri fedha za mapato ya ndani zinazotokana na utuaji wa ndege, uegeshaji wa ndege na magari katika maegesho ya viwanja ili ziweze kutumika katika shughuli za uendeshaji wa viwanja vya ndege;
- b) Serikali ihakikishe Viwanja vyote vya Ndege na mali zake zote zinakuwa na Hati Miliki; Aidha, kuhakikisha Viwanja vya Ndege vyote vinawekewa uzio kwa ajili ya kuepusha hatari

zinazotokana na wanyama au binadamu wanaokatiza katika maeneo ya viwanja vya ndege pamoja na; kuepuka migogoro ya ardhi na wananchi wanaoishi pembezoni mwa viwanja hivyo;

c) Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) na wadau wengine wa viwanja vya ndege kama Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL), wafanye vikao vya pamoja na kuangalia namna ya kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili katika sekta ya usafirishaji wa anga;

6. Mheshimiwa Spika, Kuhusu Kampuni ya Ndege Tanzania- ATCL,

a) ATCL ijitangaze kwenye vyombo rasmi vya Kimataifa ambavyo huonesha safari za ndege dunia nzima. Aidha, Kampuni hii sasa ijpange kuingia katika soko kwa kujitangaza katika vyombo vya habari, majarida na vipeperushi mbalimbali, kujali wateja na kuwa na bei nafuu ili kuhakikisha abiria wengi wanatumia ndege hizi;

b) Wafanyakazi wa Kampuni ya Ndege Tanzania- ATCL kupewa mafunzo ya huduma kwa wateja, mara kwa mara, ili kuweza kutoa huduma nzuri wakati wote. Hii itasaidia Kampuni kushindana na makampuni mengine yanayofanya biashara ya usafiri wa anga.

3.3 Sekta ya Ujenzi

1) Mheshimiwa Spika, kuhusu Wakala wa Barabara-TANROADS, Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Serikali itekeleze Sera yake ya kuunganisha Mikoa yote kwa barabara za lami kama vile, Lindi –Morogoro, Morogoro- Mlimba-Madeke Njombe, Lindi –Songea, Kigoma –Katavi- Tabora-Kagera, Mbeya-Makete-Njombe, Arusha-Mara. Aidha, miradi ya barabara inaendelea ipewe kipaumbele na ile ambayo haijaanza ifanyiwe upembuzi yakinifu. Vilevile, Serikali kujenga kwa kiwango cha lami barabara zifuatazo: -

- i. Barabara zinazounganisha nchi yetu na nchi nyigine hususani Mikoa ya Kagera, Kigoma, Katavi, Ruvuma na Mtwara;
 - ii. Barabara zinazounganisha Makao Makuu ya Mikoa kama vile Kigoma-Kasulu-Kagera, Katavi – Kigoma – Tabora;
 - iii. Barabara za Kiuchumi, kama vile, Mtwara – Newala – Masasi, ambayo ni barabara inayopita katika maeneo ambayo yanazalisha korosho kwa wingi; ukizingatia kwamba zao la korosho linachangia kwa kiasi kikubwa uchumi wa mikoa ya kusini na nchi kwa ujumla; na barabara ya Singida – Chemba – Handeni – Tanga ambayo ni barabara yenye tija kiuchumi kutokana na kuwapo kwa bomba la mafuta linalounganishwa na nchi ya Uganda. Aidha, umuhimu wa makubaliano ya nchi ya Rwanda kutaka kutumia bandari ya Tanga; na
 - iv. Barabara zilizohaidiwa za Marais waliostaafu na Rais aliye madarakani.
- b) Serikali kupitia Bodi ya Usajili wa Wahandisi na Bodi ya Usajili wa Makandarasi kuchukulia hatua kali kwa wakandarasi wanaofanya kazi chini ya kiwango;
- c) Serikali kupitia Bodi ya Usajili wa Wahandisi na Bodi ya Usajili wa Makandarasi kuendelea kutoa mafunzo kwa wahandisi washauri na wakandarasi wa ndani ili waweze kusimamia na kutekeleza ujenzi wa barabara kikamilifu. Aidha, kuhamasisha wakandarasi wazalendo kujunga na kuomba zabuni kwa utaratibu wa ubia na kupata dhamana kupitia mfuko Maalum wa kutoa dhamana ya kusaidia makandarasi wadogo na wa kat;
- d) Sekta ya Ujenzi isimamie ipasavyo Sheria ya barabara kwa kutoa elimu kwa wananchi kwa kutumia vyombo vy ya habari, kama runinga, magazeti, redio na simu za mkononi. Aidha, vyombo vinavyohusika na usimamizi wa sheria ya barabara kuwa macho wakati wote na endapo kutaonekana mtu anajenga ndani ya hifadhi ya barabara kuzuiwa na

kubomolewa mapema. Aidha, Wakala wa Barabara iendelee na zoezi la kuweka alama za mipaka katika maeneo ya barabara ili kuepusha usumbufu wakati maeneo hayo yanapohitajika;

- e) Serikali iharakishe kuleta Sheria ya Vyuma Chakavu bungeni ili kuweza kusaidia kupambana na watu wachache waliokosa uzalendo ambao wanaiba vyuma vya alama za barabarani na kuviuza kama vyuma chakavu. Vilevile, kuchukuwa hatua kali za kulipa faini kwa magari ambayo yanagonga vibao vya alama barabarani;
- f) Serikali iendelee na juhudhi kufunga mizani ya kisasa zinazopima magari huku yakiwa kwenye mwendo katika vituo ambavyo vinamsongamano mkubwa wa magari kwenye mizani ili kuokoa muda, fedha na usumbufu kwa wasafiri na wasafirishaji;
- g) Serikali iongeze kasi ya ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi ambavyo vinajengwa katika Ukanda wa Kati na Ukanda wa Dar es Salaam ili kurahisisha usafirishaji wa bidhaa pamoja na kuokoa muda wa mizigo kukaa barabarani;
- h) Wakati wa ujenzi wa barabara ni vema wakala wa barabara wahakikishe wanaweka sehemu maalum kwa ajili ya kuvukia mifugo, kwani, maeneo mengi ambayo mifugo inatumia kuvuka kumekuwa na uharibifu mkubwa sana wa barabara;
- i) Wakati wa ujenzi wa barabara zipo taasisi nyingi za Serikali zinapeleka madai kwa wakandarasi wa barabara kwa ajili ya ulipiaji malighafi zinazotumika kwenye ujenzi, kama vile Wizara ya Madini (kokoto, mawe, kifusi), Wizara ya Maji na umwagiliaji (vima vya maji), Wizara ya Viwanda na Mazingira (uharibifu wa mazingira); pamoja na, ushuru unaotozwa na Halmashauri za miji; gharama hizi zinaongeza gharama za ujenzi wa barabara, hivyo, Kamati inaishauri Serikali isamehe kodi hizo kwani zinalipwa na Serikali na si wakandarasi;

- j) Serikali iendelee kutoa kazi za ujenzi wa barabara kwa wakandarasi wazawa ili kuweza kuongeza ujuzi na uzoefu katika shughuli za ujenzi; na
- k) Serikali ihakikishe inaweka mikakati ya kupunguza msongamano ya magari kwenye miji inayokua kwa kasi, kama vile, Mbeya, Mwanza, Arusha na hivi sasa Dodoma. Miji hii imekuwa ikitabiliwa na msongamano mkubwa wa magari na kusababisha kutumia muda mwingu kusafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine

2) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu ujenzi wa viwanja vya ndege, Kamati inashauri yafuatayo: -

- a) Serikali ikamilishe kwa haraka ujenzi unaoendelea wa kiwanja cha ndege cha Mwanza hasa ujenzi wa jengo la abiria. Aidha, ikamilishe ujenzi wa jengo la mizigo; pamoja na, jengo la kuongozea ndege ambayo yote yamefikia asilimia 90. Kamati inasisisitiza ushauri huu kutokana na umuhimu wa kiwanja hiki ambapo yapo mashirika mengi ya ndege kama Ethad, Fly Dubai, Rwanda Air, Jambo Jet ya Kenya yameonyesha nia ya kufanya safari zake katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza na hivyo kukifanya kiwanja hiki kuwa cha kimataifa;
- b) Serikali itoe fedha zote zilizoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 kwa ajili ya ujenzi wa Viwanja vya Ndege ili miradi hii iweze kukamilika kwa wakati na kuepuka riba ambazo hutokana na miradi kutokamilika kwa wakati;
- c) Serikali iwekeze kwa wataalam wa ndani, hasa, katika kazi za ujenzi; kama vile, shughuli za usanifu wa miradi mbalimbali. Hii itapunguza gharama kubwa ya kuajiri wataalam hao kutoka nje. Vilevile, itasaidia kuimarisha wataalam wetu wa ndani ya nchi. Ni vema wataalam wa ndani, mathalani, wahandisi wapewe nafasi ya kwenda kujifunza katika nchi nyingine duniani ili kuweza kujenga miundombinu ya kisasa kulingana na dunia inavyokwenda;

- d) Ni muhimu Serikali ijenge na kuimarisha Viwanja nya Ndege vitakavyozalisha mapato na kuijendesha; kama vile, Kiwanja cha Ndege cha Moshi (kwa ajili ya utalii), Kiwanja cha Ndege cha Iringa (kwa ajili ya Utalii) na Kiwanja cha Ndege cha Mtwara (kwa ajili ya uwekezaji);
- e) Serikali ilipe fidia mapema na kwa wakati kwa wananchi wanaopisha ujenzi mathalani kiwanja cha Ndege cha Dodoma, Songea, Lake Manyara, Simiyu na Msalato;
- f) Serikali iweke taa haraka za kuongozea ndege hususan katika Kiwanja cha Ndege cha Dodoma na Songwe-Mbeya ili ndege ziweze kutua na kuruka wakati wote;

3) Mheshimiwa Spika, kuhusu Wakala wa Ufundu na Umeme-TEMESA, Kamati inashauri yafuatayo: -

- a) Wakala uharakishe mchakato wa kuchagua karakana za kutengeneza magari ya Serikali kwenye Wilaya ili kuondoa usumbufu wa magari ya Serikali kusafiri umbali mrefu kwenda kufanya matengenezo kwani kuna Wilaya zingine ziko umbali mrefu kwenda Makao Makao ya Mkoa;
- b) Wakala uchukue hatua za makusudi na kuweka mkakati wa kudumu ili kukusanya madeni yake ambayo, kwa kiasi kikubwa, inazidai taasisi za Serikal ili Wakala huu uweze kijijidesha kiblashara badala ya kutegemea ruzuku kutoka Serikalini; na
- c) Serikali iajiri wataalaum waliobobea kwenye fani ya ufundu wa magari na kuhakikisha kunakuwa na mitambo ya kisasa ili kuendana na kukua kwa teknolojia kwani mara nydingi magari ya Serikali yamekuwa yaktengenezwa kwenye karakana binafsi za mitaani jambo ambalo si sahihi;

4) Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto ya wakandarasi wa ndani kuwa na mtaji mdogo wa kuwawezesha kufanya kazi, Kamati inasisisitiza Wizara; pamoja na, Bodi ya usajili wa wakandarasi kuhamasisha wakandarasi wa ndani kujunga

katika Mfuko Maalum wa Kutoa dhamana ya kusaidia wakandarasi wadogo na wa kati.

3.4 Sekta ya Mawasiliano

1) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu mradi wa Anuani Makazi na Misimbo ya Posta, Kamati inashauri yafuatayo; -

- a) Serikali itoe kipaumbele kwa mradi wa anwani za makazi na misimbo ya posta kwani mradi huu ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu. Aidha, Kamati inashauri Wizara husika ikiwemo Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; TAMISEMI na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano zikae na kuona namna nzuri ya kuhakikisha mradi huu muhimu unatekelezwa haraka na kwa ufanisi mkubwa;
- b) Ili mradi huu uwe wa kisasa na kuendana na wakati, ni vema wataalam wakajifunze nchi zingine na kuona namna nchi nyingine zilivyofanya na kuweka mfumo huu;
- c) Vibao vinavyoonesha majina ya mitaa viandikwe kwa lugha ya Kiswahili; na
- d) Wakati zoezi la kuweka majina ya mitaa linaendelea, ni muhimu Serikali za Mitaa kuhakikisha zinaweka ulinzi wa nguzo dhidi ya wahalifu wanaochukua vyuma chavu.

2) **Mheshimiwa Spika**, Kuhusu Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA, Kamati inashauri; -

- a) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania- TCRA, ikabiliane na changamoto za kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano, kama vile, uhalifu mitandaoni unaojumuisha kashfa kwa watu, usambazaji wa picha zisizostaili hivyo kuharibu maadili, mila na desturi zetu. Aidha, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA iendelee kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kutekeleza sheria ya uhalifu wa kimtandao na kuwabana wahalifu;

- b) Kamati inaendelea kusisitiza kuongezwa kasi ya zoezi la usajili wa namba za simu ili kuwa na taarifa za kila mmiliki au mtumiaji wa simu kwa ajili ya usalama na kutekeleza Sheria ya Mawasiliano na Posta. Vilevile, Serikali iongeze kasi ya kutoa vitambulishao vya Taifa ili kila Mtanzania aweze kutambuliwa na kuepuka udanganyifu unaofanywa kwenye mitandao; na
- c) Kuendelea kudhibiti mawasiliano ya ulaghai hatimaye kupunguza vitendo viovu vinavyofanyika kupitia njia ya mtandao na kuimarisha usalama wa watu na mali zao.

3) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote-UCSAF, Kamati inashauri

a) Serikali ipitie na kuangalia upya taratibu za umilikishwaji ardhisi hasa maeneo ya ardhisi yanayojengwa minara ili kuweka utaratibu wa maeneo yaliyokodiwa ama kununuliwa kwa ajili ya ujenzi wa minara kumilikiwa na Serikali za vijiji husika. Hii itasaidia kwani fedha zitakazopatikana kutokana na malipo kukodi ama kununua eneo la mnara zitatumika kwa maendeleo ya wananchi walio wengi tofauti na ilivyo sasa ambapo maeneo mengi yaliyojengwa minara yananufaisha watu wachache na baadhi ya Serikali za vijiji kutokuambulia chochote;

b) Serikali ihakikishe inaweka mabango yanayoonesha ushiriki wake katika ujenzi wa minara ambayo imetoa ruzuku. Hii ni kutokana na ukweli kuwa Serikali za Mikoa, Wilaya hadi ngazi ya chini pamoja na wananchi hawatambui uwepo wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote UCSAF; na kwamba, miradi hiyo ya ujenzi wa minara ni kwa ruzuku ya Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. Dhana iliyoko maeneo mengi ni kuwa minara inajengwa na Makampuni ya ya simu yenyewe; hivyo mchango wa Serikali katika kusambaza mawasiliano hautambuliki kabisa;

Aidha, wakati wa uzinduzi wa kuwasha minara iliyojengwa kwa ruzuku za Serikali, licha ya kuweka bango la kuonesha mchango wa Serikali; ni muhimu pia kufanya uzinduzi kwa kualika vyombo mbalimbali vya habari ili kujulisha wananchi

kazi na maendeleo ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote-UCSAF;

c) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-(TCRA) iwekea masharti ya kutoa leseni kwa Makampuni ya Simu pamoja na masharti mengine iwe kupeleka mawasiliano katika maeneo ya pembezoni kama mchango wa kijamii (Corporate Social Responsibility);

d) Serikali iweke mpango wa uwiano wa mawasiliano nchi nzima hasa maeneo ya mipakani ambapo mara nyingi watu katika maeneo hayo hupata mawasiliano ya nchi jirani jambo ambalo linawakosesha haki ya kukosa taarifa za nchi yao;

e) Serikali ihakikishe inasimamia kuwepo kwa ushirikiano katika mifumo ya miundombinu (*Infrastructure Sharing*) na kuyaelekeza makampuni ya simu kushirikiana katika ujenzi wa minara na kufunga antenna zao katika mnara mmoja ili kuepuka matumizi ya eneo kubwa la ardhi kwa kuwa mlundikano wa minara katika eneo moja;

f) Halmashauri na Serikali za vijiji zitoe ushirikiano wa kutosha na wa haraka pale ambapo maeneo yanahitajika kwa ajili ya ujenzi wa minara ili kuweza kurahisisha kupata mawasiliano kwa haraka;

g) Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote utoe elimu kwa wananchi ili wajue umuhimu na uwekezaji unaofanywa na Serikali katika kuleta maendeleo hususan katika ujenzi wa minara ya mawasiliano ili wananchi watoe ushirikiano wa ulinzi ili vifaa vya minara view salama; na

h) Kuongeza rasilimali watu kwenye Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ili Mfuko uweze kusimamia ipasavyo kwa kukagua na kutembelea maeneo ambayo Serikali imewekeza fedha kwa ajili ya ujenzi wa minara na kuhakikisha kazi hiyo imefanyika na mawasiliano yanapatikana kama ilivyokusudiwa;

- i) Serikali ijenge miundombinu ya barabara katika maeneo yaliyojengwa minara ili kurahisisha utoaji wa huduma za minara na wananchi kwa ujumla. Vilevile kurahisisha shughuli zingine za maendeleo kama vile utalii, kilimo na hata uwekezaji; na
- j) Kwa kuwa teknolojia imeendelea na wananchi wengi wamekuwa na mwamko katika huduma za TEHAMA; na hivyo, kuhitaji huduma ya *data (mtandao)*. Ni muhimu sana, minara yote iliyojengwa na inayoendelea kujengwa iwe na uwezo wa 3G na 4G tofauti na ilivyo sasa katika viwango vya 2G ambayo inanyima wananchi wengi fursa ya huduma ya data ambayo ingeweza kurahisisha huduma za afya (afya mtandao), elimu mtandao n.k
- k) Serikali ifanye jitihada za kuweka na kusambaza mawasiliano nchini katika maeneo mengi zaidi hasa mipakani kwani mawasiliano ni maendeleo na hasa sasa ambako nchi yetu inawekeza katika viwanda. Kuwepo kwa mawasiliano kutarahisisha usafiri na uuzwaji wa malighafi na mazao hata kuinua kipato cha Mwananchi mmoja mmoja na hata Tiafa kwa ujumla

4) Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la Posta Tanzania, Kamati inashauri yafuatayo: -

- a) Serikali iharakishe kulipa madeni ya pensheni kwa wafanyakazi wa iliyokuwa Posta ya Jumuia ya Afrika Mashariki ili kuliondolea Shirika mzigo wa kulipa deni hilo kila mwezi, fedha ambazo zingeelekezwa kwenye uendeshaji wa shirika; na
- b) Serikali iliondoe Shirika la Posta katika orodha ya mashirika yanayosubiri kurekebishwa ili liweze kutumia rasilimali zilizopo kufanya uwekezaji kwa lengo la kuijendesha kwa tija;

5) Shirika la Simu Tanzania- (TTCL Corporation)

- a) Shirika la Mawasiliano Tanzania- TTC liweke mikakati madhubuti ya kukusanya madeni kwa Wizara/Taasisi na

Mashirika ya Serikali ambayo madeni hayo yameripotiwa hadi Juni 2018 kufika Jumla ya **Shilingi Bilioni 28**; na

b) Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhakikisha kunakuwa na mpango endelevu wa kuulinda na kuuendeleza Mkongo wa Taifa. Hili lifikasiye kwa kuangalia upya utaratibu ambao umeruhusu Makampuni ya Simu mengine kumiliki Mikongo yao sambamba na Mkongo wa Serikali kwani Mikongo hii binafsi itafifisha maendeleo ya Mkongo wa Serikali na hata kuhatarisha usalama wana nchi pamoja na kuikosesa Serikali Mapato;

4.0 **HITIMISHO**

Mheshimiwa Spika, sekta hii ni muhimu sana katika kuharakisha na kuchochea maendeleo ya nchi. Miradi iliyo ndani ya Sekta hii ni mikubwa na inahitaji fedha nydingi ili yote iweze kukamilika kwa wakati uliopangwa. Hivyo, Kamati inaona ni muhimu Serikali kushirikisha Sekta binafsi katika kutekeleza miradi hii mikubwa.

4.1 **Shukrani**

Mheshimiwa spika, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao waliyointoa wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti pamoja na kuandaa taarifa hii. Naomba kuwatambua wajumbe wa Kamati hii kwa kuwataja majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Moshi Selement Kakoso, Mb- Mwenyekiti
2. Mhe. Hawa Mchafu Chakoma, Mb- M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Eng. Ramo Mataala Makani, Mb
4. Mhe. Daniel Nicodemus Nsanzugwako, Mb
5. Mhe. Susan Limbweni Kiwanga, Mb
6. Mhe. Joyce John Mukya, Mb
7. Mhe. Asha Mshimba Jecha, Mb
8. Mhe. Susan Chogisasi Mgonukulima, Mb
9. Mhe. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb
10. Mhe. Nuru Awadhi Bafadhili, Mb
11. Mhe. James Francis Mbatia, Mb
12. Mhe. Saul Henry Amon, Mb

13. Mhe. Ahmed Makbhuty Shabiby, Mb
14. Mhe. Dkt. Chuachua Mohamed Rashid, Mb
15. Mhe. Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mb
16. Mhe. Bhagwanji Maganlal Meisuria, Mb
17. Mhe. Dua William Nkurua, Mb
18. Mhe. Raphael Japhary Michael, Mb
19. Mhe. Agness Mathew Michael, Mb
20. Mhe. Charles Kitwanga, Mb
21. Mhe. Rukia Kassim, Mb
22. Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb
23. Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka, Mb
24. Mhe. Munde Abdallah Tambwe, Mb
25. Mhe. Abdulaziz Mohamed Aboot, Mb

Mheshimiwa spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni na Ushauri kwa niaba ya wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Kwa namna ya pekee naomba niwashukuru Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Eng. Isack Kamwelwe, (Mb) akisaidiana na Manaibu Mawaziri Mhe. Justus Atashasta Nditiye, (Mb) na Mhe. Elias Kwandikwa, (Mb).

Aidha, Kamati inawashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara hii Arch.Elius A. Mwakalinga (Sekta ya Ujenzi), Eng. Dkt. Leonard Chamuriho (Sekta ya Uchukuzi), Eng. Dkt. Maria Sasabo (Sekta ya Mawasiliano) pamoja na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Jim Yonaz. Kamati pia inawashukuru Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na wafanyakazi wote ambao wameipa Kamati ushirikiano mkubwa.

Vilevile, shukrani ziende kwa Katibu Mkuu Dkt. Leonard M. Chamuriho akisaidiana na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati wakati wote wa kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, vilevile nachukuwa fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake. Aidha, shukrani za pekee ziende kwa Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu. Dickson M. Bisile pamoja na Makatibu wa

Kamati Ndugu Hosiana John na Ndugu Francisca Haule pamoja na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao uliolwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Moshi Seleman Kakoso, (Mb)
MWENYEKITI
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE
YA MIUNDOMBINU

9 Mei, 2019

MWENYEKITI: Ahsante kwa kusoma kwa muda na kwa flow nzuri sana. Ahsante sana Mwenyekiti.

Sasa namwita Msemaji Mkuu Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Susan.

MHE. SUSAN L. KIWANGA - K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa James Francis Mbatia kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2018/2019 na Mpango wa Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Yanatolewa chini ya Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(9), Toleo la mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa najua muda hautoshi naomba Hotuba yote ya Kambi Rasmi ya Upinzani iingie kwenye *Hansard* za Bunge lakini mimi natoa kwa muhtasari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utangulizi, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa siha njema kuweza kusimama mbele ya Bunge hili ili niweze kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya mwaka 2018/2019 na Mpango wa Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa utangulizi huo, saa naomba kujielekeza katika hoja ilio mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mapitio ya jumla kuhusu Wizara; Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inajumuisha sekta kuu tatu ambazo ni Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Kwa kila sekta, mbali ya kusimamia sera inayoendesha sekta hiyo, pia inasimamia Idara na taasisi nyingine zilizopo katika sekta husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na 2017/2018, 2018/2019 ndiyo Wizara iliyokuwa na miradi ya kipaumbele katika mgawanyo wa bajeti ya maendeleo. Mwaka wa fedha 2016/2017, Sekta ya Ujenzi - Fungu 98 iliidhinishiwa shilingi trillioni 2.1 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Sekta ya Uchukuzi - Fungu 62 iliidhinishiwa shilingi trillioni 2.4 na Sekta ya Mawasiliano - Fungu 68 iliidhinishiwa shilingi 92.7. Jumla ya bajeti ya maendeleo katika Wizara hii ilikuwa shilingi 4.7. Kiasi hiki kilikuwa ni sawa na asilimia 40.3 ya bajeti nzima ya miradi ya maendeleo ya Taifa kwa mwaka huo ya shilingi trillioni 11.8

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2017/2018 Sekta ya Ujenzi - Fungu 98 iliidhinishiwa shilingi trillioni 2.4 kwa ajili ya miradi ya maendeleo; Sekta ya Uchukuzi - Fungu 62, iliidhinishiwa shilingi 2.4 na Sekta ya Mawasiliano - Fungu 68

iliidhinishiwa shilingi bilioni 14. Jumla ya bajeti ya maendeleo kwa Wizara hii ilikuwa shilingi trilioni 4.9. Kiasi hicho kilikuwa ni sawa na asilimia 40.85 ya fedha zote za maendeleo kwenye bajeti ya Serikali ya shilingi trilioni 11.9

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Sekta ya Ujenzi - Fungu 98 kwa miradi ya maendeleo iliidhinishiwa shilingi trilioni 1.8; Sekta ya Uchukuzi - Fungu 62 iliidhinishiwa shilingi trilioni 2.3 na Sekta ya Mawasiliano - Fungu 68 iliidhinishiwa shilingi bilioni 15. Jumla ya bajeti ya maendeleo katika Wizara hii ilikuwa shilingi trilioni 4.1 sawa na asilimia 34.46 ya bajeti yote ya maendeleo ya Serikali ya shilingi trilioni 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha miaka mitatu yaani 2016/2017, 2017/2018 na 2018/2019 Wizara hii iitengewa jumla ya shillingi trilioni 13.8. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kupatiwa takwimu za ajira za kudumu au za muda zilizotokana na uwekezaji huo kwa kipindi tajwa hapo juu ili Watanzania waweze kupima thamani ya fedha za walipa kodi kwenye miradi hii kama zinaleta matokeo chanya au hasi kwa maendeleo shirikishi na endelevu kwa maslahi mapana ya Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Ujenzi mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2006; kwa kuwa sekta ya ujenzi inakua kwa kasi kubwa hasa kiteknolojia; na kwa kuwa sera hii inatakiwa kutumika kwa mazingira rafiki na yenye tija; Kambi Rasmi ya Upinzani inaomba kupata taarifa kutoka Serikalini kuhusu uhalsia wa sera ilivyo kwa sasa, kwani tangu mwaka 2016 sera hii ilipohuishwa na kupelekwa kwa wadau mbalimbali hakuna taarifa rasmi za mchakato huo umefikia wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa tafiti uliofanywa na Tanzania *Civil Engineering Contractors Association* unaonesha kuwa masuala ya mikakati mingi iliyohitajika kwenye Sekta ya Ujenzi na kuelezweta kwenye sera haiwezi kutekelezeka kama rasilimali haikuwekewa mpango maalum wa upatikanaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya msingi katika sera ambayo yalikuwa yanahitajika kutekelezwa kwa haraka ili sekta iweze kubeba dhamana ya kuwa kiungo cha kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa viwanda na kipato cha kati, ni kama ifuatavyo:-

- (a) Mikataba ya ujenzi kutayarishwa ikiwa na lengo la kuruhusu ushiriki mpana wa makandarasi wachanga/wadogo kuweza kushiriki na kushinda zabuni;
- (b) Uanzishwaji na utekelezekaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Ujenzi;
- (c) Uimarishaji wa taasisi zinazohusika na utungaji wa kanuni, utawala na usimamizi kwenye Sekta ya Ujenzi;
- (d) Kutokuwepo kwa mfumo wa uratibu toka utekelezaji wa programu za kazi kulingana na matakwa ya sera;
- (e) Kutokuwepo kwa mfumo wa uratibu utakaofanya kazi kati ya Kamati Tendaji iliyoundwa na Wizara ya Ujenzi;
- (f) Ugomvi kati ya Baraza la Ujenzi (*NCC*) na Bodi ya Usajili wa Wadau wa ujenzi kutokana na kutokuwepo kwa mfumo makini wa kutenganisha majukumu na miongozo ya kiutendaji baina yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya udhaifu kama ulivyobainishwa na *TACECA* ni kwamba hakuna sheria au kanuni za kusimamia utekelezaji wa sera; uwezo hafifu (fedha na ujuzi) mionganoni mwa taasisi za utekelezaji wa Sera ya Ujenzi; na kutokuwepo kwa idara maalum ndani ya Wizara kwa ajili ya utekelezaji wa sera husika (*CIP*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera hii inaonyesha kuwa sehemu kubwa ya shughuli za kikandarasi inafanyika katika sekta isiyo rasmi na takribani asilimia 80 ya Watanzania wanaishi maeneo ya vijijini, majengo na miundombinu

midogo midogo kwa wananchi wanaoishi katika maeneo hayo yanajengwa na sekta isiyo rasmi pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba sekta ya ujenzi isiyo rasmi inahusisha kwa kiasi wananchi ambao hawana kinga na mnyororo mzima wa uchumi kama vile vibarua, vifaa na ujenzi. Mara zote sekta hii inafanya kazi kulingana na matakwa ya mteja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaomba Serikali itoe maelezo yake Bungeni, ni kwa namna gani upungufu huu wa kisekta kama ulivyoainishwa hapo juu umefanyiwa kazi ili Sekta ya Ujenzi iweze kukidhi malengo yake ya kisera?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Mpango wa Pilli wa Miaka Mitano, ukurasa wa 53 na 54 unaonyesha kuwa sekta ya ujenzi hadi mwaka 2020 imewekewa lengo la kukua kwa kiwango cha asilimia 9.6, mchango wa Sekta kwenye pato la Taifa uwe ni asilimia 11.8 na sekta iweze kuchangia asilimia 3.7 ya ajira zote. Aidha, makampuni ya ndani katika kupata kazi ya ujenzi iwe ni asilimia 60 ya thamani ya jumla ya kazi za ujenzi hapa nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaomba kujua malengo haya hadi sasa yametekelawa kwa kiwango gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Majengo (*TBA*), *TBA* ilianzishwa kwa madhumuni ya kuongeza ubora wa utoaji huduma kwa kutumia njia za kibiashara na usimamizi bora wa fedha ili kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa Taifa, huduma bora ya makazi kwa Serikali na nyumba za gharama nafuu kwa watumishi wa Umma. Wakala ilianzishwa Mei, 2002 kwa mujibu wa sheria mama ya Wakala Na. 30 ya mwaka 1997.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa mwaka 2018/19 aya ya 94 ukurasa wa 49 inasema kuwa, “*TBA* imeendelea kutekeleza miradi ya ubunifu na ujenzi (*Design and Build*) ambayo inatekelezwa nje ya bajeti. Miradi hii ni kutoka katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali.

Pia wakala una jumla ya miradi 90 ya *Design and Build* inayotekelawa ambayo ina thamani ya jumla ya shilingi bilioni 154.9."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni kumekuwepo malalamiko kutoka Serikalini kutokana na utendaji usioridhishwa wa *TBA*. Kwa mfano, Serikali imewaonya Wakala wa Majengo Nchini *TBA* kutokana na kutumia gharama kubwa zilizoingiwa thamani ya majengo huku wakichelewesha kukamilisha ujenzi kwa wakati. Onyo hili lilitolewa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Profesa Ndlichako, Mbunge alipokuwa akikagua miradi ya ujenzi ya nyumba za madarasa, mabweni, maabara na Chuo cha Ufundı Stadi (*VETA*) yaliyojengwa kwa Wakala wa Wilayani Makete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri alibalini, licha ya *TBA* kuchelewesha kukamilisha mradi huo ambao ultakiwa kukamilisha mwezi Oktoba mwaka 2018, wametumia zaidi ya shilingi milioni 637 kujenga nyumba nne zenye vyumba vitatu gharama ambayo inasema hailingani na thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijiji, ameagiza Wakala wa Majengo Tanzania (*TBA*) kutekeleza kwa wakati mradi wa ujenzi ya Ofisi ya Halmashauri ya Mji wa Kasulu mkoani Kigoma ili kuепusha Serikali kutumia fedha nydingi kutokana na kuongezeka kwa gharama za miradi. Kutokana na ucheleweshaji huo, Ofisi mpya ya Halmashauri ya Mji wa Kasulu zilizojengwa na Serikali kwa zaidi ya shilingi bilioni 2.5 na kutaarifiwa kuwa *TBA* wamechelewa kuanza ujenzi kwa zaidi ya miezi 12 wakati fedha zilikwishatolewa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukirejea mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa iliyotolewa mwezi Januari, 2019 hapa Bungeni kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI irejee mikataba ambayo Serikali imeingia na *TBA* kuhusu ujenzi wa ukarabati wa shule kongwe iwapo itabaini kasoro za utekelezaji, basi hatua stahiki zichukuliwe ikiwa ni

pamoja na kusitisha au kuvunja mkataba kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa maendeleo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni 17.45 kwa lengo la ujenzi wa ukarabati wa nyumba kwa ajili ya makazi ya viongozi na watumishi wa Serikali pamoja na majengo ya Serikali ikiwa ni vipaumbele vyta ujenzi na nyumba za viongozi Dodoma na mikoani pamoja na ujenzi wa nyumba za Majaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, taarifa inaonyesha kuwa *TBA* inahudumia miradi 90 ya *design and build* kwa nchi nzima. Kwa kuwa sekta binafsi ni injini na ukuaji wa uchumi wa nchi yetu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri miradi mingine inaweza kutekelezwa na sekta binafsi au kwa ubia kati ya Serikali na sekta binafsi badala ya miradi yote kuwalundikia *TBA*. Hii italeta ufanisi na kuaminika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uchukuzi inahusisha usafirishaji wa njia ya anga, njia ya majini, njia ya baharini na maziwa, njia ya reli na njia ya barabara. Pia inahusisha na mamlaka ya udhibiti wa uchukuzi wa usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Sekta ya Uchukuzi ilitengewa jumla ya shilingi trilliuni 2.3 zikiwa fedha za kutekeza miradi ya maendeleo, lakini hadi mwezi Februari, 2019 fedha zilizopokelewa Sekta husika ni shilingi bilioni 391.1 tu sawa na asilimia 17 tu ya fedha zote zillizoidhinishwa na Bunge. Aidha, Randama inaonesha kuwa kuna fedha zilizokuwa zimebaki kwenye Akaunti ya Amana kwa ajili ya utekelezaji wa miradi iliyokuwepo na hivyo kufanya fedha za maendeleo kuwa shilingi bilioni 947.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika fedha hizo, miradi iliyopewa fedha ni ununuzi wa ndege, ukarabati wa reli ya Tanga - Arusha jumla ya shilingi bilioni sita, ukarabati na ujenzi wa meli katika maziwa jumla ya shilingi bilioni tatu na ununuzi wa vifaa vyta hali ya hewa shilingi bilioni sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri, ni vyema Serikali ikapanga mipango yake kibajeti kihalisa hasa uwezo wa Serikali kimapato na kuwa kutekeleza kwa vitendo sheria ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa Usalama wa Usafiri wa Anga (*TCAA*) unahusisha ukaguzi wa viwanja vyatya ndege ili vikidhi ubora na usalama wa Kimataifa kwa ndege na abiria. Hivyo, mamlaka hii ndiyo mwajibikaji wa miundombinu yote ya kiusalama kama vile Rada za kuongozea ndege, mifumo ya uokozi nikitaja kwa uchache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu huduma za viwanja vyatya ndege, uboreshaji wa miundombinu ya viwanja ili kuongeza ushindani na kupunguza gharama za usafiri wa anga hapa nchini. Huduma zinazotolewa katika viwanja vyatya ndege ni pamoja na mizigo, wasafiri (abiria), huduma ya chakula, mfumo wa kukata tiketi na nyaginezo zinazohitajika kwa mujibu wa taratibu na kanuni za uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa ndege za Serikali (*TGFA*), ndiye mwenye jukumu la kufanya mchakato mzima wa manunuzi wa ndege ya Serika. Ndege zote ambazo zimenunuliwa katika kipindi cha Serikali, Awamu ya Tano ni mali ya Serikali ila zimekodishwa kwa kampuni ya ndege *ATCL* kwa ajili ya kufanya biashara. Hii ni kutokana na sababu kuwa kampuni hiyo ilikuwa mufilisi na bado inadaiwa madeni makubwa na taasisi mbalimbali za nje kutokana na huduma ambazo taasisi hizi zilitoa kwa *ATCL* miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tangazo la Serikali (*Government GN*) Na. 252 ya tarehe 8 Juni, 2018 kuwa wakala huyo ana majukumu yanayoainishwa Ofisi ya Rais, majukumu yake yanahamishiwa Ofisi ya Rais Ikulu kutoka Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano katika kutimiza majukumu yake kwa mwaka 2019. Wakala inatakiwa kutimiza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitaja kwa uchache ni kusimamia mikataba ya ukodishwaji wa ndege kwa kampuni

ya ndege ya Taifa (*ATCL*); kufanya matengenezo na ununuzi wa vipuri vya ndege za Serikali; kufanya ukarabati wa karakana ya ndege za Serikali; kulipia gharama za bima za ndege; kugharamia uendeshaji wa ofisi; na kulipia gharama za mafuta ya ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kila kazi zilizotajwa ambazo kwa njia moja au nyingine zinatakiwa kufanywa na Serikali, hii ni sawa kabisa na kile kilichokuwa Kimetokea miaka ya nyuma kwenye suala la *IPTL* wakati wa manunuzi ya mafuta ya mitambo ambapo *TANESCO* haikuwa na sauti bali Wizara ndiyo ilikuwa imeshika hatamu; na kilichokuwa kilichotokea wakati huo kiko wazi kwa kila mmoja wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za usafiri wa anga. Kwa mujibu wa taarifa Kamati ya Bunge ya *P/C* ya mwezi Januari, 2019 inasema wazi kuwa kumekosekana na sera madhubuti ya mpango mkakati ndio kusababisha utendaji usioridhisha kwa shirika la *ATCL*. Rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ni kwamba shirika liwe na wataalamu wenyewe ujuzi usio na shaka wa kuendesha na kulisimamia hatimaye liweze kutengeneza faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, taarifa hiyo ya Kamati ya Bunge ya *P/C* inafafanua kwamba *ATCL* kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo, yaani mwaka 2014/2015 *ATCL* ilipata hasara ya shilingi bilioni 94.3 na mwaka 2015/2016 ilipata hasara ya shilingi bilioni 109 na mwaka 2016/2017 shilingi bilioni 113.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Uongozi *ATCL* inaonyesha kuwa mapato ya kampuni hiyo yanapanda shilingi milioni 700 kwa mwaka 2016 hadi kufikia shilingi bilioni 4.5 kwa mwaka 2017. Pia, hasara imepungua kutoka shilingi bilioni 14 mwaka 2016 hadi shilingi bilioni 4.3. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Wizara ya mwaka 2018/2019, aya ya 164, ukurasa wa 87, inasema kuwa, katika kipindi cha Julai, 17 hadi Machi, 18 kampuni ilisafirisha abiria

100,518 ikilinganishwa na abiria 107,207 kwa kipindi cha mwaka 2016 na hiyo kufanya ongezeko la asilimia 46. Ongezeko hili limewezesha kampuni kuongeza mapato kutoka shilingi bilioni 34.4 yaliyokusanywa mwaka 2016/2017 hadi shilingi bilioni 43.8 mwaka 2017/2018. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya *PIC* ni kwamba katika kipindi hicho ilichofanyiwa kazi na Kamati ya Bunge, matumizi yaliongezeka kwa kiwango cha juu kulinganisha na mapato yaliyopatikana na hali hiyo ikiendelea hivyo uhai wa kampuni hiyo utakuwa shakani. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali inapokuja, inatoa taarifa kuhusu utendaji wa shirika lile iwe wazi kwa kulinganisha mapato na gharama za uendeshaji ili tupime kama tuko kwenye upande wa faida au hasara katika uendeshaji wa shirika hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Awamu ya Tano imeendelea kupuuza ushauri tunaoendelea kuutoa kuhusiana na *ATCL*. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunapozungumzia mwenendo wa Shirika letu la Ndege ni kwa maslahi mapana ya nchi yetu na kuona kuwa linafanya kazi zake kwa weledi na hatimaye kuongeza faida. Wahenga wanasema, kawia ufile, kuliko harakia ukaishia njiani, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuishauri Serikali kutafakari upya kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kutafuta wataalam huru kulisimamia shirika letu na ikiwezekana kuijendesha kwa faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usafiri wa Usafirishaji wa Reli; Tanzania tuna mashirika mawili ambayo yanatoa huduma ya usafiri wa usafirishaji wa reli. Mashirika hayo ni Shirika la Reli Tanzania, *TRC* na Shirika la Reli la Tanzania-Zambia, *TAZARA*. Katika bajeti imetengwa Sekta ya uchukuzi kwa mwaka 2019/2020 kwa miradi ya maendeleo ya shilingi triliioni 3.5, kati ya fedha hizo shilingi triliioni 2.9 sawa na asilimia 81 ya fedha zote za bajeti ya maendeleo katika Sekta hii ni kwa ajili ya kuimarisha reli hapa nchini. Hili ni jambo zuri kama fedha hizo zitatolewa kwani kwa mwaka 2018/2019, kati ya triliioni 2.3 zilitolewa asilimia 17 tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *SGR* na manufaa ya kiuchumi kwa wananchi. Mradi huu ulitegemewa kuwa na manufaa makubwa ya kiuchumi kwa maana ya kutoa ajira kwa vijana wetu na kutumia malighafi hapa nchini katika kuijienga mradi huo na hivyo kukuza uchumi wetu. Hata hivyo, matumaini haya yamefifia kutokana na malighafi ya ujenzi wa mradi huo kununuliwa kutoka nje, jambo ambalo linasababisha kupungua sana kwa akiba yetu na fedha za kigeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupungua kwa fedha za kigeni kuna athari kubwa sana katika ukuaji wa uchumi wa Taifa, hii ni kwa sababu; moja, uwezo wetu wa kununua bidhaa nje kwa kutumia fedha za kigeni unapungua, lakini pili, thamani ya shilingi hupungua kutokana ukosefu wa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni. Mradi wa *SGR* ungefanyiwa utafiti kwa muda mrefu na kuona ni namna gani utalinufaisha Taifa katika hatua za awali. Tungeweza kutumia malighafi ya hapo nchini katika kujenga mradi huo hususan chuma cha Linganga jambo ambalo lingetoa ajira nyingi kwa vijana wetu, lakini pia fedha ambayo inatumika kununua vifaa vyta ujenzi huo kutoka nje, zingebaki katika mzunguko wa ndani hivyo kuimarisha uchumi wetu. Kutokana na mradi huo kulikosesha Taifa fursa hizo za kiuchumi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuacha kujigamba na mradi huo kwa kuwa ni mradi unaotumia fedha nyngi na haujulikani gharama hizo zitalipwa lini. *To break even*; ili mradi huo uweze kuwa na faida kwa wananchi na Taifa, (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Usimamizi Bandari Tanzania; Tanzania imebahatika kuwa na ukanda mrefu wa bahari na pia kuwa nchi inayoweza kuhudumia mataifa ambayo kijiografia hayajapakana na bahari na kwa hiyo kuwa kitovu cha biashara katika ukanda huu kama iliyuo Dubai, Singapore, Hong Kong kwani imepakana na nchi sita zilizokuwa na bahari. Bandari ya Dar es Salaam ambayo hapa kwetu ndiyo kubwa kuliko zote, imeendelea kuwa ya mwisho ikilinganishwa na bandari ya ukanda huu kama vile Durban, Beira na Mombasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushindani wa mamlaka ya bandari kwa bandari tajwa hapo juu hautakuwepo kwa sasa kutokana na sababu kubwa kwamba, majukumu ambayo yanatakiwa kufanywa na bandari kama mamlaka sasa hivi yatakuwa yanafanywa na *TASAC*kama *Shipping Agency* na hivyo kuacha mamlaka kuwa na kazi ya kupokea na kupakua mizigo kama ilivyo *TICTS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam unatekelezwa kwa kupitia mradi mkubwa ujulikanao kama Dar es Salaam *Maritime Gateway Project* unaotekelezwa kwa gharama ya Dola za Kimarekani milioni 421. Katika gharama hizo 82% ni mkopo hata Benki ya Dunia, 2.8% ni msaada toka *DfID* na 15.2% ni mapato yetu ya ndani. Changamoto kubwa ya mradi huu ni ulipaji wa kodi ya ongezeko la thamani (*value added tax*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika makubaliano yaliyowekwa mradi huu umesamehe kodi hii, kwa kupitia msamaha huo una mlolongo mrefu sana kiasi cha kupunguza kasi ya ujenzi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kupitia Wizara ya Fedha kuondoa urasimu uliokithiri ili kuwawezesha kumaliza kazi kwa muda. Mradi huu ulipitia hatua zote za upembuzi yakinifu kwa gharama kubwa uliohusisha makampuni makubwa ya nje *M/S Ihros Lackerya* Ujerumanî ambayo ilisaini Mkataba na *TPA* Juni 21, 2017 kwa gharama za *Euro* milioni 2.9. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Ghati Namba 13 na 14; katika hotuba zetu za nyuma tulionomba kupatiwa maelezo juu ya ushauri tuliontoa sambamba na ule wa Kamati ya Bunge Miundombinu kuhusu ujenzi wa ghati hizo, nanukuu:

"Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa katika Bunge la Kumi, Mkutano wa Saba wa Bunge hilo kulikuwa na majadiliano ya kina kuhusiana na ujenzi wa ghati hizi na Bunge liliagiza kuwa mradi huo utekelezwe kwa kutumia mkopo kutoka Benki ya China kama ilivyopendekezwa na Mamlaka ya Bandari. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kupata majibu juu ya masuala yafuatayo:-

(a) mchakato wa ujenzi wa ghati 13 na 14 umefikia wapi mpaka sasa?

(b) Baada ya kusitishwa kwa mchakato wa mkatuba wa awali ni hatua gani zimechukuliwa na serikali dhidi ya waliohusika na mchakato ambao ulikiuka sheria za nchi?

(c) ni lini ujenzi wa ghati hizi utakamilika ili kuweza kuendana na mpango mkuu wa bandari nchini?"

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kufanya hivyo, Serikali haikuona nia thabiti ya kutekeleza mradi huo. Aidha, miaka mitatu baadaye Kamati ya Bunge lako Tukufu nayo inaona kuwa tija ya Serikali kujenga ghati namba 13 na 14 kwa mkakati wa kuliongezea taifa mapato. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza ushauri huo kama ilivyoshauri katika bajeti ya mwaka 2013/2014, ushauri ambao sasa Kamati ya Bunge ya Miundombinu pia imeendelea kushauri katika vikao vyao na TPA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi katika hotuba yake mwaka wa fedha 2016/2017, wakati anasoma utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2015/2016 kuhusu ujenzi wa ghati bandarini inalisema kuwa, nanukuu;;

"Kazi ya uboreshaji wa uongezaji wa kina katika ghati namba 1-7 ya ujenzi wa ghati jipya ya kushushia magari eneo la Gerezani Creek katika bandari ya Dar es Salaam kwa ufadhili wa Benki ya Dunia, TMEA na DfID zinaendelea. Nyaraka za zabuni hatua ya pili na ya mwisho ya kupata mkandarasi wa kazi za ujenzi zilitolewa Machi, 2016 kwa wakandarasi sita waliofuzu katika hatua ya kwanza ya zabuni na zinatarajiwaa kufunguliwa Juni, 2016. Aidha, kampuni ya M/S Inros Lackner Ag kutoka Ujerumanii tayari imeteuliwa kuwa msimamizi wa kazi za ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya TPA na Mshauri Mwelekezi wa kufanya upembuzi yakinifu na namna bora ya kupanua na kuchimba ili kuongeza kina cha langa la kuingilia meli na eneo la kugeuzia meli ulisainiwa Desemba, 2015. Mshauri mwelekezi alianza kazi Januari, 2016 na akakamilisha Julai, 2016. Aidha, kazi ya kupanua, kuchimba na kuongeza zinatarajiwa kuanza Oktoba, 2016 na kukamilika Novemba, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016, mamlaka ilipanga kujenga ghati namba 13 na 14 kwa kushirikiana na Sekta binafsi utaratibu na usanifu, Jenga, Endesha na Rejesha (Design, Build, Operate and Transfer). Hata hivyo, kazi hiyo haikutekelezwa kutokana na kutokamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa awali utakaoonesha hali halisi ya mradi na gharama zake. Ujenzi wa ghati hizi unatarajiwa kuanza mwaka 2017 kwa ufadhilli wa Benki ya Dunia. Baada ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali kukamilika, ni matarajio yetu kuwa, Sekta binafsi itawekeza katika utoaji huduma na ujenzi wa maghala katika magati hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ilitakiwa kuanza mwaka 2017, sasa ni mwaka 2019, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunasisitiza kupatiwa majibu kama tulivoomba katika hotuba yetu ya mwaka 2016/2017 kuhusiana na ujenzi wa ghati 13 na 14.

MWENYEKITI: Haya malizia, malizia.

MHE. SUSAN L. KIWANGA - K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwisha sema kwamba hotuba hii yote iingie kwenye Hansard.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika hotuba hii tumezugumzia kidogo kuhusu *data centre* na ukusanyaji, lakini katika *data centre* tumeonesha kabisa kwamba kuna watu binafsi 23 tu ambao wanahifadhi data huko na kuingiza

Serikalini kiasi kisichopungua bilioni 4.9, je, haya mashirika mengine yako wapi? Tunahoji Serikali tunataka watupe majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumzia vilevile kuhusu *UCSAF* na kuhusu fedha nyingi zinazotolewa kuhusu *Halotel, Vodacom, Airtel* na *TTCL* na madhumuni ya mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumezungumzia miundombinu mikubwa imekuwa ikichukua fedha nyingi kwenye bajeti ya Taifa. Vilevile, namalizia, kuwa miundombinu kwa kiwango kikubwa imekuwa ikichukua fedha nyingi kwenye bajeti ya Taifa na kwa kuwa baadhi ya makampuni yaliyohusishwa na uwekezaji na miundombinu hiyo ni kutoka nje na uwekezaji mzuri muda mrefu kwa nchi zote zillizoendelea ulifanyika kwenye elimu na rasillimali watu; na kwa kuwa sisi Watanzania tumebakia kuwa mwangaliaji na siyo mshiriki katika uwekezaji huo ipasavyo. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri changamoto zote tajwa zifanyiwe kazi kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha. Ahsante. (*Makofii*)

**MAONI YA MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI MHESHIMIWA JAMES FRANCIS MBATIA (MB)
KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA
2018/19 NA MPANGO WA MAPATO NA MATUMIZI YA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO KWA
MWAKA WA FEDHA WA 2019/2020 - KAMA
YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

*(Yanatolewa chini ya Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(9),
Toleo la Mwaka 2016)*

I. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na nguvu katika kipindi hiki kigumu

sana katika ufanyaji wa siasa hasa kwa upande shindani na Chama Tawala na kuweka kusimama mbele ya hadhira hii ili kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu sekta nzima ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

2. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa kushirikiana na wananchi wote wanaojali na kuheshimu utu wa mwanadamu; inapingga na kukemea kwa nguvu zote kitendo cha kinyama cha kumvamia na kumteka Kijana Mdude Nyagali ambaye mpaka sasa haijulikani kama yuko hai au ameuwawa.

3. Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa kiti cha Spika kilitoa maelekezo kwa Serikali kuleta Bungeni haraka iwezekanavyo taarifa kamili kuhusu suala la kutekwa na kupelekwa kusikojullikana kwa kijana huyo ambaye ni mkazi wa Vwawa-Mbozi; Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali: mosi kutoa taarifa hiyo kwa mujibu wa maelekezo ya kiti; na pili kutoa hakikisho kwa wanandugu na watanzania wote kuhusu usalama wa kijana huyo na usalama wa watanzania wote kufuatia muendelezo wa matukio ya utekaji hapa nchini. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza kwamba, kama kuna makosa yoyote yanayofanywa na mtu ye yeyote, mamlaka pekee yenye uwezo wa kutoa adhabu ni mahakama na si vinginevyo.

4. Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa utangulizi huo, sasa naomba kujielekeza katika hoja iliyo mbele yetu;

II. MAPITIO YA JUMLA KUHUSU WIZARA

5. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inajumuisha sekta kuu tatu ambazo ni Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Kwa kila sekta mbali ya kusimamia Sera inayoendesha sekta hiyo, bali pia inasimamia Idara na taasisi zingine zilizopo katika sekta hiyo.

6. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2016/17 na 2017/18 ndiyo

Wizara iliyokuwa na miradi ya kipaumbele katika mgawanyo wa bajeti ya maendeleo na hiyo ndiyo Wizara iliyopewa sehemu kubwa ya fedha za walipa kodi. Mwaka wa fedha 2016/17, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano – sekta ya Ujenzi Fungu 98 iliidhinishiwa shilingi **2,176,204,557,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Sekta ya uchukuzi Fungu 62 ambayo iliidhinishiwa shilingi **2,495,814,130,000.00**, na sekta ya Mawasiliano Fungu 68 zilitengwa jumla ya shilingi **92,730,110,000.00** na hivyo kuifanya sekta nzima ya miundombinu kutengewa fedha za maendeleo jumla ya shilingi **4,764,748,797,000.00** kiasi hiki kilikuwa ni sawa na **asilimia 40.3** ya bajeti nzima ya miradi ya maendeleo kwa mwaka huo **ya shilingi bilioni 11,820.5**

7. Aidha, **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka **2017/18** Sekta ya Ujenzi Fungu 98 imetengewa jumla ya shillingi **2,411,026,062,496.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambayo ni ya kimkakati na isiyo ya kimkakati. Uchukuzi Fungu 62, fedha za miradi ya maendeleo zilitengwa Shilingi **2,477,931,183,000.00** na Fungu 68, mawasiliano zilitengwa jumla ya shilingi **14,000,000,000** na hivyo kufanya bajeti nzima ya maendeleo kwa Wizara hii kuwa shilingi **4,902,957,245,496.00**. Kiasi hicho kilikuwa ni sawa na **asilimia 40.85** ya fedha zote za maendeleo kwenye bajeti ya Serikali ya shilingi **bilioni 11,999.6**

8. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka huo wa fedha 2018/19 Sekta ya Ujenzi Fungu 98 kwa miradi ya maendeleo ilitengewa jumla ya shilingi **1,822,093,269,360.00**, Sekta ya Uchukuzi Fungu 62 kwa mwaka huo wa fedha zilitengwa jumla ya shilingi **2,300,739,000,000.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo, aidha kwa sekta ya Mawasiliano Fungu 68 ilitengewa jumla ya shilingi **15,000,000,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hivyo kufanya kuwa Wizara kwa mwaka huo kutengewa fedha za miradi ya maendeleo yenye jumla ya shilingi **4,137,832,269,360.00** sawa na **asilimia 34.46** ya bajeti nzima ya **shilingi bilioni 12,007.3** matumizi kwa miradi ya Maendeleo kwa mwaka huo wa fedha.

9. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na takwimu hizo ni rahisi sana kuona kuwa kwa kipindi cha miaka mitatu yaani 2016/17, 2017/18 na 2018/19 Wizara hii imetengewa jumla ya **shilingi 13,805,538,311,856.00 au (trilioni 13.806)**. Vyano vikuu vya fedha hizo vilikuwa ni mikopo ya masharti ya kibiashara na misaada ya kibajeti.

10. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kupatiwa takwimu za ajira za kudumu au za muda zilizotokana na uwekezaji huo kwa kipindi tajwa hapo juu, ili watanzania waweze kupima kama fedha za walipa kodi zinaenda kwenye miradi ambayo inaleta matokeo chanya kwa watanzania wote au ni matokeo chanya kwa kundi fulani katika jamii ya watanzania.

III. SEKTA YA UJENZI
i. Sera ya Ujenzi

11. **Mheshimiwa Spika**, Tanzania ilitengeneza sera ya sekta ya ujenzi (the Construction Industry Policy (CIP) mwaka 2003 na kanuni zake za utekelezaji zilitolewa rasmi mwaka 2006. Kwa mujibu wa wadau ni kuwa ni sehemu ndogo sana ya sera ndiyo ilikuwa inaweza kutumika kwa kulingana na mazingira halisi ya sekta yenye.

12. **Mheshimiwa Spika**, mwaka 2016 sera hiyo ilihuushwa na kupelekwa kwa wadau ili waweze kutoa maoni yao kabla ya sera hiyo kukamilika na kuanza kutumika rasmi. Lakini hadi hivi sasa tunapotoa maoni haya Sera ya Tasnia ya Ujenzi bado haijatoka rasmi. Kambi Rasmi inataka kufahamu ni lini hasa sera hiyo itatolewa ili iweze kuwa mwongozo kwa tasnia hiyo ambayo kwa sasa tunaweza kusema kuwa inakabiliwa na changamoto kadhaa.

13. **Mheshimiwa Spika**, sera hii inaonesha kuwa sehemu kubwa ya shughuli za kikandarasi inafanyika katika sekta isiyo rasmi, na takriban asilimia 80 ya watanzania wanaishi maeneo ya vijijini. Majengo na miundombinu midogo midogo kwa wananchi wanaoishi katika maeneo hayo yanajengwa na sekta isiyo rasmi pia.

- 14.** **Mheshimiwa Spika**, ni ukweli kwamba sekta ya ujenzi isiyo rasmi inahusisha kwa kiasi kikubwa wananchi ambao hawana kinga mnyororo mzima wa uchumi; kama vile vibarua, vifaa vya ujenzi na mara zote sekta hii inafanyakazi kulingana na matakwa ya mteja¹.
- 15.** **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Mpango wa Pili wa Miaka Mitano uk. 53 na 54 unaonesha kuwa sekta ya ujenzi hadi mwaka 2020 imewekewa lengo la kukua kwa kiwango cha asilimia 9.6, mchango wa sekta kwenye pato la taifa uwe ni 11.8% na sekta iweze kuchangia asilimia 3.7 ya ajira zote. Aidha makampuni ya ndani katika kupata kazi za ujenzi iwe ni asilimia 60 ya thamani ya jumla ya kazi ujenzi hapa nchini.
- 16.** **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua katika malengo hayo tuliojijwekea hadi sasa tumeyatekeleza kwa kiwango gani?
- 17.** **Mheshimiwa Spika**, kwa masikitiko makubwa ni kuwa, tulikuwa tunaingia katika uchumi wa gesi na tumeaminishwa hivyo na Serikali yetu na hadi kupelekea ujenzi wa Bomba la gesi kati ya Mtwara hadi Dar. Kwa mujibu wa wataalam wanasesma bomba hilo linatumika kwa asilimia 6 tu ya uwezo wake. Jambo la ajabu ni kuwa mradi huo umepigwa chini na sasa tunakimbizana na Ujenzi wa Stiegler's Gorge. Kambi Rasmi ya Upinzani inapata mashaka sana na umakini wetu katika kuhakikisha tunafikia uchumi wa kati.
- 18.** **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na TACECA (TANZANIA CIVIL ENGINEERING CONTRACTORS ASSOCIATION) unaonesha kuwa masuala na mikakati mingi inayohitajika kwenye tasnia ya ujenzi na kuelezewa kwenye sera haiwezi kutekelezeka kama rasilimali hazikuwekewa mpango maalum wa upatikanaji.
- 19.** **Mheshimiwa Spika**, maeneo ya msingi katika sera ambayo yalikuwa yanahitajika kutekelezwa kwa haraka ili

¹Construction Industry Policy - 2003

tasnia iweze kubeba dhamana ya kuwa kiungo cha kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi viwanda na kipato cha katii ni kama ifuatavyo:-

- (a) Mikataba ya ujenzi kutayarishwa ikiwa na lengo la kuruhusu ushiriki mpana wa makandarasi wachanga/ wadogo kuweza kushiriki na kushinda zabuni
- (b) Uanzishwaji na utekelezekaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Ujenzi (*Operationalisation of the Construction Industry Development Fund (CIDF)*).
- (c) Uimarishaji wa taasisi zinazohusika na utungaji wa kanuni, utawala na usimamizi kwenye tasnia nzima ya ujenzi.
- (d) Kutokuwepo kwa mfumo wa uratibu toka utekelezaji wa program za kazi kulingana na matakwa ya sera *the Implementation Action Programme for the Construction Industry Policy (IAP-CIP)*
- (e) Kutokuwepo kwa mfumo wa uratibu utakavyofanyakazi kati ya kamati tendaji iliyoundwa na Wizara ya Ujenzi.
- (f) Ugomvi kati ya baraza la ujenzi(NCC) na Bodi za usajili wa wadau wa ujenzi kutohana na kutokuwepo kwa mfumo makini wa kutenganisha majukumu na miongozo ya kiutendaji baina yao.

20. Mheshimiwa Spika, kuna madhaifu kama ambavyo yalibainishwa na TACECA ni kwamba; hakuna sheria au kanuni za kusimamia utekelezaji wa SERA; Uwezo hafifu (fedha na Ujuzi) mionganoni mwa taasisi za utekelezaji wa Sera ya ujenzi; Kutokuwepo kwa idara maalum ndani ya Wizara kwa minajili ya sera ya ujenzi (CIP).

21. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge ni kwa vipi mapungufu hayo ya kisera kama ambavyo yanajionesha yamefanyiwa kazi ili Tasnia ya Ujenzi iweze kukidhi malengo yake ya kisera?

ii. Wakala wa Majengo (TBA)

22. **Mheshimiwa Spika**, TBA ilianzishwa kwa madhumuni ya kuongeza ubora wa utoaji huduma kwa kutumia njia za kibiashara na uongozi bora wa fedha ili kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa nchi kwa kupunguza gharama za uendeshaji, huduma bora ya makazi kwa Serikali na nyumba za gharama nafuu kwa watumishi wa umma na pia kutoa huduma bora ya ushauri wa kwa Serikali. Wakala ilianzishwa Mei 2002 katika mujibu wa sheria mama ya Wakala Na. 30 ya mwaka 1997 kutokana na iliyokuwa Idara ya Majengo ndani ya Wizara ya Ujenzi (zamani ilijojulikana kama Wizara ya Miundombinu).

23. **Mheshimiwa Spika**, hivi karibuni kuna malalamiko mengi toka Serikali kutokana na utendaji usioridhisha, kama ifuatavyo; "*Serikali imewaonya Wakala wa Majengo nchini (TBA) kutokana na kutumia gharama kubwa zisizolingana na thamani ya majengo huku wakichelewesha kukamilisha ujenzi kwa wakati. Onyo hilo lilitolewa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Joyce Ndalichako alipokuwa akikagua miradi ya Ujenzi wa vyumba vya madarasa, mabweni na maabara ya Chuo cha Ufundistiadi (VETA) yanaoyojengwa na Wakala hao Wilayani Makete Waziri alibaini licha ya TBA kuchelewesha kukamilisha mradi huo ambao ultakiwa kukamilika mwezi Oktoba mwaka jana, wametumia zaidi ya shilingi milioni 637 kujenga nyumba nne zenye vyumba vitatu, gharama ambazo amesema hazilingani na thamani.*"

24. **Mheshimiwa Spika**, sambamba na hilo pia kuna malalamiko yaliyotolewa na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango. Dkt. Ashatu Kijiji, kuhusu utendaji wa TBA kuwa; "ameiagiza Wakala wa Majengo Tanzania-TBA, kutekeleza kwa wakati mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Halmashauri ya Mji wa Kasulu Mkoani Kigoma ili kuiepusha Serikali kutumia fedha nyingi kutokana na kuongezeka kwa gharama za miradi husika kunakotokana na ucheleweshwaji huo. Ofisi mpya za Halmashauri ya Mji wa Kasulu zinazojengwa na Serikali kwa zaidi ya shilingi bilioni 2.5 na kutaarifiwa kuwa TBA, wamechelewa kuanza ujenzi huo kwa zaidi ya miezi 12 wakati fedha zilikwisha tolewa na Serikali".

- 25.** **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa tatizo hilo linatokana na ukweli kwamba TBA wanapewa na kwa kulazimishwa kufanya kazi za Serikali bila ya wao kuingia kwenye mfumo rasmi wa manunuzi wakati uwezo wao wa kufanyakazi ni mdogo. Jambo hili linaondoa dhana nzima ya utawala bora katika kuleta ushindani kwenye utendaji Serikalini. Hili ni tatizo kubwa sana.
- 26.** **Mheshimiwa Spika**, hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa mwaka 2018/19 aya ya 94 uk wa 49 inasema kuwa TBA imeendelea kutekeleza miradi ya ubunifu na ujenzi (Design and Build) ambayo inatekelezwa nje ya bajeti. Miradi hii ni kutoka katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali (MDAs). Pia wakala una jumla ya miradi 90 ya Design and Build inayotekelawa ambayo ina thamani ya jumla ya shilingi 154,974,576,390.26.
- 27.** **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kufahamu hiyo miradi inayotoka Wizara na katika Idara na Taasisi za Serikali inaletwa tu kwa TBA kama zawadi au kuna utaratibu wa kufuata sheria ya manunuzi unafanyika, kama utaratibu haufanyiki ni hatua gani za kinidhamu wa wahusika zinachukuliwa?
- 28.** **Mheshimiwa Spika**, aidha, taarifa inaonesha kuwa TBA inahudumia miradi 90 ya Design & Build kwa nchi nzima, hii ni miradi mingi sana na kwa hali ya kawaida si rahisi thamani ya fedha ikaonekana kwa taasisi moja kuwa na idadi kubwa ya miradi kama hiyo. Hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kufahamu, kwa utaratibu huu wa kurundika miradi kwa taasisi moja ya Serikali. Sekta binafsi itapata wapi kazi za kufanya katika tasnia ya ujenzi?
- 29.** **Mheshimiwa Spika**, kutokana na hali halisi ya Raslimali watu na raslimali vifaa ni dhahiri kwamba TBA ina sub contract kazi hizo kwa wakandarasi wengine. Jambo hili linapelekea ubora wa kazi kuwa hafifu kutokana na ukweli kwamba kazi itafanyika ili mradi imefanyika na sio kufanyika ili kukidhi viwango vinavyohitajika.

30. **Mheshimiwa Spika**, rejea mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa iliyotolewa Mwezi Januari 2019 kwamba;

"Ofisi ya Rais Tamisemi irejee mikataba yote ambayo Serikali imeingia na TBA kuhusu ujenzi na ukarabati wa shule kongwe, na iwapo itabaini kasoro za utekelezaji basi hatua stahiki zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kusitisha au kuvunja mkataba kwa mujibu wa sheria."

31. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa TBA inatatizo kubwa sana na tatizo hilo sio kama kwamba limeanza leo au jana bali ni la muda mrefu sana, hivyo ni muda mwafaka kurejea utendaji wake wa kazi kisheria ili kudhibiti na kuondoa ukiritimba wa taasisi hiyo.

32. **Mheshimiwa Spika**, katika mpango wa maendeleo kwa mwaka wa fedha 2018/19, Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni 17.45 kwa lengo la ujenzi na ukarabati wa nyumba kwa ajili ya makazi ya viongozi na watumishi wa Serikali pamoja na majengo ya Serikali. Ikiwa na vipaumbele ujenzi wa nyumba za viongozi Dodoma na Mikoani pamoja na ujenzi wa nyumba za Majaji.

33. **Mheshimiwa Spika**, kabla sijatoa mtazamo wa Kambi kwa jambo hili, naomba kurejea hoja yangu nillioitoa hapa Bungeni tarehe 17 Mei, 2016 kuhusiana na suala zima la nyumba za Serikali zilizouzwa;

"Mheshimiwa Spika, wakala huyu wa majengo ndiye mhusika mkuu katika kuhakikisha nyumba za Serikali zinakuwa katika hali nzuri kwa watumishi wa serikali kuishi. Katika muktadha huo Kambi Rasmi ya Upinzani inalikumbusha Bunge kwamba, kati ya mwaka 2002 mpaka 2004 Serikali iliuza nyumba zipatazo 7,921 na mpaka mwaka 2008 Serikali ilikuwa imejenga nyumba 650 tu.

Mheshimiwa Spika, katika biashara hiyo kwa kuuza zilizokuwa mali ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Serikali ilipata Sh. 252,603,000/- sasa inahitaji kusaka nyumba zaidi ya maradufu ya kiasi hicho kujenga

nyumba za fidia. Kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge juu ya uuzaji wa nyumba za serikali kinyume cha taratibu, serikali itatumia Sh. 677,606,000/- kujenga nyumba mpya ili zirejeshwe kwa Tamisemi, Rejea taarifa ya Serikali Bungeni tarehe 25 Aprili, 2008.

Mheshimiwa Spika, Kwa vile hata wale waliouziwa nyumba hizo, kuna taarifa kati yao wapo walioziua na kujipatia faida kubwa kinyume na mikataba ya mauzo hayo, KRUB inapendekeza wanyang'anywe nyumba hizo kwa kukiuka mikataba na malengo ya mauzo.

Mheshimiwa Spika, Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge zinaonesha kwamba Serikali ilitoa taarifa ndani ya Bunge hili kuwa, kuna Kamati iliundwa kuchunguza mchakato wa mauzo ya Nyumba za Serikali na Kamati hiyo ilitegemewa kumaliza kazi mwezi Februari, 2007, lakini hadi Bunge la Tisa na Bunge la Kumi linamaliza uhai wake hakuna taarifa iliyotolewa na Serikali. KRUB, inaitaka serikali ya awamu ya tano irejeshe nyumba hizo”.

34. Mheshimiwa Spika, mbali na Serikali kushindwa kutekeleza Azimio la Bunge la kurejeshwa nyumba hizo na pia Waheshimiwa mbalimbali wameishatoa hisia zao kuhusiana na kurejeshwa kwa nyumba hizo. Kambi Rasmi ya Upinzani inarudia tena kuitaka Serikali ya Awamu ya Tano kuzirejesha nyumba za Serikali ambazo kwa kiasi kikubwa zilitolewa kwa watu ambao hawakustahili na zoezi zima lligubikwa na rushwa na upendeleo mkubwa wa kiundugu na uchafu mwingine wa aina hiyo.

35. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa awamu ya tano ni serikali ya kunyoosha nchi itakuwa vyema kunyoosha pale ambapo zoezi la uuzwaji nyumba za Serikali na wahusika walioendesha zoezi hilo kuchukuliwa hatua za kinidhamu na kisheria. KRUB inauliza ni lini TAKUKURU itachukua nafasi yake katika hili?

36. Mheshimiwa Spika, ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri iliyosomwa hapa Bungeni mwezi Aprili, 2018 Uk.191 aya

ya 365 inasema kuwa; "Jumla ya shilingi 1,864,991,280,426.00 za Fungu 98 (Ujenzi) zinajumuisha shilingi 42,898,011,066.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi 31,075,545,000.00 ni za mishahara na shilingi 11,822,466,066.00 ni matumizi mengineyo. **Bajeti ya maendeleo ni shilingi 1,822,093,269,360.00**".

37. **Mheshimiwa Spika**, ukisoma randama iliyotolewa mwezi Machi, 2019 uk. 6 aya ya 5.3 inasema kuwa "kwa mwaka wa fedha 2018/19 Wizara Fungu 98-Ujenzi ilitengewa **shilingi 1,976,442,353,141.38** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo, kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni shilingi 1,540,514,754,141.38 na za nje ni shilingi 435,927,599,000.00

38. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuangalia takwimu hizo za fedha za miradi ya maendeleo kuna tofauti ya **shilingi 154,349,083,781.38**. Kiasi hiki cha shilingi bilioni 154.349, slo fedha ndogo, hivyo basi, Kambi Rasmi inataka kupatiwa ufanuzi juu ya tofauti hiyo ya fedha.

39. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2019/20 sekta ya ujenzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 1,204,037,604,268.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kati ya fedha hizo shilingi **900,000,000,000.00** ni fedha za ndani na zilizobakia shilingi **304,037,604,268.00** ni fedha za nje.

IV. SEKTA YA UCHUKUZI

40. **Mheshimiwa Spika**, kama ilivyo kwenye sekta ya ujenzi sekta hii ya uchukuzi inahusisha, usafirishaji wa njia ya anga, njia ya baharini na maziwa, njia ya reli na njia ya barabara. Aidha, kuna mamlaka za udhibiti pamoja na wakati wa huduma kwa baadhi ya tasnia kwa njia hizo tajwa za uchukuzi na usafirishaji.

41. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2018/19 sekta ya uchukuzi ilitengewa jumla ya shilingi 2,300,739,000,000.00 kama fedha za kutekeza miradi ya maendeleo, lakini hadi mwezi Februari 2019 zilipokelewa **shilingi 391,161,650,000.00** sawa na asilimia 17 tu ya fedha

zote zilizokuwa zimetengwa kwa maendeleo. Aidha Randama inaonesha kuwa kuna fedha zilizokuwa zimebakia kwenye Akaunti ya Amana kwa ajili ya utekelezaji wa miradi iliyouwepo na hivyo kufanya fedha za maendeleo kuwa shilingi **947,722,663,252.62**

42. **Mheshimiwa Spika**, katika fedha hizo miradi iliopewa fedha ni ununuzi wa ndege, ukarabati wa reli ya Tanga-Arusha jumla ya **shilingi milioni 6,000.00**, ukarabati na ujenzi wa meli katika maziwa jumla ya **shilingi milioni 3,068.61** na ununuzi wa vifaa vyta hali ya hewa **shilingi milioni 6,084.98**

43. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa ni muda mwafaka sasa tupange kulingana na uwezo wetu, kitendo cha kupanga kutumia shilingi trilioni 2.3 na tunapata shilingi bilioni 391.26 ni hadaa kubwa sana kwa Bunge na wananchi. Je tutaendelea kufanya hadaa za namna hii hadi lini?

i. **Usafiri na Uchukuzi kwa njia ya Anga.**

a. Udhibiti wa Usalama wa Usafiri wa Anga-TCAA unahusisha ukaguzi wa viwanja vyta ndege ili vikidhi ubora na usalama wa kimataifa kwa ndege na abiria. Hivyo mamlaka hii ndio muwajibikaji wa miundombinu yote ya kiusalama kama vile Rada za kuongozea ndege, mifumo ya uokozi pale inapotokea ajali au tukio lolote ambalo halikutarajiwa n.k.

b. **Huduma za viwanja vyta ndege-**

44. **Mheshimiwa Spika**, uboreshaji wa miundombinu ya viwanja ili kuongeza ushindani na kupunguza garama za usafiri wa anga hapa nchini. Huduma zinazotolewa katika viwanja vyta ndege ni pamoja na mizigo (Cargo handling), wasafiri (Passengers handling), huduma ya chakula (Catering), mifumo wa kukata tiketi (Booking system) na kazi nytingine.

45. **Mheshimiwa Spika**, fursa zingine katika kuhakikisha huduma za viwanja vyetu vinakuwa shindani ni pamoja na kuhakikisha huduma za fedha zinapatikana kwa muda wote,

ujenzi wa "shopping malls" kwenye maeneo jirani na viwanja vyetu nya ndege sambamba na kuwa na mahotel ya kisasa kwa ajili ya wasafiri/abiria ambao wanakuja au kuondoka hapa kwetu kutokea mikoa mbalimbali. Hoja hapa ni je tuna mipango hiyo au tunaboresha viwanja tu bila kuwaboreshea huduma zingine ambazo zitatoa ajira za kudumu kwa watanzania?

c. **Wakala wa ndege za Serikali(TGFA)**

46. **Mheshimiwa Spika**, wakala huyu ndiye mwenye jukumu la kusimamia na kuendesha ndege ambazo zinasafirisha viongozi wa kitaifa wa Serikali. Kwa mwaka wa fedha 2018/19 wakala ulikuwa na malengo ya kuimarisha na kuboresha huduma za usafiri wa anga kwa viongozi wakuu wa nchi kwa kuifanyia matengenezo ndege moja aina ya Fokker 50. Kwa mwaka wa fedha 2018/19 ilidhinishiwa na hadi Februari 2019 ilikwishapewa kiasi cha shilingi milioni 2,313.16

47. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa inaonesha kuwa wakala wa Ndege za Serikali(TGFA) ndio mwenye jukumu pia la kufanya mchakato mzima wa manunuzi ya ndege zote za Serikali. Na tukumbuke kwamba ndege zote ambazo zimenunuliwa katika kipindi cha Serikali ya awamu ya tano ni ndege za Serikali bali zimekodishwa kwa Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL) ili ifanye biashara zake. Hii ni kutokana na sababu kuwa Kampuni hiyo ilikuwa bado inadaiwa madeni makubwa na taasisi mbalimbali za nje kutokana na huduma ambazo taasisi hizo zilitoa kwa Kampuni yetu ya Ndege (ATCL) miaka ya nyuma.

48. **Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha huo mchakato mzima na manunuzi ya ndege zote zilizonunuliwa na Serikali umefanywa na Wakala wa Ndege za Serikali kwa kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

49. **Mheshimiwa Spika**, ni jambo la kustua kwamba kwa tangazo la Serikali-(Government Notice) namba 252 ya tarehe 8 Juni ya mwaka 2018, kuwa wakala huyo na majukumu yake yanahamishiwa Ofisi ya Rais Ikulu kutoka

Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Katika kutimiza majukumu yake kwa mwaka 2019 wakala inatakiwa kutimiza yafuatayo:

- i. Kusimamia mikataba ya ukodishwaji wa ndege kwa kampuni ya ndege ya Taifa(ATCL);
- ii. Kufanya matengenezo na ununuzi wa vipuri vyta ndege za Serikali- Maana yake ni ndege zote zilizonunuliwa katika awamu ya tano;
- iii. Kufanya ukarabati wa karakana ya ndege za Serikali;
- iv. Kulipia gharama za bima za ndege;
- v. Kugharamia uendeshaji wa ofisi na kulipia gharama za mafuta ya ndege.

50. Mheshimiwa Spika, kwa kila kazi zilizotajwa ambazo kwa njia moja au nyingine zimehamia lkulu, ni sawa na kabisa na kile kilichokuwa kinatoka kwenye suala la IPTL wakati wa kununua mafuta ya mitambo ambapo TANESCO haikuwa na sauti bali Wizara ndiyo ilikuwa imeshika hatamu, na kilichokuwa kinatoka kwenye hilo kila mtu anafahamu.

51. Mheshimiwa Spika, katika "Corporate Strategic Plan" ya ATCL kuna kitu kinaitwa Kilimanjaro Maintenance Facility (KIMAF) na kimetengewa budget na katika majukumu ya TGFA ni pamoja na kufanya ukarabati wa karakana ya ndege za Serikali ambazo pia ni pamoja na ndege mpya za ATCL.

52. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaiasa Serikali kuangalia kwa makini uamuzi unaofanywa na Serikali wa kuhamisha wakala huu kutoka Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ni jambo la hatari sana kwa matumizi ya hela za walipa kodi.

i. **Huduma za Usafiri wa anga- ATCL**

53. **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa taarifa ilivyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya PIC - kuhusu ATCL alisema kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka 2014/2015 ATCL ilipata hasara ya shilingi bilioni 94.3 na mwaka 2015/2016 ilipata hasara ya shilingi bilioni 109.2 na mwaka 2016/2017 ilipata hasara ya shilingi bilioni 113.7 na huo ndio ukweli Wakati huo huo, Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL, Ladislaus Matindi akizungumza wakati akijadiliana na mawakala wa shirika hilo, alisema kuwa mapato ya kampuni hiyo yalipanda kutoka shilingi milioni 700 kwa mwaka 2016 hadi kufikia shilingi bilioni 4.5 kwa mwaka 2017. Pia, hasara zimepungua kutoka shilingi bilioni 14 mwaka 2016 hadi shilingi bilioni 4.3.

54. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kufahamu hilo ongezeko la mapato kama liliyotolewa na Mheshimiwa Waziri limefikia hapo kwa kutumia gharama kiasi gani? Ni muhimu Bunge likawa na taarifa sahihi kuhusu utendaji wa Kampuni hiyo.

55. **Mheshimiwa Spika**, kwa kawaida tunaposema mapato maana yake ni fedha zote zilizokusanya bila ya kuangalia gharama zilizotumika ni kiasi gani katika makusanyo hayo. Hivyo basi kwa msingi huo ni dhahiri kuwa tutaendelea kuwaaminisha watanzania kuwa tunafanya vizuri kwa mapato kuongezeka lakini bila ya kuangalia mapato hayo yako kwenye mizania na matumizi au gharama za uendeshaji?

56. **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa taarifa ya PIC ni kwamba "Katika kipindi hicho kilichofanyiwa kazi na Kamati ya Bunge matumizi yaliongezeka kwa kiwango cha juu kulinganisha na mapato yaliyopatikana na hali hiyo ikiendelea hivyo uhai wa kampuni hiyo utakuwa shakani. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itakapokuwa inatoa taarifa kuhusu utendaji wa shirika hilo iwe wazi zaidi kwa kulinganisha mapato na gharama za uendeshaji ili tupime kama tuko kwenye upande wa faida au hasara katika uendeshaji wa shirika hilo.

57. Mheshimiwa Spika, ni bahati mbaya sana kuwa ATCL inao watendaji wenyewe ujuzi na uzoefu lakini inaingiliwa sana kiutendaji na maamuzi kutoka juu ambayo yanatolewa na watu wasiokuwa na utaalam wa biashara ya uendeshaji usafiri wa anga na pia wasiokuwa na utaalam wa kifundii kuhusu ndege na mwisho wa siku wataalam wetu wanashindwa kuwa huru kutumia utaalam wao.

58. Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba tunapozungumzia mwenendo wa shirika letu la ndege ni kwa maslahi mapana ya nchi yetu kuona shirika linafanya kazi zake kwa weledi na hatimae kutengeneza faida, Kambi Rasmi Bungeni kwa masikitiko makubwa Serikali ya awamu ya tano imeweka pamba masikioni na kupuua ushauri tunaoendelea kuutoa kuhusiana na Shirika la ATCL. Ukipitia ripoti ya Kamati ya PIC ya mwezi Januari imesema wazi kuwa kukosekana sera madhubuti na mpango mkakati ndio kunapelekea utendaji usioridhisha kwa Shirika la ATCL, aidha ukipitia ripoti ya CAG iliyowasilishwa Bungeni hivi karibuni inaonesha mionganoni mwa makapuni yaliyo katika hali mbaya kifedha ni ATCL na TTCL (ukurasa (19 au 21 ripoti ya PIC) Tulisema bajeti ya 2015/16 vilevile 20116/17 na pia 2017/18 shirika linahitaji wataalamu huru kusimamia shirika ili liendeshwe kwa mafanikio na faida maana yake hata ununuwaji wa ndege ungefanyika kwa mujibu wa mahitaji.

59. Mheshimiwa Spika, ukichukua mfano wa Kenya Airways miaka mitatu mfululizo inaripoti hasara 2015/16 ya \$252 milioni, 6.1 billion Kenya shillings 2017 na mwaka 2018 hasara ikawa 4.035 billion shillings, vile vile Qatar mwaka 2018 nao wameripoti hasara ya \$69 milioni miezi 12 iliyopita hii inatokana na ukweli kwamba ushindani ni mkubwa katika biashara, Emirate Airways na Ethiopian Airline wameripoti faida 2018 lakini imeshuka ukilinganisha na mwaka 2017.

60. Mheshimiwa Spika, wahenga wanasema KAWIYA UFIGE KULIKO KUHARAKIA UKAISHIA NJIANI. Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuishauri Serikali kutafakari upya kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kutafutwa wataalamu huru kulisimamia shirika letu ili liweze kujiedhesa kwa faida hasa

ukuzingatia tayari ndege zishanunuliwa tusiendelee kufanya makosa na kulibebesha taifa hasara kwani gharama zote za uendeshaji zinatoka Serikalini hii inapelekea huduma nyingi za kijamii kusimama kwa sababu fedha nyingi zinahudumia ATCL ukizingatia kuwa hatukuwa na uhitaji wa kununua Boeing 787-8 Dreamliner kwa sasa.

ii. **Usafiri na usafirishaji wa Reli**

61. **Mheshimiwa Spika**, kwa Tanzania tuna mashirika mawili ambayo yanatoa huduma za usafiri na usafirishaji kwa njia ya Reli, mashirika hayo ni Shirika la Reli Tanzania (TRL) na Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) na pia kwa maeneo mengine ambayo reli ilianzia kule na sasa hivi maeneo hayo yako kwenye mkakati wa kufufuliwa upya ili yafanye kazi .

62. **Mheshimiwa Spika**, historia ya Reli imeanzia mbali sana na hii ndiyo historia yenye;

63. **Mheshimiwa Spika**, reli ya kwanza kabisa kujengwa hapa nchini ni ile ya Usambara (Usambara-Railway). Reli hii ilijengwa baada ya kuanzishwa kwa kampuni moja ya reli mwaka 1891 ikiwa na dhamira ya kuiunganisha bandari ya Tanga katika Bahari ya Hindi na Ziwa Nyanza (Ziwa Victoria) kupitia kusini mwa Milima ya Usambara. Wahusika walipanga kwamba reli hiyo iwe na geji 1,000mm (futi 3 na inchi 3 3D 8). Tangu Juni 1893 ujenzi wa reli hiyo ukaendelea kuanzia Tanga kwenda bara.

64. **Mheshimiwa Spika**, baada ya hapo reli hiyo ikawa chini ya Shirika la Reli la Kijerumanii liliolahamika zaidi kama Ostafrikanische Eisenbahngesellschaft (East African Railway Cooperation), kampuni ambayo ilikuwa imeundwa ili kujenga na kuendesha Reli ya Kati ya Tanganyika (Zentralbahn) kutoka Dar es Salaam hadi Kigoma. Kati ya Pongwe na Ngommi kwenye Reli ya Usambara kulikuwa na michepuko miwili (double hairpin turn). Mnamo Septemba 26, 1911 reli hiyo ilifika Moshi kwenye Mlima Kilimanjaro ukiwa ni umbali wa kilometra 351.4 kutoka Bandari ya Tanga. Safari kwenye njia hiyo zilianza

Oktoba 4, 1911 na uzinduzi rasmi ulifanyika Februari 7, 1912. Mwaka 1914 treni moja ilifanya safari kati ya Tanga na Buiko na kurejea kila siku na kwa siku mbili kwa wiki safari zilifanyika kati ya Tanga na Moshi.

65. Mheshimiwa Spika, Kuanzia Juni 4, 1912 – Mei 12, 1913 reli hiyo ikaitwa Reli ya Kaskazini (Nordbahn - Northern Railway) kwa kipindi kifupi. Mipango ya kuiendeleza reli hiyo hadi Arusha ilikuwa inafanya na fedha tayari zilikuwa zimetolewa lakini haikuweza kujengwa kutokana na kuanza kwa Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia. Waingereza walipoanza kuitawala Tanganyika wakaamua kuiunganisha Reli ya Usambara kati ya Moshi na Voi na ile Reli ya Uganda nchini Kenya na kuiongezea mwaka 1929 hadi katika kituo chake cha sasa cha Arusha².

66. Mheshimiwa Spika, reli nyingine kujengwa ni Reli ya Kusini iliyokuwa na urefu wa kilometra 275 ikitoka Masasi, Lukuledi, Nachingwea Nangana, Mkware, Mtama, Mtua Narunyu Mashamba ya Mkone, Mkwaya, Mingoyo, Lindi, Kilindu, Nyamgamara, Mpapua, Namgongoni, Mikindani, Ufukoni hadi bandari ya Mtwara. Pia ilikuwa na mchepuo mwininge wa kwenda Lindi wa urefu wa kilometra 18 uliojengwa mwaka 1921 kwenye mashamba ya Mkunge ya Narunyu. Sababu kubwa ya ujenzi wa Reli hiyo ilikuwa ni mradi mkubwa wa kilimo cha Karanga (*Tanganyika Groundnut Scheme*), uliokuwa ukiendeshwa Nachingwea, hivyo kurahisisha usafirishaji wa bidhaa kutoka kiwandani hadi bandarini Mtwara ikalazimu uwepo wa usafiri wenye uhakika wa Reli³.

67. Mheshimiwa Spika, Kumbukumbu zinaonesha kuwa train hiyo iliyokuwa inafanya kazi kati ya Masasi na Mtwara hadi mwaka 1949 ilikuwa inafanya kazi zake.

² <http://issamteki.blogspot.com/2014/03/hii-ndiyo-reli-ya-kwanza-kujengwa.html>

³HISTORIA YA MTWARA - Na Cosmas J. Pahalah)

68. Mheshimiwa Spika, kutokana na matatizo mbalimbali ya uzalishaji wa Mradi wa Karanga, bahati mbaya Mwaka mmoja baada ya kupata uhuru Reli ya Kusini (Southern Line) Masasi hadi Mtwara Bandarini iling'olewa kutokana na kuamini kuwa reli ilikuwa ni mradi isyo na tija kwa wananchi na taifa kwa ujumla (white elephant). Leo hii serikali inafikiria kujenga reli hukohuko Kusini kwenye Ukanda wa Kusini, "The Mtwara Development Corridor."

69. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema Tanzania itaendelea kuwa hapa tulipo kutokana na ukweli kwamba viongozi wetu kutojipa muda wa kufanya tafakuri kwa miradi ambayo imeanzishwa na watangulizi wao na kuona walikuwa wanalenga nini hasa katika uanzishwaji wa miradi hiyo.

70. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imetoa historia hiyo kuwakumbusha kuwa Reli mbali ya kubeba abiria lakini inatakiwa kuwa na jicho la kibashara ambalo ndilo linafanya Reli iwe endelevu, sasa ujenzi wa SGR kwenda Mwanza kabla ya kuwahi kuipeleka Kigoma ili kubeba mzigo mkubwa wa madini ya Copper kutoka DRC na pia kuangalia ni jinsi gani Mradi wa Nickel kule Kabanga ungeongeza manufaa kwa Shirika la Reli katika kujidesha kwa faida. Kama hayo hayakuangaliwa kwa makini, mradi huu unaweza kuwa ni "white Elephant". Tukumbuke kuwa Rais mpya wa DRC tayari amekwishaingia makubaliano na Rais Uhuru Kenyatta ili kutumia Bandari ya Mombasa na Reli yao, kwa maana kuwa ili kitu "coalition of the Willing" tayari DRC imeishaingizwa.

71. Mheshimiwa Spika, katika bajeti iliyotengwa kwenye Sekta ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2019/20 kwa miradi ya Maendeleo ya **shilingi 3,543,722,242,895.00** kati ya fedha hizo shilingi **2,947,722,242,895.00** sawa na **asilimia 81.22** ya fedha zote za bajeti ya maendeleo ni kwa ajili kuimarisha reli hapa nchini. Hili ni jambo zuri kama fedha hizo zitatolewa, kwani kumbukumbu kwa mwaka 2018/19 ambapo kati ya triliioni 2.3 zilitolewa asilimia 17 tu.

- iii. **Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA)**
72. **Mheshimiwa Spika**, Tanzania imebahatika kuwa na ukanda mrefu wa bahari kuu na pia kuwa nchi inayoweza kuhudumia mataifa ambayo kijigrafia hajizapakan na bahari na hivyo kuwa kitovu cha biashara katika ukanda huu kama ilivyo Dubai, Singapore na Hongkong kwani imepakana na nchi sita zisizokuwa na bandari.
73. **Mheshimiwa Spika**, Bandari ya Dar es Salaam ambayo hapa kwetu ndiyo kubwa kuliko zote, imeendelea kuwa ya mwisho ikilinganishwa na bandari za ukanda huu kama vile Durban, Beira na Mombasa.
74. **Mheshimiwa Spika**, ushindani wa Mamlaka ya Bandari kwa bandari tajwa hapo juu hautakuwepo kwa sasa kutokana na sababu kubwa kwamba, majukumu ambayo yanatakiwa kufanywa na bandari kama mamlaka sasa hivi yatakuwa yanafanywa na TASAC kama shipping agent, na hivyo kuiacha mamlaka kuwa na kazi za kupokea na kupakua mizigo kama ilivyo TICTS.
75. **Mheshimiwa Spika**, sheria namba 17 ya mwaka 2004 (The Ports Act No17) imetaja bandari zilizopo kwenye mwambao wa Bahari ya Hindi Dar es salaam, Tanga, Mtwara, Kilwa Kivinje, Mkindani, Bagamoyo, Kwale, Pangani, Mafia, na Songosongo. Pia sheria hiyo imetaja bandari zingine 24 zilizoko Ziwa Victoria, 19 katika Ziwa Tanganyika na 11 katika Ziwa Nyasa.
76. **Mheshimiwa Spika**, sheria hiyo haitaji bandari 6 za mwambao wa bahari ya Hindi, mfano Kisiju, Nyamisati, Mwambani, Chongolani Kilwa Kisiwani na Rukirya, 7 Ziwa Victoria 6 – Ziwa Tanganyika na 4 – Ziwa Nyasa lakini pia zipo jumla ya bandari zisizo rasmi (bubu) jumla la 312. Lakini ndizo zinazopewa kipaumbele na Mamlaka ya Bandari katika kuziendezea.
77. **Mheshimiwa Spika**, bandari hizi bubu zinaendelea kutumika na serikali haipati mapato Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka TPA kuzirasimisha bandari hizi bubu zifanye

kazi kulingana na kanuni na sheria ili kuongeza ukusanyaji wa mapato na pia masuala ya ulinzi na usalama wa nchi. Aidha, TPA ina mpango gani wa kuziendeleza Bandari hizo ili ziweze kufanyakazi vyema na kuongeza mzunguko wa biashara katika maeneo husika?

78. Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Kambi ya Upinzani Bungeni imekuwa inapigia kelele suala la muda mrefu wa kontena kukaa bandarini (Dwell time). Katika bandari ya Dar es salaam kwa mujibu wa taarifa zilizopo muda huo umeongezeka kutoka wastani wa siku 9.8 mwaka 2015/2016 hadi wastani wa siku 10.5 mwaka 2017/2018. Hali hii bado inachangia sana wafanyabiashara wengi kuondoa mizigo yao toka bandari ya Dar es Salaam na kwenda bandari za nchi za jirani

79. Mheshimiwa Spika, hali hii pia inachangiwa sana na uwezo mdogo wa usaferishaji kwa njia ya reli. Aidha, kuwepo kwa tozo ya kuhifadhi shehema ("Storage chargers") inayotozwa na TPA kwa upande mmoja na warehouse rent" inayotozwa na TRA kwa shehena ileile kumeendelea pia kuwafanya wasafirishaji kukimbia bandarini ya Dar es Salaam kwa utaratibu uliopo sasa mzigoto unaruhusiwa kutunzwa bandarini kwa siku 21 tu na baada ya hapo kuwekwa chini ya idara ya fedha kwa ajili ya kupigwa mnada. Ni katika muda huu "Customs warehouse rent" inaanza kutozwa. Bandari zingine shindani katika ukanda huo haitozi kabisa hii na hivyo kuwavutia wasafirishaji.

80. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuharakisha ujenzi wa bandari kavu nje ya mji (Ubungo (ICD)

81. Mheshimiwa Spika, mpango wa uboreshaji wa bandari ya Dar es salaam unatekelezwa kwa kupitia mradi mkubwa ujulikanao kama Dar es salaam Maritime Gateway Project (DMGP) unaotekelizwa kwa gharama ya Dola za Kimarekani 421 milioni. Katika gharama hizo 82% ni mkopo hata Benki ya Dunia, 2.8% ni msaada toka DFID na 15.2% ni mapato yetu ya ndani.

- 82.** **Mheshimiwa Spika**, changamoto kubwa ya mradi huu ni ulipaji wa kodi ya ongezeko la thamani (Value Added Tax)
- 83.** **Mheshimiwa Spika**, katika makubaliano yaliyowekwa mradi huu umesamehewa kodi hii utaratibu wa kupatia msamaha huo una mlolongo mrefu sana kiasi cha kupunguza kiasi ya Ujenzi. KRUB inataka serikali kupitia Wizara ya Fedha kuondoa urasimu uliokithiri ili kuwawezesha kumaliza kazi kwa muda.
- 84.** **Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulipitia hatua zote za upembizi yakinifu kwa gharama kubwa uliohusisha makampuni makubwa ya nje (M/S Inros Lacker- ya Ujerumanji) ambayo ilisaini Mkataba na TPA Juni 21, 2017 kwa gharama ya Euro 2.9 milioni.
- 85.** **Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa gati la kushushia meli za magari (RoRo Berth) umekumbana na tatizo la udongo dhaifu (soft soil). Hali hii imechelewesha ujenzi kutokukamilika kwa muda na pia kuongeza gharama ya ujenzi. KRUB inataka kupewa maelezo ni kwa nini aliyefanya upembizi yakinifu hakuona udhaifu huu wa udongo na wasimamizi wetu wa TPA nafasi yao ilikuwa nini?
- 86.** **Mheshimiwa Spika**, ukiangalia Sheria ya Mamlaka ya Bandari kifungu cha 25(c),((j) kuhusu kazi za Mamlaka ukiangalia kazi za TASAC na kwenye vifungu vya 7(1)(c)na kuhusu exclusive mandate ya kufanya ship Tallying service, pia vifungu vya 10, 11 na 12 kuhusu; "**Regulation of Maritime Environment, Safety and Security na kile cha Regulation of Maritime Transport Services**". Ukiangalia mengi ya majukumu haya yalikuwa ynafanywa na Mamlaka ya Bandari, sasa yamehamishwa kwenda TASAC.
- 87.** **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza kwa mazingira haya ya kisheria Mamlaka ya Bandari itawezaje kuwa shindani zaidi ya kuwa chombo cha kusubiri kupokea mizigo ya kupakia na kupakua kutoka kwenye meli? Pia katika mazingira ambayo wafanyakazi wanaidai mamlaka malimbikizo ya mishahara na stahili zingine kwa

miaka miwili na wafanyakazi zaidi ya robo wanafanyakazi kwa miaka minne lakini hawajapewa barua za kuthibitishwa kazini. Ari ya kuifanya mamlaka iwe shindani na Bandari zingine katika Ukanda wa Bahari ya Hindi itatoka wapi?

iv. Ujenzi wa gati 13 na 14

88. Mheshimiwa Spika, katika hotuba zetu za nyuma tuliomba kupatiwa maelezo juu ya ushauri tulioutoa sambamba na ule wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu ujenzi wa gati hizo, nanukuu;

"Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa katika Bunge la 10 Mkutano wa Saba wa Bunge hilo kulikuwa na majadiliano ya kina kuhusiana na ujenzi wa ghati hizo, na Bunge liliagiza kuwa mradi huu utekelezwe kwa kutumia mkopo kutoka Benki ya China kama ilivyopendekezwa na Mamlaka ya Bandari.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitaka kupata majibu juu ya masuala yafuatayo:

a. Mchakato wa ujenzi wa Ghati 13 & 14 umefikia wapi mpaka sasa?

b. Baada ya kusitishwa kwa mchakato na mkataba wa awali ni hatua gani zimechukuliwa na serikali dhidi ya waliohusika na mchakato ambao ullikiuka sheria za nchi.

c. Ni lini ujenzi wa Ghati hizo utakamilika ili kuweza kuendana na mpango mkuu wa bandari nchini?

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kufanya hivyo, serikali haikuona nia thabiti ya kutekeleza mradi huo. Aidha miaka mitatu baadaye Kamati ya Bunge lako tukufu nayo inaona kuna tija kwa serikali kujenga gati namba 13 & 14 kama mkakati wa kuliongezea taifa mapato. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasilitiza ushauri huo kama ilivyoshauri katika bajeti ya mwaka 2013/2014, ushauri ambao sasa Kamati ya Bunge ya Miundombinu pia imeendelea kushauri katika vikao vyao na TPA."

89. **Mheshimiwa Spika**, ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri Ujenzi katika Hotuba yake mwaka wa fedha 2016/17, wakati anasoma utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2015/16 kuhusu ujenzi wa Gati Bandarini alisema kuwa, nanukuu;
- "146. Mheshimiwa Spika, kazi ya uboreshaji na uongezaji wa kina katika gati Na. 1 hadi 7 na ujenzi wa gati jipya la kushushia magari eneo la Gerezani Creek katika bandari ya Dar es salaam kwa ufadhili wa Benki ya Dunia, TMEA na DfID zinaendelea. Nyaraka za zabuni kwa hatua ya pili na ya mwisho ya kupata mkandarasi wa kazi ya ujenzi zilitolewa Machi, 2016 kwa Wakandarasi sita waliofuzu katika hatua ya kwanza ya zabuni, na zinatarajiwa kufunguliwa Juni, 2016. Aidha, kampuni ya M/S Inros Lackner Ag kutoka Ujerumani tayari imeteuliwa kuwa Msimamizi wa kazi za ujenzi (Consultant for Works Supervision).*
147. *Mheshimiwa Spika, Mkataba kati ya TPA na Mshauri Mwelekezi wa kufanya Upembuzi Yakinifu wa namna bora ya kupanua na kuchimba ili kuongeza kina cha lango la kuingilia meli na eneo la kugeuzia meli (entrance channel and turning basin) ulisainiwa Desemba, 2015. Mshauri Mwelekezi alianza kazi Januari, 2016 na atakamilisha Julai, 2016. Aidha, kazi za kupanua, kuchimba na kuongeza kina zinatarajiwa kuanza Oktoba, 2016 na kukamilika Novemba, 2017.*
148. *Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Mamlaka ilipanga kujenga gati Na. 13 na 14 kwa kushirikisha sekta binafsi kwa utaratibu wa Sanifu, Jenga, Endesha na Rejesha (Design, Build, Operate and Transfer - DBOT). Hata hivyo, kazi hiyo haikutekelezwa kutokana na kutojamiliika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa awali utakaoonesha hali halisi ya mradi na gharama zake. Ujenzi wa gati hizi unatarajiwa kuanza mwaka 2017 kwa ufadhili wa Benki ya Dunia, TMEA na DfID baada ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali kukamilika. Ni matarajio yetu kuwa sekta binafsiitawekeza katika utoaji huduma na ujenzi wa maghala katika magati hayo."*
90. **Mheshimiwa Spika**, ukisoma vyema ni kwamba kazi ilitakiwa kuanza mwaka 2017, sasa ni mwaka 2019. Kambi

Rasmi ya Upinzani tunasisitiza kupatiwa majibu kama tulivyoomba katika hotuba yetu ya mwaka 2016/17 kuhusiana na ujenzi wa Gati 13 na 14.

V. SEKTA YA MAWASILIANO

91. Mheshimiwa Spika, Data center (NIDC) ni kituo cha kisasa kabisa na kimejengwa kwa fedha nyingi. Kituo hiki pia ni chanzo cha mapato ya serikali kikitumika kikamilifu. Kuna taarifa kwamba kuwa ni makampuni /mashirika ya umma 56 tu na binafsi 23 tu ndiyo inayohifadhi data zao huko na kuingiza serikali kiasi cha shilingi bilioni 1.56 kwa mwaka.

92. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri serikali kikitangaza kituo hiki ili makampuni mengi watunze data zao huko.

93. Mheshimiwa Spika, serikali imetoa fedha nyingi kwa makampuni ya simu kuititia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) makampuni yалиyonufaika sana na uwekezaji huu ni Halotel, Vodacom na TTCL. Madhumuni ya mfuko huo ni kuwafikishia huduma ya mawasiliano wananchi kwenye maeneo ya nchi ambayo hayana mvuto wa kibiashara pia.

VI. HITIMISHO

94. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, miundombinu kwa kiwango kikubwa imekuwa ikichukua fedha nyingi kwenye bajeti ya Taifa :

Na kwa kuwa; baadhi ya makampuni yanayojihusisha na uwekezaji wa miundombinu hiyo ni kutoka nje;

Na kwa kuwa uwekezaji mzuri na wa muda mrefu kwa nchi zote zilizoendelea ulifanyika kwenye elimu au rasilimali watu;

Na kwa kuwa; sisi watanzania tumebakia kuwa muangaliaji na sio mshiriki katika uwekezaji huo ipasavyo,

Hivyo basi, , Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri changamoto zote tajwa zifanyiwe kazi kwa masilahi mapana ya Taifa letu.

95. Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

.....
James F. Mbatia, (Mb)

**MSEMAJI MKUU- KAMBI RASMI YA UPINZANI-WIZARA YA
UJENZI,
UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

09.05.2019

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaanza uchangiaji wetu, sasa hivi saa sita kasoro dakika tisa, tunaanza na Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mheshimiwa Richard Ndasa, Mheshimiwa Ahmed Shabiby na Mheshimiwa Salome Makamba wajiaandae.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hotuba iliyoko mbele ya Bunge letu Tukufu. Kwanza nitoe pongezi za dhati kwa Waziri mwenye dhamana pamoja na Manaibu Waziri kwa kazi kubwa na nzuri sana wanayoifanya. Pia pongezi hizi ziende kwa Watendaji wa Wizara na Mashirika yote yaliyoko chini ya Wizara hii kwa maana kwamba tunajua bila wao utekelezaji wa llani ya Chama ni jambo ambalo ni gumu. Kwa hiyo tunatoa pongezi na jukumu letu sasa ni kushauri kwa yale maeneo ambayo tunaona kwamba yanaweza yakawasaidia kufanya kazi yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipekee kabisa naomba kwanza nitoe pongezi za dhati kwa Meneja wa *TANROAD* Mkoa wa Tanga, Injania Ndumbaro kwa kazi kubwa sana anayoifanya. Mkoa wa Tanga hususan Wilaya ya Lushoto, Korogwe na Muheza ni za milima, kwa hiyo mara nyingi sana barabara zinasumbua hasa nyakati za mvua, lakini injinia huyo amekuwa halali na kuhakikisha kwamba barabara hizi wakati wote zinapitika. Mvua za mwaka jana zilileta mafuriko makubwa sana katika eneo la Lukozi lakini ndani ya kipindi kifupi aliweza kutujengea daraja pale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, lakini pia nitoe masikitiko kidogo kwa watendaji wa *TANROAD* hasa ngazi ya Taifa kwa sababu barabara yetu ya kutoka Mlalo kwenda Lushoto, lakini pia kutoka Mlalo kwenda Mng'aro hadi Maramba kule Mkkinga kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo tumekuwa tukipanga katika vipaumbele vyetu kwenye *RCC* kwamba ifanyiwe upembuzi yakinifu, lakini pia ifanyiwe na usanifu wa kina. Mara zote inapofika kwenye meza ya Watendaji wa Kitaifa kwa maana ya Injinia Mfugale, walikuwa hawaipangji fedha. Kwa hiyo niombe sana kwamba barabara hii ni muhimu kwa sababu inaelekeza eneo muhimu sana la kiuchumi hasa kwa mazao ya mbogamboga na matunda ambaao ndiyo uzalishaji mkubwa katika eneo letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naomba nitoe mchango wangu katika eneo zima la usafirishaji hasa usafirishaji wa anga. Kwanza kabisa kipekee nimpongeze sana Mtendaji Mkuu wa *ATCL* ndugu yangu Ladislaus Matindi amekuwa akifanya kazi kubwa sana na kazi nzuri ya kuhakikisha kwamba shirika hili linasimama. Pongezi hizi pia zimuendee Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa ununuzi wa ndege hizi nane ambazo kwa kweli zinafanya vizuri katika soko la ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunataraji kuiona ikifanya vizuri zaidi *ATCL* katika soko la nje kwa maana kushiriki katika ushindani. Tumeona hapa yapo maeneo kadhaa wameanzisha safari lakini bado tunataka kuiona *ATCL* ikifanya kazi vizuri, itafanyaje vizuri; kwanza ni lazima tusiweke *ATCL* kwenye mikono ya Wizara peke yake, *ATCL* lazima tuichukue kama ni mradi wa kimkakati wa nchi, tuone kama nchi tunataka kwenda wapi na shirika hili la ndege. Utaona wenzetu wa mashirika kama ya Turkish ya Uturuki, *Rwanda Air* na Qatar ya Doha kule wameyaweka kama ya kimkakati ni ya nchi nzima inayabeba haya mashirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ukifika pale Kigali leo, wanaitangaza Kigali kama kituo cha kibashara cha

mikutano, kwa hiyo nchi mbalimbali tunaona kabisa katika *forum* mbalimbali za kimataifa wanafanya mikutano Kigali lakini kwa kupitia *Rwanda Air*. Ukipika Doha pale Qatar ni mji mkubwa sana wa kibashara sasa hivi, lakini umechagizwa kabisa na uwepo wa Qatar Air, lakini pia ukipika kule Istanbul, Uturuki utaona kabisa sasa hivi imekuwa ni kituo kikubwa cha kibashara kati ya Asia na Ulaya kupitia hili Shirika la Ndege la Turkish.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yanafanikiwa tu kwa sababu wenzetu hawa wameweza kutoa ruzuku kwenye haya mashirika kwa sababu yamechukuliwa kama ni miradi ya kimkakati ya nchi na hayajaachiwa kwenye Wizara kama ambavyo tunafanya sisi. Utaona kwamba gharama kama za *landing* na *navigation charges* ziko chini au wamezitoa kabisa kwamba yanaruhusu sasa biashara kufanyika kwa wepesi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo *ATCL* ni kweli wamenunua ndege nane, lakini mpaka sasa hivi tunavyozungumza hawana hata ndege moja ya kubeba mizigo. Sasa tunapozungumza Tanzania ya viwanda ambayo pia tuna mazao ambayo tunataka tuyapeleke kwenye masoko ya kimataifa, bila kuwa na ndege za kubeba mizigo jambo hili litakuwa ni gumu. Kwa mfano, tu hapa tuna viwanda zaidi ya kumi na nne katika Kanda ya Ziwa ambavyo vinachakata minofu ya samaki, lakini kwa masikitiko makubwa viwanda vyote hivi vinasafirisha minofu kwenda uwanja wa Nairobi ama uwanja wa Entebbe kiasi kwamba sisi hatuonekani kama tuna-*export* hii samaki kutoka katika eneo letu. Sababu kubwa ni kwamba hatuna viwanja, hatuna ndege za kubeba mizingo lakini pia viwanja vyetu vya ndege gharama za kutua ndege za mizigo ni kubwa sana kiasi ndege hazivutiki kuja kutua katika viwanja vyetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona hata juzi hapa Waheshimiwa Wabunge wanalamika kwamba maparachichi yanapelekwa Kenya halafu Kenya ndiyo wanayapeleka kwenda Uchina. Hili tunaweza tu tukaliepuka kama tutakuwa na gharama rafiki kwenye viwanja vyetu,

lakini pia tutakuwa na ndege zetu ambazo ni za mizigo, ili sasa hata hivi viwanja tunavyoendelea kupanua huko Songwe, huko Mwanza na kadhalika viweze kutumika kama sehemu mojawapo ya kuchochea uchumi wa nchi yetu na ndiyo maana katika hatua ya awali nilizungumza kwamba bila kuifanya ATCL kuwa ni mkakati wa kitaifa tukaiacha peke yake kwenye Wizara hii moja, ile tija ambayo tunaikusudia itakuwa haijafanikiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumza, ni suala zima la kupanua Bandari ya Tanga. Tumeona katika kitabu, ukurasa wa 117, kuna upanuzi wa Bandani ya Tanga. Hii ni bandari muhimu sana kimkakati na ndiyo maana nadhani hata Wakoloni wa Kijerumani walianza kujenga bandari Tanga kabla ya maeneo mengine na hata reli ya Tanga nadhani ndiyo reli ya kwanza kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe sana Serikali kwamba ni muhimu sana bandari hii iboreshwe kwa wakati. Pia itasaidia kwa sabau sasa hivi tumeona hata wenzetu Wazanzibar kuna baadhi ya bidhaa wanazipitishia Mombasa lakini tukiboresha Bandari ya Tanga kutakuwa na uwezo mkubwa wa kupitisha mizigo hata ya Zanzibar. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ni ukarabati wa reli ya Tanga – Moshi - Arusha - Musoma. Hili nalo tunamshukuru sana ndugu yetu Kadogosa, jitihada zimeanza lakini jitihada hizi zisiishie kufufua reli hii ya zamani. Tunatamani na sisi pia tuone *SGR*ikiwa katika maeneo haya, inachukua mkondo huo wa reli za kimataifa ili kuboresha sasa huduma za usafiri na kuunganisha usafiri wa reli na usafiri huu wa majini. Hii ni kwa sababu kuna mizigo mingi ambayo inaenda nchi jirani ikiwemo Uganda na Kenya ikiweza kupita katika bandari hii na kupitia reli kwenda mpaka Musoma inaweza ikasaidia hata sisi kama nchi pia kuwa na mkakati wa kushindana katika soko la Sudani Kusini kwa kupitia Bandari ya Tanga na reli hii ya kwenda Moshi – Arusha - Musoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho lakini siyo kwa umuhimu ni suala zima la mawasiliano. Ndugu yangu Mheshimiwa Eng. Nditiye tumezungumza mara kadhaa kwamba kuna maeneo katika Jimbo la Mlalo bado mawasiliano ya simu hayapatikani. Kwa hiyo, naomba sana Wizara ihakikishe yale maeneo mahsusili niliyowaandikia yanafikiwa na huduma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ndassa, Mheshimiwa Shabiby na Mheshimiwa Salome wajialdae.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi hii lakini niseme tu kwamba naunga mkono bajeti ya Wizara hii nyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu. Nimpongeze sana *Engineer* Mfugale kwa kazi nzuri sana anayoifanya. Tunaweza tukamuita huyu ni gwiji wa barabara na madaraja ya juu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niwapongeze sana ma-*Engineer* wa mikoa yote nchini kwa sababu tumekuwa tukiona Mheshimiwa Rais akipita huko na huko akifungua barabara au akiweka mawe ya msingi. Bila hawa ma-*Engineer* nafikiri kazi hii isinge kuwa inafanyika vizuri.

Kwa hiyo, niwapongeze sana sana Mameneja wa *TANROADS* wa Mikoa yote Tanzania kwa kazi nzuri mnayofanya chini ya gwiji wa barabara ndugu *Engineer* Mfugale. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia *Engineer* wa Mkoa wangu, *Engineer* Luviga kwa kazi nzuri sana anayoifanya. Nimpongeze pia Kaimu *Engineer* wa Mkoa wa Dar es Salaam Julius Ngusa kwa kazi nzuri anazozifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu la kwanza linahusiana na ATCL. Tumwombe CEO wa ATCL, ikiwezekana, tumeshaleta maombi upande wa kwako, tuwe na ndege ya kutoka Dodoma kwenda Mwanza na Mwanza kuja Dodoma itasaidia sana Wabunge na watu wengine. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 28 Januari, 2016 niliuliza swali humu ndani na likajibwa na Serikali. Swali langu lilikuwa linasema hivi, je, ni lini barabara ya Magu – Bukwimba – Ngudu – Hungumalwa itajengwa kwa kiwango cha lami? Majibu ya Serikali yanasema: "Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 na 2015/2016, Serikali ilitenga jumla ya Sh.200,000,000 kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara yenye urefu wa kilometra 70 na taratibu za kumtafuta Mhandisi Mshauri zinaendelea. Baada ya kukamilika kwa usanifu na gharama za mradi huu kujulikana, Serikali itatafuta fedha za kuanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami". (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa 2014/2015, 2015/2016, 2016/2017, 2017/2018, 2018/2019 leo ni 2019/2020. Nataka nipate majibu ya Serikali, nimeona humu mmetenga Sh.440,000,000 kwa kilometra 10 sijui ni za nini, ni za changarawe au za nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Eng. Mfugale najua kabisa barabara hii unaifahamu vizuri sana umuhimu wake. Ili Mji wa Ngudu ufunguke, barabara hii inakwenda kuunga ile barabara ya lami ya kutokea Musoma, barabara hii ukiifungua inakwenda kuunga kwenye barabara inayotokea Mwanza kwenda Shinyanga. Kwa kufanya hivyo, utakuwa unapunguza msongamano wa mabasi ya kwenda Mwanza, mabasi yanayotoka Dar es Salaam kwenda Musoma badala yake yanapitia Hungumalwa kwenda Mara, ili tupunguze huu msongamano barabara hii ni muhimu. Mji huu wa Ngudu umedumaa kwa sababu hakuna miundombinu ya barabara. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Mfugale kwa utendaji wako mzuri mpaka unapewa daraja la *flyover*

(*Mfugale flyover*) sifa zote hizo, unashindwa kweli ka barabara haka ka kilometra 74, kweli? Bwana Mfugale, bee kamwene bee bwana Mfugale, kilometra 74. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri barabara hii iko kwenye Ilani ya Chama chetu. Barabara hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais alipokuja Ngudu wakati wa kampeni. Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alipokuja Ngudu, nafikiri wewe bwana Mfugali ulikuwepo, kama hukuwepo basi msimamizi wako aliquuwepo, Mheshimiwa Rais aliahidi lakini wakati huo Rais wetu wa sasa ndio aliwa Waziri wa Ujenzi. Sasa wazee na mimi mzee humu ndani hata ka heshima kadogo tu bwana Mfugale? Barabara hii ni muhimu sana naomba muishughulikie na kwa kufanya hivyo mtakuwa mmefungua...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ndassa, unatakiwa unitazame mimi sio Mfugale. (*Kicheko*)

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nimkuona. Ni macho tu na unajua macho yana *degree* 180. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri *Engineer Kamwelwe*, nilikuja ofisini kwako na kama unakumbuka ukaniambia niandike barua pale *Water Front*. Nikaandika barua na nikakuletea ya barabara hiyo, sasa leo rafiki yangu Mheshimiwa *Engineer Kamwelwe* unaniwekea kilometra 10 za changarawe badala ya lami wakati barabara hii imeshafanyiwa upembuzi wa kina? Nikuombe sana Mheshimiwa Kamwelwe na labda sasa nimuombe Mheshimiwa Rais barabara hii wewe unaifahamu vizuri zaidi...

WABUNGE FULANI: Hayupo humu.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Nyamazeni ninyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Rais, barabara hii ni muhimu sana kwa wananchi wa Wilaya ya Kwimba. Barabara hii ikitengenezwa itafungua milango

ya uchumi kwenye Wilaya ya Kwimba hasa Ngudu. Barabara hii ni muhimu sana, nikuombe sana Mheshimiwa Kamwelwe, utakaposimama kuja kihitimisha nipate majibu hasa kwa barabara hii muhimu kwa Wilaya ya Kwimba. Barabara hii iko kwenye llani ya Chama chetu cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Iakini pia tuangalie uwezekano, Waheshimiwa wakubwa kabisa wa kujenga barabara ya kutoka Fulo – Mantale – Nyambiti Junction. Barabara hii ni muhimu sana inajumuisha Wabunge watatu kwa maana ya Majimbo matatu. Jimbo la Misungwi, Sumve na Kwimba, barabara hii ni muhimu sana ikitengenezwa kwa kiwango cha lami. Nimeshaleta mapendekozo kwenu muangalie angalau muiingize kwa mwaka ujao wa fedha ili barabara hiyo iweze kujengwa kwa kiwango cha lami kwa sababu inatumia pesa nyingi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, barabara ya kutoka Mwanza kwenda Shinyanga *border* yenyeye urefu wa kilometra 102 imekuwa ikitumia pesa nyingi sana za matengenezo ya mara kwa mara. Waziri anafahamu na nafikiri *Engineer* wa mkoa anafahamu na *Engineer* wetu anafahamu kwa nini barabara hiyo isifumuliwe angalau hata kilometra 10 za kwanza baadaye kilometra 10...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Shabiby, jiandae Mheshimiwa Salome, Mheshimiwa Mndolwa na Mheshimiwa Mwambalaswa.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu pamoja na wakuu wote wanaoongoza taasisi kwenye Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu mimi nianze na barabara ya Gairo – lyogwe ambayo inakwenda mpaka Mkao wa Tanga kwenye Wilaya ya Kilindi pale kwa ndugu yangu Mheshimiwa Kigua. Nafikiri hii barabara Mheshimiwa Waziri amefika muda si mrefu kama miezi miwili iliyopita na Mheshimiwa Naibu Waziri naye amefika kwenye barabara hii kama miezi mitatu iliyopita na kwa bahati nzuri wakati unafika Mheshimiwa Waziri ulishuhudia pale magari yakiwa yamekwama watu hata kwa miguu wanashindwa kupita, ulijiona kwa macho. Kwa bahati nzuri ukaongea na Eng. Mfugale ukaahidi kwamba patakuwa na madaraja ya *temporary* angalau barabara hii ipitike lakini katika kitabu changu cha bajeti hapa sjaona matengenezo ya barabara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ikumbukwe kwamba iko katika ahadi ya Rais ya kuwekwa lami kwa sababu inaunganisha Mkao wa Morogoro na Mkao wa Tanga kuititia Wilaya ya Gairo na Wilaya ya Kilindi na ni barabara muhimu sana na wote mnaifahamu. Hata katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi pale Gairo tarehe 26 Juni, 2014 aliitaja sana barabara hii, mpaka leo iko *Youtube* humu bado sijajua ni kwa nini haipo lakini nafikiri ataangalia namna ya kufanya ili iweze kuitika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ile barabara ya Gairo Mjini ambayo toka mwaka jana ilipewa shilingi bilioni 1.5, mwaka jana ilitolewa shilingi milioni 500 mkandarasi amejenga madaraja lakini mwaka huu mmetoa hela chache kabisa shilingi milioni 120. Kwa hiyo, nina wasiwasi kama kuna mkandarasi atakayekubali kuanza kutengeneza barabara ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea ile barabara pale Gairo Mjini haipitiki tena ya kutoka pale njiapanda ya hospitali mpaka Magoeka kwa sababu *TARURA* tena hawamo na *TANROADS* nao hawaishughulikii, sasa haipitiki. Kwa hiyo, naomba hii barabara ya Gairo Mjini iweze kupangiwa pesa ya kutosha ili iweze kushughulikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ile barabara ya Gairo – Nongwe. Ukiangalia katika bajeti ya mwaka huu imepangiwa vihela hela vingivangi sana vidogo vidogo. Kweli lazima nishukuru, mara nyingi imekuwa inapangiwa pesa lakini hakuna hata mara moja imeshawahi kuwekewa changarawe. Kila mwaka tunaitengeneza na mvua za mwanzo tu imeharibika. Pesa zinazopangwa hata nikiangalia hapa ni nyingi zinatosha hata changarawe lakini haijawahi kuwekewa changarawe hata mwaka mmoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri mliangalie hili la barabara ya Gairo – Nongwe kwa sababu pesa mnazozipangia ni nyingi lakini hakuna sehemu iliyowekewa changarawe. Kwa hiyo, hata manyunu kidogo haipitiki na ile barabara imekaa kama ya Lushoto, unavyoona milima ya Lushoto au zaidi ya milima ya Lushoto ndiyo inakopita barabara hii ya Gairo – Nongwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia minara ya simu, nilikuwa nataka ndugu zangu Mheshimiwa Waziri na Naibu wako Mheshimiwa Nditiye muangalie sana. Minara ya kijiji cha Masenege na Idibo ipo siku nyingi na ni ahadi ya siku nyingi na hata katika vitabu vyenu kila siku ipo. Mnara katika Kata hii ya Idibo, Makao Makuu ya Kata mpaka leo hauna hata dalili ya kujengwa. Tukiweka minara hii ya Gairo pale Idibo, Masenge na Chogoa katika Kata ya Chogoa tutakuwa tumemaliza kabisa shida katika wilaya ya Gairo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho nataka nikizungumzie ni habari ya bandari. Lazima niseme ukweli au nikiri Bandari ya Dar es Salaam kwa sasa hivi inafanya vizuri sana, wizi wote uliokuwa pale katika Bandari ya Dar es Salaam sasa hivi haupo. Mmoja ambaye alikuwa hatumii Bandari ya Dar es Salaam ni mimi hapa lakini sasa hivi nina mwaka wa tatu natumia Bandari ya Dar es Salaam na huwa naweka mpaka mitego, naweka vitu *loose* nione kama vitaibiwa lakini iko vizuri sana. Haina wizi na ina *speed* ya hali ya juu sana na ndiyo maana mnaona sasa hivi inaleta changamoto ya malori. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uzuri wa bandari hii sasa hivi kumekuwa na malori ambayo yamepita kiasi kwenye barabara zetu. Tulizungumza sana na mimi bahati nzuri ni mjumbe wa Kamati kwa muda mrefu katika hii Kamati ya Miundombinu kwamba tuanzishe *dry port* ya pale Vigwaza ili haya malori yote yawe yanaishia pale. Ukifika pale mzigo wote wa bandari uwe unachukuliwa na ile reli ambayo sasa hivi hata haifanyi kazi ya kwenda Tanga na Arusha, mizigo iletwe mpaka pale Vigwaza, malori yote yaishie pale Vigwaza yasiende mjini. Tumelizungumza sana suala hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba muangalie malori yamezidi, sasa hivi foleni ya Dar es Salaam sio ya kawaida. Pamoja na kuwa tunatengeneza reli ya *standard gauge* kuja Dodoma lakini suala hili hata tukitengeneza *dry port* hapa Ihumwa itasaidia tu mikoa ya Kanda ya Ziwa pamoja na Burundi, Rwanda na Uganda. Hata hivyo, bado ile bandari kavu (*dry port*) ya pale Vigwaza itasaidia sehemu zote za Malawi, Congo, Zambia na sehemu nyingine na cha zaidi ni kuondoa msongamano ambaa upo sasa hivi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa *TPA* walishatoa mpaka pesa zaidi ya *USD 2,000,000* kwa ajili ya kutengeneza kichwa cha treni na tulikiona pale Morogoro kwa ajili ya kufanya kazi kama hizi. Je, kile kichwa cha treni kiko wapi? Kwa sababu ukiangalia *dry port* za Dar es Salaam zinavyochaji usafiri ule tu wa kutoka pale bandarini kwenda kwenye *dry port* pale *Mandela Road* au sehemu nyingine ni pesa nyingi kuliko hata kukodisha hiyo treni kutoka mjini mpaka pale Vigwaza. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana mjitahidi kuhakikisha kwamba ile *dry port* naisha. Sisi tulienda kuikagua na ilishaanza kujengwa, tunaomba haraka sana ifanye kazi na malori yote yaishie Vigwaza ili kuondokana na foleni. Maana sasa yanababisha vifo, mara utasikia kontena limeangukia *hiace* na limeua watu, mara limefanya nini, tunaombeni sana mtusaidie kwa hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, mimi si Mbunge wa Wilaya ya Mpwapwa, lakini kwa usafiri nafanya biashara na ndiyo nilikoanza kwenda katika biashara yangu ya mabasi, kwenda Mpwapwa, Dar es Salaam, jamani huyu mzee Mheshimiwa Lubeleje mtamuua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka na miaka analalamikia habari ya barabara ya Mpwapwa kuja Kongwa, kipande kile kidogo cha lami, kila siku mzee mpaka sasa hivi mzee meno yameng'oka bado anaongea lakini hamtaki kumsikiliza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naombeni sana, kwa uwezo wako Mheshimiwa Mfugale, barabara ya Mpwapwa ni barabara muhimu sana, kulinganisha na barabara zingine za wilaya zingine. Tunaomba jamani kwenye bajeti hii nimeangalia na mzee wangu, lakini hatujalona hii, na imo katika llani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015/2020. Lakini haina dalili yoyote mpaka leo. Tunaomba sana hii barabara ya Mpwapwa, nayo iwemo kwenye mpango huo na ninajua Mheshimiwa Waziri ni *Engineer* na bahati nzuri na wewe Mpwapwa huwa unakwenda mara nyingi, kwa hiyo, nayo mtaishughulikia, ahsante sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Naunga mkono hoja, asilimia 100. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Makamba, Mheshimiwa Mndolwa, Mheshimiwa Mwambaliaswa.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nichangie Wizara hii muhimu na Wizara ambayo imepelekewa fedha nyingi kuliko Wizara zote katika Serikali hii ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa baraka aliyotujalia ya kuweza kupatikana kwa ndugu yetu bwana Mdude Nyangari. Akiwa hai japo amejeruhiwa vibaya sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo moja kabla sijaanza kuchangia, jana ilizunguka taarifa ambayo inasemekana imetoka Ikulu, ikionyesha kwamba Mheshimiwa Rais anasikitishwa sana na vitendo vya utekaji na upoteaji wa watu vinavyoendelea katika nchi hii, na akasema kwamba vitendo hivi vinaichafua nchi na ameliagiza jeshi la polisi kufanya kazi na ataunda tume na ikibidi...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Makamba jielekeze kwenye hoja, ambayo ko mbele yako.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda kwenye hoja. Ghafla bini vuu tukapata taarifa kutoka Ikulu ikikanusha habari hiyo...

MWENYEKITI: Makamba, jielekeze kwenye hoja ambayo iko mbele yako.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kukanusha taarifa inayotoka Ikulu ni taarifa nzuri sana...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Makamba nitakukalisha sasa hivi, jielekeze kwenye hoja ambayo ipo, kwa mujibu wa kanuni, jielekeze kwenye hoja ambayo iko mbele yako.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wa Nchi yetu amefanya kazi kubwa sana katika kusimamia Wizara ya Uchukuzi na Mawasiliano, na mtizamo wake Mheshimiwa Rais, katika kusimamia suala la ununuzi wa ndege, Mheshimiwa Rais amehamishia Mamlaka ya Usimamizi wa Ndege zote za Serikali katika Ofisi ya Rais. Jambo hili, katika miradi mikubwa katika nchi hii, katika miradi mikubwa, mradi wa ndege ni mmoja kati ya miradi mitatu mikubwa iliyoanzishwa katika hii nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 20*, haikaguliwi na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Fedha za wananchi ambazo ndizo nyingi zinatumika katika mradi huu, zimehamishiwa Ofisi ya Rais, hazikaguliwi na Mkaguzi, na siyo tu hivyo, amesoma Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani hapa, anasema katika

sehemu ambayo tunaonyesha hasara kubwa katika Taifa hili ni katika Mamlaka ya Ndege. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo haja kubwa sana ya kuliangalia suala hili kwa sababu kuna kioja kimoja kiliwahi kutokea kwenye Bunge moja nilikuwa nasoma kwenye mitandao, wakati mwagine tunaweza tukawa tunapiga makofi kumbe tumetukanwa. Yule Mbunge alisimama akasema, nusu ya Wabunge walioko humu ndani ni wajinga! Watu wakasema afute kauli, afute kauli, akafuta kauli akasema, nusu ya Wabunge waliomo siyo wajinga! Wakapiga makofi! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwagine tunaweza kuwa tunalitukanisha Bunge letu bila sisi kujua kutokana na matendo yanayoendelea. Kinachoonekana, katika suala la kuhamisha mamlaka, anayenunua ndege ni Ofisi ya Rais, akinunua nzima, akinunua mbovu ni juu yake. Halafu huyo huyo ndiyo anapitisha bajeti ya matengenezo ya ndege, iwe labda alinunua nzima au mbovu! (*Makofu*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, akitoka hapo huyo huyo ndiyo ananunua mafuta kwa ajili ya hizo ndege bila kujali fuel consumption ya ndege kama ilizingatiwa wakati wa manunuzi. Ipo haja ya Bunge kujitafakali kwa nini tumetoa mamlaka ya usimamizi wa ndege za Serikali, kutoka Wizara ya Ujenzi, tukapeleka Ofisi ya Rais, ipo haja ya kujitafakari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye matumizi ya wakandarasi, ipo dhana potofu ambayo Serikali ya Chama cha Mapinduzi inawaaminisha wananchi kwamba wakandarasi wazawa ndiyo ambao wanapewa kazi nydingi. Nataka nilieleze Taifa leo hii, ni kweli asilimia 85 ya wandarasi wa kitanzania ndiyo wanaopewa kazi, lakini ile asilimia 15 ya wakandarasi kutoka nje, ndiyo wanaolipwa zaidi ya asilimia 85 ya fedha zinazokwenda kwenye Wizara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuone ile asilimia kubwa inayopewa, ndiyo inayokwenda nje ya nchi, hao

wakandarasi wanaoitwa wazawa, wanapewa kazi za kawaida ambazo asilimia 15 tu ya bajeti ndiyo inatumika kuwalipa. (*Makof*)

MHE. JOHN W. HECHE: Wanapewa kuchimba mitaro.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye Mamlaka ya Hali ya Hewa...

**NAIBU WAZIRI, UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Katika Mamlaka ya Hali ya Hewa...

**NAIBU WAZIRI, UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, anapotosha.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Si una muda wa kujibu baba!

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITII: Taarifa, taarifa, taarifa! Mheshimiwa Heche, Mheshimiwa Heche kaa chini, Heche kaa chini.

MHE. JOHN W. HECHE: *Is wrong!*

MWENYEKITI: *That is not wrong*, kaa chini!

MHE. JOHN W. HECHE: *Is wrong!*

MWENYEKITI: *You are wrong* kaa chini!

MHE. JOHN W. HECHE: Siyo utaratibu!

MWENYEKITI: Sikiliza Mheshimiwa Heche, Bunge linaendeshwa na taratibu zake, huwezi ukaamuka tu na mkali

yako ukasimama ukasema unavyotaka, kwanza sijakuruhusu usimame. *No! No!* anaweza kwa *any time aka-inter*, aka nini, tulia. Mheshimiwa Waziri!

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kitabu cha bajeti, Wizara inanunua ndege na utaona hapa katika ukurasa wa 467, kwa hiyo, nimelazimika kusimama kwa sababu dada yangu Mheshimiwa Makamba anatupotosha, analipotosha Bunge lako.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Makamba!

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Waziri una nafasi ya kujibu, nafasi yako itakuja mwishoni, na mimi nafanya hivi kuisaidia Wizara yako, kwa sababu, Mheshimiwa Waziri, suala la ununuvi wa ndege zote zillzonunulliwa leo hii, hakuna *performance* inayoonekana katika Taifa hili zaidi ya hasara. Ukitetea kwamba wewe ndiye unayenunua utakuwa *answerable at the end of the day* na ninasikia vibaya sana kwa sababu wewe ni baba yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee habari ya Mamlaka ya Hali ya Hewa, wiki iliyopita, Waziri alikuja hapa akasema kwamba kuna hali ya tataruki katika hali ya hewa, Lindi na Mtwara watapatwa na matatizo makubwa sana, tukasema sawa. Hii mamlaka ya hali ya hewa, ku-*bate*kuhusu mamalaka ya hali ya hewa ni afadhari u-*bate* game ya Yanga na Lipuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafuriko na madhara makubwa yamekwanda kutokea Shinyanga, Kahama, Mwanza, badala ya Lindi na Mtwara. Nataka kuhoji, hivi hawa watu wa mamlaka ya hali ya hewa ni wapiga lamri au ni *professional people* wamewekwa kwa ajili ya kutusaidia! (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nihoji tu kuhusu hao watu, na kwa nini hawajibishwi? Wanaleta tataruki kwenye hii nchi na wanamwangusha Mheshimiwa Waziri, Ofisi

ya Rais, mama anajitahidi kweli kuongea kwa ajili ya Chama cha Mapinduzi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu suala la ucheleweshaji wa mizigo, *I do no*, shida ya mitandao. Tulitenga fedha nyingi sana hapa tena mkaja kwa mbwembwe kuhusu *TTCL*, leo hii Mheshimiwa Waziri haoni hata aibu kusema tumewapa *VIATEL*, anajibu maswali ya Wabunge hapa, ananadi makampuni ya nje, hivi hii *TTCL* imeshindwa kufanya kazi au kuna tatizo gani! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mmeshindwa, si mtoe tu tamko kwamba, jamani na makampuni mengine yaje ili waendelee kufanya kazi. Mheshimiwa Waziri, siyo uzalendo, siyo uzalendo kuja kujisifia hapa kwamba umeimarisha au umesambaza mitandao ya makampuni ya nje, wakati *TTCL* tumekupa fedha hapa na umeshindwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee kwa haraka kuhusu Mamlaka ya Bandari. Tunafahamu kuna kazi kubwa sana inafanyika na niwapongeze wafanyakazi. Katika eneo lolote la kazi, maslahi ya wafanyakazi yanakuja kwanza! Kinachotokea mamlaka ya bandari, yule Mkurugenzi wa Mamlaka ya Bandari anawafanyisha watu kazi pale mpaka saa sita, saa saba za usiku. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wabunge hapa maslahi yetu huwa yanakuja kwanza, niseme, mtu anatoka kazini saa sita za usiku, kesho asubuhi saa 12 kamili anatakiwa aripiti ofisini, hatuwezi kufanya kazi kwa kukiuka sheria za kazi katika nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *just* kwa sababu tunalazimisha mipango ambayo tulipanga bila kufanya *consultation* iweze kufanikiwa. Niombe sana, Mawaziri, muangalie sekta zenu mnazofanya kazi, kufanya kazi sema punda afe mizigo ufile, Tanzania tunafanya kazi kwa kuangalia kwanza maslahi ya wafanyakazi na ndiyo maana juzi hapa, jambo la kwanza Kambi Rasmi ya Upinzani ilisisitiza

ni kuhusu maslahi na mishahara ya wafanyakazi katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme jambo la mwisho, kuhusiana na suala la mitandao, tena nilikuwa nimesahau jambo la muhimu sana. Kule kwetu Kahama, zipo kata ambazo ndiyo zinaongoza kwa uzalishaji, wale watu hawawezi kutoka kata moja kwenda nyine kwa sababu hakuna barabara, hawawezi kutoka kata moja kwenda kata nyine kwa sababu hakuna mawasiliano ya simu, hawawezi kutoka kata moja kwenda kata nyine kwa sababu tumewatelekeza wamekuwa kama wanaishi watu walioko kwenye ujima. Nitazitaja kata chache tu ambazo wao wamenituma kwa dhati nifikishe suala hili kwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo Kata ya Wendere, tunayo Kata ya Ngogwa, Kata ya Ubagwe, Kata ya Nyandekwa na Kata ya Uleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako, ningemuomba Mheshimiwa Waziri, akija kuhitimisha hapa leo, awaaahidi wananchi hawa, ambao Mheshimiwa Rais anajinadi kwamba wasukuma ndiyo wamempigia kura. Hivi leo ni mwaka 2019, ni lini mtawatengenezea barabara, ni lini mtawapelekea mawasiliano ya simu, maana wale watu wanashida zote katika nchi hii, na mimi, yaani, ningekuwa siyo mpenzi wa watanzania ningesema afadhali msipeleke ili tuendelee kuchaguliwa chama cha CHADEMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme, kwa sababu nawapenda watanzania wenzangu, naomba nisisitize, Mheshimiwa Waziri, wapelekee wale watu huduma! Waonee huruma wanaishi maisha ya kijima.

MWENYEKITI: Ahsante, muda wako umekwisha.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mndolwa, Mheshimiwa Mwambalaswa, Mheshimiwa Kisangi.

MHE. ZAINAB M. AMIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa fursa hii ili kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema ili nami kwa siku ya leo kuweza kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitaanza kwa fedha zitolewazo katika Wizara hii ya Uchukuzi, kinachotakikana hapa fedha zifkishwe kwa wakati ili miradi iliyopangwa na Serikali iweze kutekelezeka kwa wakati. Endapo Bunge litapanga bajeti na fedha hazitafika kwa wakati ndiyo chanzo cha miradi mingi kutotekelze. Naishauri Serikali ipeleke fedha kwa wakati katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kuzungumzia kuhusu minara ambayo imejengwa katikati ya makazi ya watu hususan katika Mkoa wa Dar es Salaam. Watu wengi wanasema kuwa minara ile ina madhara, wengine wanasema ina mionzi, lakini ningependa kuona sasa Serikali itoe tamko na kutoa hofu kwa wananchi wetu, kwamba ile minara kama ina madhara yoyote au haina madhara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake watu wengi hutoa maeneo yao katikati ya mji ili kuweza kuweka ile minara ya simu, lakini wengine wanasema ina mionzi lakini bado utafiti haujafanyika. Naomba kama Serikali itakapokuja hapa kujibu itueleze kwamba, je, minara ile ina madhara yote kwa binadamu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaona majengo marefu yanajengwa katika Mkoa wetu wa Dar es Salaam, lakini majengo hayo hayana ile *fire escape*, tumena majengo ya kizamani, wakati mimi nasoma Chuo Kikuu cha Mzumbe, mwaka 1993/95 kuna majengo mabweni ambayo ngazi ambazo ziko nje ya jengo, ambayo hiyo hata ikitokea hatari ya moto watu huweza kukimbia, lakini majengo mengi

yanayojengwa katika Mji wetu wa Dar es Salaam, hayaonyeshi kama hatari yoyote ikitokea watu wakimbilie eneo gani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri katika ujenzi unaojengwa sasa hivi, ionyeshe *fire escape* kwamba watu ikitokea tahadhari yoyote ya moto au chochote watu wanaweza ku, isitokee eneo hilohilo wanaloingilia ndio eneo hilohilo wanalookea ili kuwaondosha madhara zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuongelea kuhusu barabara zetu zinazojengwa hivi sasa, barabara nyingi kuu zinazojengwa zina matatizo sidhani kama wakandarasi hao wako *competent* au *vipi*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia barabara hii ya Chalinze mpaka Mlandizi, barabara hii ni ya muda mrefu na hata katika bajeti ya mwaka jana nilizungumzia, kwamba barabara ile imejengwa chini ya kiwango na pia hupelekea ajali nyingi hususan magari ya mizigo, na bado hapo katika hotuba ya Wizara Waziri anasema kwamba upembuzi yakinifu unaendelea kwa kilomita 12. 6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado ipo haja, kwa umuhimu wa barabara hii nadhani ipi haja sasa, barabara hii ijengwe kwa kiwango ambacho ni madhubuti, itapelekea kutosababisha ajali katika barabara hii. Kwa sababu barabara hii ni kubwa, ya kuitisha magari ya kwenda Mikoa ya Kaskazini pia kwenda Mikoa ya Iringa, Mbeya na kwingineko. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona pia wakandarasi wetu, katika barabara kuu. Nitatolea mfano barabara ya Dodoma mpaka Morogoro, utakuta mkandarsi amepewa labda eneo la kukarabati, anachimba shimo, utakuta wiki tatu wiki mbili shimo lile halikarabatiwi na huweza kusababisha ajali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri wakandarasi wetu pindi wanapopewa hii mikataba,

watahadharishwe kwa sababu unakuta eneo wamechimba mashimo, wanataka wajenge na unakuta wiki mbili wiki tatu bado lile shimo halijazibwa na hii hupelekea kusababisha ajali kwa magari yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na pia ipo haja sasa ya kujua kwamba kwenye kitabu cha Waziri amesema kuanzia Morogoro mpaka hapa Dodoma ni kilomita 260 na upembuzi yakinifu unafanywa ili barabara hii ijengwe kwa kiwango, lakini sasa hivi naona kuna uakarabati unaendelea, hususan maeneo ya Dumila, barabara inatanuliwa, lakini sasa sijauja kama ndiyo imeingizwa kwenye hii bajeti au lile ni zoezi lingine linaendelea labda bajeti itakuja na barabara ile pia itabomolewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua, pindi unapokuja hapa, lile zoezi linaloendelea maeneo ya Dumila pale, la kupanua barabara, lile linahusiana na huu upembuzi yakinifu unaoendelea? Maana yake naona ni vilaka vinazibwa, na eneo lile lina usumbufu wameweuka mapipa barabarani na barabara yenewe ni mbovu. Nataka nijue hawa wakandarasi wetu wanapopewa hii miradi, je, wanaelezewa kiwango cha upana wa barabara? Sidhani kama magari yetu sasa hivi yameongezeka ukubwa au upana, kwa sababu sasa hivi kinachoonekana ni barabara zinaongezwa upana. Kwa hiyo, nashauri Serikali, pindi mnapotoa tenda kwa wakandarasi wetu, muwaeleze upana halisi unaofaa katika barabara zetu za Tanzania, ili kuepusha upotevu wa fedha za Serikali katika kukarabati kila siku katika barabara hizi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kuelezea kuhusu reli, reli sasa hivi inajengwa reli hii ya mwendokasi, lakini bado kuna tatizo katika makutano ya pale Kamata. Ule ujenzi wa reli umepelekea sasa hivi kutokana na mvua za Dar es Salaam kuwa na mafuriko. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri, yule mkandarasi aliyepo maeneo yale aweze kufanya jitihada za makusudi sasa kuweka miundombinu ambayo itawezesha sasa barabara ipitike kwa urahisi ambayo sasa hivi inaleta mafuriko kutokana na ujenzi unaoendelea,

amezungusha mabati yake ambayo yanapelekea sasa hivi mafuriko katika eneo lile la Kamata. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kuelezea kuhusu reli yetu hii, reli inayojengwa ya mwendokasi watu wengi katika vijiji vyetu huwa wanaona kama ni jambo geni kwao, na ninashauri sasa hii reli inayojengwa sasa hivi ya kisasa ianze kuwekwa alama, mwisho ambao mwananchi anapaswa afanye shughuli zake. Kwa sababu isijeikatokea mwananchi sasa ameona reli imepita karibu na eneo analoishi, akaanza kuanza ujenzi ambao baadaye utapelekea sasa migogoro ya ardhi wakati sasa reli ilishakamilika na kukabidhiwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sasa wakati ujenzi unaendelea, alama ziwekwe katika hii reli ambayo inaanza ya mwendokasi, mpaka huku Makutupora, mpaka Kigoma. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kuelezea kuhusu hii *double parking*, kuna maeneo mengi ambayo yako katika vituo, hizi barabara kubwa. Kwa mfano natolea mfano maeneo ya pale Kibaigwa, maroli makubwa yameweka *double parking* pande zote, kiasi kwamba yanasaababisha magari ambayo yako katika mwendo anashindwa kupishana. Nashauri elimu itolewe kwa hawa wenye magari makubwa kwamba...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, dakika zenu zilikuwa ni saba tu. Mheshimiwa Mwambalaswa.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye hoja hii iliyo mbele yetu. Nataka kuchukua nafasi hii kumpompngeza sana Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu, Watendaji wote walioko kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imechukua moja ya sita ya bajeti ya Serikali, moja ya sita, karibu troni tano katika troni 30, hii inaonyesha umuhimu wa Wizara hii. Wizara hii ndiyo inayoweza kutupeleka kwenye uchumi wa katii, Wizara hii ndiyo ina miundombinu yote ambayo inachochea kukua kwa uchumi. Kwa hiyo, naomba Wizara hii wajue kwamba wanadhamana kubwa sana ya kuivusha nchi hii kwenda kwenye uchumi wa katii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea vipengele vitatu, vinne, cha kwanza niongelee Bandari, naipongeza sana Serikali kwa kuamua kuboresha Bandari zetu, Bandari ya Dar es Salaam, Bandari ya Mtwara, Bandari ya Tanga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kiongozi mmoja wa nchi jirani amewahi kutania, akasema, Tanzania nipeni Bandari ya Dar es Salaam niendeshe, nitawapeni bajeti yenu yote. Hakuwa anatukejeri, ana maana kwamba, kwa jinsi ya uchumi wa jiografia ulivyo, Bandari zetu zimekaa kimkakati sana. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa kuziboresha bandari hizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, Wizara, tusiboreshe miundombinu peke yake, tuboreshe na huduma. Wizara hii imejaa wasomi wengi waliobobe, wana taaluma, tufanye utafiti, tuangalie je, kwenye bandari ambazo tunashindana nazo, Mombasa, Beila, Duban, vitu gani ambavyo wafanyabishara wanakimbilia kule ili na sisi tuviboreshe kwetu? Kwa hiyo, naomba tusiboreshe miundombinu peke yake, tuboreshe na huduma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee reli. Naishukuru tena vilevile Serikali kwa kujenga reli mpya *Standard Gauge* na kuboresha reli ya zamani *Miter Gauge*, naishukuru sana. Naishauri Wizara kila inapowezekana wanunue *rolling stock* ambayo unaweza ukatumia kwenye reli zote ili kuweza kupunguza gharama. Wanunue *rolling stock* ambayo unaweza ukatembeza kwenye *Standard Gauge* na vilevile *rolling stock* ambayo unaweza ukatembeza kwenye *Meter*

Gauge na vilevile hata unaweza kutembeza kwenye *Cape Gauge* kwa reli yetu ya *TAZARA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii reli ya katii *Standard Gauge* ikitumiwa vizuri inaweza kubeba tani ya mizigo zaidi ya milioni 20 kwa mwaka na hapo ndiyo itachochaea kukua kwa uchumi wetu. Sasa nimefurahi sana kuona kwenye bajeti ya mwaka huu Mheshimiwa Waziri amesisitiza reli hii ya kutoka Uvinza kwenda Msongati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Msongati Burundi kuna *Nickel* zaidi ya tani milioni tano, tuna *Platinum* zaidi ya tani milioni sita, saba, reli hii itabeba mizigo hiyo. Namshauri Mheshimiwa Waziri aanze kuwa-*engage* Mawaziri wenzake wa Burundi na Kongo ili reli ya ina hiyo ijengwe kuto Msongati kwenda kwenye bandari ya Uvira. Hapo tutakuwa tume-*capture* mizigo ya Burundi na mizigo ya Kongo, wakati hii ya kutoka Isaka kwenda Kigali ina-*capture* mizigo ya Rwanda na mizigo ya *Central African Republic*. Umuhimu wa reli hii ni katika kubeba mizigo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee reli ya *TAZARA*. Reli hii inahitaji maboresho madogo sana, lakini shida ya reli ya *TAZARA* nadhani ni sheria. Reli hii ilijengwa na Serikali ya Awamu ya Kwanza, lengo ilikuwa kuisaidia Zambia ambayo ilikuwa *Landlocked* wakati tunapigania uhuru wa nchi za Kusini mwa Afrika, ilikuwa ya muhimu mno, lakini leo inaonekana kwa majirani zetu reli hiyo haina umuhimu, ndiyo maana inatusumbua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri aiangalie sheria na mkataba kwa reli hii ili ikiwezekana alete sheria hapa Bungeni tuweze kuirekebisha iende na wakati ambao tunautaka kwa sababu Tanzania tunaitaka kwa kukuza uchumi wetu. Wenzetu sasa hivi wanategemea Bandari ya Durban na Bandari ya Beira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri aiangalie sheria alete Bungeni tuweze kuiboresha kwa manufaa ya Tanzania zaidi. Ilikuwa kwa

manufaa ya wenzetu, naona wenzetu hakuna umuhimu, sasa tuiboreshe kwa manufaa ya Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo hilo la reli ya TAZARA pale Inyara, Mheshimiwa Mbunge wa Mbeya Vijijini anaiongelea sana. Naiomba Serikali iweze kujenga pale bandari kavu ili mizigo ifike pale, ili baadaye tuweze kujenga reli kutoka Inyara kwenda Itungi *Port* kwa ajili ya mizigo ya Malawi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya ziara nchini Malawi hivi karibuni. Namshukuru sana, maana yake ziara yake hiyo imerudisha mahusiano ya kibashara kati ya Tanzania na Malawi kwenye reli nzuri. Ninamshukuru sana. Akiwa huko pamoja na Rais mwenzie walishauri kwamba Mawaziri waunde tume ya mashirikiano ya pamoja. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri anayehusika waunde haraka tume hiyo kwa sababu Awamu ya Kwanza ilisaidia sana Malawi, ilijenga *Cargo Centers*; Dar es Salaam, *Cargo Centers*, Mbeya, lakini hizo *Cargo Centers* hazifanyi kazi. Kwa hiyo, biashara kati ya Tanzania na Malawi imekufa kinyemela nyemela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali ifufue hizo *Cargo Centers* haraka ili biashara kati ya Tanzania na Malawi iweze kuendelea kama kawaida. Kuna wenzetu nchi za majirani ambao bandari zao zimepata msuko msuko kidogo. Kwa hiyo, naomba bandari zetu zichukue hiyo kama ni *opportunity* ili kuweza ku-*capture* biashara hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee barabara kidogo. Mheshimiwa Rais akiwa Mkoani Mbeya aliongelea barabara ya mchepuko, kutoka mlima Nyoka kwenda Mbalizi, aliongelea na uwanja wa ndege wa Songwe na aliona umuhimu wa barabara hiyo, maana yake aliona msongamano uliopo Mbeya Mjini ni mkubwa sana. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa aweke umuhimu sana kwa barabara hiyo ya mchepuko ya kutoka Mlima wa Nyoka kwenda Mbalizi na vilevile kuboresha barabara ya kati

ambayo sasa hivi ina *lane* mbili aiboreshe iwe *lane* nne kuweza kupunguza msongamo pale Mbeya Mjini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara ya Mheshimiwa Rais nilibahati sana, Mheshimiwa Rais alifika Chunya kufungua barabara ya Mbeya - Chunya na pia kuweka jiwe la msingi barabara linayojengwa sasa hivi kwa kiwango cha lami ya kutoka Chunya kwenda Makongorosi. Wananchi wa Chunya wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais, wanamshukuru sana Mheshimiwa Waziri na wanawashukuru sana Watendaji wote wa Wizara hii ya Ujenzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara hiyo *Architect* Mwakalinga na *Engineer* Mfugale nilikuwa nao pale tukanywa nao chai, walilona barabara hiyo ambayo wamenizawadia, lakini pale mlimani waliona kuna matundu mawilli, matatu ambayo yanachafua barabara hiyo ambayo ni nzuri sana ambayo kwetu sisi ni mboni ya jicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba *Architect* Mwakalinga na Eng. Mfugale watununulie *weighbridge*, hata kama ni *mobile weighbridge* kwa sababu huko Chunya tuna mazao mengi ya misitu, tuna mazao mengi ya tumbaku. Wafanyabiashara huwa wanaweka malori makubwa ya lumbesa usiku, wanapita kwenye barabara hiyo wanaiharibu, wakifika Mbeya ndiyo wanagawa kwenye malori mawili matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba sana hawa Mainjia wanisaidie sana, watusaidie Chunya, watununulie hata *mobile weighbridge* kuweza kuiokoa barabara hii idumu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunamalizia na Mheshimiwa Yahaya Massare.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami nichangie katika Wizara hii ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, ambayo ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu. Niendelee kupongeza kama walivyopongeza Wabunge wenzangu kwa utendaji mzuri wa Mawaziri, Mheshimiwa Waziri Kamwelwe, wasaidizi wake, Manaibu Waziri wote wawili, Katibu Mkuu wa Wizara hii na Watendaji wote katika Wizara hiyo. Wamekuwa wakifanya kazi nzuri, lakini zipo changamoto ambazo tunatakiwa tuwasaidie na kuendelea kuishauri Serikali kuona namna iliyo bora ya kufanya sasa nchi hii iweze kukaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inasimamia suala zima la barabara. Suala la barabara, dhamira ya Serikai na llani ya chama cha Mapinduzi ni kuunganisha Mikoa yote kwa njia ya barabara za kiwango cha lami. Tunayo barabara moja katika Mkoa wa Singida inayounganisha Mkoa huu wa Singida na Mkoa wa Mbeya. Ametoka kuzungumza sasa hivi mwenzangu hapa ambaye nimepakana naye, Mheshimiwa Mwambalaswa, kule kwake wanajenga barabara hiyo hiyo kwa kiwango cha lami. Awamu ya kwanza walianza Mbeya kwenda Rwanjilo, ya pili Rwanjilo kwenda Chunya, sasa wanajenga kutoka Chunya kwenda Makongorosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka Mkoa ambao tunapakana nao mwaka 2017 barabara hii ilipata mkandarasi, ilitangazwa mchakato ukaisha. Mheshimiwa Rais alipokuja Itigi mwezi wa Saba tarehe 25 alikuta tatizo katika barabara hii. Mchakato ulionekana una harufu ambayo siyo nzuri, akazuia, akasema kwamba kwa pesa ambazo zinatolewa, aidha, mkandarasi afanye *negotiation* na *TANROADS* waongeze kilometa au kilometa zipunguzwe kulingana pesa na mchakato ambao ulikuwa umeingia katika mkataba ule,

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia 2017 mpaka leo hii waliposhindana kwenye mazungumzo mkandarasi mwaka 2018 aliondoka. Mwaka 2018 katika bajeti iliyokwisha ikaoneshwa kwamba barabara hii iko katika mpango wa kujengwa. Katika kitabu hiki ukurasa wa 181 barabara hii

imeoneshwa kwa pesa kiduchu ambazo zimeoneshwa katika jedwali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu yangu, wananchi wa Mkoa wa Singida Jimbo la Manyoni Magharibi, aidha watanichukua mimi Mbunge wao au wataichukia Serikali yao, kwa sababu hawajaambiwa neno la ukweli toka mwaka 2017. Naiomba Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, Mawaziri mlioteuliwa, Mheshimiwa Waziri Kamwelwe, mnaaminiwa na Mheshimiwa Rais, barabara hii hata wewe Mheshimiwa Waziri inakufaa sana. Kwenda kwako kule badala ya kupita Tabora utapitia Itigi, utakwenda Rungwa, Rungwa - Ipole, Ipole unakwenda Mpanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii kama hutajenga Mheshimiwa Waziri maana yake unataka nami mwakani nsiende kuomba kura; au nikombwa kura nitapata taabu sana namna ya kuwaeleza wananchi waelewe. Namwomba Mheshimiwa Waziri barabara hii nilliona humu basi mwaka huu tuone mkandarasi anapatikana na ujenzi unaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri wataalam wote wako hapa, Katibu Mkuu yuko hapa. Eng. Nyamwanga alishafikisha pazuri sana barabara hii katika kutaka kuijenga, lakini Katibu Mkuu mpya naamini ni msikivu, Eng. Mfugale uko hapa, mimi ndiyo natoka Itigi, siku ile ulikuwepo pale. Naomba sasa masikio yako yarudi yafunguke yaone ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa wananchi wale. Tunawategemea ninji, 2015 tunakwenda katika Uchaguzi wa Vijiji mwaka huu, tunataka tushinde vijiji vyote. Nami naahidi nitasimama imara CCM itashinda vijiji vyote, lakini hili litaweza kuja kutugharimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona Mheshimiwa Waziri ananiangalia, naamini hili limeingia. Naomba tu mnisaidie, nami sitaongea tena suala la barabara. Tusaidiane, barabara hii ina maslahi mapana na watu wa Mkoa wa Singida, Katavi na Mbeya. Makao Makuu ya Serikali yako Dodoma. Mtu wa Katavi anapokuja Dodoma, akipita Tabora anaongeza urefu

wa safari, lakini ukipitia Rungwa - Itigi ni kwelesi, hata Mheshimiwa Mwambalaswa atakuwa hawesi kuzungukia tena Makao Makuu yake ya Mkoa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niendelee kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa inayofanya ya ujenzi wa reli kwa kiwango cha *Standard Gauge*. Sisi watu wa Mkoa wa Singida reli inapita Itigi katika eneo langu. Naomba tu juhudzi ziendelee, lakini kwa hakika tunafarrijika sana na kazi inayofanywa na Serikali hii kupitia Wizara yenu hii. Hayo mengine tunasema ili nanyi mtuone.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la minara ya simu. Suala hili linaonesha kuna shida kidogo. Mwaka 2018 karibu na bajeti tulipitishiwa makaratasi hapa ya kuonesha mnara utajengwa mahali kadhaa, mahali kadhaa; na mwaka huu umekuja mpango ule ule. Ile ya mwaka 2018 haujajengwa, lakini mwaka huu umekuja utaraibu ule ule.

Sasa naomba sana Waheshimiwa Mawaziri mnapokuja na yale makaratasi na kuchukua majina, basi tuone yana-reflect kwa wananchi wetu. Ukihaniambia mimi, nami nikifanya mikutano, nawaambia wananchi hapa Serikali inaleta hiki. Sasa ninapokwenda kwa mara nyingine tena nakuja na *story* inakuwa haipendezi na hasa sisi wenzeni wa upande huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kazi nzuri inayofanya, lakini niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja ili mkipata pesa mkatekeleze miradi hii ambayo mmeiomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja hii. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunamalizia na Mheshimiwa Bhagwanji, dakika tano.

MHE. BHAGWANJI MAGANLAL MEISURIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kupata nafasi hii. Kwanza

naipongeza Kamati yangu, tumekwenda ziara. Vile vile nampongeza Mheshimiwa Rais, nampongeza pia Mheshimiwa Waziri kwa kufanya kazi nzuri katika Kamati hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze kuhusu bandari iliyojengwa Tanga, Mtwara na Dar es Salaam. Hiyo yote imeboresha zaidi. Vilevile nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kufanya juhudhi sana kuhusu barabara. Tulitembea Mbeya na Kamati, tumeona kazi ya barabara imefanyika na watu wananchi wameridhika sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati yangu katika ziara yake tumeona *Standard Gauge* inakaribia kukamilika kutoka Dar es Salaam kwenda Morogoro. Hata hivyo wamejenga bandari kavu.

Kwa hiyo, tunapongeza, ila kwa kuwa *containerzote* zinakaa Dar es Salaam, basi zitakuwa zinakaa katika bandari ile kavu ya kule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amechukua hatua nzuri sana katika mambo mbalimbali ya mawasiliano ya barabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umenipa nafasi haraka haraka, lakini nilikuwa sijajiaandaa, nilikuwa nimejandaa kwa jioni, lakini kidogo umenipa nafasi siyo mahala pake, mawasiliano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze kuhusu bandari iliyojengwa Mtwara. Tulipokwenda Mtwara, tuliona bandari ya zamani ilikuwa ndogo lakini sasa imepanuliwa zaidi. Nimeona hata Bandari ya Dar es Salaam, Kamati tumeambiwa kwamba kunafanyika uboreshaji wa njia ya meli, badala ya kupita meli moja, zitapita meli mbili pamoa.

Kwa hiyo, nashukuru kwamba hayo yote yatafanyiwa kazi. Namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati amefanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mheshimiwa Rais ameboresha uwanja wa ndege wa Dar es Salam tumeona, amenunua ndege nyingi na wanaleta utalii. Pia ndege itakwenda katika nchi nyingine kama India, China na sehemu nyingine na Iringa hivyo hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, namshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, anajitahidi kwa kukusanya pesa na kazi kwa Watanzania wanyonge na wengine wote. Kupitia mabasi ya mwendokasi, watu wamefaidika kwa bei ndogo na tunaingiza mapato chungu nzima, ila tu sasa hivi siku za mvua nashauri yajengwe madaraja kwa sababu tunapata taabu sana kwa kuja maji barabarani. Hata hivyo...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Haya, ahsante Mheshimiwa.

MHE. BHAGWANJI MAGANLAL MEISURIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge jioni tutaanza na Mheshimiwa Mbarouk dakika saba, Mheshimiwa Ngombale dakika saba na Mheshimiwa Masele dakika kumi.

Nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 jioni)

(Saa 10:00 Jioni Bunge Lilirudia)

MWENYEKITI: Tukae. Katibu!

NDG. MOSSY LUKUVI - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi,
Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Niiimtaja Mheshimiwa Mbarouk ajiandae
Mheshimiwa Ngombale dakika saba.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia afya njema ya kukutana katika Bunge letu hili na kuzungumza masuala ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda baada ya kusema hapo kwanza nitoe shukrani kwa Wizara yetu ya Ujenzi kwa taarifa ambazo walinipa kwenye Bandari yetu ya Tanga, kwamba kuna fedha zilitengwa na zimekwishafika kwa ajili ya kuongeza kina cha maji ya Bandari yetu ili Meli ziweze kufunga *a long side* nishukuru sana kwa hili takribani shilingi bilioni 1.8 kama sikosei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo jingine nipende kuzungumzia Bandari yetu ya Tanga; Bandari yetu ya Tanga ni Bandari ya muda mrefu na ya kihistoria lakini bado inafanyakazi chini ya kiwango. Sasa niiombe na kuishauri Serikali, Bandari ile pamoja na kuongeza kina, pamoja na pia taarifa nyininge kwamba baada ya ile *green* *ya forty foot container* kupata mpya lakini bado inahitaji ifanyakazi kama ilivyokuwa zamani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanini nasema hivyo? Zamani Bandari ya Tanga ilikuwa ikisafirisha mizigo mingi sana ya Kahawa, ya Pamba, ya Katani, Alizeti na vitu vingine sasa, sasa hivi Bandari ile imekuwa inafanyakazi chini ya kiwango. Niseme hata alipokuja Mheshimiwa Rais katika kuweka jiwe la msingi la uzinduzi wa bomba la mafuta nilimuomba basi

angalau bandari zetu hizi zifanye kazi kwa kiwango angalau japo kukaribiana, kwa sababu gani nasema hivyo? Kama unakwenda Zanzibar ama kwa ndege, ama kwa meli utakuta kuna msururu wa meli zimekaa zinasubiri zamu ya kuingia Bandarini kupakua mizigo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme tu, kanini basi tusifanye *category* hizi za mizigo kwa mfano, Bandari yetu ya Tanga ichukue mizigo yetu ya Tanga, ichukue mizigo ya Moshi, Arusha, Manyara lakini hata Musoma na Bukoba na Nchi kama Rwanda na Uganda angalau ingekuwa inafanyakazi hivyo ingekuwa imerudia kufanya kazi katika kiwango chake kama ilivyokuwa zamani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Bandari nydingine pia labda ya Mtwara tuseme ingechukua nayo mizigo labda ya Mtwara yenyewe, Mbeya, Sumbawanga, Katavi huko, Malawi na kwingineko ingekuwa Bandari inafanyakazi. Sasa tumekuwa kama wafanyabiashara ya mayai ambao mayai yote tumeyatia katika chombo kimoja ukijikwaa tu ni kwamba umeshapoteza mtaji.

Nashauri Serikali ifanye *categories* za mizigo; mizigo iwe kwa Kanda fulani, Bandari fulani itumike, Kanda fulani, Bandari fulani itumike lakini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo pia, zipo Bandari Bubu hatuwezi kukataa na hatuwezi kuepuka Bandari Bubu kwa sababu wananchi wetu ama wawe wavuvi au wasafirishaji wa vyombo vidogo vidogo wanazitumia. Mfano, Bandari ya Kipumbwi, mfano Bandari ya Kigombe hizi nasema zingeboreshwa zikajengwa kama ilivyojengwa Bandari ya Pangani pakajengwa Gati, pakawa pale na majengo kwa ajili ya kuchukua ushuru wa forodha, wakawepo wafanyakazi wa *TRA* tukakusanya mapato. Lakini kuendelea tu kuzitamka tu Bandari Bubu, Bandari Bubu hatuwezi kuziepuka. Ni vyema tungeweka Maafisa wa forodha pale wakawa wanapokea bidhaa zinazotoka Zanzibar kwa sababu hizo ndiyo ambazo mara nyingi tumekuwa tukizilalamikia kwamba zinapitishwa katika Bandari Bubu na kuikosesha Serikali mapato.

Kwa hiyo, hilo nilikuwa nashauri Bandari ya Kipumbwi, Bandari ya Kigombe zifanyekazi na pia zitaongeza ajira kwa vijana wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo jingine nipende kuzungumzia barabara ya Pangani; barabara ya hii ni barabara ya kihistoria. Iliwekewa ahadi na Rais wa Awamu ya Kwanza, Mwalimu Nyerere, Rais wa Awamu ya Pili, Rais Mwinyi, Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa, Rais wa Awamu ya Nne, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na sasa imeingia madarakani Serikali ya Awamu ya Tano. Kwa maneno ambayo yamekuwa yakisemwa mara kwa mara kwamba hii Serikali ya Awamu ya Tano ni sikivu na tumeona kwenye Bajeti fedha nyingi zimepelekwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namuomba Mheshimiwa Magufuli autafune ule mfupa uliomshinda Fisi, kwanini? Barabara ya Pangani kama itajengwa itakuwa ni kichocheo kwanza cha kiuchumi kwa sababu gani? Wanaotoka nchi jirani kama Kenya kupitia Mombasa na sisi watu wa Tanga tutaokoa muda wa kufika Dar es Salaam, kama tunavyoijua Dar es salaam ni Jiji la kibashara na biashara nyingi zinafanywa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa leo kusikia kupitia Bunge hili, pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri tumekwishanong'ona kidogo kaniambia fedha zimekwishapatikana, Mkandarasi amekwishapatikana, hiyo *feasibility study* ilikwishafanyika. Basi Serikali itoe nneo, itoe tamko ili ioneckane kwamba lini barabara ya Pangani inaanza kujengwa rasmi.

Naamini tamko litakalotoka hapa leo, Mheshimiwa Waziri utaona watu wa Tanga watakavyoshangilia, watakavyokuombea dua na vilevile pia watakavyonipongeza Mbunge wao ambae niliyekuwa nazungumzia mara kwa mara. Kwa hiyo, hapa nategemea kupata tamko la Serikali kwamba rasmi lini barabara itajengwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, hata wale ambao walizuiwa ama kuendeleza mashamba yao au kuendeleza nyumba zao ambao wako pembezoni mwa barabara wamekuwa wakihoji kuhusu fidia pia nilitaka leo Serikali itoe tamko lini watu wale wataanza kulipwa fidia zao kwa sababu wamekubali kutokuendeleza mashamba na majengo kwamba wanataka barabara ijengwe ili tuweze kusogeza maendeleo ya wananchi. Kwa mfano, barabara ya Pangani kama itajengwa kuna mazao ya nazi, kuna mazao ya muhogo maeneo ya Kirare lakini kuna mazao mengine pia kama ya Matikitimaji n.k yataweza kusafirishwa kwa urahisi kupelekwa katika soko la Dar es Salaam. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine, barabara...

MWENYEKITI: Ahsante muda wako umekwisha.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: ...naomba nazo pia changarawe zifanyiwekazi kwa sababu sikuona humu katika kitabu. Naomba mtakapokuja Mawaziri basi mtuelezee barabara za changarawe nazo zinajengwa lini kama vile kutoka Mabokweni kwenda hadi Daluni, Maramba na Korogwe. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ngombale, Mheshimiwa Masele jiandae Nsanzugwanko.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isaac Aloyce Kamwelwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano imethibitisha kwamba ni Serikali ya watu iliyowekwa na watu kwa ajili ya watu na ndiyo maana utaiona tu hotuba ya Mheshimiwa Waziri Kamwelwe imesheheni miradi mbalimbali ya maendeleo yenye kulenga kuitengeneza Tanzania mpya katika sekta mbalimbali za Uchukizi, Ujenzi na Mawasiliano. Nimpongeze Mheshimiwa Rais, Makamu wake, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri, Makatibu Wakuu na Watendaji

mbalimbali ambao wamehusika katika maandalizi ya hotuba nzuri hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ipo barabara ya kutoka Butengorumasa-Iparamasa-Mbogwe-Masumbwe inatakiwa sasa iendelezwe ili iweze kuiunganisha sasa Mkoa wa Geita, Mkoa wa Shinyanga, Mkoa wa Tabora, Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Rukwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii itarahisisha sana mawasiliano baina ya Wananchi wa Mikoa hii niliyoitaja kwa sababu Wananchi wa Geita hawatakuwa na sababu sasa ya kupita Nzega ndiyo aende Tabora. Atatakiwa tu anatoka Geita anapita Mbogwe, anakwenda Ushetu, anakwenda Kaliua, Kaliua sasa hapa anachangua; kama anakwenda Kigoma atapita Urambo atakwenda Kigoma huko, akifika Kaliua anaweza akakata kuelekea Mpanda-Sumbawanga au anarudi kwenda Tabora, Tabora anakuja Singida mpaka hapa Dodoma na Dar es salaam. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri nilikuwa naomba barabara hii kwasababu sehemu ya Butengorumasa-Iparamasa-Mbogwe mpaka Masumbwe imeshapandishwa kuwa barabara ya *TANROADS*, nilikuwa naomba na hiki kipande kilishosalia sasa cha kutoka Masumbwe-Mwabomba-Nyankende-Bomba A-Uroa-Uyoa-Sungwa-Mwamnange-Buhindi mpaka Kaliua na yenewe ichukuliwe na Serikali ili iweze kupandishwa kwa kiwango cha *TANROADS* na ikibidi ufanyike usanifu wa kina ili hatimaye ije ijengwe kwa kiwango cha lami ili iweze kuwasaidia wananchi wa maeneo haya waweze kuwa na mawasiliano ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze pia Serikali kwa kukubali ombi la kuipandisha hadhi barabara ya kutoka Bwelo, Makao Makuu ya Wilaya ya Mbogwe kwenda Karumwa katika Wilaya mpya ya Nyang'hwale, jambo hili na lenyewe litatufungua kwahiyio tutakuwa na urahisi wa kuwez kutoka Wilaya moja hadi nyingine bila ya kupata kikwazo cha aina yoyote katika usafiri wa watu na vitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee pia kuipongeza Serikali kwa hatua yake ya kutenga fedha kwa ajili ya usanifu wa reli na kuanza kuijenga kwa kiwango cha Kimataifa (*standard gauge*) na mpaka sasa ujenzi unaendelea kutoka Dar es salaam mpaka Morogoro na hatua ni nzuri na hatimae tutaona kutoka Morogoro kuja Dodoma na baadaye Dodoma-Tabora-Isaka-Mwanza na kutoka Tabora hadi Kigoma baadaye Kaliua mpaka Mpanda na Kadema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa lolote na tunaamini kabisa kwamba uwepo wa miundombinu namna hii ambayo ni rafiki itachochea ukuaji wa uchumi katika Taifa letu hasa ikizingatiwa kwamba Nchi yetu imejaaliwa kuwa ni lango la Nchi mbalimbali ambazo ziko *land locked* ambazo hazina Bahari na bahati nzuri sisi tumekuwepo katika ukanda ambao tuna Bahari, tuna Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo uwepo wa Maziwa na Bahari unarahisisha uwepo pia wa Bandari na Serikali yetu imejipambanua katika kuhakikisha kwamba zinakuwepo Bandari ambazo zina uhakika na zinazoweza kutoa huduma kwa nchi zetu ambazo ziko jirani na sisi. Kwa mfano, Bandari ya Dar es salaam, Bandari ya Tanga, Bandari ya Mtwara na ile Bandari ya Bagamoyo ambayo inatarajiwaa kujengwa hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naishauri Serikali iendelee kuziangalia pia zile Bandari za kwenye Maziwa kwa mfano, tunazo Bandari katika Ziwa Victoria, kwa Geita pekee tunayo Bandari ya Nyamirembe, Bandari ya Nkome, Bandari ya Nungwe, zote hizi zinahitaji kuwekewa miundombinu ili kusudi ziweze kutoa huduma kwa Wananchi wa Mkoa wa Geita na ili waweze kuwasiliana na wenzano wa Mikoa ya jirani, kwa mfano, Mkoa wa Kagera na Mkoa wa Mara na Nchi jirani kwa maana ya Uganda na Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mawasiliano ya anga, niipongeze Serikali kwa kununua

ndege mpya na ambazo zinaendelea kufanya kazi. Vilevile niipongeze Serikali kwa kuendelea na upanuzi wa viwanja vyta ndege ikiwemo kiwanja cha ndege cha Mwanza. Niungane na Wabunge wenzangu ambao wanatoa mapendekezo kwa Serikali kwa sababu hedges zimepatikana basi zianze kuwepo *route* za kutoka Mwanza kuja Dodoma ambapo ndiyo Makoa Makuu ya Serikali ili kusudi Wananchi wa Mwanza na Mikoa mingine ya Kanda ya Ziwa wawewe kufika kwa urahisi katika Makoa Makuu ya Nchi pamoja na kwenda sehemu za Dar es salaam na Mikoa mingine kama kule Mbeya kwa uwanja wa Songwe na uwanja wa Nduli kule Iringa na sehemu zingine ambazo kama Kilimanjaro na sehemu zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa kwamba Serikali yetu imejipanga na ndiyo maana inatekeleza kwa kiwango kikubwa mambo mengi ambayo yanahitajika kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itoshe tu kusema maneno haya kwa sababu kazi kubwa iliyofanywa na Wizara hii inatosha na niseme tu kwamba naiunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri asilimia 100 kwa 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Nsanzugwanko jiandae Mariam Kisangi.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwanza nianze kwa kuwapa pole familia ya Mzee Mengi na Watanzania wote kwa kuondokewa na Ndugu Mengi. Kwetu sisi watu wa Kigoma huyu alikuwa Shemeji yetu kwa hiyo tunatoa pole nydingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba kwa namna ya pekee pia Mheshimiwa Waziri wewe nikupongeze Injinia Kamwelwe na Manaibu wako Injinia Nditiye na Mhasibu aliyebolea Ndugu Kwandikwa, Makatibu Wakuu wote, Architect Mwakalinga ambaye ni mgeni kwenye Wizara

ameanza vizuri, anafanyakazi vizuri na Makatibu Wakuu wenzake Ndugu Chamliho na wenzake Mama Sasabo na Jimmy Yonasi wote tunawapongeza kwa kazi nzuri ya kusimamia wenzao katika maeneo hayo. Wizara mko vizuri, Mheshimiwa Waziri mko vizuri, tunawapongeza Watendaji wote kwa maeneo yote, maeneo ya anga, maeneo ya barabara, maeneo ya majini, mawasiliano kwa kweli wako vizuri watendaji, cha msingi ni kuwatia moyo. (*Makof*)

Mheshimiwa mwenyekiti, nitakuwa na mambo machache kwa sababu hii ni Kamati yangu na mambo mengi tumeyadadavua kwenye Kamati. Ningependa tu mambo matatu ya haraka haraka:-

(i) Mheshimiwa Waziri asubuhi nilikuuliza swali kuhusu *SGR*; sisi tunaolewa vizuri mambo haya, ujenzi wa *standard gauge* ni mradi wa msingi sana, sana, ndiyo roho ya Nchi, ndiyo roho ya uchumi wa Taifa hili. Nimekuuliza moja ya matawi yake ni kutoka Uvinza kupita Kasulu kwenda Msongati na hatimae Uvira ya Congo kuchukua mzigoto mkubwa ulioko katika Jamhuri ya Congo. Ukanijibu kwamba nisiwahishe shughuli kwamba iko kwenye hotuba yako. Kwenye hotuba yako nimeangalia hakuna hata msitari umezungumzia juu ya hilo tawi la *SGR*. (*Makof*)

Mheshimiwa Waziri nikukumbushe tu na watendaji wako; reli hii ya *SGR* tunayojenga ambayo ni uamuzi wa busara sana wa Mheshimiwa Raïs Dkt. Magufuli ni mradi mzuri sana sana. Lakini faida yake, kazi yake ni kubeba mizigo mizito na mizigo mizito mingi Mheshimiwa Waziri kwa takwimu zilizopo, mzigoto mkubwa katika nchi zinazotuzunguka uko katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Ni matumaini yangu kwamba Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa utatuleza hili tawi la Uvinza-Msongati kwenda mpaka Uvira ya Congo mtaanza lini hata angalau basi hata upembuzi yakinifu wa njia hiyo maana hatimaye tunataka *SGR* hii iwe na maana pana ya kiuchumi kwa Taifa letu.

(ii) Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ambalo ningependa lizungumze na hili tunalizungumza siku zote ni

barabara; Sera ya barabara inajulikana, Mheshimiwa Waziri nikukumbushe tu na Watendaji wako kwamba Sera yetu ya barabara hasa barabara kuu ni kuunganisha Makao Makuu ya Mikoa na Makao Makuu ya Mikoa. Waziri unajua na watendaji wako wanajua kwamba katika Mikoa mitatu ambayo haijaunganishwa Makao Makuu kwa barabara za lami ni pamoja na Mkoa wa Kigoma, Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Katavi unaotoka wewe nakumbushwa hapa na Mkoa wa Morogoro kwa maana Morogoro na Lindi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri najua ziko juhudu kubwa sana zinafanywa kutuunganisha sisi na Tabora, ziko juhudu zinafanywa kutuunganisha sisi na Mkoa wa Katavi, ziko juhudu kubwa zinafanywa kutuunganisha sisi na Mkoa wa Kagera pamoja na Shinyanga yake lakini bado bado speed ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hotuba yako Mheshimiwa Waziri, ukiangalia barabara kwa mfano ya Nyakanazi hiki kipande cha Nyakanazi kuja mpaka Kabingo, barabara imeanza kujengwa kwa miaka kumi lakini mpaka sasa ni asilimia 60 tu basi ya utekelezaji wake na hoja iliyoko hapa Mheshimiwa Waziri ni kwamba mkandarasi yuko *site* lakini anasema hana fedha. Ushauri wangu kwako na kwa Wizara na kwa Serikali, hamna sababu ya kuanzisha miradi mipyka kama miradi ambayo tayari ina Wakandarasi haisogeji kwenda mbele kwa sababu ya uhaba wa fedha, kupanga ni kuchangua Mheshimiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ambayo imeshaanza ina wakandarasi, miradi hii ikamilike ndio tuanze na miradi mingine haina maana kuwa miradi nusu nusu viporo kila pahala wakati haikamiliki, haiwezekani barabara ya Nyakanazi, Kabingo miaka 10 asilimia 60. Halikadhalika barabara ya Kidahwe kuja Kasulu kidogo umepiga ahatua asilimia 70 lakini miaka 10 unajenga kilometra 63 tafsiri yake ni kwamba kila mwaka unajenga kilometra tatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali na hasa kwa Wizara na Mheshimiwa Waziri naomba hili

ulichukue seriously niwaombe sana nasema tena hakuna sababu ya kuanzisha miradi mipya kama iliyopo hajjatekelezeka, inakuwa haina maana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kuna juhudii kubwa ya fedha za *African Development Bank* kwa barabara ya Kabingo, Kibondo, Kasuli Manyovu ni juhudii kubwa na leo kama kumbukumbu zangu ziko sahihi leo tarehe 9 zabuni zimefunguliwa kuwapata wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kwamba sasa mradi huuutasogea kwenda mbele na haitakuwa tena hadithi kama ambavyo tumezoea, na sisi watu wa Mkoa wa Kigoma tumekuwa tuna mashaka kila mara miradi inaanzishwa lakini inasuasua sana katika ukamilishwaji wake. Nikuombe Mheshimiwa Waziri tumechoka kusubiri watu wa Kigoma wanataka miradi hii ikamillike na wanufaikie nayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ambalo ningependa nilizungumze ni bandari ya Katoshio najua kuna juhudii zinaendelea kujenga bandari ile tunataka pia mkandarasi yule nasikia ameshapatikana mkandarasi lakini mpaka leo hakuna ambacho kinaendelea mpaka sasa hivi ni matumaini yangu kwamba ile bandari ya nchi kavu imeshalipiwa fidia ni matarajio yangu kwamba sasa mkandarasi ataingia kazini na bandari ile iweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikukumbushe Mheshimiwa Waziri ujenzi wa *airport* ya Kigoma kuititia fedha za *European Investment Bank* taarifa tulizonazo sisi watu wa Kigoma na kuititia kwenye vikao vya *RCC* ni kwamba mkandarasi ameshapatikana tangu mwaka 2018 lakini bado hajakabidhiwa eneo la kufanya kazi, matatizo yaliyokuwepo mara ya makaburi yameshakamilika yameshakwisha nafikiri ni jukumu la Wizara sasa kufanyia *a thorough follower up* ili mradi ule sasa uanze na taarifa tulizonazo ni kwamba wenzenetu wa *European Investment Bank* tayari hawana kikwazo sasa baada ya kuwa mgogoro uliokuwepo umekamilika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo pia kuhusu bandari ya Dar es Salaam na bandari ya Mtwara. Tulibahatika kutembelea bandari hizi nikuombe Mheshimiwa Waziri jilidhishe na matatizo tuliyoyaona katika bandari ya Mtwara na matatizo ya kiutendaji tuliyoyaona katika bandari ya Dar es Salaam, dawa ya tatizo ni kuliondoa sio kujificha kwenye kichaka na hii tabia ambayo imeanza kuzuka ukisema jambo basi watu wanasema huyu bwana kahongwa kapewa fedha msitafute vichaka vya kujifichia kuna matatizo ya kimkataba katika bandari ya Dar es Salaam, matatizo haya mkae chini kaa na watendaji wako *Engineer Kakoko* yupo na wenzake mkae mezani muyamalize matatizo haya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona matatizo ya usanifu kule Mtwara kaeni na wataalam, kaeni na *Engineers* waliopo muweze kuyaondoa matatizo haya. Na kama hii dhana ya kuanza kufikiri kwamba kila likisemwa jambo basi mtu amehongwa linakuwa kwa kweli ni kujipofusha sisi wenywewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ningezungumzia kuhusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na hiyo kampuni ya PUMA *Energy* Tanzania. Mheshimiwa Waziri nakupa nakushauri tu pata muda wa kuifahamu kampuni hii ya PUMA *Energy* nimekuwa Mkurugenzi kwenye kampuni miaka saba na nilikuwa ndio Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi, hii ni kampuni ya Serikali asilimia 50 za PUMA *Energy* ni Serikali ya Tanzania na ni hisa za kihistoria. Hizi hisa alipewa mwalimu Nyerere mwaka 1966 na Malikia wa Uingereza lakini napata shaka kwamba Mheshimiwa Waziri huelewi vizuri kwamba hii kampuni ya PUMA ni kampuni ya Serikali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri sana Mheshimiwa Waziri una *TR*, kuna watu wa HAZINA kaeni chini hii kampuni ni ya kwetu imelipa *dividend* kwa miaka minane mfululizo. Sasa taarifa nilizonazo ni kwamba ina vikwazo vingi sana na Mheshimiwa Waziri umeonesha kutoipenda kampuni hii, sasa nikuishauri tu kwamba usimchukie mtoto wako kaa na Mamlaka, kaa na *TR* muweze kuelewa vizuri juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nikukumbushe tu Mheshimiwa Waziri naunga mkono hoja hii lakini niseme jambo moja kwa ruhusa yako nusu dakika tu kwamba ahadi zinatolewa na viongozi kuna ahadi zimetolewa 2017 hazijatekelezwa na kuna ahadi zimetolewa 2019...

MWENYEKITI: Ahsante mengine muandikie.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Niombe sana Mheshimiwa Waziri jambo hili naunga mkono hoja hii. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kisangi jiandae Mheshimiwa Qambalo, jiandae Mheshimiwa Profesa Jay.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi niweze kuchangia katika Wizara hili. Kwanza kabisa napenda kumpongea Mheshimiwa Waziri na Manaibu Waziri wake, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara hili kwa utendaji wao mahiri katika Serikali yetu. Lakini napenda nitoe salamu za pongezi kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wake wa busara wa kununua ndege sita. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni Wabunge tunafika sehemu lazima tuwe wa kweli nchi yetu kwa kukosa ndege ilipwaya. Leo anatoka mtu anasema kwamba ndege hizi hazina faida zina hasara kubwa lazima tuwe wa kweli faida ya ndege huwezi kuiona hivi hivi, kuna mambo hayawezni kuonekana moja kwa moja. Kwanza ndege zinasaidia katika eneo la utoaji wa huduma kwa haraka katika nchi lakini pia ndege itasaidia kutangaza Utalii, pia zinasaidia kutuletea fahari yetu kama Watanzania na sisi tunapoona Twiga wetu wa ATCL anaruka kutoka kwenye nchi yetu kwenda kwenye nchi jirani kama mtanzania na mzalendo kwa kweli unajisikia moyo wako una amani kubwa sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ndege hizo ziteleta fedha zitasaidia katika kuongeza mapato ya Serikali kuitia

uwekezaji utakaoendelea kutokana na kutangazwa kwa Utalii na mambo mbalimbali katika nchi za jirani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo napenda tena nimpongeze Mheshimiwa Rais tena wa Jamhuri ya Muungano kwa kuwa Rais wa Watanzania wote bila kujali ametoka katika mkoa gani. Nasema hayo kwa uzalendo mkubwa nikiwa na ushahidi kwa yale yaliyotendeka katika Mkoa wa Dar es Salaam. Katika Mkoa wa Dar es Salaam katika kipindi kifupi kumefanyika miadi ifutayo;

- (i) Lilikamilika daraja la Kigamboni,
- (ii) Flyover ya TAZARA ya Mfugale,
- (iii) Interchange ya Ubungo imeanza,
- (iv) Barabara nane Kimara kufika Kibaha mradi huo umeanza,
- (v) Ujenzi wa daraja la Mlelakuwa umekamilika,
- (vi) Ujenzi wa daraja la Salenda umeanza na uko kwenye hatua nzuri,
Kuanza kwa barabara na miundombinu ya mwendokasi kutoka Gerezani, Bendera Tatu mpaka Mbagara Rangitatu. (*Makof*)
- (vii) Ujenzi wa Uwanja wa ndege wa Kimataifa umekamilika kwa asilimia 90 ,
- (viii) Ujenzi wa reli na upanuzi wa bandari *gate* namba 13 umekamilika bandari ya Dar es Salaam, maboresho makubwa ya barabara katika Mkoa wa Dar es Salaam kuititia mradi wa *DMDP* kwa kweli yameleta sura nyingine kabisa katika Mkoa wa Dar es Salaam. Hayo yote yametokana na uzalendo wa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano ambaye yeye kujali nini ni Rais wa Watanzania wote akaona pamoja na kuhama kwa Makao Makuu kutoka Dar es Salaama na kuwa Mji wa kibiashara basi mambo haya yameboreshwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa pongozi hizo kwa Serikali sasa naomba nijikite mchango wangu katika ukurasa wa 24 barabara ambazo zimekamilika ziko katika upembuzi yakinifu. Barabara ambayo iko kwenye upembuzi yakinifu ni barabara ya Kibada, Tudwi, Songani, barabara hii kwa kweli yaani ni ya muda mrefu kila wakati ipo kwenye upembuzi wananchi wa kule Tundwi Songani wako katika hali mbaya sana mvua zinaponyesha wanakuwa hawana mawasiliano kabisa. Niiombe Serikali yangu waangalie kwa jicho la huruma wananchi wale wanaokaa Tundwi Songani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia barabara nyiningine ambayo ipo kwenye upembuzi na kuanza ni barabara ya Mbagala Rangi Tatu, Kongowe pamoja na daraja la Mzinga. Niiombe Serikali hii barabara ni muhimu sana watu wote wa Kusini lazima wapite kwenye daraja la Mto Mzinga lakini daraja lile sasa hivi limewekwa daraja la muda lile la kijeshi hakuna hata pembezoni sehemu ya kupita watu watu wakiwa kundi hawawezi kuvuka pale. Kwa hiyo, niiombe Serikali waharakishe barabara hii kwa ajili ya watu wanaoelekea katika mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna barabara ya Kongowe, Mji mwema Kivukoni tunaomba barabara hiyo iko kwenye mpango kabisa wa kujengwa kweli barabara hiyo itakapojengwa waangalie jinsi ya kuiongeza upana, barabara sasa ni finyu na mji wa Kigamboni sasa umekuwa tumekuwa na Wilaya mpya ya Kigamboni, kwa hiyo, barabara ile pamoja na kuboreshwa bado waongeze upana wa barabara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya Kitunda, Kivule kwenda Chanika Msongola. Barabara hii muda mrefu inajengwa vipande lakini hatuelewi kwa nini Mheshimiwa Waziri nakuomba sana utakaposimama uje unieleze hii barabara ya Kitunda, Kivule kwenda Msongola ina matatizo gani mpaka haiendelezwi? Wananchi wa kule wamechoka. Mbunge ninayetoka Dar es Salaam wameniomba nije nikuombe na utakapomaliza Bunge uende pale ukaeleze

wananchi wa kule hivi ni sababu gani zinakwamisha ujenzi
huu usiende vizuri? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye barabara ya Nzasa, Kilungule, Mwanagati, Buza. Barabara hiyo kila nikisimama hapa Bungeni hebu Mheshimiwa Waziri unionee huruma wananchi wa kule bado kunahitaji daraja la Kilungule kwenda Mparange wananchi wanavuka daraja la miti kama wako kijijini kumbe ni Jiji la Dar es Salaam ile hali haipendezi nikuombe Mheshimiwa Waziri kila siku tunaambiwa pesa iko tayari kila kitu kiko tayari mkandarasi atatangazwa kesho, kesho hii itaisha lini? Naomba sasa barabara hii itekelezwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nichangie kwenye eneo la bandari, napenda kutoa pongezi kutokana na taarifa kwamba bandari imefanya vizuri, kama inafanya vizuri basi ndio tunavyoomba niombe sasa liko tatizo bandari baada ya mkumbo wa yeti feki hakuna waajiriwa wengi walitoka, sasa hivi Serikali inawatumia SUMA JKT kuajiri vibarua. Natoka Mbagala lazima nikatishe bandarini kila siku watoto wale wanajaa pale nje wanasubiri kibarua cha shilingi 9000 lakini sasa tuone kibarua kile niiombe Serikali tumuamini kuna Mkurugenzi wa Bandari na ni Mkurugenzi mahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama ni Mkurugenzi mahili kwa nini hamna maeneo ambaayo mkaangalia jinsi ya kufanya mkataba leo hii anaajiriwa dereva wa kumbeba Mkurugenzi anamtoa Mkurugenzi wadogo wadogo hawa anamtoa Dar es Salaam mpaka Dodoma kutwa analipwa 9000 jamani hivi kweli tuangalie kada za kuiachia SUMA JKT lakini tuangalie sekta nyingine vitu vingine kama vinaangalia basi watu hao wapewe hata mikataba midogo. Mtu yupo daktari pale na yeche anachukuliwa kama kibarua *nurse* anapewa 9000 kwa kutwa jamani hii kitu hapana lazima tuangalie na *level*. Kama tunakwenda kuwachukua hawa watu wadogo, vibarua vidogo hivi wa SUMA waende lakini maeneo mengine makubwa basi Mkurugenzi apewe mamlaka ya kuangalia mikataba midogo ili wale watu wafanye kazi yao vizuri wasiwe na tamaa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niombe Serikali fungu la CSR linatolewa kwa jamii katika Mamlaka ya Bandari naomba sana nimewaona sisi kama Dar es Salaam hatuna kitu kingine tunawategemea wao niliwaona mara moja wakitoa magodoro shule ya uhuru lakini nawaomba tena waangalie kwa jicho la huruma watoto wenye mahitaji maalum wenye magonjwa ya usonzi wenye usonzi Sinza maalum, Mtoni maalum wale tukiwapa huduma jamani wana mahitaji makubwa Mamlaka ya Bandari kama inaingiza faida basi rudisheni kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije sasa kwenye reli nashukuru sana na naipongeza sana Serikali kwa kujenga reli ya *standard gauge* kwa kweli pale Dar es Salaam tu ukifika pale gerezani imeanza kubadilisha sura ya Jiji. Pia kuna mpango wa reli za mjini Dar es Salaam , reli hizo zitakuwa zilitoka uwanja wa ndege Mbagala, Chamazi, Buguruni, Kibaha, Bunju mpaka Bagamoyo ni jambo jema tunaiombea Serikali mambo haya yaende vizuri ili hii treni iweze kukamilika. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Maliza.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba barabara ya kutoka Mbuyuni Kawe, kuelekea Mbweni barabara ile iko ufukweni haina taa giza kubwa, wananchi wa kule wanapata shida naunga mkono hoja asilimia 100 ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Qumbalo, Mheshimiwa Profesa J, Mheshimiwa Ngombale, Mheshimiwa Dau.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii kuchangia pia kwenye Wizara hii, asubuhi nilipata fursa ya kuuliza swalii la nyongeza juu ya mpango wa ujenzi wa reli ya *Standard Gauge* Kaskazini mwa nchi hii na Mheshimiwa Waziri majibu yake yalikuwa ni kwamba tuisiwhishe mambo tusubiri wasilisho lake mambo mazito yanakuja. Sasa na mimi kama alivyoongea

Mheshimiwa Mzee Nsanzugwanko nimecheki kwenye kitabu hiki nimekuta hadithi ni ile ile upembezi yakinifu, usanifu wa kina muhandishi mshauri, mhandisi muelekezi. Hizi hadithi zinatakiwa zifike mahali sasa zikome. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotaka kuona ni vitu vinajengwa miundombinu ijengwe hadithi ya kujenga reli hii ya Kaskazini ya kuanzia Tanga Musoma imekuwepo tangu nikiwa mtoto mdogo wa shule leo kichwa kimekuwa cheupe bado kipande cha Arusha Musoma hata haijawahi kufanyiwa kazi. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kama haiwezekani kujenga ni bora tukae kimya tusihamasishe hivi vitu wananchi wapate moyo kwamba kuna kitu kinakuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa mwenyekiti, wenzetu wakoloni walliotutawala miaka hilo ya 1890 walikuwa na maono wakajenga reli ya mwazo Tanga kwenda Usambara sisi leo miaka 100 baadaye bado tuna mipango ambayo bado haieleweki. Niishauri Serikali tufike mahali tuwe wa kweli kama hatuwezi tuseme hatuwezi. Imeongelewa sana hii reli ya *standard gauge* sasa hivi tunajenga vipande viwili lakini kwa uhakika kama ambavyo Wabunge wengi wameshauri na makundi mbalimbali yameshauri kipande cha kutoka Tabora kwenda Kigoma ni kipande ambapo hakiepukiki kama kweli tunataka kujenga reli hii iwe na faida ya kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli inabeba abiria na mizigo tutamaliza kujenga reli hii huko tunakotaka kujenga lakini mwisho wa siku tutakosa mizigo ya kubeba kama hatutakuwa na mikakati ya kutafuta mizigo iko wapi, nadhani ni muda muafaka sasa Serikali ijielekezi hivi hi mizigo ya kubeba iko wapi? Imesemwa sana tuna soko DRC , tuna soko Burundi lakini tufahamu kwamba kuna wenzetu wa Kenya na wenyewe wana reli ya aina hii na wenyewe wanaelekea huku huku na hivi majuzi tumesikia Marais wa nchi hizo mbili wameingia mkataba wa mashirikiano, sasa kama hiyo mizigo tunayoilenga DRC itakwenda kwa wenzetu wa Kenya hivi hii ya kwetu mizigo ya kubeba itatosheleza? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri tuwe na mpango wa nini tunakwenda kubeba hata kama tunakwenda kujenga reli hii. Nafikiri sasa pia ni vizuri reli hii ya sasa ya katika tumeijenga kwa kutumia vyuma kutoka nje ya nchi, lakini sisi tunaambiwa tuna-*deposite* ya vyuma huko Mchuchuma miaka mingi, hivi hata hatuoni fahari tunaona fahari kutumia ndege kwa sababu tuna Twiga pale nyuma hivi kwa nini tuseione fahari kujenga reli hizi kwa kutumia chuma ambacho tunacho ndani ya nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tuna nia njema ya kukuza uchumi wa nchi hii hebu hizo reli mbili ambazo tunaambiwa ziko kwenye upembuzi yakinifu, usanifu wa kina kwa maana ya reli ya Mtwara na kuendelea na hii ya Tanga tuijenge kwa kutumia chuma ambacho kinapatikana ndani ya nchi yetu. Kwa namna hiyo nadhani huo uzalendo ambao tunausema kila siku tutakuwa tumeuona vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihami kwenye eneo la pili, Shirika la Mawasiliano Tanzania (*TTCL*). Shirika hili ni katika mashirika machovu nchi hii. Sote tunafahamu historia ya Shirika la *TTCL*, shirika hili lina shida kubwa ya upungufu wa mtaji, halina mtaji na ndio maana mambo yake hayaendi. Shirika hili limeshindwa kuingia kwenye soko la ushidani na mashirika mengine ya mawasiliano ambayo tunayo nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo ambalo linasikitisha Taarifa ya CAG imebaini kwamba, mmoja wa wadaiwa sugu wa shirika hili, yaani watu wanaodaiwa na shirika hili ni Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambayo Mheshimiwa Eng. Kamwelwe wewe ndiye Waziri wake. Unadaiwa shilingi billioni 20.6 fedha ambazo *TTCL* wametumia kulipa shughuli na kazi za mkongo wa Taifa, wakati huohuo Wizara yako imeshikilia akaunti ya mapato ya mkongo wa Taifa. Sasa *TTCL* kwa sura hiyo itawezaje kujiendoresha kama wewe mwenyewe baba hutaki kulipa fedha ambazo wao wenyewe wamezizalisha? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tunaomba kama *TTCL* kweli tunataka liwe shirika ambalo litaingia kwenye soko la

ushindani tuwape fedha zao. Walipeni bilioni zao 20 halafu washindane na hao wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye eneo la tatu, Uwanja wa Ndege wa *Lake Manyara*. Uwanja wa ndege wa *Lake Manyara* umekuwepo katika vitabu vyetu tangu mwaka juzi, mwaka jana hata mwaka huu, lakini sioni dalili ya uwanja ule kujengwa. Wananchi wamekubali kutoa maeneo yao, wananchi wamekubali kupisha ujenzi wa uwanja ule, lakini mpaka leo hawajalipwa fidia na uwanja haujengwi. Sasa kama Serikali haina fedha muwaambie wananchi waendelee na shughuli zao za kimaendeleo kuliko maeneo ya wananchi mmeyachukua halafu bado hakuna kitu kinachoendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom, tumeiongea mara nyingi sana. Mheshimiwa Waziri imetengwa shilingi bilioni 1.4 na imeegeshwa tu kwenye Barabara ya Mto wa Mbu, Loliondo na Nata, shilingi bilioni 1.4, barabara ya kilometa 389 zinakwenda kufanya nini? Nadhani wakati mwingine mnaturidhisha tuone vitu vimeandikwa, lakini kwa uhakika hakuna kitu unaweza kwenda kufanya kwenye barabara ile kwa hiyo, utuambie hii barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom inakwenda kujengwa lini? Na hii bilioni 1.4 ni za kujenga lami au ni kwa ajili ya kuendelea na upigaji uleule wa upembuzi yakinifu, usanifu wa kina nambo mengine kama hayo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimeona kwenye barabara ile fedha hizi umezielekeza kwenye kipande cha Mbulu – Haydom, yaani unakwenda kujenga katikati fulani, mwanzo umeacha na mwisho umeacha. Mheshimiwa Waziri hata ukiingia saluni hata kichwa hakianziwi huku katikati unaanza huku pembeni; sasa wewe kwa nini umeenda kuanza hii barabara pale katikati? Kama kweli tunataka kujenga barabara hii na tuone ina manufaa ya kibiashara na kiuchumi kipande cha Karatu – Mbulu nashauri uanzenacho ndio kipande ambacho kina magari mengi, lakini ndiyo kipande ambacho udongo wake wakati wa

mvua unateleza sana; hata muwa Mheshimiwa *Engineer Kamwelwe* unaanza kule mwisho au huku mbele, lakini wewe unapiga muwa katikati, una lako jambo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri kwamba, kwa kweli, barabara hiyo kama mna nia ya kuijenga muanze kuijenga kuanzia Karatu kwenda Mbulu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Barabara ya kuunganisha Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Simiyu iiliwa Barabara ya *Oldian Junction – Matala – Mto Sibiti* na kwenda Mkoa wa Simiyu, lakini sasa ni kama barabara hii imehamishwa ndio hii ya Karatu – Mbulu – Haydom. Hebu Serikali itoe kauli na Wananchi wajue, Waziri Mkuu alikuwa Mang'ola aliulizwa swali hilo akasema barabara imeshafanyiwa usanifu na baada ya usanifu tutapata fedha na kujenga barabara hiyo. Sasa barabara ya kuunganisha Arusha na Simiyu ni barabara ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali muwaambie wananchi, wananchi wasisubiri kitu ambacho hamuwezi kujenga. Nakushukuru. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Profesa J. Jiandae Mheshimiwa Ngombale, jiandae Mheshimiwa Dau.

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nichangie kwenye hoja iliyoko Mezani ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niungane na Taarifa ya Kambi ya Upinzani na ninaiunga mkono kwa asilimia zote, lakini pia ni Mjumbe wa *caucus* ya Bunge ya Mpango wa Maendeleo Endelevu (*SDGS*). Na nitapeleka mchango wangu katika sehemu tatu, nitaanza na masuala ya *SGR*, lakini nitaongelea Barabara ya Dumila – Kilosa – Morogoro – Mikumi, halafu nitaunganisha na masuala ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulifanya ziara pamoja na hi *caucus* yetu ya *SDGS* kutoka Dar-es-Salaam kwenda Morogoro mpaka Kilosa ambapo mradi huu wa *SGR*umeefika. Tuliona jinsi ambavyo kumekuwa na changamoto mbalimbali katika mradi huu pamoja na sifa nyngi ambazo wenzetu wamekuwa wakizisema, lakini kuna changamoto kubwa sana. Na ninasema naunga mkono Taarifa ya Kambi kwa sababu imejaribu kutoa uchambuzi jinsi gani ambavyo tungeweza kuboresha reli hii ya *SGR*, ili kuleta manufaa yenye tija kwa Watanzania ambao ndio pesa zao zinatumika mradi huu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *SGR* tumegundua kwamba, malighafi nyngi zinazotumika zinanunuliwa kutoka nje. Unaweza uka-*imagine* ukiangalia vitu kama *cement* pamoja na chuma ambacho kinatumika kwa wingi sana katika mradi huu vyote vinaagizwa kutoka nje. Na maana yake ni kwamba, kama tunaagiza hivyo vitu kutoka nje tunatumia pato letu la Taifa na pesa zote za kigeni zinakwenda kwenye mradi huu. Na ndio maana mara nyngi tumekuwa tukisema tumekuwa hatuna vipaumbele katika nchi yetu kwa sababu, mambo ambayo tunayafanya sasa hivi tungeweza kuyafanya na kuyatambua kwa wenzetu walipopita. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunagundua kwamba, katika Awamu iliyopita ya Nne kipaumbele kilikuwa ni Liganga na Mchuchuma kabla sisi wengine hatujaingia kwenye Bunge hili Tukufu tulikuwa tukisikia Liganga na Mchuchuma, Liganga na Mchuchuma, lakini sasa hivi hicho kipaumbele hatukioni kabisa. Mradi wa Liganga na Mchuchuma ungeweza kutumika chuma chake katika Mradi huu wa *SGR*ungeweza kupunguza gharama za mradi huu na ungeweza kuwana tija zaidi kuliko sasa hivi tunapotumia pesa nyngi za Watanzania katika mradi wa *SGR*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefika kipindi sasa kila mtu anakuja na vipaumbele vyake, imekuwa kama ile hadithi ya zamani kwamba, kuku na yai nani ameanza kuzaliwa na vitu kama hivyo. Ndio maana tunasema ili tuweze kufanikiwa ni

lazima tukae chini na tuendeleze yale wenzetu waliyoanza Awamu ya Tano ilipaswa kuendelea na jambo hili la Liganga na Mchuchuma, ili kuweza kufanya Mradi wa *SGR* uwe na tija zaidi kwa Watanzania wanyonge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na kutembelea huko huu Mradi wa *SGR* umepita katika Jimbo la Mikumi na *SGRMakao* yake Makuu pale Kilosa yapo katika Kijiji cha Muungano, Kata ya Mabwerebwere katika Jimbo la Mikumi. Kumekuwa na malalmiko makubwa sana ya wananchi wa pale kwamba, pamoja na kwamba, pale ndio imewekwa kambi, lakini pia wale watu hawajapata vile vipaumbele. Tunatambua kwamba, mradi wowote ambao tunakuwa tunasaini lazima vipaumbele viangalie wananchi waliokaa maeneo yale kwa ajili ya ajira na mambo madogomadogo yanayoenda katika ajira zile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *SGR* Wananchi wa Kilosa wamekuwa wanalamika sana kwamba, wanaachwa katika mradi huu, kazi za udereva, kazi zile za kutumia nguvu na vitu kama hivyo, wamekuwa wanawekwa pembedi na kilio chao kimekuwa kikubwa. Lakini pia, tulitegemea kutakuwa na kipengele katika mkataba wowote tunajua kuna kipengele kile ambacho kinahusu *social responsibilities* na vitu kama hivyo, lakini tumeona *CSR* katika mradi huu katika maeneo ya Mikumi na Kilosa yamekuwa hayazingatiwi kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, Wananchi wanaokaa pale Mabwerebwere wana changamoto nyingi mradi huu tunategemea kwamba, walivyokuwa pale wangeweza kuwasaidia kwenye masuala ya shule ambapo Wananchi sasahivi wanalamika na wanachangishana mia mbili mia mbili kwa ajili ya kujenga shule, wana changamoto kubwa ya maji, wana changamoto kubwa ya zahanati. Tulitegemea mradi mkubwa kama huu ungeweza kurudisha kidogo kwa wananchi wa maeneo yale ambao waliacha mashamba yao na vitu vingine mradi huu uweze kupita, lakini wamekuwa na kilio kikubwa sana kwa kusahauliwa na mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, mradi huu umepita katika Kijiji kinaitwa Umunisagala. Hawa watu wa Umunisagala wamekuwa wakilia na malalamiko yao yamekuwa makubwa sana kwa sababu, nao wamesahaulika katika mradi kama huu na wamesahaulika kwa sababu, wametoa ardhi yao. Reli ya zamani ile *meter gauge* ilikuwa inapita pale, lakini sasahivi *SGR* imepita eneo lingine kwa sababu ya kukwepa mmomonyoko wa ardhi pamoja na mafuriko ambayo yanatokea maramara kwa hiyo, wamechukua eneo kubwa la Kijiji cha Umunisagala, lakini hawajawazingatia katika masuala mengine ya kijamii kama hayo ya shule, zahanati, maji na vitu vingine kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitegemea hawa wakandarasi ambao wanahuksika *Yapi Merkezi* wangeweza kutoa japo kidogo ili kuweza kuwapoza wananchi wa maeneo yale nao wajisikie kwamba, wana *ownership* ya mradi ule maana tunaamini kabisa, ili tufanikiwe tunahitaji kuwa na ujirani mwema kati ya wawekezaji pamoja na wananchi wanaoishi maeneo haya. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali izingatie sana kuwaangalia Wananchi wa Wilaya ya Kilosa ambao wengi wamebomolewa nyumba zao, mradi umepita huko; Polisi imebomolewa na ratiba inaonesha kwamba, hata viwanja vya michezo vitabomolewa, itapita reli hii. Sasa hawa watu lazima tuwafikirie na tuwe na jinsi ya kuwa-*compensate* ili waweze kukaa na kupenda mradi kama huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nizungumzie suala la reli. Wakati tumeenda kwenye ziara ya *SGR* pale Kilosa nilizungumza na Mkurugenzi wa Reli Tanzania kwa sababu kulikuwa na changamoto kubwa sana Wananchi wa Mikumi, Kidodi pamoja na Ruaha waliwekewa alama za X kwa muda mrefu. Na pia kulikuwa na reli ya zamani iliyokuwa inatoka kwenye kiwanda cha Sukari Kilombero pale Ruaha inaenda mpaka Kilosa na kubeba mizigo kupeleka sehemu nytingine, kwa kweli, ile reli imekwisha hata mataluma hayapo. Na tulipoongea na Mkurugenzi kwa nini watu wamewekewa reli kama wana nia ya kufufua, walituambia bado hawajapata mtu wa kuweza kuwawezesha kutengeneza hiyo reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini leo ninavyoongea hapa leo watu wa reli wamekuja pale Mikumi kuna maeneo ya Kikwaraza Mji Mdogo wa Mikumi ambao ni Mji wa Kitalii wameweka na wameweka *barrier* wamezuia wananchi wasipite na magari yao kwenda kwenye maeneo ya Kikwaraza, maeneo ya Tambukareli ambayo kwa kweli ni sehemu ambayo ardhi yake sasa ndio wawekezaji wengi wa masuala ya *Campsites* wamenunua maeneo hayo. Kama mnaona kwenye *Tv* kuhusu Mji Mpya wa Mikumi ni maeneo hayo ambayo watu wa reli leo wameziba na kuzuulia Wananchi wasiende. Sasa unaona watu wa *Campsites* wanashindwa kuwekeza kwenye Mji wa Kitalii. Tutapata wapi pesa za utalii kama tunaanza kushindwa kuwekeza na kuweka vitu vizuri katika mpangilio kama huo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana watu wa reli wallangalle hilo. Huo Mji Mpya wa Mikumi unahitaji sana kuweza kuzingatiwa na kutoa nafasi kwa Wananchi, ili waweze kuwekeza zaidi kwenye jambo la utalii ambalo litaongeza uchumi wa Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hilo tangu nimeingia kwenye Bunge lako Tukufu nilikuwa nikizungumzia Barabara ya Dumila – Kilosa – Mikumi. Hii ni barabara ya kilometra 142 na ilikuwa ni ahadi ya tangu Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Awamu ya Nne na alipokuja Rais Dkt. Magufuli pia kwenye kampeni zake aliahidi kujenga kwa lami. Nashukuru nimeona kwamba, kuna bilioni mbili zimetengwa, lakini bado kuna nafasi kubwa sana ambayo bado haijazingatiwa maana katika kilometra 142 zilizojengwa kwa lami ni kilometra 45 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwenye kitabu cha Waziri katika ukurasa wa katikati hapa 166 inaonesha kwamba, watatengeneza kwa kilometra 20 tu, lakini awamu hizi zilisema kwamba, itatoka Dumila mpaka Ludewa kwa kilometra 45 halafu itatoka Ludewa mpaka Ulaya halafu ikitoka Ulaya itamalizia Mikumi, lakini wamesema watatengeneza kilometra 24 tu ambazo zitatoka Ludewa mpaka Kilosa. Sasa ninataka Waziri akija atuambie ni lini wataanza kujenga awamu ya

kilometra 78 kutoka pale Kilosa mpaka Mikumi ambapo kuna kata nydingi zipo katikati zinazotegemea barabara hii kwa ajili ya kujenga uchumi kwa Wananchi wa Wilaya ya Kilosa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kata ambazo ziko njiani katika barabara hii ya kilometra 78 ni Kata ya Magomeni, Kata ya Masanze, Kata ya Zombo, Kata ya Ulaya, Kata ya Muenda na Kata ya Mikumi. Unaweza ukaona jinsi ambavyo kama barabara hii itatengenezwa itaweza kusaidia na ku-boost uchumi wa Wananchi wa Mikumi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine nilitaka nizungumze kuhusu mawasiliano. Niliuliza swali wiki mbili zilizopita na Naibu Waziri alinijibu kwamba, hawawezi kupeleka mawasiliano kwenye vijiji ambavyo vina mtandao wa aina moja, lakini hivyo vijiji nillivyovitaja havina mtandao kabisa katika Jimbo la Mikumi na niko mbioni kuandika barua kukuletea Naibu Waziri, ili uweze kuona vijiji ambavyo namaanisha. Vijiji hivi viro kwenye Kata za Vidunda maeneo ya Chonwe, Naudung'u, Itembe, lakini Kata ya Kisanga, kuna Kata ya Tindiga, Malangali kule kwa Lukwambe pamoja na Malui, lakini Uleling'ombe, maeneo ya Mlunga na Lengewaa, lakini pia kuna maeneo ya Masanze, Munisagala, Chabina na Dodoma Isanga, lakini pia kuna Kata ya Muenda ambapo bado mawasiliano hayajafika katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimuombe sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuwa ulisimama na kunijibu hapa na kusema bado unaendelea na tathmini na nia yenu ni kuleta mawasiliano kwa Wananchi wa Jimbo la Mikumi, mtusaidie kuzingatia maeneo haya ambayo yanahitaji sana mawasiliano kwa ajili ya uchumi wao. Asante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ngombale, ajiandae Mheshimiwa Dau.

MHE. VEDASTO E. NGOMBALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. nianze moja kwa moja katika hotuba hii kwenye suala zima la mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka jana Wizara ilitenga bajeti na ilieleza kwamba, ingejenga minara ya mawasiliano katika vijiji vya Kinjumbi, Mwengei, Nandete, Chapita, Mtende na Mterambuko, hivi vingejengwa kwa kampuni ya *TTCL*, lakini Vijihi vya Kandawale pamoja na Mtumbempopera vingenjengwa na wenzetu wa Kampuni ya *Vietell*; mpaka hivi ninavyozungumza bado hakuna chochote kimeanza kufanyika. Niombi Wizara hizi kampuni zianze kufanya kazi kwa sababu, tayari tumeshawaambia Wananchi na Wananchi wanasubiri kwa hamu kubwa, lakini nishauri pia katika bajeti hii ya mwaka huu niombe vijiji vya Mkarango, Ngarambi, Miteja, Namakolo, Mtepela, Kibata na Ingirito vipate mawasiliano kwa sababu, vijiji hivi havina mawasiliano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine niende kwenye suala zima la barabara, awali ya yote katika suala la barabara nichukue nafasi hii kukupongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwani katika ile Barabara ya Nangurukuru – Liwale kilometra mia mbili kama na 30 hivi kwenye Kitabu cha Bajeti yako ukurasa wa 226 nimeona umetenga pesa kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu pamoja na *engineering design*. Mkupongeze sana kwa hilo, sasa angalao tuna matumaini kwamba, barabara itaenda kujengwa kwa kiwango cha lami, basi tunachosubiri ni utekelezaji. Sambamba na hilo naomba Serikali iiangalie pia, Barabara ya kutoka Tingi – Kipatimu na Ndeti. Nayo basi iingie kwenye kuwekwa bwasi kwenye upembuzi yakinifu, ili basi hatimaye ije kujengwa katika kiwango cha lami. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo naomba niendelee kukumbusha ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, katika Sherehe ya Kumbukumbu ya Vita ya Majimaji pale Nandete alisema kwamba, ye ye angejenga barabara ya kutoka Nandete – Nyamwage. Naomba niwakumbushe barabara hii ni muhimu na ni ahadi ya Mheshimiwa Rais; na nishauri, kijigrafia ukitoka Nyamwage kwenda Kipatimu ni kilometra 50 sawasawa na kutoka Njia Nne kwenda Kipatimu, lakini leo hii tukitaka kwenda Kipatimu unalazimika ufile mpaka

Nyamwage ambako utaenda kilometra 75 mpaka Njianne ndipo uende Kipatimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa barabara hii ya kutoka Nyamwage kwenda Kipatimu ya kilometra 50 kama ingekamilishwa na ingejengwa kwa changarawe tu, basi ungeturahisishia sana mawasiliano kutoka Nyamwage kwenda Kipatimu. Kwa kupitia barabara hii ukutoka Dar-es-Salaam kwenda Kipatimu ni kilometra 230 tu, lakini kwa kuzunguka tunakwenda kwa kilometra 280. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba barabara hii ambayo inapita kwa Ndugu yangu Mheshimiwa Mchengerwa halafu inakwenda kwangu ijengwe basi, iwe chini ya *TANROADS*, iimarishwe ili basi tuweze tukapata tukaweza kusafiri kwa mwaka wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo niombe sasa *TANROADS* waangalie uwezekano wa kuweka vipande vyta lami katika milima ya barabara ile ya Tingi – Kipatimu, kuna Mlima Ndundu na Mlima Ngoge, milima sumbusfu sana. Basi tuwekewe angalao vipande vyta lami, ili basi tuweze kusafiri kwa wakati wote, wakati wote tunaweza tukapita kama hivyo vipande vitawekewa vipande vyta lami. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo naomba *TANROADS* waangalie barabara ya kutoka Ndunu kwenda Somanga imewekwa lami katika kipindi ambacho hakizidi miaka mitatu minne, lakini leo ukienda ile barabara yote imefumuka. Niiombe Wizara makampuni wakati wanatekeleza miradi hii muwe makini sana vinginevyo ni upotevu wa pesa za Serikali kwasababu, barabara ya lami tunategemea ikijengwa angalao ikae miaka 20 na kuendelea, sasa ile barabara imekaa miaka mitatu tu sasa hivi mnarudia tena kufanya ukarabati mkubwa kana kwamba ilijengwa katika kiwango cha changarawe, naomba Wizara hilo waliangalie sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine ambalo ningependa nilikumbushe ni suala zima la upanuzi wa Bandari ya Kilwa Masoko. Kilwa pale tuna bandari, lakini ile bandari imekuwa

kama haitumiki ni *useless*, ipo tu. Sasa Wizara naona kama mmetusahausahau, mfanye upanuzi na ikiwezekana muifanye iwe inatumika sasa. Sambamba na hilo naomba muangalie upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Kilwa Masoko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilwa ni Mji wa Kitalii, Mji wa Kilwa ni Mji wa Kitalii, lakini tuna uwanja wa ndege ambao katika bajeti ilisema ingefanya maboresho uwanja ule, lakini hakuna chochote kimefanyika. Naomba tuboreshe ule uwanja, ili basi tuweze kutengeneza fursa ya kupata watalii, Mji wa Kilwa ni Mji wa Kitalii, tuna Mji wa Kale wa Kilwa, tuna Mapango kama ya Nang'oma, tuna Fukwe kwa Mtoni Fumang'ombe na tuna vivutio vingi tu vya utalii, lakini kama uwanja huu ukiboreshwaa basi utaweza kuvutia zaidi watalii na hivyo kuifanya Kilwa ipate ustawi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa barabara ya kutoka Nangurukuru kwenda Liwale kwa sasa kuna maeneo bado yanasmuba. Niiombe *TANROADSiyashughulikie* hayo maeneo, ili basi hiyo barabara iweze kupidika wakati wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dau, ajiandae Mheshimiwa Kuchauka, jiandae Mheshimiwa Chatanda.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa fursa hii. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wetu kwa hotuba nzuri sana alioitoa leo asubuhi na yenye kuleta matumaini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu, natoa pongezi nydingi sana kwa chama chetu Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa namna ambavyo wameweza kutekeleza llani katika Jimbo langu la Mafia. Kwa uchache tu nimeangalia kwenye kitabu humu, Mheshimiwa Waziri anasema gati la Nyamisati limekamilika kwa asilimia 32, lakini nilikuwa pale wiki iliopita,

lile gati limeshakamilika kwa asilimia zaidi ya 90 na naamini mwezi ujao atalifungua. Kwa hiyo, napongeza sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Jemedari Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kile kivuko ambacho tuliahidiwa mwaka jana hapa, kivuko cha kati ya Nyamisati na Kilindoni; nimekiona kwenye kitabu humu pamoja na matengenezo ya maegesho ya Nyamisati na Kilindoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo moja ambalo nililizungumza mwaka jana kwenye hotuba ya bajeti ya Wizara hii. Mwaka jana hapa zilitengwa shilingi bilioni 3.8 kwa ajili ya kivuko cha Nyamisati – Kilindoni bilioni tatu na bilioni nne kwa ajili ya maegesho upande wa Nyamisati na milioni 400 maegesho upande wa Kilindoni. Nilisema mwaka jana hapa, alikuwa Waziri Mheshimiwa Mbarawa, nikamwambia Mheshimiwa Waziri wanaokuangusha ni watu wako wa *TEMESA*, kuna tatizo *TEMESA*. Mwaka jana zimetengwa bilioni 3.8, leo tunamaliza bajeti hii hazijatumika kwa sababu sijui michakato imefanyaje, sijui mkandarasi kafanya vipi, imekwenda huko tenda imekosewa, imefutwa tumeanza upya. Labda hilo inaweza tukawa tumeelewa, vipi kuhusu maegesho milioni 400 Nyamisati na milioni 400 Kilindoni na yenye we nayo tatizo ni nini mpaka mwaka umekwisha fedha zinatengwa tena kwa bajeti hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa mwakani turudi tena hapa tukute wanatenga pesa nyingine kwa ajili ya kivuko na maegesho ya Nyamisati na Kilindoni. Mheshimiwa Waziri nikasema tatizo nalionna lipo *TEMESA*, nimewaona wameandika humu kwamba wanashughulikia maegesho hayo, maegesho ya milioni 400 Kilindoni, maegesho ya milioni 400 Nyamisati, mwaka mzima? Mheshimiwa Waziri anafanya kazi vizuri, watu wake wa *TEMESA* wanamwangusha na nilisema kwenye hotuba kama hii mwaka jana. Sasa nisingependa turudi mwakani tuzungumzie habari hii tena ya kivuko na maegesho ya Nyamisati na Kilindoni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la kivuko hiki ambacho kinatengenezwa pale na TEMESA. Kila tukiendelea kufuatilia pale unaambiwa sijui mkataba upo kwa Mwanasheria Mkoo, mara unaambiwa sijui tenda ile ilifutwa, mara unaambiwa subiri kuna vifaa vimeagizwa kutoka nje vinahitaji *exemption*, tatizo lipo kwa Waziri wa Fedha. Sasa ningependa Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* hotuba yake atuambie na atuhakikishie watu wa Mafia kivuko hiki kinatengenezwa na kipo katika hatua gani, maana yake hii habari ya kusema ya kwamba tunasubiri *exemption* kutoka kwa Waziri wa Fedha, ukimuliza Waziri wa Fedha anasema jambo hilo haljui. Ukienda ukizungumzia baadaye unakuja unaambiwa aah kuna tatizo kwenye *procurement* kule wamefuta tenda yenyewe; sasa tushike lipi? Sasa ningeomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie pale na watu wa TEMESA. *I wish* watu wa TEMESA wangejua tabu, dhiki, mashaka na adhabu wanayoipata watu wa Mafia kusafiri kutoka Nyamisati kwenda Kilindoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza kuna watu zaidi ya wiki nzima wako pale, vyombo vile vya mbao vimechoka havina uwezo wa kubebe watu wengi, watu wamekaa pale *stranded* wiki nzima, halafu mtu anatoa majibu mepesi tu kwamba sijui tenda imefanya hivi, mkataba sijui upo kwa Mwanasheria Mkoo, sijui Wizara ya Fedha hajatoa *exemption*; ningeomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* atuambie kwa mapana yake kivuko hiki sasa kitakuwa tayari lini? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni barabara; barabara ya Rasimkumbi mpaka Kilindoni kilometra 45. Tulinong'ona asubuhi akaniambia kwamba hiyo hukionna humo lakini msiwe na wasiwasi. Naomba sana na nilizungumza zaidi ya mara tatu hapa, ile barabara tatizo kubwa Mafia ni kisiwa *periodical maintenance* inabidi utafute udongo, udongo kule umekwisha, sasa wasipoitia lami ile barabara watakuja kujikuta kwamba wanaitengeneza kwa gharama kubwa sana. Ningeomba zile kilometra tano alizoniahidi basi azitekeleze Mheshimiwa Waziri namwamini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni Uwanja wa Ndege wa Mafia, nimeona humu kwenye kitabu viwanja vyote vya ndege humu vinafanyiwa ukarabati lakini Uwanja wa Ndege wa Mafia una matatizo makubwa manne. Tatizo la kwanza *runway* ile ni fupi, hairuhusu ndege ndefu, tunaomba iongezwe. Tatizo la pili, *terminal building* lile ni kama hakuna, limechoka, linavuja na Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuja aliona. Tatizo la tatu, hakuna taa pale; sisi ile ndiyo *escaping route* yetu, ikifika usiku upo Mafia imetokea dharura ya mgonjwa, huna namna ya kum-evacuate kuja Dar es Salaam lazima aende na ndege na kama ndege yenyewe uwanja hauna taa, ina maana kwamba huyo mtu anaweza akapoteza maisha pale akisubiri *evacuation* siku ya pili yake. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwetu sisi kutuwekea taa uwanja wa ndege wa Mafia siyo *luxury* wala siyo kwamba ni kitu cha anasa, ni *necessity* kwetu sisi. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atuambie basi hatima ya Uwanja wa Ndege wa Mafia na kuwekewa taa sambamba na kuongeza eneo lile la kupaki ndege. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *ATCL*; tulizungumza hapa Mafia ni kisiwa cha kitalii, kwa siku kuna *flight* pale zaidi ya nne zinakwenda ndogo ndogo na zote zipo *full*. Nashangaa kwa nini *bombardier* haiji Mafia, abiria wapo wa kutosha, lakini watu wa *ATCL* bado wanasuasua kutuletea usafiri wa ndege kubwa pale kwa ajili ya Kisiwa cha Mafia. Nataka niwahakikishie kwamba watakapoleta *bombardier* pale...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Malizia malizia

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kusisitiza kuhusu suala la kutuletea *bombardier* kwa ajili ya kupunguza tatizo la usafiri Mafia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa fursa hii na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Chatanda, Mheshimiwa Flatei na Mheshimiwa Kiswaga ajiandae.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara hii. Awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha mchana huu wa leo kusimama hapa na kutoa mchango wangu. Vilevile kabla sijasema chochote naomba nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Wenyeviti wa Bodi zote zilizopo kwenye Wizara hii. Vilevile pongezi zangu ziende kwa Katibu Mkuu na Makatibu wote wa kisekta ambao wanahudumu kwenye Wizara hii na bila kuwasahau Wakurugenzi wanaoendesha taasisi mbalimbali zilizopo ndani ya Wizara hii, wanafanya kazi nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kuonyesha kwamba ni namna gani sasa wafanyakazi au wateule hawa wa Mheshimiwa Rais wanaanza kumfahamu Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli anataka kuipeleka nchi sehemu gani, tunataka kwenda wapi. Kwa hiyo, nawapa pongezi, Mwenyezi Mungu awajaalie, awape umri mrefu, waendelee kuhudumu kwenye Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nimeingia kwenye Bunge hili nilitoa hotuba ambayo nilipewa mwongozo na Mheshimiwa Jenista pale. Niliomba kuitoa Liwale kwenye nchi hii kwa sababu ilikuwa kama vile haihitajiki na nikapewa mwongozo kwamba huo ni uhaini. Nilisema Liwale tuitoe kisiwani na leo nasimama hapa napenda kusema rasmi kwamba Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli imesikia kilio change, sasa mwelekeo wa kuitoa Liwale kisiwani unakwenda kutoka. Nilisema tuitoe Liwale kisiwani kwa mawasiliano, leo asilimia 70 ya Liwale tunawasiliana, nasema hongereni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi zangu kubwa sana kwa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, kwa kweli kwa Wilaya ya Liwale umetutendea haki. Napenda kutoa pongezi kwa CEO wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, najua leo hii wanasherehekea miaka 10 ya mafanikio na nawaunga mkono kwa mafanikio waliyoyafikia na kuitoa Liwale kisiwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, nilisema tuitoe Liwale kwa mawasiliano ya barabara na mara nyingi nimesimama hapa nilikuwa naiongelea barabara ya Nangurukulu - Liwale, Liwale - Nachingwea. Namwambia Mheshimiwa Waziri ahsante sana, kwa sababu barabara hizi nimekwenda nimeziona kwenye maandishi yake tayari ametutengea fedha kwa ajili ya kwenda kufanya upembuzi yakinifu na hatimaye iweze kujengwa kwa kiwango cha lami na naomba Mwenyezi Mungu ajalie hilli na tupate fedha hizo ili barabara hii iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijikite kwenye upande wa TAZARA. TAZARA kama ambavyo Mheshimiwa Mwambalaswa amesema, wenzetu wa Zambia wameshapoteza *interest* na reli hii kwa sababu tayari wana reli mbadala kwa ajili ya uchumi wao, sisi ndiyo tumebakika na umuhimu wa kubakia kwenye hii reli. Kwa hiyo, naiomba Serikali hebu wajaribuni kufanya mapitio ya mikataba ya hii reli. Kwanza reli hii kwa kiasi kikubwa kwa upande wa uongozi ipo upande wa Zambia zaidi, ndiyo wenyewe maamuzi, lakini Wazambia hawa pamoja na kwamba ndiyo wenyewe maamuzi kwa kiasi kikubwa lakini bado hawahitaji tena hii reli. Kwa hiyo, naiomba Serikali ifanye mapitio ili tuone ni namna gani tunaweza kuihodhi hii reli, ikiwezekana basi kila upande wa-operate kipande chao ili na sisi tuweze kujikwamua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ndiyo maana sasa hivi TAZARA wanakwenda kwa kusuasua hata mishahara yao ni ya kusuasua kwa sababu bado hawajapewa ile *full mandate* ya kuendesha hii barabara ya TAZARA. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi zote nilizosisema kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa barabara ya Nachingwea - Liwale na Nangurukuru - Liwale, sasa naomba nirejee Mheshimiwa Waziri barabara inayotoka Masasi kwenda Nachingwea. Barabara hii imefanyiwa upembuzi yakinifu tangu mwaka 2015, leo hii kila unapofungua kwenye bajeti unaikuta barabara hii bado inatafutiwa fedha. Barabara hii ni muhimu sana na kwa nini naiongelea barabara hii, naiongelea barabara hii kwa sababu najua hata hiyo barabara ya Nachingwea – Liwale inayokwenda kufanyiwa upembuzi yakinifu, kama barabara ya Nachingwea –Masasi haitojengwa kwa kiwango cha lami, haiwezi kujengwa barabara ya Nachingwea – Liwale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali waiangalie sana hii barabara ya Masasi – Nachingwea, iende sasa ijengwe, huu ni mwaka wa tatu upembuzi yakinifu umekamilika, naomba Mheshimiwa Waziri aitengee fedha ili barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami. Barabara hii inakwenda sambamba na barabara ya Nachingwea – Nanganga. Barabara hizi mbili zikijengwa kwa kiwango cha lami, napata ahuweni kwamba sasa Liwale – Nachingwea inakwenda kujengwa kwa kiwango cha lami. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana na napenda kuisistiza Serikali iendelee kuangalia hii barabara, iweze kujengwa kwa kiwango cha lami ili nami kule barabara ya Nangurukuru –Liwale iweze kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba niongelee hii taasisi ya *MSL*. Mheshimiwa Rais ameonesha nia ya kufufua hii taasisi kwa maana tayari tunaweza kujenga meli kama vile tunavyojenga meli zile pale Mwanza - Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika, tumeona miradi inakwenda kujenga vivuko na meli. Hata hivyo, hii kampuni bado hajaimarika, kampuni hii bado ina madeni makubwa sana, hata wale watumishi bado wanaidai kampuni kwa kiasi kikubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali basi ikiwezekana basi madeni haya Hazina wayachukue ili kampuni hii iweze kujilendesha kwa faida. Kwa inavyoonekana na kwa jinsi *CEO* wa kampuni hii alivyo-committed ni kwamba Serikali watakapowapa *full mandate*, kampuni hii inaweza ikafanya vizuri na ikatuinua kiuchumi na vilevile ikatusaidia kwenye usafirishaji wa mazao mbalimbali ya bahari na maziwa makuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba niongelee hii kampuni ya *TTCL*, kampuni hii ni kampuni ya Serikali au Umma, tulitaraji sana kampuni hii iweze kwenda mbali kwa maana kwamba iweze kupeleka mawasiliano vijijini huko mahali ambapo hakuna mvuto wa kibiashara. Tatizo la kampuni hii ni mtaji, kampuni hii ina tatizo kubwa sana la mtaji na kwa nini ina tatizo la mtaji? Ina tatizo la mtaji kwa sababu kampuni hii vilevile ina madeni makubwa inazidai taasisi mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naiomba Serikali sikivu ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, wawape fedha/mtaji *TTCL* ili waweze kufika mbali kwa sababu sasa hivi *TTCL* wapo kwenye mashindano na makampuni mbalimbali, lakini kama hawatakuwa wanapata mtaji wa kutosha, kampuni hii hawawezi kwenda mbele na hawawezi kuingia kwenye ushindani wakashinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali iendelee kuifutia madeni au ikiwezekana Hazina waifutie madeni basi hii *TTCL* nayo ili iweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo watu hapa wanabeza ununuzi wa ndege, wanayo haki ya kubeza kwa sababu ili waendelee kubaki kule...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Malizia.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: ...ili waweweze kuendelea kubaki kule ni lazima waseme hayo wanayoyasema, lakini kwa kweli ununuzi wa ndege una tija kubwa kwa nchi yetu kwa ajili ya kukuza utalii... (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Chatanda, atafuatiwa na Mheshimiwa Flatei, Mheshimiwa Kiswaga na tutamalizia na Mheshimiwa Lubeleje, *senator*.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasialiano. Kwanza, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara hii. Vile vile nampongeza Meneja wangu wa *TANROAD* wa Mkoa wa Tanga kwa kazi nzuri ambayo ameendelea kuifanya ndani ya Mkoa wetu wa Tanga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye kitabu nimetengewa fedha kwa ajili ya kujenga madaraja; daraja la silabu moja ambalo linakwenda Old Korogwe kwenda Bombo Mtoni ile barabara ya kwenda Bombo mtoni na silabu mbili ambalo ni Maguzoni kwenda Old Korogwe.

Naomba nichukue nafasi hii kushukuru kwani nisiposhukuru katika hili, nitakuwa sijamtendea haki Meneja wangu wa Mkoa kwa sababu eneo hili ni sugu na sasa hivi mvua zinanyesha pale Korogwe, huwa mara nydingi kunatokea mafuriko makubwa pale Old Korogwe. Kwa hiyo, kwa kitendo cha kutengewa hizi fedha, niombe sana basi fedha hizi zikitoka iende ikafanye kazi ili kusudi wananchi wa Old Korogwe waondokane na yale mafuriko ambayo wanayapata kila mwaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie barabara inayotoka Old Korogwe - Kwamote kwenda Kwashemshi – Dindira – Bumbuli - Soni, nimeona imeandikwa humu. Marehemu Profesa Maji Marefu alikuwa anaizungumzia sana barabara hii, iliwekwa kwenye llani ya Uchaguzi lakini naona wameweka hapa kwa ajili ya upembuzi yakinifu. Niwaombe sana fedha hizi zkipatikana, huu upembuzi yakinifu uende ukafanye kazi kwa sababu ni miaka 15 sasa tunasikia tu upembuzi yakinifu; hata watu wa milimani wanahitaji barabara za lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimwombe Waziri pamoja na kututengea fedha hizi, fedha hii itoke ili kusudi ikafanye hiyo kazi ya upembuzi yakinifu, isiwe kila baada ya miaka mitano inaandikwa tu kwamba upembuzi yakinifu. Niombe sana barabara hii ni muhimu kwa uchumi na utalii. Barabara hii inazalisha kwa maana ya Kata zilizopo kule milimani kwa Korogwe Vijiji wanazalisha hiliki, maharage na chakula chungu nzima, kuna soko kubwa pale chini. Niombe sana safari hii naomba ifanyike hii kazi ili kusudi na watu wa milimani waweze kuonja barabara za lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba barabara ya *Old Korogwe* – Kwa Mndolwa – Bombo Mtoni – Maramba – Mabokweni, nayo iingizwe angalau kwenye upembuzi yakinifu. Hii barabara nayo ni ya kiuchumi, mkitusaidia barabara hii itasaidia masuala ya kiutalii na kiuchumi. Pia ni barabara muhimu sana kiusalama, endapo kunakuwa na jambo lolote kwa hizi barabara zilizopo huku mjini barabara hii itatumika. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri barabara hii muitazame kwa jicho la huruma angalau na yenye we iingie kwenye upembuzi yakinifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe barabara ya *Old Korogwe* – Rwengela Darajani – Maguzoni nayo ianze kutazamwa. Barabara hii ikitokea pale Maguzoni, maana akitoka Tanga akija Maguzoni, anakuja Rwengela Darajani anatokea moja kwa moja Korogwe kwenda Arusha. Barabara hii kwanza inafupisha mwendo wa mabasi kuzunguka kutoka Tanga kupitia Segera lakini vilevile ni

barabara ya kiuchumi. Engineer wangu Ndumbaro anaijua barabara hii, naomba sana ikiwezekana na yenyewe iwekwe kwenye mpango angalau wa upembuzi yakinifu ili iweze kuwekwa lami, hayo ndiyo maendeleo yenyewe tunayapeleka vijijini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la *TBA*. *TBA* wanakabidhiwa miradi mingi ya ujenzi lakini inaonekana kabisa kwamba kazi wanazopewa ni nyngi kuliko uwezo wao. Mimi nikio kwenye Kamati ya *LAAC*, tumekwenda kutembelea miradi pale Kahama, tumekuta kuna mradi ambao wamepewa kuujenga hawajaukamilisha na wameutelekeza hapo na fedha wamepewa wanakwenda kujengea miradi mingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana *TBA* wanaonekana hawana fedha, wanasubiri wapewe fedha ndipo waende wakajenge miradi. Kwa kufanya hivyo tunachelewesha miradi, *TBA* ni lazima iwe na fedha za kwenda kufanya hiyo miradi siyo wanapewa kazi halafu ndiyo itafutwe fedha waende wakatengeneze ile miradi. Kwa hiyo, naomba sana *TBA* ikiwezekana wapunguziwe miradi waliyopewa kwa sababu uwezo wa kuikamilisha hawana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nisaidiwe; kutoka pale Kwa Meta kwenda Kwa Mndolwa kumewekwa alama za X kwenye nyumba za wananchi. Nataka nielezwe; hawa wananchi wamewekewa alama za X toka 2016 na mwaka huu tena kuna nyumba zingine zimeenda kuwekewa alama za X, sijajua labda ndiyo hili ombi ninaloomba kwamba mnataka kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuweka lami, kama sivyo basi mniambie mmeweka alama za X kwa ajili ipi na kama hawa wananchi wangu waliowekewa alama za X watalipwa au hawatalipwa? Kwa sababu mmesitisha wasiendelee kujenga kwenye yale maeneo ambayo wamewekewa alama za X, kwa hiyo, wameacha kufanya maendeleo katika nyumba zao. Sasa niombe mniambie kwamba kwa kuwekewa alama zile za X watalipwa ili waweze kuendelea na shughuli zingine? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kushukuru, nimeona tumetengewe fedha kwa ajili ya kufunga mitambo ya ulinzi na usalama katika viwanja vya ndege pale Tanga. Pamoja na hilo, tunaomba basi tutengewe fedha ili uwanja ule uweze kukarabatiwa kama vinavyokarabatiwa viwanja vingine. Na sisi tunahitaji bombadier itue pale Tanga, tunaihitaji sana. Kwa hiyo, pamoja na kuweka hivyo vifaa vya ulinzi lakini iwe ni pamoja na kufanya ukarabati wa kutosha ili bombadier iweze kutua pale Tanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishukuru Serikali kwa kazi kubwa ambayo wameifanya ya ukarabati wa reli ile ya kutoka Tanga – Korogwe – Mombo na kuendelea huko mbele. Tumeona kabisa kazi nzuri ambayo inafanyika, naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sijatenda haki endapo sitampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akiifanya lakini kwa maamuzi ambayo ameyafanya ya uthubutu wa kutekeleza miradi mbalimbali kama vile ya ujenzi wa Reli ya *Standard Gauge*, ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Malizia Mheshimiwa Chatanda.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Flatei na Mheshimiwa Kiswaga ajiandae.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kuunga mkono hoja. Pili, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kweli kwa kufanya kazi ambayo inaonekana kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri wake, Mheshimiwa Eng. Nditiye na Mheshimiwa Kwandikwa, kwa kweli wamefanya ziara kwenye eneo langu, Mungu awabariki sana, chapeni kazi, mimi nawapongeza mno. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru pia kwa minara ambayo kimsingi nimepata kwenye jimbo langu, mawasiliano walau yameanza kuonekana. Niwaombe sasa uko mnara ambao uko Maga na mwingine Dinamo haujawaka bado, imekaa miaka miwili pale. Najua mki-press kidogo tu ile minara itafanya kazi na mawasiliano yataongezeka na kwa ajili hiyo niwashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru pia nimeona kwenye hotuba hapa wametuwekea fedha kidogo kwa ajili ya barabara ya kutoka Dongobesh kwenda Babati itajengwa kwa kiwango cha lami na ile ya Mogitu – Haydom, niwashukuru sana. Sasa nilete ombi ambapo nimeona pia mmeweka kidogo na mmeizingatia barabara hii ya Karatu – Haydom – Sibiti, kwa kweli barabara hii tumeomba kwa miaka mingi sana; Mbulu imezaliwa 1905, mpaka leo kwa kweli haina barabara ya lami kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbulu hii imezaa Karatu ina barabara ya lami; imezaa Babati ina barabara ya lami; imezaa Hanang ina barabara ya lami. Kwa hiyo, Mbulu imekuwa wilaya mama tangu mwaka huo wa 1905, nashukuru kuona walau sasa inakumbukwa na nimeona hela kidogo mmeiweka humu. Nasikitika kuona mchangiaji mmoja ni rafiki yangu sana, Mheshimiwa Waziri wewe msamehe tu, amekuwa akisema unajenga barabara kama kitu kinachoitwa nywele, unajenga kwa huku unakata kwa huku, mimi nikuombe msamehe ni kaka yangu, hana tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe anzia kujenga barabara hapo ulipopanga. Kama tumeomba kwa miaka mingi namna hii barabara ya lami ijengwe kutoka Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti, mimi nikuombe jenga hapo ulipoanza ukianzia Mbulu kwenda Haydom sawasawa, jenga; ukianzia labda Haydom kuja Mbulu, jenga na Mungu akubariki sana. Nimeona hela kidogo umeweka, sasa mimi nikuombe; ongeza kidogo hela hii ili barabara nayo ikamilike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mbulu imesahaulika sana. Kwa nini nasema hivi? Leo ukitaka kupita kwenda Shinyanga na hata ukitoka Simiyu lazima upite Singida, hakuna njia ya mkato kwenda Arusha, kwa hiyo kiuchumi tunaitegemea sana barabara hii ya Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti. Barabara hii inakwenda kwenye majimbo tisa ambayo kimsingi hayana lami kabisa. Mimi leo ukimwambia hata mwanafunzi lami inafanana hawezi kuijua kwa sababu wala hasafiri, ukijua hiyo basi ujue kwamba lami hakuna kwenye maeneo yetu kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nimeshukuru sana na itakuwa mara ya kwanza kukupongeza sana Mheshimiwa Waziri na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu barabara hii imeonekana kwenye kitabu hiki. Kutokana na haya yaliyoonekana hapa isije ikaishia kwenye vitabu na kwa sababu Rais aliahidi na kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi imo, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbulu Vijijini, Jimbo la Mjini, Jimbo la Singida kule Iramba na kila mahali naomba imalizike kwani inahitajika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii kwanza inaunganisha Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Manyara lakini isitoshe inaunganisha Mkoa huu wa Manyara na Mkoa wa Singida. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri kwa kuweka barabara hii utakuwa umetimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais lakini pia utakuwa umefungua eneo la uchumi ambao unatokea maeneo haya barabara ilikopita. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nikupongeze sana na nikuombee Mungu udumu na Mungu akubariki sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitafurahi sasa kuona barabara hii inajengwa, itajengwa wapi mimi sijali, anzia kipande chochote. Muungwana anasema unapoanza jambo unaonesha nia ya dhati kwamba unajenga. Naona kwamba hela ni kidogo lakini kwa kuwa mimi ni muungwana sana na ni Mkristo, naomba nikupongeze hata kama umeweka kidogo lakini nimeona umeweka na Mungu akubariki sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri katika suala la mawasiliano. Leo tunasajili laini za simu kwa kutumia Vitambulisho vya Taifa lakini ukiangalia wenzetu wa *NIDA*, Tume ya Taifa na Uhamijaji ni kama wanafanya kazi zinazofanana. Mimi nishauri tu unaposajiliwa kwenye kitambulisho kimoja kwa mfano Kitambulisho cha Taifa wanapochukua *finger prints* (alamu ya vidole) basi iwe tu katika kumbukumbu moja kwa sababu sisi tuna *Data Center* moja Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *National Data Center* itumike vizuri ili huyu wa *NIDA* akichukua *particulars* (kumbukumbu) za mtu, kumbukumbu hizo zitumike kwenye *NIDA*, Tume ya Taifa na Uhamiaji. Kwa maana hiyo basi mtakuwa mmesaidia kuondoa usumbufu kwa mwananchi ili wakati wa kupiga kura pia alama ya vidole akishaweka inaonekana kila mahali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa nilete ombi jipya kwako; tunayo Hospitali ya Haydom ambapo kimsingi barabara ile ya Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti inaelekea, tuna uwanja wa ndege uko pale na ni muhimu sana. Mheshimiwa Waziri naomba kabisa utuangalie, tuwekee kilometra chache katika kujenga Uwanja wa Ndege wa Haydom ili basi wanapokuja wagonjwa, maana hospitali ile ni ya rufaa na inakwenda kuwa ya kanda, utakuwa umesaidia wagonjwa wakitua pale waweze kufika kwa urahisi katika huduma hii ya kibingwa ya hospitali, nikuombe sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nishukuru sana kwa kupata nafasi hii na nirudie kukupongeza sana na Mungu

akubariki kwa sababu nimeona barabara hii umeiweka. Naamini mwaka huu 2019 kwenda 2020 utajenga barabara ya lami kutoka Mbulu – Haydom – Sibiti na Mungu akubariki sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Kiswaga na Mheshimiwa Lubeleje ajiandae.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano kwa namna ambavyo inatekeleza miradi yake ya kimkakati. Nchi zote duniani zilizofanikiwa kiuchumi ni pamoja na kuwekeza katika miundombinu ya reli, baharini kwa maana ya meli pamoja na anga. Hizo nchi zimefanikiwa sana kiuchumi duniani. Jambo hili limefanywa na Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na barabara ya Magu – Bukwimba – Ngudu na Hungumalwa. Barabara hii imeelezwa asubuhi na kaka yangu, Mheshimiwa Ndassa hapa, ni barabara ambayo iko kwenye ilani, lakini inafungua uchumi kwa sababu inaunganisha barabara kuu mbili; barabara ya kutoka Mwanza – Shinyanga na barabara kutoka Mwanza – Musoma – Nairobi, kwa hiyo, barabara hii ni muhimu sana kiuchumi. Ni vizuri Mheshimiwa *Engineer Kamwelwe, Waziri*, tunajua ni mchapakazi pamoja na Manaibu pamoja na mzee wa *TANROADS, Engineer Mfugale*. Mfugale kwetu maana yake huwezi kufa haraka, kwa hiyo, ndio maana Eng. Mfugale upo hapo, Rais alikuteua, tuone barabara hii unaiweka kwa sababu huwezi kufa haraka kwa maana ya Kisukuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo barabara ya Magu – Mahaha – Itubukilo – Bariadi, inaunganisha Mkoa wa

Mwanza na Mkoa wa Simiyu. Pale katikati Itubukilo na Mahaha tunahitaji daraja. Ni vizuri sasa Mheshimiwa Waziri uone, hili nimekuwa nikiomba kila ninapochangia kila mwaka. Naomba sasa kwenye bajeti hii sasa tusaidie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye Daraja la Sukuma, daraja mmeshatangaza na mkandarasi ameshapatikana, tatizo kibali tu Daraja la Sukuma lianzu kutengenezwa. Hii nadhani ni ile Sheia ya Msamaha wa VAT, inachelewesha sana kwa sababu *documents* za nchi nzima zinakwenda Wizarani kurundikana, inachukua muda mrefu sana kibali kwa ajili ya ujenzi kupatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hizi ambazo tunaziweka Waheshimiwa Wabunge, mimi nishauri tu zile ambazo zinakwamisha kufanya miradi yetu kwenda haraka ni vizuri zikaletwa tukazirekebisha. Kwa sababu hizi sheria zinataka mpaka miradi hii itangazwe kwenye *GN* na inachukua muda mrefu sana kutangazwa kwa sababu ni miradi ya nchi nzima. Hata linapotokea dharura mhusika hawezu kutangaza kazi iweze kutekelezwa, anachukua muda mrefu kwa sababu ya sheria ambazo tumeziweka, ni vizuri tukazirekebisha sheria hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya Mwanangwa - Misasi - Kahama, usanifu tayari umeshafanyika, ni vizuri sasa zikatengwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Pia tunayo barabara muhimu sana ya Nyakato - Igombe TX na barabara ya lami ambayo inatokea *airport*kuja Nyanguge - Kayenze, hizi ni za *ring roads* ambazo zinafungua Mji wa Mwanza kuondokana na misongamano ambao upo. Mheshimiwa Eng. Kamwelwe nakuangalia hapo huandiki, andika ili niweze kuona kweli uko *serious* na jambo hili. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa Ndege wa Mwanza kwa kweli unaendelea kubaki nyuma. Nimeona mmetenga fedha, ni vizuri sasa utekelezaji wake ukaanza, hasa jengo la abiria ili kuweza kuchukua abiria wengi kama ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Iakini kwenye hilihili, Mheshimiwa Eng. Kamwelwe na mnaohusika na ndege, hebu wekeni ndege ya kutoka Dodoma - Mwanza, Mwanza - Dodoma, kuna Mikoa mitano ya Shinyanga, Geita, Mara, Simiyu, Mwanza yenyewe, watumishi tu wa Serikali wanaokuja Dodoma kila siku ni wengi sana, wanatumia magari, ni *risky*. Nawahakishia mkiweka *route* hii mtapata abiria wengi sana, hata mara mbili tu kwa wiki. Tusaidie Mheshimiwa Eng. Kamwelwe, hili tumeshakwambia na tumeshalizungumza mara nyingi na Mheshimiwa Ndassa amezungumza hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe barabara tatu ambazo zipo kwenye Wilaya yetu ya Magu; barabara ya Kisamba - Sayaka - Salama - Bariadi inaunganisha Mkoa wa Simiyu, Wizara ichukue barabara hizi. Mheshimiwa Eng. Kamwelwe ulipoanza kazi kwenye Wizara hii nilikuomba tutembelee pale, nikuombe tena, kama utamaliza bajeti yako wakati wowote twende tuione barabara ya Kisamba - Sayaka - Salama - Bariadi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunayo barabara ya Kabilia - Isawida ambayo inatoka kwa Mheshimiwa Ndassa, Maligisu na Kabilia tuna *junction* sasa ya kwenda Isawida ambako ni Wilaya ya Itilima, Mkoa wa Simiyu. Hizi ni barabara muhimu sana za kutufungua kiuchumi katika mikoa hii miwili. Niombe Wizara izitilie maanani barabara hizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la mawasiliano, Naibu Waziri nimekueleza na nimekuandikia maeneo ambayo Wilaya ya Magu inapata taabu kwa mawasiliano katika Vijiji vya Mwamabanza, Salong'we, Sayaka, Ndagaluh, Nobola, Mahaha, Kigangama pamoja na Bundiria. Hebu tusaidie minara hii angalau wananchi waweze kupata mawasiliano na kuingia kwenye uchumi kirahisi zaidi kwa sababu mawasiliano ya simu yanarahisisha ukuaji wa uchumi kwa wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo barabara ya kutoka Nyanguge kwenda *border* kwa maana ya Musoma, kule

Musoma imetengenezwa mpaka Lamadi lakini kipande hiki cha kilometra 80 kutoka Nyanguge mpaka Lamadi ni barabara kama uko kwenye *bumps*, unaijua vizuri. Mheshimiwa *Engineer Kamwelwe*, hebu fanyeni utaratibu wa kujenga upya barabara hii ili iweze kukamilishwa kama ambavyo Musoma mmeshakamilisha. Nikuombe sana jambo hili ni muhimu, pamoja na Daraja lenyewe la Simiyu, naamini upembuzi yakinifu umeshakamilika. Tunapata adha sana hasa wakati wa masika hakuna mahali popote pa kuweza kupita Mto Simiyu ukiwa umefurika. Hebu daraja hili lijengwe ili angalau watu wa Musoma na Mwanza wasipate adha yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Lubeleje.

WABUNGE FULANI: Hayupo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Justin Monko.

MHE. JUSTIN J. MONKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hotuba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda sana niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano kwa namna ambavyo imewekeza kwenye Wizara hii na inavyojitahidi kutatua matatizo yaliyopo katika *subsectorshizo* tatu ambazo nimezitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na Manaibu Waziri kwa kazi kubwa ambayo wanafanya na kwa namna ambavyo wanajitahidi sana katika kujibu hoja zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudhi kubwa ambazo zinafanyika ningependa nichangie katika maeneo machache katika changamoto ambazo tunaziona kutokana

na hotuba ya Mheshimiwa Waziri ambayo ameitoa hivi leo asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi kubwa ambayo imeshafanyika, katika hotuba ya Waziri ameainisha baadhi ya maeneo ambayo yamefanyiwa kazi, yakiwemo ujenzi wa barabara kuu, lami lakini barabara za Mikoa kwa ujenzi wa lami na vilevile kwa ujenzi kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia vizuri, katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri kazi kweli imefanyika, lakini kwa kweli nimuombe Mheshimiwa Waziri tunahitaji kuongeza kasi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kuongeza kasi kubwa kwa sababu kiwango cha barabara ambacho kimekwisha kutengenezwa mpaka kufikia mwezi wa tatu mwaka huu, kwa barabara kuu ni asilimia 31.9 peke yake ambazo zimekwisha kukamilika kwa mujibu wa takwimu ambazo tumezipata kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ukienda kwenye barabara za Mikoa, hali bado iko vilevile, kwa upande wa barabara za lami, tumefikia asilimia 20 na upande wa barabara za changarawe tumefikia asilimia 12. Kwa hiyo, kasi hii hairidhishi sana, pamoja na kwamba tunafanya mambo makubwa, juhudhi kubwa zinafanyika lakini kasi hii ni ndogo na maana yake ni kwamba maeneo mengi ambayo yalikuwa yamepangwa kwenye bajeti iliyopita mpaka sasa bado hayajafanyiwa kazi na ukizingatia kati ya mwezi wa nne na mwezi wa sita tumbekiwa na sehemu chache sana, au katika miezi mitatu hii hatuna uwezo wa kukamilisha kwa ukamilifu wake maeneo ambayo yamesalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pia hata katika ukarabati, hata katika ukarabati utaona tumeweza tu kukarabati barabara zenye urefu wa km 10,000, 968,000 kati ya 34 ambazo zilikuwa zimekusudiwa. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali kutoa fedha kwa ukamilifu ili kusudi miradi ambayo

tulikuwa tumeshaipanga katika bajeti iliyopita ya mwaka 2018/2019 iweze kukamilika na tunapokuwa tunapanga kwenye bajeti mpya tuwe na uhakika kwamba zile ambazo tutapitisha kwenye bajeti hii ya mwaka huu wa 2019/2020 tunaweza basi tukapata hizo fedha na zikafanya kazi ambayo imekusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu tunakuwa na mashaka mara nyingi kwamba tunapitisha bajeti hapa lakini baadaye fedha zisipotoka miradi ile haikamilik. Nikitolea mfano wa barabara inayotoka Singida, inayokwenda Hydom mpaka Karatu, barabara hii imekuwa kwa muda mrefu kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi kwa zaidi ya miaka saba, imekuwa ikiahidiwa. Na niseme tu mpaka sasa tunashukuru kwamba tumeona kwamba kuna fedha zimetengwa kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ambayo inaanzia pale Singida kwenda mpaka Haydom, na zingine kutoka hydom kwenda karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niiombe sana Serikali, mara, mwaka wa fedha utakapoanza ni vyema sana shughuli hii ikaanza mara moja ili katika mwaka unaofuata tuweze kutengewa fedha za kujengwa kwa kiwango cha lami kwa kuwa barabara hii ni muhimu sana, hasa kwa wananchi wa Mkoa wa Singida na Mkoa wa Manyara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wote ambao wanategemea kusafirisha mazao yao, lakini barabara hii pia ina huduma nyingi hasa huduma za afya kwa sasa tunajenga Hospitali ya Ilongero pale, ambayo wananchi wengi wataitegemea kupata rufaa kutoka kwenye vituo vya afya, lakini tunayo Hospitali ya Haydom, tunayo Hospitali ya Nkungi na maeneo mengi ambayo sasa ya uzalishaji ambayo yanategemea sana uwepo wa barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambasamba na hilo, ipo ahadi ya Rais aliyoitoa pale Mkoani Singida mwaka jana mwezi wa tatu alipotembelea Mkoa wa Singida katika barabara inayotoka Singida mjini, Kinyeto, Merwa inakwenda

mpaka Msange inakwenda kuunganisha na barabara kuu inayokwenda Arusha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sana Wizara hii ikishirikiana na TARURA kutoka TAMISEMI watafuta fedha, watenge fedha ili kusudi upembuzi yakinifu na usanifu wa kina uanze mara moja kwa barabara hii ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ili wananchi wa Jimbo la Singida Kaskazini waweze kunufaika na uwepo wa barabara ya lami, waweze kusafirisha mazao pamoja na wao wenye. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda katika suala la mawasiliano, kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wenzangu mwaka jana hapa tulitoa orodha ndefu sana, kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge ya maeneo ambayo bado hayana mawasiliano ya kutosha na mimi Jimboni kwangu yako maeneo mengi. Ziko Kata tano zina matatizo makubwa kabisa ya usikivu wa mawasiliano, na wawekezaji hawa wa Makampuni haya hawajaweza kuwekeza kule kwa sababu hawawezi kupata faida kutoptana na uchache wa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niiombe sana Serikali iweze sasa kutumia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote kuhakikisha maeneo haya ambayo hayana mawasiliano yaweze kupata mawasiliano. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la mizani, nimeona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wameeleza, lakini niisemee mizani ambayo iko katika barabara ya kutoka Singida kwenda Arusha, tunayo mizani pale Mughamo lakini uko mwingine uko Mkoa wa Manyara, mizani hii inafanya kazi masaa kumi na mbili ya mchana peke yake. Mizani hii haina umeme, mizani hii hazina maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hatuna uwezo wa kulinda barabara zetu kwa masaa ishirini na nne, kwa hiyo, niiombe sana Serikali kujaribu kuwekeza katika maeneo haya, kwa sababu wako watu ambao sasa wanakuwa wanasubiri Watumishi wakishaondoka ile saa kumi na mbili. Wanaanza

kupitisha magari yenyewe uzito mkubwa na matokeo yake barabara zinaharibika na pia Serikali inashindwa kudhibiti hali hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo sio kupata fedha za tozo, lakini lengo ni kulinda barabara zetu ili tusiendelee kujirudia na mtaona barabara ile bado ni mpya lakini tayari imekwisha kuanza kupata maeneo ambayo kwa kweli yana upungufu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niombe sana Wizara, kwa unyenyekevu mkubwa, iko pia barabara inayotoka Singida kwenda Ilongero, kwenda Ngamu hii ni barabara ya Mkoa, na inaenda kuunganisha tena kwenye Mkoa wa Manyara. Barabara hii ni muhimu sana kwa wananchi wa Mkoa Singida na Manyara, niombe sasa ilikuwa imetangazwa km 12.6 za ujenzi kutoka Singida kuelekea Ilongero. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwaka jana ilipotangazwa mwezi wa kumi na moja mpaka sasa, bado hatua za manunuvi hajijakamilika. Nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, aweze kufatilia jambo hili, ili ujenzi wa kiwango cha lami katika barabara hiyo uweze kuanza mara moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja ya Waziri tuweze kupata fedha kwa ajili ya kukamilisha miradi yote ambayo imepangwa kwa bajeti hii ya mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Lubeleje dakika tano, Mheshimiwa Hongoli dakika tano.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza samahani sana nilipata dharura kidogo, kwanza nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja hii ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nimshukuru Waziri, Naibu Waziri, Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi zuri wanayofanya, na tatu nitazungumzia mambo mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza barabara ya Kongwa, Mpwapwa. Kwa kweli naishukuru sana Serikali, imesikia kilio changu imesikia kilio cha wananchi wa Mpwapwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na leo hapa pasingetosha kwa kweli, lakini nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, Mungu akubariki sana umenikumbuka. Pamoja na kwamba umenipa fedha kidogo sana, lakini nisiposhukuru hiki kidogo, hata hicho kikubwa nisingeshukuru. Kwa hiyo, nakushukuru sana, sana na naomba hiyo barabara ianze mapema ili wananchi wa Mpwapwa waone kwamba Mbunge wao kweli anashughulkia suala hili la bararaba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu barabara ni siasa kwa sisi Wabunge, kama umeahidi halafu haitengenezwi, kwa kweli unapata matatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nishukuru sana daraja la Godegode, hili daraja liliisombwa na maji mwaka huu mwezi wa tatu, kwa kweli nashukuru sana, pamoja na kwamba ilikuwa ni dharura lakini Mheshimiwa Waziri nilikuomba. Kwa sababu daraja hili ndiyo kiungo kikubwa cha Jimbo la Kibakwe na Jimbo la Mpwapwa, na kule upande wa Kibakwe kuna Kata saba, sasa zile Kata saba walikuwa wanashidwa kuvuka pale maji yakijaa.

Kwa hiyo, wanazunguka kwenda Kibakwe ndiyo waje Makao Makuu ya Wilaya ambayo ni zaidi ya km 55 na nauji ni kubwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikushukuru sana, sana Mheshimiwa Waziri umesikia kilio cha wananchi wa Mpwapwa na umenitengea fedha daraja la Godegode nina hakika kabisa daraja hili litajengwa kwa wakati muafaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana, nakushukuru na Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hongoli.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupewa nafasi nami kuweza kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri wote, na Watendaji wote wa Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa namna wanavyofanya shughuli zao vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, niongelee tu suala la barabara, suala la barabara, hasa barabara inayotoka Kibena, Lupembe, Madeke na hatimaye Morogoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni barabara muhimu sana, ni barabara muhimu kwa sababu kwanza inaunganisha Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Morogoro kwa hiyo, Mkoa wa Njombe na Morogoro ulikuwa haujaungana muda mrefu sana, lakini kuititia barabara hii sasa utaweza kuunganishwa na hatimaye wananchi wa Njombe wataweza kusafiri kirahisi kwenda Morogoro na kusafirisha mazao yao na mambo mengine. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Mchane tu.

MHE. JORAM I HONGOLI: Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni muhimu sana kwa sababu mazao mengi yanayozalishwa Mkoa wa Njombe yanatokea Lupembe. Mazao kama, mbao, miti, chai, kahawa, matunda parachichi, matunda kama nanasi yanazalishwa sana kwenye barabara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama vile haitoshi, barabara hii pia kuna mazao mengine, kama mazao ya mahindi na maharagwe yanatoka kwenye eneo hili. Kwa hiyo, unaweza ukaona namna gani jinsi ilivyo ya muhimu sana,

kwa uchumi wa Mkoa wa Njombe lakini pia uchumi wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, lakini pia Halmashauri ya Wilaya ya Njombe asilimia 80 ya uchumi wake unategemea sana hii barabara ya Lupembe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama vile haitoshi, barabara hii ya Lupembe inategemewa sana, kwa maana ya wakati wa kifuku. Hii barabara huwa haipitiki, kwa hiyo mazao kama nanasi ambayo yanalinwa eneo la Madeke, ukienda Madeke utakuta kuna mashamba mengi, kuna kama zaidi ya ekari, kuna kama *estates* hizi zipo kule lakini wakati kama huo ambapo mvua inanyesha mazao yale kule yanaozeza shambani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili kuweza kuboresha uchumi na kuinua uchumi wa Mkoa wa Njombe lakini kuuinua uchumi wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ni muhimu sana hii barabara iweze kutengenezwa, lakini nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri na Manaibu Waziri lakini pia na Mheshimiwa Rais kwa kuiweka sasa kwenye mpango sasa tayari kutafutiwa fedha ianze kujengwa kwa kiwango cha lami, kwa hiyo, nawashukuru sana kwa kazi kubwa ambayo mmeifanya mkishirikiana na watendaji wote wa wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo, barabara hii ikitengenezwa kwa kiwango cha lami, uchumi wa Njombe utakua, lakini pia uchumi wa nchi utakua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine niongee nalo kidogo juu ya minara ya simu kuhusu mawasiliano. Tuna changamoto pia ya minara ya simu katika eneo letu hasa maeneo ya Kata Mfiriga eneo la madeke, halifikiki mawasiliano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini eneo la Mfiriga, eneo la Idamba, kuna eneo la Ninga pia halifikiki mawasiliano. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na jitihada nimeziona za Serikali mmetuletea mnara kwenye Kata ya

Ikondo, tayari Ikondo imefunguka japo bado kidogo kuna matatizo kidogo ya kurekebisha, nafikiri mtayarekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tukipata minara hii pia, itasaidia sana kuboresha uchumi. Kwa sababu, uchumi lazima yawepo mawasiliano, mawasiliano ya barabara lakini pia mawasiliano ya simu, ili wananchi au wakulima kwanza waweze kusafirisha bidhaa hizo ambazo wanazalisha ziweze kufikia soko kwa wakati. Lakini pili waweze kuwasiliana na ambako masoko yanapatikana kwa hiyo tukiboresha barabara ikajengwa kwa kiwango cha lami, kwanza tutapunguza muda wa kusafirisha haya mazao kufikia soko, lakini pili wananchi wataweza kupata faida kubwa kwa sababu gharama za usafirishaji zitapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana, niombe kwa Mwenyezi Mungu lakini pia niombe kwa maana ya Mheshimiwa Rais na Waziri, nakuamini sana Mheshimiwa Eng. Kamwelwe na Manaibu wako Waziri na Watendaji wote mtahakikisha kwamba fedha zinapatikana ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami na hatimaye uchumi wa maeneo hayo uweze kupanda na mazao yaweze kufikia soko kwa wakati, lakini pia na ikiwekwa minara ya simu itatusaidia sisi Wakulima wa Lupembe kuweza kuwasiliana na soko. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake, sasa hivi mambo ya ki-digitali, mambo ya teknolojia, lazima kuwe na mawasiliano na hatimaye uweze kuuza kwa wakati na uweze kufikia kujua soko liko wapi na uweze kuuza mazao yako. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nikuombe sana najua una kazi nyingi na unafanya mengi, lakini naomba utusaidie kwa haya mambo mawili makubwa ya barabara na hili la minara ili wananchi wetu wa Lupembe waweze kuuza mazao yao lakini waweze kusafirisha mazao yao na nguzo ziweze kufikia soko na hatimaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hizi nguzo zinatumika kwenye usambazaji wa umeme, ili tusiwe na tatizo la nguzo, sisi tunalima miti mingi sana, na tunazalisha nguzo nyingi lakini pia zinauzwa kwa bei nzuri. Kwa hiyo, kumbe

mkitengeneza hii barabara tutaweza kuuza nguzo na hatimaye tatizo la nguzo nchini litapungua kwa sababu zile nguzo zipo kule na zinapatikana na zinasafirishwa kira hisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo machache nishukuru sana kwa nafasi lakini niunge mkono hoja iliyopo mbele yetu, ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa nawashuruku muda wetu umekwisha, na wachangiaji wote wamekwisha niwapongeze kwa michango mizuri, nahairisha shughuli mpaka kesho saa tatu asubuhi. (*Makof*)

*(Saa 12.01 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 10 Mei, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*